# KUCHUNGUZA FANI YA BIBLIA KATIKA FASIHI ANDISHI YA KISWAHILI: MIFANO KUTOKA KATIKA TAMTHILIYA ZA EMMANUEL MBOGO

**EMMANUEL OSCAR MSANGI**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMIVU KATIKA KISWAHILI YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA, IDARA YA TAALUMA ZA ISIMU NA FASIHI**

**2023**

# ITHIBATI

Walioweka saini hapa chini wanathibitisha kuwa wameisoma tasnifu hii iitwayo: "**Kuchunguza Fani ya Biblia Katika Fasihi Andishi ya Kiswahili: Mifano kutoka katika Tamthiliya za Emmanuel Mbogo"** na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha masharti ya Shahada ya Uzamivu katika Kiswahili (PhD in Kiswahili Literature) ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Idara ya Taaluma za Isimu na Fasihi.

..................................

Dkt. Mohamed Omar Maguo

(Msimamizi)

.................................

(Tarehe)

.................................

Dkt. Felistas Mahonge

(Msimamizi)

...............................

(Tarehe)

## HAKIMILIKI

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa njia yoyote ile, iwe kazi nzima au sehemu ya kazi hii bila kibali cha maandishi cha Mkuu wa Kurugenzi ya Taaluma Elimu ya Juu, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, kwa niaba ya mwandishi, isipokuwa kwa shughuli halali, kama vile kwa ajili ya utafiti, kujisomea au kufanya marejeo ya kitaaluma.

# TAMKO

Mimi **Emmanuel Oscar Msangi,** ninathibitisha kwamba tasnifu hii ni kazi yangu halisi na kwamba haijawahi kuwasilishwa na haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya masharti ya kupata shahada kama hii au nyingine yoyote.

……………………..………………

**Sahihi**

…………………………

**Tarehe**

## TABARUKU

Kazi hii ninaitabaruku kwa mtoto wangu mpendwa Lilian Emmanuel Oscar Msangi kwa sala na dua zake alizofanya kipindi chote cha masomo haya ili yakamilike. Sala na dua hizo zilikuwa ngazi njema kufikia maono haya yaliyodumu kipindi chote hiki cha utafiti. Kazi hii iwe kumbukumbu yake na wajumbe wote wa familia ya Mzee Oscar Msangi zama zote za maisha yao.

## SHUKRANI

Ninamshukuru NIKO AMBAYE NIKO kwa unyenyekevu mkuu, Mungu wa Ibrahim muweza wa yote kwa kunijalia uzima na afya, ulinzi na maarifa wakati wote wa masomo ya uzamivu. Mungu Mwenyezi amekuwa nami wakati wote wa masomo ya daraja hili. Mola aliniongoza, alinishika kwa mkono wake na kunipa kibali, nikapokelewa vema pote nilipoingia na kutoka kipindi chote cha utafiti huu wa shahada ya uzamivu.

**Pili**, napenda kuwashukuru kwa dhati wasimamizi wangu, Dkt. Mohammed Omar Maguo na Dkt. Felistas Mahonge kwa kuniongoza vema katika kila hatua ya utafiti huu. Wasimamizi hawa hawakusita wala hawakuchoka kunishauri na kuirekebisha kazi hii katika hatua zote mpaka ilipokamilika. Wamenilea kitaaluma na kunipa misingi ya nadharia za fasihi, mwingilianomatini sambamba na mbinu za utafiti ambazo zimesaidia kukamilika kwa kazi hii. Kwa dhati ya moyo wangu namsihi Rabuka awabariki na awape afya njema na kuwazidishia mema katika huduma wanayoitoa kwa wazamivu wa fasihi ya Kiswahili kila uchao katika ndaki mbalimbali ndani na nje ya Tanzania. Amin!

**Tatu**, ninatoa shukrani zangu za dhati kwa Dkt. Dunlop Ochieng, Mtiva Kitivo cha Sanaa na Sayansi za Jamii, hapa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kupitia Idara ya Taaluma za Isimu na Fasihi chini ya Dkt. Zelda Elisifa, Mudir wa Idara kwa kukubali kudhamini sehemu ya masomo yangu ya uzamivu. Ninashukuru mno!

**Nne**, Ninawashukuru wahadhiri wote wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, katika Idara ya Taaluma za Isimu na Fasihi kwa kunilea kitaaluma na kunikuza kinadharia

na vitendo. Wahadhiri hao ni Dkt. Zelda Elisifa, Dkt Hadija Jilala, Dkt. Nasra Habib, Dkt. Salma Hamad, Dkt. Jacob Mwalongo, Dkt. Ancyfrida Prosper, Dkt. Elizabeth Kyara, Dkt. Anna Kyamba, Dkt. Lazaro Charles, Mwl. Bakati Kombo, Mwl. Mosi Masatu, Mwl. Faustine John, Mwl. Theresia Mbogo, Mwl. Frida Mbwafu pamoja na Mwl. Yohana Makeja.

Mwisho (si kwa umuhimu), ninawashukuru Dkt. Edith Lyimo, Dkt. Elizabeth Mahenge, Dkt. Angelus Mnenuka wa Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Dkt. Wallace Mlaga wa Taasisi ya Elimu Kigali. Ninawashukuru wanazuoni hao kwa ushauri walionipatia nilipowafuata wakati wa utafiti na wengine wote ambao wameshiriki kwa namna mbalimbali kusaidia utafiti na uandishi wa tasnifu hii kukamilika. Mungu ambariki sana kila mtu aliyeshiriki kwa namna yoyote katika kukamilisha utafiti huu.

Emmanuel, ninashukuru!

## IKISIRI

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa *Kuchunguza Fani ya Biblia katika Fasihi Andishi ya Kiswahili: Mifano kutoka katika Tamthiliya Teule za Emmanuel Mbogo.* Katika kulifikia lengo kuu la utafiti kulikuwa na malengo mahsusi matatu. Malengo hayo yalikuwa: kubainisha fani za Biblia katika tamthiliya teule za Emmanuel Mbogo, kutafuta sababu za kujitokeza kwa fani za Biblia katika tamthiliya teule za Emmanuel Mbogo pamoja na kubainisha dhamira zinazojidhihirisha kutokana na kuhusishwa kwa fani za Biblia katika tamthiliya teule. Katika utafiti huu ilitumika sampuli moja; sampuli lengwa. Sampuli lengwa ilirejea Biblia na maandiko ya Emmanuel Mbogo yaani *Tanzia ya Patrice Lumumba* (2015), *Wangari Maathai* (2015), *Mtumwa hadi Siti Binti Saad* (2016), *Nyota ya Tom Mboya* (2016), *Malkia Bibi Titi Mohamed* (2016) na *Mondlane na Samora* (2016). Ukusanyaji, uchambuzi na mjadala wa data uliongozwa na Nadharia ya Mwingilianomatini. Data za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia mbinu moja, mbinu ya usomaji matini. Mkabala wa kimaelezo ndiyo ulitumika kuchambua data za utafiti huu. Kimsingi, matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa kuna fani nyingi za Biblia katika tamthiliya za Emmanuel Mbogo. Vipengele vya kifani ndivyo vilitumika katika kuchanganua Ubiblia huo: nukuu za Biblia, wahusika wa Biblia, hadithi za Biblia, sajili ya Biblia na mandhari ya Biblia. Tamthiliya zote sita zilizotafitiwa, taswira ya Biblia imeonekana ndani yake. Mathalani simulizi ya kuzaliwa na kufa kwa Yesu Kristo katika Biblia huko Uyahudi zimesikika katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya*. Wafuasi wa Nadharia ya Mwingilianomatini wanaeleza kuwa kazi yoyote ya fasihi ni zao la kazi tangulizi (Kristeva, 1981). Kimsingi, tulibaini athari ya kitabu cha Biblia katika tamthiliya teule zilizoandikwa zaidi ya miaka 2000 mbele tangu Biblia iandikwe. Pia utafiti umebaini kwamba, fani za Biblia mbalimbali alizohusisha mtunzi teule katika kazi zake zililenga kuwasilisha dhamira fulani kwa hadhira. Mfano, umuhimu wa kutunza historia katika jamii. Emmanuel Mbogo ameandika tamthiliya nyingine karibuni kama vile tamthiliya ya *Julius Nyerere Kizimbani* (2022) na *Mwinyi na Manyani ya Adili* (2022). Tunapendekeza tafiti nyingine zifanyike ili kuendelea kustawisha uga wa fasihi andishi kupitia maandiko ya mwandishi teule.

# YALIYOMO

**ITHIBATI** .......... **ii**

**HAKIMILIKI** .......... **iii**

**TAMKO** .......... **iv**

**TABARUKU** .......... **v**

**SHUKRANI** .......... **vi**

**IKISIRI** .......... **viii**

**YALIYOMO** .......... **ix**

**ORODHA YA VIFUPISHO** .......... **xv**

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI** .......... **1**

1. 1 Utangulizi .......... 1

1. 2 Usuli wa Tatizo la Utafiti .......... 1

1. 3 Emmanuel Mbogo katika Fasihi ya Kiswahili .......... 4

1. 4 Mihtasari ya Tamthiliya Teule .......... 5

1. 4. 1 Muhtasari wa Tamthiliya ya Nyota ya Tom Mboya .......... 6

1. 4. 2 Muhtasari wa Tamthiliya ya Wangari Maathai .......... 6

1. 4. 3 Muhtasari wa Tamthiliya ya Tanzia ya Patrice Lumumba .......... 7

1. 4. 4 Muhtasari wa Tamthiliya ya Mondlane na Samora .......... 8

1. 4. 5 Muhtasari wa Tamthiliya ya Malkia Bibi Titi Mohamed .......... 9

1. 4. 6 Muhtasari wa Tamthiliya ya Mtumwa hadi Siti Binti Saad .......... 10

1. 5 Tamko la Tatizo la Utafiti .......... 11

1. 6 Malengo ya Utafiti .......... 12

1. 6. 1 Lengo Kuu .......... 12

1. 6. 2 Malengo Mahsusi .......... 12

1. 7 Maswali ya Utafiti ........................................................................ 13

1. 8 Umuhimu wa Utafiti ........................................................................ 13

1. 9 Mipaka ya Utafiti ........................................................................ 13

1. 10 Mpangilio wa Tasnifu ........................................................................ 14

**SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDIKO NA KIUNZI CHA NADHARIA ........................................................................ 15**

2. 1 Utangulizi ........................................................................ 15

2. 2 Utalii wa Dhana Mahsusi katika Utafiti huu ........................................................................ 15

2. 2. 1 Fasihi ya Kiswahili ni ipi? ........................................................................ 15

2. 2. 2 Fasihi Andishi ya Kiswahili ........................................................................ 17

2. 2. 3 Dhana ya Tamthiliya ........................................................................ 18

2. 2. 4 Biblia katika Fasihi ........................................................................ 21

2. 3 Tafiti Tangulizi Kuhusu Maandiko ya Emmanuel Mbogo ........................................................................ 22

2. 5 Pengo la Maarifa ........................................................................ 29

2. 6 Muhtasari ........................................................................ 30

**SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI ........................................................................ 31**

3. 1 Utangulizi ........................................................................ 31

3. 2 Eneo la Utafiti ........................................................................ 31

3. 3 Usanifu wa Utafiti ........................................................................ 31

3. 4 Usampulishaji ........................................................................ 32

3. 5 Vyanzo vya Data ........................................................................ 32

3. 6 Ukusanyaji wa Data ........................................................................ 32

3. 7 Usahihi wa Mbinu za Utafiti ........................................................................ 33

3. 8 Uchanganuzi wa Data ........................................................................ 34

3. 9 Kuaminika kwa Matokeo ya Utafiti ........................................................... 34

3. 10 Maadili ya Utafiti ........................................................................................ 34

3. 11 Muhtasari ..................................................................................................... 35

**SURA YA NNE: UWASILISHAJI WA DATA, UCHAMBUZI NA MJADALA WA MATOKEO ........................................................................................ 36**

4. 1 Utangulizi ...................................................................................................... 36

4. 2 Fani za Biblia na Sababu za Kujitokeza kwake katika Tamthiliya Teule .... 36

4. 2. 1 Nukuu za Biblia katika Tamthiliya Teule .................................................. 38

4. 2. 1. 1 Nukuu za Biblia katika Tamthiliya ya *Mondlane na Samora* ............................... 39

4. 2. 1. 2 Nukuu za Biblia katika Tamthiliya ya Wangari Maathai ..................................... 40

4. 2. 1. 3 Nukuu za Biblia katika Tamthiliya ya Nyota ya Tom Mboya ............................. 42

4. 2. 1. 4 Nukuu za Biblia katika Tamthiliya ya Tanzia ya Patrice Lumumba ................... 43

4. 2. 1. 5 Nukuu za Biblia katika Tamthiliya ya Mtumwa hadi Siti Binti Saad ................. 45

4. 2. 1. 6 Nukuu za Biblia katika Tamthiliya ya Malkia Bibi Titi Mohamed ..................... 47

4. 2. 1. 7 Muhtasari ............................................................................................................ 48

4. 2. 2 Simulizi za Biblia katika Tamthiliya Teule ............................................. 49

4. 2. 2. 1 Simulizi za Biblia katika Tamthiliya ya Mondlane na Samora .......................... 50

4. 2. 2. 2. Simulizi za Biblia katika Tamthiliya ya Wangari Maathai ............................... 55

4. 2. 2. 3 Simulizi za Biblia katika Tamthiliya ya Nyota ya Tom Mboya ....................... 56

4. 2. 2. 4 Simulizi za Biblia katika Tamthiliya ya Tanzia ya Patrice Lumumba .............. 60

4. 2. 2. 5 Simulizi za Biblia katika Tamthiliya ya Mtumwa hadi Siti Binti Saad ............. 61

4. 2. 2. 6 Simulizi za Biblia katika Tamthiliya ya Malkia Bibi Titi Mohamed ................. 63

4. 2. 2. 7 Muhtasari ........................................................................................................... 64

4. 2. 3 Sajili ya Biblia katika Tamthiliya Teule .................................................. 65

4. 2. 3. 1 Sajili ya Biblia katika Tamthiliya ya Mondlane na Samora .................................. 66
4. 2. 3. 2 Sajili ya Biblia katika Tamthiliya ya Wangari Maathai ...................................... 69
4. 2. 3. 3 Sajili ya Biblia katika Tamthiliya ya Nyota ya Tom Mboya ............................... 75
4. 2. 3. 4 Sajili ya Biblia katika Tamthiliya ya Tanzia ya Patrice Lumumba....................... 78
4. 2. 3. 5 Sajili ya Biblia katika Tamthiliya ya Mtumwa hadi Siti Binti Saad ..................... 81
4. 2. 3. 6 Sajili ya Biblia katika Tamthiliya ya Malkia Bibi Titi Mohamed.......................... 86
4. 2. 3. 7 Muhtasari.......................................................................................................... 89
4. 2. 4 Wahusika wa Biblia katika Tamthiliya Teule.............................................. 89
4. 2. 4. 1 Wahusika wa Biblia katika Tamthiliya ya Mondlane na Samora ........................... 92
4. 2. 4. 2 Wahusika wa Biblia katika Tamthiliya ya Wangari Maathai................................ 95
4. 2. 4. 3 Wahusika wa Biblia katika Tamthiliya ya Nyota ya Tom Mboya ........................ 97
4. 2. 4. 4 Wahusika wa Biblia katika Tamthiliya ya Tanzia ya Patrice Lumumba.............. 99
4. 2. 4. 5 Wahusika wa Biblia katika Tamthiliya ya Mtumwa hadi Siti Binti Saad ............ 102
4. 2. 4. 6 Wahusika wa Biblia katika Tamthiliya ya Malkia Bibi Titi Mohamed............... 105
4. 2. 4. 7 Muhtasari........................................................................................................ 107
4. 2. 5 Mandhari ya Biblia katika Tamthiliya Teule ............................................ 108
4. 2. 5. 1 Mandhari ya Biblia katika Tamthiliya ya Mondlane na Samora ......................... 110
4. 2. 5. 2 Mandhari ya Biblia katika Tamthiliya ya Wangari Maathai ............................... 112
4. 2. 5. 3 Mandhari ya Biblia katika Tamthiliya ya Nyota ya Tom Mboya....................... 114
4. 2. 5. 4 Mandhari ya Biblia katika Tamthiliya ya Tanzia ya Patrice Lumumba ............... 116
4. 2. 5. 5 Mandhari ya Biblia katika Tamthiliya ya Malkia Bibi Titi Mohamed................ 117
4. 2. 5. 6 Muhtasari........................................................................................................ 119
4. 4 Dhamira Zilizowasilishwa kupitia Fani za Biblia Zilizobainishwa katika Tamthiliya Teule ......................................................................... 119

4. 3. 1 Nafasi ya Dua na Sala katika Jamii ........ 123
4. 3. 2 Nafasi ya Viongozi wa Dini katika Jamii ........ 126
4. 3. 3 Uadilifu na Unyenyekevu katika Jamii ........ 129
4. 3. 4 Kutokukata Tamaa katika Maisha ........ 133
4. 3. 5 Nafasi ya Ubatizo kwa Waumini wa Kikristo ........ 138
4. 3. 6 Waumini wa Kikristo kuwa Makini na Manabii wa Uongo ........ 141
4. 3. 7 Nafasi ya Shukurani kwa Mwenyezi Mungu ........ 144
4. 3. 8 Kuheshimu Wazazi na Walezi katika Jamii ........ 148
4. 3. 9 Umuhimu wa Elimu katika Jamii ........ 151
4. 3. 10 Mapenzi na Ndoa katika Jamii ........ 154
4. 3. 11 Ukombozi wa Kisiasa Afrika ........ 168
4. 3. 12 Ukombozi wa Kifikra ........ 182
4. 3. 14 Burudani kwa Jamii ........ 218
4. 5 Muhtasari ........ 228
**SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........ 230**
5. 1 Utangulizi ........ 230
5. 2 Muhtasari ........ 230
5. 3 Hitimisho ........ 235
5. 4 Mapendekezo ........ 235
**MAREJELEO ........ 237**

## MAJEDWALI

Jedwali Na. 4. 1 Fani za Biblia Zilizojitokeza katika Tamthiliya Teule ………...... 38

Jedwali Na. 4. 2: Kuonyesha Maajabu ya Nabii Musa huko nchini Misri ……...… 77

Jedwali Na. 4. 3 Wanawake Waliotumika Kufanya Mambo Makubwa Katika Jamii Zao Katika Biblia ………………………………………….…..... 88

Jedwali Na. 4. 4: Kuonyesha Wahusika Waliorejewa kama Pauline kutoka katika Biblia ……………………………………………………….. 101

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| AAPC | The All African People's Congress |
| B. K | Baada ya Kristo |
| BAKITA | Baraza la Kiswahili la Taifa |
| DRC | Democratic Republic of Congo |
| FRELIMO | Frente de Libertação de Moçambique |
| K. W. K | Kabla ya Wakati wa Kristo |
| Ktj. | Keshatajwa |
| SUV. | Swahili Union Vision |
| TANU | Tanganyika African Nation Union |
| TATAKI | Taasisi ya Taaluma za Kiswahili |
| TUKI | Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili |
| TY | Tafsiri yangu |

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1. 1 Utangulizi

Sura hii imebainisha tatizo lililofanyiwa uchunguzi katika utafiti huu. Hali kadhalika imeeleza usuli wa tatizo la utafiti, wasifu wa Emmanuel Mbogo, mihtasari ya tamthiliya teule, tamko la utafiti, malengo ya utafiti na maswali ya utafiti. Pamoja na hayo mtafiti ameeleza umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti hatimaye akahitimisha kwa kubainisha mpangilio wa tasnifu.

## 1. 2 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Fani ni jumla ya mbinu, mtindo na nyenzo anazotumia mwandishi kuwasilisha maudhui yake kwa msomaji (Martin, 2021). Mwanazuoni huyu anaendelea kushadidia kuwa, mwandishi hawezi kusema analotaka kulisema bila ya kutumia vipengele vya kifani mathalani muundo, mtindo, wahusika; mandhari na matumizi ya lugha. BAKITA (2022) wanafasili fani kama kipengele katika uwanja wa fasihi kinachojihusisha na umbo la nje la kazi ya fasihi. Kimsingi, fani inaweza kuelezwa kama jumla ya vipengele vinavyotumiwa na watunzi wa kazi za fasihi kuwasilisha maudhui kwa hadhira lengwa. Wanazuoni katika uga wa fasihi wanakubali kwamba fani na maudhui hukamilishana ili kufikisha ujumbe kwa hadhira (Oiko, 2017). Hivyo basi fani huchukuliwa kama kiunzi cha kufikisha maudhui kwa hadhira lengwa.

Mtafiti aliitumia dhana ya **fani ya Biblia** kurejea vipengele vya kifani vilivyojitokeza awali kwenye Biblia kisha vikaonekana baadaye kwenye fasihi andishi ya Kiswahili.

Vipengele hivyo ni nukuu za Biblia, wahusika wa Biblia, mandhari za Biblia, hadithi za Biblia, majina ya vitabu ndani ya Biblia, misamiati ya Biblia na semi za Biblia.

Wanazuoni katika uga wa fasihi ulimwenguni wametafiti kwa namna mbalimbali maingiliano ya vitabu vya kiimani na fasihi. Miongoni mwa watafiti hao ni Kaufuman (1976), Ngugi na Alter (1981), Mulokozi (1999), Karisa na Mwinyifaki (2013), Ryken (2014), Osore (2015), Ren (2015), Kohm III (2016), Msangi (2018) na Wamitila (2019). Vitabu vya kiimani vilivyorejewa muda mwingi tafiti hizo zilipofanyika ni Biblia (Wakristo) na Kurani (Waislamu). Tafiti hizo tangulizi zinakiri kuwepo kwa mahusiano ya fasihi na vitabu vya kiimani. Biblia inaelezwa kuathiri fani na maudhui ya kazi za fasihi kulingana na dhehebu alilomo mtunzi wa kazi mahsusi.

Ryken (2014) anasema, "Biblia inachukuliwa kama chanzo cha msingi kabisa cha fasihi ya Kiingereza na Kimarekani." Mwanazuoni huyo alitumia *Utenzi wa Kaedmon*, utenzi wa kale mno katika fasihi ya Kiingereza kubainisha mahusiano ya fasihi na Biblia. Tungo hiyo inadaiwa kuchota maudhui yake kutoka katika Biblia, kitabu cha Mwanzo 1 & 2 kisha kitabu cha Zaburi kikatumika kupangilia beti zake. Utafiti huu ulikuwa daraja zuri kwa utafiti tuliofanya kwani ulithibitisha kuwepo kwa muingiliano wa fasihi na Biblia kwa kuhusisha fani na maudhui ya kazi za fasihi na Biblia.

Mtaalam mwingine aliyetafiti kuhusu muingiliano wa Biblia na fasihi ni Ren (2015). Mwanazuoni huyo alitafiti mchango wa Biblia katika kufasili kazi za fasihi. Ren (Ktj) anaendelea kushadidia kuwa Biblia imeathiri sana fasihi katika nchi za

Magharibi kwa namna isiyoweza kuelezeka. Ndipo sasa washairi na wanathari kutoka kanda hizo wakaonekana kumezwa mno na mitindo mbalimbali ya kifasihi iliyotumika katika Biblia hapo kwanza.

Fauka ya hayo fasihi andishi ya Kiswahili imehusishwa na vitabu vya dini za Ukristo na Uislam. Vitabu viwili vinavyotumika kwenye dini hizo, *Biblia* na *Kurani* vimeelezwa kuathiri watunzi wa kazi za fasihi ya Kiswahili. Athari zake zinajitokeza katika namna mbalimbali. Vipengele vya fani na maudhui vya *Biblia* na *Kurani* vinajitokeza kwenye bunilizi za waandishi wa fasihi ya Kiswahili kutokana na dini au dhehebu mwandishi alilomo. Mwandishi akiwa muumini wa Kikristo, dini inayotumia kitabu cha *Biblia*, basi fani za Biblia zinadhihirika katika kazi zake. Endapo mtunzi ni Muislam na anatumia kitabu cha *Kurani* basi fani za Kurani zinadhihirika ndani ya tungo zake.

Mulokozi (1999) alieleza kuwa Utenzi wa Mwanakupona umejikita katika nguzo za Uislamu. Hakuna shaka kwamba mtunzi, Mwanakupona binti Mshamu Nabhany alichota wosia wake kutoka katika Kurani na Sunnah za Mtume Muhammad (SAW). Dhamira zote msingi zilizojadiliwa katika Utenzi wa Mwanakupona ni tokeo la mafundisho yaliyotolewa katika kitabu cha *Kurani* kinachotumiwa na waumini wa dini ya Kiislam.

Ngugi (2004), alipohutubia katika Kongamano la 57 la Baraza la Kitaifa la Makanisa Nchini Kenya alidhihirisha kwamba, Biblia imeathiri fasihi ya Kiswahili. Mwanazuoni huyo alieleza kwamba watunzi wa fasihi huchota visa, matukio au aya

kutoka ndani ya Biblia na kuandika kazi za kifasihi katika jamii zao. Mwanazuoni huyo anasema,

> *"Katika Afrika, jinsi ilivyo katika maeneo mengine duniani, Biblia ndiyo andiko la kimsingi la fasihi za mataifa mbalimbali."*
> Ngugi wa Thiong'o (2004)

Kimsingi tafiti mbalimbali kuhusu uhusiano wa vitabu vya dini na fasihi mathalani fasihi andishi umehusisha tanzu hizi; riwaya, tamthiliya na ushairi. Wanazuoni katika ndaki mbalimbali za elimu ukanda wa Afrika Mashariki wanakiri kuwepo kwa uhusiano baina ya vitabu vya dini na fasihi ya Kiswahili.

Pamoja na hayo, tafiti tangulizi kuhusu muingiliano wa Biblia na fasihi zimebainisha fani za kibiblia katika kazi za fasihi. Watafiti hawakueleza sababu ya kutokea kwa fani za Biblia katika kazi za fasihi. Pia tafiti hazikutazama dhamira zinazodhihirika katika fani za Biblia ndani ya kazi teule. Vilevile tamthiliya teule zilizotumika kwenye utafiti huu hazikutafitiwa kwa mlengo huo.

Kutokana na hayo mtafiti aliona kwamba kuna haja ya kufanya utafiti kuhusu mwingiliano wa vitabu vya dini na fasihi andishi ya Kiswahili akirejelea kazi teule za Emmanuel Mbogo ambazo bado zilikuwa hazijatafitiwa. Mifano katika kushadidia hoja za utafiti huu ilitolewa kutoka katika tamthiliya hizo teule za Kiswahili. Tafiti kutoka Ulaya, Asia, Amerika, Afrika na Tanzania zilisaidia kusogeza mbele utafiti huu kwa kutoa data mbalimbali za upili.

## 1. 3 Emmanuel Mbogo katika Fasihi ya Kiswahili

Emmanuel Mbogo ni mwandishi wa tamthiliya, riwaya na hadithi fupi. Mtunzi huyu alizaliwa tarehe 01/03/1947, wilayani Kongwa, mkoa wa Dodoma, nchini Tanzania.

Bunilizi za kinathari ndizo zilizomshughulisha Emmanuel Mbogo katika tasnia ya fasihi andishi ya Kiswahili. Tanzu mbili za fasihi andishi; tamthiliya na riwaya ndizo zimenufaika zaidi na kipawa cha mwandishi huyu katika utunzi wa kazi za fasihi.

Baadhi ya vitabu vya fasihi ya Kiswahili alivyoandika ni hivi vifuatavyo: *Watoto Wetu* (1972), *Giza Limeingia* (1977), *Tone la Mwisho* (1981), *Ngoma ya Ng'wangamalundi* (1988), *Morani* (1993), *Sundiata* (2011), *Vipuli vya Figo* (2008), *Fumo Liongo* (2009), *Watoto wa Mama Ntilie* (2002), *Bustani ya Edeni* (2002), *Dawa Dhidi ya Magonjwa Yote* (2012), *Mizungu ya Manabii* (2019), *Siri za Maisha* (2010), *Sadaka ya John Okello* (2014), *Ndoto za Josef* (2016), *Wachawi wa Bongo* (2018), *Nyerere na Safari ya Kanaani* (2015), *Wangari Maathai* (2015), *Nyota ya Tom Mboya* (2016), *Malkia Bibi Titi Mohamed* (2016), *Mtumwa hadi Siti Binti Saad* (2016), *Kumng'oa Nduli* (2021), *Julius Nyerere Kizimbani* (2021), *Nyerere na Vijiji vya Ujamaa* (2021), *Shujaa Mirambo* (2021) *pamoja na Mwinyi na Manyani ya Adili* (2022).

Kazi zilizofanyiwa uchunguzi katika utafiti huu ni hizi; *Tanzia ya Patrice Lumumba* (2015), *Wangari Maathai* (2015), *Nyota ya Tom Mboya* (2016), *Mondlane na Samora* (2016), *Malkia Bibi Titi Mohamed* (2016) na *Mtumwa hadi Siti Binti Saad* (2016). Mtafiti alichagua tamthiliya hizi sita kwa kuwa zilitosha kumpatia data za kuweza kujibu maswali yaliyopelekea kufanikisha lengo kuu la utafiti huu.

## 1.4 Mihtasari ya Tamthiliya Teule

Katika sehemu hii mtafiti ameeleza mihtasari ya tamthiliya teule zilizotumika katika utafiti huu. Kila tamthiliya imeelezwa muhtasari wake pekee. Vipera vya fani na maudhui vimehusishwa kwa pamoja katika mihtasari hii kuhusu kazi teule.

### 1. 4. 1 Muhtasari wa Tamthiliya ya Nyota ya Tom Mboya

Tamthiliya hii imeandikwa na Emmanuel Mbogo mwaka 2016. Ni tamthiliya iliyoandikwa kwa ustadi mkubwa. Tamthiliya hii imepangwa katika sehemu kuu sita. Ndani ya kila sehemu kuna maonesho mawili. Mhusika mkuu kwenye tamthiliya hii ni Tom Mboya.

*Nyota ya Tom Mboya* ni tamthiliya ya kihistoria inayosawiri uwezo, hekima na umahiri wa mwanasiasa mashuhuri nchini Kenya, aliyefahamika kwa jina la Tom Mboya. Mboya aliheshimika kwa uwezo wake mkubwa wa kupanga mikakati madhubuti iliyolenga kuleta maendeleo kwa Wakenya wote. Licha ya mikinzano na hila za kisiasa; licha ya mizengwe na minyukano ya chini kwa chini ya ukabila; siku zote Tom Mboya alikubalika na makabila yote na kupata ushindi katika kila uchaguzi; akawa mbunge katika jimbo ambalo asilimia kubwa ya wapiga kura hawakuwa watu wa kabila lake. Jambo hili si rahisi kwa zama hizi.

Katika masuala ya Afrika na ulimwengu kwa ujumla, Tom Mboya alikuwa Tai aliyedhibiti anga hizo kisiasa kwa ufanisi mkubwa uliodumu na kukumbukwa hadi leo. Lakini: Afanaaleyki! Ghafla nyota hii, kama kimondo ilizimika kabla ya wakati. Emmanuel Mbogo ameiandikia jamii ya Waswahili kazi hii ili wabaini yaliyomsibu gwiji huyu katika uga wa siasa. Dhamira ya ukombozi wa Kisiasa Afrika imetamakani sehemu pana katika tamthiliya hii.

### 1. 4. 2 Muhtasari wa Tamthiliya ya Wangari Maathai

*Wangari Maathai* ni tamthiliya iliyoandikwa na Emmanuel Mbogo (2015). Tamthiliya hii inaakisi habari za mwanaharakati mmoja nchini Kenya, almaarufu

kama Wangari Maathai. Mwanamke huyo alikuwa kiongozi wa chama cha kuhifadhi mazingira (Green Belt Movement). Mwaka 2004 historia inatanabaisha kwamba alitunukiwa tuzo ya "Nobel Peace Award" kutokana na mchango wake mkubwa katika kupigania amani, demokrasia, utawala bora na matumizi sahihi ya mazingira na rasilimali zama hizi za sayansi na teknolojia. Tamthiliya hii imejengwa katika maonesho nane tu.

Emmanuel Mbogo katika tamthiliya hii anaonyesha migogoro ya kisiasa, kiuchumi na kijamii aliyopambana nayo mwanaharakati huyu. Wengi waliokutana na tamthiliya hii wamebaini mambo mbalimbali yaliyomsibu mwanaharakati huyu maarufu kutoka nchini Kenya zama za uhai na mapambano yake. Kupitia mwanamama huyu Emmanuel Mbogo anabainisha nafasi wa wanawake katika kukomboa jamii dhidi ya masaibu mbalimbali yanaisibu kijamii, kisiasa na kiuchumi. Kenya ilifaidika mambo mengi kupitia kwa mwanamke huyu ingawa alipambana na vikwazo kutoka kwa raia wenzake, humo ndani ya mipaka ya Kenya.

### 1. 4. 3 Muhtasari wa Tamthiliya ya Tanzia ya Patrice Lumumba

Tamthiliya hii inayosisimua, imeandikwa na mwandishi nguli katika fasihi ya Kiswahili Emmanuel Mbogo (2015). Tanzia ya Patrice Lumumba ni tamthiliya ya kihistoria, inadokeza masuala muhimu ya kihistoria, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni ndani ya bara letu Afrika. Mhusika mkuu ni Patrice Lumumba. Mhusika huyu, Patrice Lumumba alikuwa Waziri Mkuu wa kwanza, Nchi ya Demokrasia ya Kongo (DRC). Ndugu huyu alishiriki kwa nguvu kubwa katika harakati za Kongo kujikomboa kutoka pingu za ukoloni, kwa Wabelgiji.

Kongo ilipata uhuru 30/6/1960. Baada ya miezi sita tu tangu wapate uhuru, yaani tarehe 17/1/1961, Lumumba akauliwa kikatili na kinyama. Leo hii nchini Kongo hakuna kaburi la mwanasiasa huyu kwani chini ya usimamizi wa Joseph Mobutu na Moise Tshombe (Vibaraka wa Marekani, Ubelgiji, Ufaransa na Uingereza) mwili huo ulikatwakatwa vipande vipande na kutumbukizwa ndani ya pipa la tindikali na hivyo ukamalizwa kabisa.

Kilichomponza Lumumba hadi akauawa ilikuwa fikra zake za kutaka utajiri wa Kongo uwanufaishe Wakongo wenyewe, badala ya kuwaachia mabeberu waendelee kunyonya rasilimali za Kongo kwa faida ya nchi zao.

Emmanuel Mbogo ameandika tamthiliya hii kutunza historia ya kiongozi huyu muhimu katika bara la Afrika. Ni miaka 60 sasa imepita tangu Lumumba atoweke duniani, lakini Kongo na Afrika bado zinapambana na mawazo hayo aliyoanzisha Kiongozi huyo wa kwanza nchini Kongo. Nchi nyingi Afrika watu wake wanaishi maisha ya kimaskini, wakati ndani ya mipaka yao kumejaa rasilimali tele.

Tamthiliya hii inalenga zaidi kumkomboa mwananchi wa Kiafrika dhidi ya minyororo ya uchumi tegemezi kutoka nchi za kigeni, na kuikatilia mbali. Mbogo anakiri safari ni ndefu kufikia ukombozi huu kikamilifu, vita ni kali lakini Afrika itashinda! Afrika inakumbushwa kufanyia kazi mawazo ya ukombozi wa kikweli yaliyoasisiwa na wanaharakati wengi wa Kiafrika, waliokomboa nchi zao kutoka pingu za kikoloni, akiwamo Patrice Lumumba.

### 1. 4. 4 Muhtasari wa Tamthiliya ya Mondlane na Samora

*Mondlane na Samora* ni tamthiliya ya kihistoria inayosimulia kuhusu harakati za

ukombozi wa Msumbiji kwa mtutu wa bunduki. Tamthiliya hii imeandikwa na Emmanuel Mbogo (2016). Edwardo Mondlane, kiongozi wa FRELIMO ndiye aliyeongoza mapigano dhidi ya ukoloni wa Mreno kwa ujasiri mkubwa; lakini akiwa Dar es Salaam, tarehe 3/2/1969, Mondlane alipokea paseli kutoka Lisbon, Ureno akaifungua na bomu likalipuka na kumuua.

Baada ya Mondlane kuuawa aliinuka kiongozi mwingine wa FRELIMO, Samora Machel akaendeleza mapambano dhidi ya wakoloni hadi Msumbiji ikapata uhuru tarehe 25/6/1975. Samora Machel aliitawala Msumbiji kwa miaka 12. Mwaka 1986 kiongozi huyo alikufa kwa ajali ya ndege iliyotunguliwa na makombora ya makaburu wa Afrika ya Kusini.

Emmanuel Mbogo ndani ya tamthiliya hii anaonesha jinsi Nyerere na Watanzania walivyoshiriki kwa hali na mali ili kuung’oa ukoloni barani Afrika. Askari wengi wa Tanzania waliang’amia kwa kushiriki katika mapigano mbalimbali ya ukombozi wa nchi za Kiafrika mathalani Msumbiji, Angola, Zimbabwe, Namibia na Kongo. Sambamba na hayo humu ndani zimewasilishwa dhamira mbalimbali mathalani ukombozi wa kisiasa, ubepari na ujamaa, historia ya ukoloni Afrika, usaliti, umuhimu wa elimu sambamba na umoja wa bara la Afrika.

### 1. 4. 5 Muhtasari wa Tamthiliya ya Malkia Bibi Titi Mohamed

Tamthiliya ya *Malkia Bibi Titi Mohamed* (2016) imeandikwa na mtunzi mahiri katika fasihi ya Kiswahili, Emmanuel Mbogo. Tamthiliya hii inaakisi maisha ya mwanaharakati wa uhuru, Tanganyika na Afrika Mashariki miaka ya 1960. Bibi Titi alikuwa mtunzi na muimbaji wa nyimbo mahiri. Emmanuel Mbogo kupitia kazi hii anatujulisha kwamba Bibi Titi alikuwa mwanasiasa hodari na jasiri.

Bibi Titi alikuwa mwanaharakati aliyejitoa kupigania uhuru wa Tanganyika na Afrika kwa akili zake zote. Kwa maneno yake mwenyewe anasema, "Ni mimi niliyewashawishi wanawake wa Guinea kushiriki mapinduzi ya Ukombozi chini ya Dialo, Katibu Mkuu wa AAPC, alikuja hapa 1960..." Tamthiliya hii imejengwa katika maonesho makuu saba tu. Maonesho hayo yametambulishwa kwa kutumia mandhari linapofanyika tendo husika. Mf. Jela Isanga, Nyumbani kwa Bibi Titi n.k.

Kwa jumla, tamthiliya hii inaakisi harakati mbalimbali alizofanya Bibi Titi Mohamed katika kupigania uhuru wa Tanganyika. Emmanuel Mbogo anataka kuonyesha nafasi ya wanawake katika kupigania uhuru wa Tanganyika. Dhamira ya ukombozi wa kisiasa na historia ya ukoloni ndizo zimetamakani zaidi. Pamoja nazo mwandishi anafundisha kwamba ili kufikia mafanikio ya kweli kirahisi katika jambo lolote jamii linalopambana nalo, ni vema wanaume na wanawake kushirikiana kisawasawa. Upande mmoja usiachwe nyuma kwenye jitihada za maendeleo katika nyuga zote muhimu katika maisha; uchumi, siasa na utamaduni.

### 1. 4. 6 Muhtasari wa Tamthiliya ya Mtumwa hadi Siti Binti Saad

*Mtumwa hadi Siti Binti Saad* ni tamthiliya ya Kiswahili iliyoandikwa na Emmanuel Mbogo (2016). Hii ni tamthiliya ya kihistoria. Inaeleza maisha ya Binti Saad kama yalivyosawiriwa na Shaaban Robert na Nasra Mohamed Hilal. Katika tamthiliya hii Emmanuel Mbogo amelenga kufundisha jamii kwamba, ushindi maishani unawezekana hata kama umetoka familia ya watu maskini kiasi gani. Siti binti Saad alitoka katika familia duni, utumwani lakini kwa jitihada zake katika jamii, kupitia muziki wa Taarab, aliweza kufanikiwa sana hata akaketi na watawala, watu wenye uwezo.

Hii ni tamthiliya ya kihistoria. Watu wengi watang'amua mengi kuhusu Siti binti Saad kupitia kazi hii. Kupitia nyimbo zake mwanaharakati huyu alijikita katika dhamira za kisiasa, matabaka, mapenzi pamoja na tamaduni. Dhamira hizo zote zimesawiriwa na Emmanuel Mbogo, mtunzi wa tamthiliya hii katika bunilizi hii kupitia wahusika mbalimbali. Kifani tamthiliya hii imeumbwa katika maonesho 13. Maonesho yote yamemakinikia dhamira kuu ya ukombozi wa kisiasa, kwa kuonyesha harakati mbalimbali zilizofanyika nchini Tanganyika wakati wa kupambania uhuru wa nchi hiyo.

### 1. 4. 7 Muhtasari wa Jumla kuhusu Tamthiliya Teule

Kimsingi, tamthiliya teule zote tulizotumia katika utafiti ziko katika mkondo wa kihistoria. Mtunzi ameandika kuhusu wanaharakati mbalimbali walioshiriki katika ukombozi wa mataifa ya Afrika dhidi ya dhuluma mbalimbali katika mataifa yao kabla ya uhuru. Vilevile punde mara baada ya ukombozi kutoka nchi za kigeni, na viongozi waliorithi utawala kutoka nchi za kikoloni. Pamoja na hayo tamthiliya teule zimeandikwa ndani ya muongo mmoja. Tunawaza kwa sauti kwamba limepelekea fani kati yake kuhusiana. Kwamba fani ya Biblia inasikika ndani ya kazi za mwandishi teule alizoandika ndani ya kipindi hicho.

## 1. 5 Tamko la Tatizo la Utafiti

Biblia imeshaelezwa kuwa ndani ya kazi za fasihi andishi ya Kiswahili. Mwanazuoni wa fasihi Marisya (2017) alitafiti mchango wa sajili ya dini katika kufanikisha riwaya mbili alizoandika Ken Walibora; *Kidagaa Kimemwozea* (2012) na *Ndoto ya Almas* (2006). Matokeo ya utafiti huo yalidhihirisha kwamba Biblia ilishahusishwa katika fasihi ya Kiswahili. Pamoja naye, Mayo (2020) alitafiti matumizi ya maneno

ya Biblia katika riwaya ya *Rosa Mistika* (1971) na *Gamba la Nyoka* (1979) zilizotungwa na Kezilahabi. Kwa jumla matokeo ya utafiti huo yalifanya tubaini kuwa Biblia katika fasihi andishi ya Kiswahili ilishatafitiwa. Tafiti hizo tangulizi zimebainisha vipengele vya fani ya Biblia lakini hazielezi sababu ya kutokea au kutumiwa kwa vipengele hivyo katika kazi za fasihi andishi ya Kiswahili. Pia hazielezi mchango wa fani za Biblia zilivyotumika kudhihirisha dhamira katika fasihi ya Kiswahili. Mtafiti alipata sababu ya kufanya utafiti katika hili kwani kuna malengo hayakushughulikiwa kama ilivyobainishwa.

## 1. 6 Malengo ya Utafiti

Utafiti ulikuwa na lengo kuu moja na malengo mahsusi matatu. Malengo hayo yamebainishwa katika sehemu inayofuata.

### 1. 6. 1 Lengo Kuu

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa moja, kuchunguza fani ya Biblia katika fasihi andishi ya Kiswahili: Mifano kutoka katika tamthiliya teule za Emmanuel Mbogo.

### 1. 6. 2 Malengo Mahsusi

Ili kulifikia lengo kuu, utafiti ulikuwa na malengo mahsusi matatu. Malengo hayo yalikuwa yafuatayo;

Kubainisha fani za Biblia katika tamthiliya teule za Emmanuel Mbogo.

Kuchunguza sababu za kujitokeza kwa fani za Biblia katika tamthiliya teule za Emmanuel Mbogo.

Kubainisha dhamira zinazowasilishwa na fani za Biblia katika tamthiliya teule za Emmanuel Mbogo.

## 1. 7 Maswali ya Utafiti

Malengo ya utafiti huu yalitufanya tujiulize maswali makuu matatu yafuatayo;

Ni fani zipi za Biblia zinazojitokeza katika tamthiliya teule za Emmanuel Mbogo?

Kwa nini fani za Biblia zilizobainishwa katika (i) hapo juu zinajitokeza katika tamthiliya teule za Emmanuel Mbogo?

Ni dhamira zipi zinazowasilishwa kutokana na fani za Biblia katika tamthiliya teule za Emmanuel Mbogo?

## 1. 8 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu utatumika na watafiti kubaini jinsi fani za Biblia zilivyojitokeza katika fasihi andishi ya Kiswahili. Pamoja na hayo kupitia utafiti huu fasihi ya Kiswahili imenufaika pahala pote itakaposomwa nchini Tanzania, Afrika na Ulimwenguni wote kwa ujumla watafiti wanapochunguza uhusiano wa kazi za fasihi. Vilevile utafiti huu umekuwa ngazi kwa wasomaji wa kazi za fasihi kuelewa dhamira mbalimbali zilizowasilishwa katika kazi za fasihi andishi ya Kiswahili kupitia fani za Biblia. Kimsingi, utafiti umeeleza sababu za kujitokeza fani za Biblia katika fasihi andishi ambazo zinategemewa kusaidia walengwa wengi zaidi kupata ujumbe uliopo kwenye Biblia kupitia kazi  za fasihi hata kwa wasio waamini wa kitabu hicho.

## 1. 9 Mipaka ya Utafiti

Emmanuel Mbogo ameandika matini mbalimbali za kifasihi kama tamthiliya, riwaya na hadithi fupi. Utafiti huu ulichunguza tamthiliya sita pekee. Mbinu ya uteuzi kifani ilimwezesha mtafiti kuchagua tamthiliya sita kwa kuwa zilitosha kumpatia data za kuweza kujibu maswali yaliyopelekea kufanikisha lengo kuu la utafiti huu. Kazi

zilizotafitiwa ni hizi; *Tanzia ya Patrice Lumumba* (2015), *Wangari Maathai* (2015), *Nyota ya Tom Mboya* (2016), *Mondlane na Samora* (2016), *Malkia Bibi Titi Mohamed* (2016) na *Mtumwa hadi Siti Binti Saad* (2016). Mtafiti alishughulika na vipengele vya kifani vya Biblia pekee siyo vinginevyo.

**1. 10 Mpangilio wa Tasnifu**

Tasnifu hii imepangiliwa katika sura tano. Sura ya kwanza inajumuisha usuli wa utafiti, tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti na mipaka ya utafiti. Fauka ya hayo sura ya pili inajumuisha mapitio ya maandiko ama kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia. Pamoja na hayo sura ya tatu imeeleza mbinu za utafiti zilizotumika katika utafiti huu. Hali kadhalika sura hii imejumuisha eneo la utafiti, usanifu wa utafiti, sampuli na usampulishaji, data zilizokusanywa na mbinu zilizotumika kukusanya data hizo. Zaidi ya hapo sura zilizofuata baada ya hii umefanyika mjadala kuhusu matokeo ya utafiti, yaani uwasilishwaji na uchambuzi wa data. Sura ya nne imebainisha fani za Biblia katika tamthiliya teule za Emmanuel Mbogo, sababu za kujitokeza kwa fani hizo na dhamira zinazodhihirika kupitia fani za Biblia katika katika kazi teule. Hatimaye katika sura ya tano muhtasari, hitimisho pamoja na mapendekezo ya utafiti huu mtawalia.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDIKO NA KIUNZI CHA NADHARIA

## 2. 1 Utangulizi

Sura hii ilipitia kwa undani dhana mahsusi katika utafiti uliofanyika. Vilevile mtafiti amechunguza Biblia katika fasihi ya Kiswahili sambamba na tafiti tangulizi kuhusu maandiko ya Emmanuel Mbogo. Pamoja na hayo, mtafiti amebainisha pengo la maarifa la utafiti uliofanyika pamoja na kiunzi cha nadharia. Sehemu ya mwisho ni Muhtasari la sura ya pili ya tasnifu ya utafiti huu.

## 2. 2 Utalii wa Dhana Mahsusi katika Utafiti huu

Utafiti huu ulihusisha dhana mahsusi zilizotamakani kwa sehemu kubwa. Mtafiti alichunguza dhana hizo kwa mujibu wa Wanazuoni mbalimbali katika sehemu inayofuata hapa chini. Fauka ya hayo mtafiti alifanya tathmini kwa kila fasili iliyotolewa na wanazuoni kuhusu dhana hizo.

### 2. 2. 1 Fasihi ya Kiswahili ni ipi?

Sengo (1993) anafafanua dhana ya fasihi ya Kiswahili kama taaluma ya maneno ya Kiswahili ya Waswahili, ya Wapwani. Mwanazuoni huyu anaeleza katika makala hiyo ni kwamba, fasihi ya Kiswahili kama utanzu wa kisanaa lazima iwasilishwe kwa lugha ya Kiswahili pia ihusu jamii ya Waswahili. Hali kadhalika anatambulisha Waswahili kama wenyeji wa Upwa wa Afrika Mashariki.

Vilevile Sengo (1993) anaendelea kueleza kwamba kwa kuwa wenyeji wa Upwa wa Afrika Mashariki lugha yao asili karne na karne ni Kiswahili basi ni vema fasihi yao ikatambulishwa kama fasihi ya Kiswahili. Mtaalam huyu anasisitiza kwamba aina ya

lugha inayotumika na jamii inayohusika ndiyo inapaswa kutumika kama nguzo msingi katika kutambulisha fasihi ya jamii fulani mahsusi, kama ilivyo kwa fasihi ya Kiswahili na wakazi wake. Fasili hii ina mashiko kwani inataja mambo msingi ya kuitambulisha fasihi; lugha na jamii lengwa.

Hali kadhalika fasihi ya Kiswahili inaelezwa kama fasihi inayotolewa kwa lugha ya Kiswahili (Mulokozi, 2017). Mwanazuoni huyo anaendelea kueleza kwamba fasihi inayotolewa kwa lugha ya Kiswahili imetamakani eneo pana la Afrika Mashariki (Pwani na Bara). Wenyeji wa eneo hilo huimba, kusimulia na kuandika fasihi yao kwa lugha ya Kiswahili. Fauka ya hayo mwanazuoni huyu katika fasihi anaeleza kwamba lugha zinazotumika na jamii lengwa ndiyo zinapaswa kuzingatiwa katika kutoa fasili stahiki ya fasihi mahsusi. Ndipo sasa anahitimisha kuwa, fasihi ya Kiswahili inawahusu wakazi wa Afrika Mashariki na lugha yao ya Kiswahili wanayoitumia kueleza maisha yao.

Kimsingi, fasihi ya Kiswahili ni aina ya fasihi ambayo husemwa au kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Mtunzi anaweza kuwa mwenyeji au mtu mwenye asili ya eneo la Afrika Mashariki na Kati lenye kuzungumza lugha ya Kiswahili. Fasihi hiyo hutumia lugha ya Kiswahili. Vilevile fasihi ya Kiswahili huakisi mila na desturi za jamii aliyotokea mwandishi. Hivyo basi, mambo yote yanayosemwa katika kazi ya fasihi huwa ni zao la jamii husika. Fanani au mtunzi husema yanayojiri katika jamii yake.

Fasihi ya Kiswahili inawasilishwa kwa namna mbili; mazungumzo na maandishi (Mulokozi, 1996). Unapotumika mtindo wa lugha ya mazungumzo basi unapatikana utanzu wa fasihi simulizi na inapotumika lugha ya maandishi unapatikana utanzu wa

fasihi andishi. Katika utafiti huu tuliofanya, tulichunguza kazi za fasihi andishi ya Kiswahili, tukiegemea utanzu wa tamthiliya. Hivyo Mulokozi (Ktj) alituwezesha kung'amua kwamba fasihi andishi ya Kiswahili huwasilishwa kwa kutumia lugha ya maandishi. Tamthiliya teule katika utafiti tuliofanya zimeandikwa kwa lugha ya maandishi ili kuifikia hadhira lengwa, Waswahili kutoka Afrika Mashariki na Kati (Bara na Visiwani).

**2. 2. 2 Fasihi Andishi ya Kiswahili**

Dhana ya fasihi kwa jumla inafasiliwa kama tawi la sanaa linalotumia lugha ya mazungumzo au maandishi kufikisha ujumbe kwa jamii husika. Mtoaji au mzalishaji wa kazi ya fasihi huitwa fanani na mpokeaji huitwa hadhira. Nguzo msingi inayotumika kuainisha fasihi ni mtindo wa lugha inayotumika (Mulokozi, 2017). Mwanazuoni huyu anaendelea kushadidia kwamba, ikitumika lugha ya mazungumzo basi inapatikana fasihi simulizi na inapotumika lugha ya maandishi basi inapatikana fasihi andishi.

Syambo na Mazrui (1992) wanasema kuwa fasihi andishi ya Kiswahili ni ile iliyoandikwa kwa Kiswahili tu, bila kujali inazungumzia utamaduni wa Kiswahili au mwingine. Suala msingi ni fasihi hiyo kutumia lugha ya Kiswahili na kufuata mbinu za ufasaha wa lugha hiyo. Wataalam hawa katika fasili wanayoitoa wameilenga zaidi fasihi ya kuandikwa (fasihi andishi). Fasihi simulizi haijumuishwi katika fasili yao. Kusema kwamba, fasihi ya Kiswahili ni ile ya kuandika tu, kunaibua ukakasi kwani ipo fasihi ya Kiswahili inayotolewa kwa njia ya mdomo yaani fasihi simulizi.
Vilevile Syambo & Mazrui (1992) wanaendelea kukazia kwamba swala msingi la kuitambulisha fasihi ni lugha inayotumika. Hivyo ikitumika lugha ya Kiswahili

kufikisha ujumbe kwa hadhira basi tunapata fasihi ya Kiswahili. Hoja hii ni sahihi kwani lugha ndiyo huitambulisha fasihi ya jamii husika. Mambo yanayozungumzwa ndani ya fasihi hiyo kama vile utamaduni si sifa msingi za kuitambulisha aina hii ya fasihi.

Hivyo basi, fasihi andishi ya Kiswahili katika utafiti huu ilichukuliwa kama aina ya fasihi inayowasilishwa kwa lugha ya Kiswahili kutoka Afrika Mashariki (Bara na Pwani). Tanzu kuu za fasihi andishi ni riwaya, tamthiliya na ushairi. Utafiti huu ulishughulika na utanzu wa tamthiliya. Sehemu inayofuata hapa chini mtafiti anadadavua dhana ya tamthiliya jinsi ilivyoelezwa katika uga wa fasihi andishi ya Kiswahili ili kuondoa kiza kwa wasomaji kila watapokutana na dhana hiyo katika utafiti huu.

**2. 2. 3 Dhana ya Tamthiliya**

Tamthiliya ni miongoni mwa tanzu kuu tatu za fasihi andishi. Utanzu huu umefasiliwa kwa namna mbalimbali na wanazuoni katika uga wa fasihi ya Kiswahili. Hapa chini mtafiti amebainisha fasili zilizotolewa kuhusu dhana ya tamthiliya na sifa msingi zinazoutambulisha utanzu huu wa fasihi andishi ya Kiswahili.

Mlama (1983) anafasili tamthiliya au drama kama aina mojawapo ya sanaa za maonyesho ambayo usanii wa utendaji wake hutegemea zaidi vitendo na uongeaji, tofauti na aina nyingine kama vile ngoma ambazo hutegemea zaidi uchezaji ngoma na upigaji muziki. Vilevile Gichamba (2005) anafasili tamthiliya kama utungo ambao unaweza kuandikwa au la. Utungo huo huliweka wazo linalohusika katika tukio la kuliwezesha kutendeka mbele ya hadhira.

Mawazo ya wanazuoni hao wawili pamoja yalisaidia kuzipambanua tamthiliya teule katika utafiti uliofanyika. Tamthiliya za Emmanuel Mbogo zimewekwa kwenye lugha ya maandishi. Hali kadhalika kazi hizo zinaweza kusanwa jukwaani katika vitendo na uongeaji.

Pamoja nao Wamitila (2010) anafafanua tamthiliya kama dhana inayorejelea kazi ya kifasihi iliyoandikwa kwa ajili ya kuwasilishwa jukwaani, kwa njia ya maneno na ishara. Fasili aliyotoa mtaalam huyu inashadidia kwamba, tamthiliya ni kazi ya fasihi andishi inayokusudiwa kuwasilishwa jukwaani. Msanii huiweka kazi yake katika maandishi kisha wasanii huichukua kuiwasilisha jukwaani kwa vitendo. Mtindo wa kifani anaoeleza mwanazuoni huyo ndiyo ulitumika kuumba tamthiliya teule za utafiti huu. Wasanii wanaweza kuchukua tamthiliya hizi na kuzicheza jukwaani mbele ya hadhira.

Fasili aliyotoa mwanazuoni Wamitila (ktj) kuhusu dhana ya tamthiliya imepungua upande wa maudhui. Mtaalam amejikita zaidi kwenye upande wa fani. Hakueleza huo utanzu unapowasilishwa mbele ya hadhira jukwaani huzungumza nini? Kwa hivyo wasomaji wake wanashindwa kung'amua yanayozungumzwa katika mchezo huu ulioandikwa kwa lengo la kuonyeshwa jukwaani.

Fauka ya hayo, Mulokozi (2017) anaeleza tamthiliya au drama kama igizo la kifasihi lililokusudiwa kutendwa jukwaani kwa ajili ya hadhira fulani. Ndipo sasa lugha ya kawaida tamthiliya huitwa mchezo wa kuigiza. Mulokozi anaendelea kuandika kuwa, kwa kawaida tamthiliya huwa na masimulizi ambayo huigizwa na wahusika wa pande mbili au zaidi zinazosigana. Mgongano huo hujenga mgogoro ambao

usiposuluhishwa au kutatuliwa mchezo huwa umemalizika. Fasili hii iliyotolewa ilimsaidia mtafiti alipoziendea tamthiliya teule. Hapana shaka tamthiliya hizo zote zimejengwa katika pande mbili au zaidi zinazosigana, ambazo zimesaidia kuzaliwa kwa bunilizi hizi. Kupitia misigano hiyo mtafiti aliweza kubaini fani mbalimbali kutoka kwenye Biblia ndani ya tamthiliya teule.

Tamthiliya ya Kiswahili inaelezwa kuwa na sifa msingi zifuatazo; dhana inayotendeka, utendaji, uwanja wa kutendea, watazamaji, kusudio la kisanaa, muktadha wa kisanaa na ubunifu (Wamitila, 2010). Sifa hizi alizozibainisha mtafiti huyu zinatosheleza hakika katika kuuelezea utanzu huu wa fasihi andishi ya Kiswahili.

Kimsingi, tamthiliya inaweza kufasiliwa kama utanzu wa fasihi andishi ambao huwasilishwa kupitia mazungumzo na uigizaji ili kufikisha ujumbe wake kwa hadhira. Utanzu huu huliweka wazo katika matendo na mazungumzo. Kwa kuzingatia kigezo cha dhamira kuna tamthiliya za aina mbalimbali. Kwa mfano; tamthiliya cheshi/komedia hii ni aina ya tamthiliya ambayo maudhui yake hujengwa kwa lengo la kumfurahisha hadhira. Vilevile tamthiliya simanzi/tragedia ni aina ya drama iliyojaa huzuni, mikasa, mikosi na visa vya kutisha. Aghalabu wahusika wake wakuu hupoteza maisha. Tamthiliya tatizo, domestiki drama, melodrama na tamthiliya tanzia zinabainishwa pia kama aina za tamthiliya katika kigezo hiki cha dhamira. Uanishaji huu wa tamthiliya ulimsaidia mtafiti katika utafiti huu kwani aling’amua mkondo zilizomo tamthiliya teule na hivyo kuzielewa vizuri alipokuwa akizisoma.

### 2. 2. 4 Biblia katika Fasihi

Biblia inafasiliwa kama kitabu cha kifasihi (Metzger na Coogan 1993). Wanazuoni wengine wanaokiri umuhimu wa Biblia katika fasihi ni Milton (1667), Woodworth (1768) na Scott (1976). Tafiti zilizofanyika awali na wanazuoni tuliorejea hapo juu zinaeleza kuwa mitindo ya Kibiblia yaani nathari na ushairi imejitokeza zaidi katika bunilizi za wanafasihi mbalimbali ulimwenguni. Kwa kuwa awali Biblia ilichukuliwa kama kipimo cha ustaarabu basi wanafasihi wengi pamoja na hadhira walivutiwa zaidi na ufasihi uliojitokeza katika kitabu hicho. Jambo hili lilipelekea wanafasihi wengi kuiga kaida za fani na maudhui zilizomo ndani ya kitabu hicho. Nchi za Magharibi na Marekani zimeathiriwa sana na kitabu hiki katika kazi zake za fasihi (Poveteva, 2012).

Osore (2015) anaeleza kwamba hapa Afrika pia Biblia imejitokeza katika kazi za watunzi mbalimbali. Wole Soyinka ni miongoni mwa watunzi waliotajwa kutumia fani za Biblia katika kazi yake ya *A Grain of Wheat* (1967). Vilevile Ngugi wa Thiong'o na riwaya yake ya *The Devil on the Cross* (1980). Katika uga huu wa fasihi imebainika kwamba Biblia imeathiri watunzi kifani na kimaudhui. Kwa upande wa maudhui, historia ya Afrika ndiyo inajitokeza zaidi katika fasihi. Katika fani mitindo ya nathari na ushairi ndiyo imetamakani zaidi.

Fauka ya hayo nchini Tanzania mahusiano ya Biblia na fasihi andishi ya Kiswahili yalikwishatafitiwa. Wanafasihi mbalimbali, hasa wa mwanzo kama Euphrase Kezilahabi na William Mkufya kupitia bunilizi zao walitumika kuzungumzia Ubiblia unavyotokeza katika fasihi ya Kiswahili hapo kwanza. Riwaya ya *Rosa Mistika* (Kezilahabi, 1971) na *Ziraili na Zirani* (Mkufya, 1999) zimehusishwa mjadala huu

ulipofanyika. Hali kadhalika tamthiliya za *Nyerere na Safari ya Kanaani* (Mbogo, 2015) na *Sadaka ya John Okello* (Mbogo, 2015).

Kimsingi, upo uhusiano kati ya fasihi na Biblia. Tafiti mbalimbali kuhusu mahusiano haya hapa ulimwenguni zimefanyika na kubainisha hilo (Rej. Usuli). Nchi za Ulaya, Asia, Amerika, Afrika na Tanzania zilitumika kuonyesha mtagusano uliopo kati ya fasihi na Biblia. Biblia na fasihi zinahusiana katika vipengele vya fani na maudhui. Utafiti huu ulishughulikia fani za Biblia katika tamthiliya teule za Emmanuel Mbogo.

**2. 3 Tafiti Tangulizi Kuhusu Maandiko ya Emmanuel Mbogo**

Mwanafasihi Emmanuel Mbogo, katika fasihi ya Kiswahili kazi zake zimetafitiwa na wanazuoni mbalimbali. Mtunzi huyo ameandika zaidi katika tanzu kuu mbili; tamthiliya na riwaya. Watafiti wametazama mada mbalimbali, kila mmoja sawa na uhitaji wake. Mtafiti katika sehemu hii amebainisha tafiti mbalimbali zilizofanywa na wanazuoni kuhusu maandiko yake hapo awali. Mtafiti alifanya hivi ili kubaini pahala pa kusimama akitafiti maandiko ya mtunzi huyo katika fasihi ya Kiswahili.

Mningo (2015) alitathimini mwingilianomatini katika utunzi wa Emmanuel Mbogo, akilinganisha tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liyongo*. Lengo kuu la mtafiti huyo lilikuwa kubaini namna mtunzi Emmanuel Mbogo anavyofumbata mbinu ya mwingilianomatini katika kazi zake za fasihi na jinsi mbinu hiyo inavyotumika kuibua dhamira ndani ya kazi teule.

Mningo katika utafiti huo alibaini kwamba, Emmanuel Mbogo anafumbata mbinu ya mwingilianomatini ndani ya kazi zake, pamoja na kwamba kazi hizo zinapishana

takribani miaka 21 tangu kutungwa kwake. Kupitia andiko lake tuling'amua kwamba mtindo wa mwingilianomatini umetumiwa tangu kale na mtunzi teule katika utafiti huu. Upya ulioletwa na utafiti huu ni kubainisha fani za Biblia zilivyotumika sasa katika tungo za mtunzi huyu.

Vilevile Shemweta (2015) alichunguza itikadi katika tamthiliya za Emmanuel Mbogo: Utafiti Linganishi wa Tamthiliya za *Ngoma ya Ngw'anamalundi* na *Fumo Liyongo*. Nadharia ya simiotiki ndiyo iliyomuongoza mtafiti huyo katika kufikia malengo ya utafiti wake. Mtafiti alibaini kwamba katika tamthiliya teule za Emmanuel Mbogo kuna itikadi mbalimbali zilizotumika ndani yake. Mathalani itikadi za kiuchumi, kisiasa na kitamaduni. Vipengele vya kifani vilitumika kuchambua data za utafiti, hasa matumizi ya lugha. Fani za Biblia hazikuguswa katika utafiti huo. Mtafiti huyo alitusaidia kupata pengo la utafiti huu. Ndipo sasa tukawaza kutafiti mada mpya, ambayo watafiti tangulizi hawakuigusa.

Mtafiti mwingine aliyechunguza maandiko ya Emmanuel Mbogo ni Bwelele (2016). Yeye alichunguza mtindo katika tamthiliya teule za Emmanuel Mbogo; *Sadaka ya John Okello na Nyerere* na *Safari ya Kanaani*. Bwelele alilinganisha mitindo mbalimbali iliyotumika katika tamthiliya teule zilizoandikwa na Emmanuel Mbogo. Fauka ya hayo kipengele cha kifani ndicho kilimshughulisha zaidi mtafiti huyo.

Kwa jumla vipengele vingine vya kifani kama vile wahusika, matumizi ya lugha na hadithi za kibiblia havikuguswa katika utafiti huo, kutokana na malengo ya mtafiti. Utafiti huo ulitusaidia kupata pengo la utafiti huu hata tukakusudia kuongeza maarifa kwenye uga wa fasihi kupitia tamthiliya teule za Emmanuel Mbogo. Utafiti huu

ulisonga mbele zaidi kwa kutafiti fani za Biblia zilizojitokeza katika tamthiliya za mwandishi teule ambazo hazikushughulikiwa hapo awali na mwanazuoni tangulizi.

Vilevile Khamis (2017) alichunguza matumizi ya lugha na dhamira katika tamthiliya teule za Emmanuel Mbogo; *Sadaka ya John Okello* na *Fumo Liyongo*. Utafiti huo uliongozwa na malengo mahsusi mawili. Mosi, kuchunguza matumizi ya lugha katika tamthiliya teule za Emmanuel Mbogo. Pili, kubainisha namna matumizi ya lugha yalivyotumika kubaini dhamira mbalimbali katika tamthiliya hizo teule. Matokeo ya utafiti huo yalidhihirisha namna utumizi wa lugha ulivyoibua dhamira mbalimbali katika kazi hizo teule.

Mtafiti huyu alitusaidia katika kupata pahala pa kusimama kwenye utafiti tuliokusudia kuufanya. Kifani alitafiti kipengele cha matumizi ya lugha pekee. Hali kadhalika alitafiti mahusiano ya fani na maudhui katika kazi za fasihi akirejea maandiko ya Emmanuel Mbogo. Fani ya Biblia kutumia kipengele zaidi ya kimoja, haikuguswa katika utafiti wake. Utafiti tuliofanya umechunguza matumizi ya lugha sambamba na vipengele vingine kama vile majina ya wahusika, mtindo wa usimulizi, majina ya vitabu sambamba na nukuu za kibiblia ndani ya kazi teule.

Msangi (2018) katika shahada yake ya uzamili alifanya pia utafiti katika tamthiliya za Emmanuel Mbogo. Mwanazuoni huyu alichunguza ubiblia katika tamthiliya za Emmanuel Mbogo. Katika utafiti huo alirejea tamthiliya mbili; *Nyerere na Safari ya Kanaani (2016)* na *Sadaka ya John Okello (2015).* Matokeo ya utafiti huo yalibainisha kuwepo ubiblia mwingi katika tamthiliya hizo teule za Emmanuel Mbogo. Vipengele vya kifani ndivyo vilitumika zaidi kuakisi Ubiblia. Mchango wa

vipengele hivyo vya kifani kutoka kwenye Biblia katika kubaini dhamira haukushughulikiwa awali na Msangi, kutokana na malengo ya utafiti wake. Hivyo basi tuliona kwamba iko haja ya kufanya uzamivu kuhusu mtindo aliochagua kutumia Emmanuel Mbogo ili kufikisha ujumbe kwa hadhira lengwa.

Ismail (2019) alichunguza mtindo na dhamira katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora* (Mbogo, 2016). Katika utafiti huu mtafiti aliweka bayana kwamba Emmanuel Mbogo ametumia vipengele mbalimbali vya lugha na sajili za namna namna kama vile mawasiliano ya simu, matangazo ya redio na barua ili kuwasilisha dhamira zake kwa hadhira lengwa. Nadharia ya umitindo ndiyo ilitumika kufanya utafiti huo katika tamthiliya ya Emmanuel Mbogo. Matumizi ya lugha na sajili mbalimbali ndizo zilitumika kuchunguza na kuchambua data za utafiti.

Mtafiti katika kazi yake alichunguza vipengele cha matumizi ya lugha. Utafiti huo ulituwezesha kupata pahala pa kusimama kwa kufikiri kupanua eneo la utafiti. Tulikusudia kuongeza vipengele vingine vya kifani katika utafiti huu mfano; wahusika na mandhari katika kubainisha fani za Biblia katika tamthiliya teule za Emmanuel Mbogo.

Kwa jumla wanazuoni mbalimbali wametafiti maandiko ya Emmanuel Mbogo kama tulivyobainisha. Kila mtafiti aliongozwa na malengo ya utafiti wake. Kupitia kazi hizo mtafiti alibaini kwamba, sababu za kutumia fani za Biblia na mchango wake katika kubaini dhamira katika tamthiliya za Emmanuel Mbogo zilikuwa hazijatafitiwa. Tafiti nyingi tangulizi zilibainisha tu vipengele vya kibiblia katika kazi za fasihi andishi ya Kiswahili.

## 2. 4 Nadharia ya Mwingilianomatini

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Mwingilianomatini. Mtafiti alitumia nadharia hiyo kuchunguza na kuchambua data za utafiti. Nadharia ya Mwingilianomatini inahusishwa na wanazuoni watatu katika taaluma ya isimu. Wanazuoni hao ni Ferdinand Ferdinand de Saussure(1917), Mikhail Bakhtin (1969) na Julie Kristeva (1981). Mwanaisimu Ferdinand de Saussure katika maandiko yake anajikita zaidi katika ufafanuzi wa ishara katika lugha. Bakhtin anasogea mbele zaidi kwa kutafiti jinsi ishara katika lugha zinavyoweza kuungana ili kuleta maana. Kristeva ndiye ametamalaki zaidi kama mwasisi wake kwa kujumuisha mawazo ya wanazuoni wenzake, Ferdinand de Saussurena Bakhtin.

Njogu na Wafula (2007) wanaeleza kwamba ili hadhira ielewe kazi yoyote ya fasihi ni muhimu kuhusisha kazi hiyo na vipengele vingine nje ya muktadha wa usomaji au usimulizi. Mtindo wa kuingiza vipengele hivyo ndiyo huitwa mwingilianomatini. Pahala pengine wanazuoni hawa wanaitambulisha nadharia hii kama nadharia ya usemezano, aliyoiasisi Mikhail Bakhtin.

Hivyo basi mawazo ya wanazuoni hao yanabainisha kwamba nadharia hii inawahusu hadhira pia si watunzi peke yao. Katika utafiti huu mtafiti amezungumzia namna hadhira wanavyoweza kubaini dhamira katika tamthiliya teule zilizoandikwa na Emmanuel Mbogo kwa kuhusisha fani za Biblia. Hapo tulijibu swali hili la utafiti, ni dhamira gani zinazowasilishwa katika fani za Biblia zilizojitokeza katika matini teule? Kimsingi, hii pia ilikuwa nadharia inayokidhi katika utafiti huu tuliofanya.

Bosire (2016) anaeleza kwamba Julie Kristeva aliendeleza mawazo ya Ferdinand de Saussurenamna ishara inavyopata maana katika muundo wa matini. Pia alichukua

maoni ya Bakhtin kuhusu maana za maneno katika miktadha mbalimbali ya kijamii. Mtaalam huyu anaendelea kushadidia wazo kwamba, nadharia hii ni chipukizi la uga wa isimu, waliko akina Ferdinand de Saussure. Fauka ya hayo inaelezwa kwamba ishara fulani inaweza kuleta maana katika muundo wa matini. Hivyo basi ishara zinazobainishwa kuwa za kibiblia katika tamthiliya za Emmanuel Mbogo zitakuwa zimekusudia kufikisha maana fulani kwa hadhira. Mtafiti amebaini hayo alipokuwa akifanya utafiti wake.

Bosire (2016) anabainisha mihimili ya Nadharia ya Mwingilianomatini ifuatayo;

- Hamna matini yoyote ile ya kifasihi ambayo inaweza kuangaliwa kivyake au kujitegemea.
- Matini yoyote ile ni mabadiliko ya mpangilio wa matini nyingine tangulizi.
- Kazi za kifasihi huundwa kutokana na mifumo ya kanuni na tamaduni mbalimbali zilizowekwa na kazi tangulizi za kifasihi ambapo taswira za maisha ya kawaida na uhusiano wa kimaana huunganishwa na kubadilishwa.
- Matini moja hufafanua usomekaji wa mkusanyiko wa matini zote za kongoo moja, ambapo matini tangulizi hufyonza na kujibiwa na matini mpya.
- Kila usomaji wa matini huwa ni kijalizo cha matini tangulizi na hivyo basi huigeuza kwa kiwango. Kwa jinsi hii kauli inayonukuliwa hubadili na kuelezea upya kauli asilia kwa kuiambatanisha na muktadha mwingine wa kiisimu na kijamii.

Nadharia hii pia hujulikana kama Nadharia ya Usemezano. Kutokana na mawazo ya Bakhtin, utanzu wa fasihi kuwa na vipengele vya utanzu mwingine wa fasihi hakuondoi sifa ya utanzu huo. Mwingiliano anaosema mhakiki huyo ni huu, yaani kazi moja ya fasihi kuwa na sifa za tanzu nyingine ndani yake.

Kaida ya mwingilianomatini inaelezwa kujitokeza sana katika fasihi andishi ya Kiswahili; Riwaya, Tamthiliya na Ushairi. Watafiti wengi wameitumia nadharia hii katika tafiti zao (Kyovi, 2015; Mningo, 2015; Okemwa, 2017; Massoud, 2018) tukitaja wachache. Tafiti hizo zinadhihirisha kuwa kazi za fasihi ya Kiswahili zina uhusiano wa kimwingilianomatini. Tungo hizo huathiriana kifani pamoja kimaudhui.

Kimsingi, nadharia hii ina umuhimu mkubwa kwani imesaidia wanataaluma kubainisha mahusiano ya kazi za fasihi za kilimwengu. Vilevile uhusiano wa kazi za fasihi ndani ya jamii moja ulipotafitiwa, nadharia hii imetumika. Katika utafiti huu mtafiti amebainisha mwingilianomatini unavyojitokeza katika fasihi ya Kiswahili kwa kutafiti tamthiliya za Emmanuel Mbogo.

Kwa jumla, maoni ya wanazuoni wengi walioandika kuhusu mwingilianomatini katika kazi za fasihi walitengeneza njia hata tukafika hitimisho hili; Mwingilianomatini ni sifa inayojitokeza katika kazi mbalimbali za fasihi. Sifa hii inaweza kujitokeza kama mwangwi wa dhamira au maudhui na fani. Kazi moja ya kifasihi inaweza kuakisi kazi nyingine katika vipengele mbalimbali. Katika utafiti uliofanyika mtafiti alichunguza kama tamthiliya za Emmanuel Mbogo zinahusiana na Biblia.

Fauka ya hayo nadharia hii ilimsaidia mtafiti katika kukidhi malengo ya utafiti ikiwemo kubainisha fani za Biblia katika tamthiliya teule alizofanyia kazi. Vilevile

ilimsaidia kueleza sababu za kutokea kwa fani za Biblia katika tamthiliya za Emmanuel Mbogo. Hali kadhalika ilimsaidia mtafiti kueleza dhamira zinazodhihirika katika tamthiliya teule kupitia fani za Biblia zilizotumika katika tamthiliya teule. Kimsingi aliitumia kujadili na kuchambua data za utafiti huu.

Vilevile mawazo ya nadharia hii yalimsaidia mtafiti kubaini maana na dhamira zilizojiegemeza katika mbinu za mwingilianomatini, zilizobainika katika matini hizo. Mhimili mkuu wa Nadharia ya Mwingilianomatini ulimuongoza pia katika kutoa majumuisho ya mwingilianomatini katika utunzi wa Emmanuel Mbogo na kutoa hitimisho la usanii wake.

Kimsingi, nadharia hii ilimsaidia mtafiti kubaini fani za Biblia zilizojitokeza katika tamthiliya za Emmanuel Mbogo. Pia amebainisha sababu za kujitokeza fani za Biblia katika kazi hizo. Biblia imeandikwa karne nyingi zilizopita, kwa nini ijitokeze kwa namna nyingine katika miaka hii? Haipitwi na wakati? Pia amebainisha dhamira zinavyodhihirika kupitia vipengele au fani za Biblia zilizojitokeza katika tamthiliya teule.

## 2. 5 Pengo la Maarifa

Fani za Biblia katika fasihi ya Kiswahili, hasa fasihi andishi katika tanzu za riwaya, tamthiliya na ushairi zimetafitiwa kwa sehemu. Watafiti walibainisha fani za Biblia katika kazi walizotafiti (Osore 2015, Mkufya 2005 n.k.). Ziko tafiti tangulizi zinazozungumza itikadi za kidini katika maandiko ya fasihi ya Kiswahili. Tafiti tangulizi zimetafiti mahusiano ya Biblia na fasihi kwa jumla, zikibainisha mitindo ya kibiblia katika kazi teule. Utafiti huu ulisonga mbele zaidi kwa kubainisha fani za

kibiblia na kueleza sababu za kutumiwa kwa fani hizo katika kazi za fasihi. Vilevile mtafiti alitazama mchango wa vipengele hivyo katika kubaini dhamira ndani ya kazi teule.

## 2. 6 Muhtasari

Kwa jumla, katika sura hii mtafiti amechunguza dhana ya fasihi andishi ya Kiswahili na dhana ya tamthiliya. Ametazama pia mwingilianomatini katika fasihi ya Kiswahili kisha akamtambulisha mwandishi teule na tamthiliya zake teule. Hali kadhalika ametazama tafiti tangulizi katika maandiko ya Emmanul Mbogo, mwandishi teule. Mtafiti amebainisha pengo la maarifa kisha akaeleza mahusiano ya Biblia na fasihi ya Kiswahili. Vilevile mtafiti ameandika kiunzi cha nadharia katika utafiti uliofanyika. Katika utafiti huu mtafiti alitumia Nadharia ya Mwingilianomatini.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3. 1 Utangulizi

Sura ya tatu inahusu; eneo la utafiti, sampuli na usampulishaji, mchakato wa kukusanya data na uchambuzi wa data ulivyofanyika katika utafiti huu. Hivyo basi, istilahi ya 'Mbinu za Utafiti' katika utafiti huu ilitumika kurejea methodolojia yote iliyotumika katika kufanikisha utafiti huu. Methodolojia inaweza kuufanya utafiti kuwa wa kiufafanuzi au kitakwimu.

## 3. 2 Eneo la Utafiti

Eneo la utafiti huu lilikuwa tamthiliya ya Kiswahili. Tamthiliya teule za Emmanuel Mbogo ndizo zilitumika kutupatia data za msingi za utafiti lengwa. Taarifa nyingine kutoka katika machapisho na vyanzo mbalimbali vya maarifa zilitumika kama taarifa za ziada katika kusheheneza utafiti huu.

## 3. 3 Usanifu wa Utafiti

Utafiti huu ulitumia mbinu ya uchunguzi kifani katika kukusanya data. Mbinu ya uchunguzi kifani ni aina ya usanifu ambayo mtafiti huteua tu sehemu, jambo au kitu maalum ambacho atakifanyia utafiti kati ya vingi vilivyopo ili afanikiwe kukidhi haja ya utafiti wake (Yin, 1994). Katika utafiti huu, mtafiti alinuia kutumia tamthiliya teule za Emmanuel Mbogo ili kuchunguza fani za Biblia zinazojitokeza katika fasihi andishi ya Kiswahili. Tamthiliya hizo ni Tanzia ya Patrice Lumumba (2015), Wangari Maathai (2015), Mtumwa hadi Siti Binti Saad (2016), Nyota ya Tom Mboya (2016), Malkia Bibi Titi Mohamed (2016) na Mondlane na Samora (2016).

### 3. 4 Usampulishaji

Sampuli ni kundi dogo la watafitiwa lililochaguliwa katika kundi kubwa ili kuwakilisha kundi lote (Keys, 1980). Katika utafiti uliofanyika ilitumika sampuli lengwa pekee.

**Sampuli lengwa** ni aina ya sampuli ambayo mtafiti huiteua akiwa na hakika kwamba ndiyo rasilimali kuu itakayompatia data zitakazomwezesha kukamilisha malengo ya utafiti wake. Katika utafiti huu sampuli lengwa ilirejea Biblia na maandiko ya Emmanuel Mbogo, zaidi tamthiliya. Tamthiliya hizo ni Tanzia ya Patrice Lumumba (2015), Wangari Maathai (2015), Mtumwa hadi Siti Binti Saad (2016), Nyota ya Tom Mboya (2016), Malkia Bibi Titi Mohamed (2016) na Mondlane na Samora (2016). Mahali popote mtafiti alipokutana na data inayoakisi fani ya Biblia katika tamthiliya teule aliinukuu katika shajara maalum hatimaye akaitumia katika uchambuzi wa data.

### 3. 5 Vyanzo vya Data

Utafiti huu ulikusanya data za msingi. Data za msingi ni zile zinazokusanywa kwa mara ya kwanza na mtafiti na hazijawahi kukusanywa pahala pengine na mtafiti mwingine kwa minajili ya utafiti kama huo (Msami, 2019). Data za msingi katika utafiti huu zilikusanywa katika tamthiliya teule za Emmanuel Mbogo na Biblia, kitabu kinachotumiwa na dini ya Kikristo katika mafundisho yao.

### 3. 6 Ukusanyaji wa Data

Mtafiti alitumia mbinu ya usomaji matini katika kukusanya data za utafiti huu. Mbinu ya usomaji matini inarejea ukusanyaji wa data za msingi na data za upili

katika matini mbalimbali za kitaaluma, yaani machapisho mbalimbali, kutegemeana na uga anaoshughulikia mtafiti (Zelda, 2018). Mtafiti aliitumia mbinu hii katika kukusanya data za msingi katika matini teule, Biblia na tamthiliya za Emmanuel Mbogo. Katika mbinu hii mtafiti alisoma, kuchunguza na kuchambua tamthiliya teule ili kubaini fani za Biblia zilizojitokeza. Hali kadhalika mtafiti alisoma na kuchambua Biblia ili kubaini fani zilizojitokeza katika tamthiliya teule. Hatua tulizoorodhesha hapa chini ndizo zilituongoza kukusanya data kwa kuongozwa na mbinu hii;

- Kusoma vitabu teule vyote.
- Kusoma vitabu teule kwa kudondoa vipande vya fani ya Biblia ndani yake.

Kwa jumla, hatua hizo ndizo zilizingatiwa wakati wa ukusanyaji wa data tukitumia mbinu ya usomaji matini.

**3. 7 Usahihi wa Mbinu za Utafiti**

Utafiti wa kisayansi usahihi wake huanza kutazamwa katika mbinu ya utafiti. Katika maandiko ya fasihi, utafiti wa kifafanuzi ndiyo huonekana muafaka zaidi. Utafiti huu umekuwa wa kifafanuzi. Mkabala uliotumika kuwasilisha data ni muafaka kutokana na aina ya utafiti tuliofanya. Mkabala wa kimaelezo ndiyo umetumika kuwasilisha data za utafiti huu. Tafiti tangulizi za kifasihi zimetumia mkabala huu, hivyo kuogelea bwawa moja na watafiti waliotangulia, kulituwezesha kupima usahihi na uaminifu wa data za utafiti huu.

## 3. 8 Uchanganuzi wa Data

Katika maandiko ya fasihi, utafiti wa kifafanuzi ndiyo huonekana muafaka zaidi (Ponera, 2019). Utafiti tuliofanya ulikuwa wa kifafanuzi. Hivyo basi mkabala kimaelezo ndiyo tuliutumia kuwasilisha data za utafiti. Mkabala wa kimaelezo huhusu ufafanuzi wa namna watu wanavyofikiri kuhusu hali, kitu au jambo fulani na kutathmini hisia za watu juu ya hali, kitu au jambo hilo (Kothari 2004). Mkabala huu ulikuwa muafaka kutokana na utafiti tuliofanya. Lengo kuu sambamba na malengo mahsusi yalichambuliwa kupitia mkabala huu. Uchambuzi wa data uliongozwa na dira hii; kubainisha fani za Biblia katika tamthiliya teule, kutafuta sababu za kujitokeza kwa fani za Biblia katika tamthiliya teule hatimaye kubainisha dhamira zinazowasilishwa kutokana na fani za Biblia zilizojitokeza katika tamthiliya teule.

## 3. 9 Kuaminika kwa Matokeo ya Utafiti

Mbinu zilizotumika katika utafiti ndizo huchangia kuaminika kwa matokeo ya utafiti (Ponera, 2019). Zikitumika mbinu sahihi basi kuna uwezekano mkubwa wa kupata matokeo sahihi. Utafiti huu umetumia mbinu sahihi kutokana na utafiti tuliokuwa tunafanya, usomaji matini. Zelda (2018) anasema matumizi ya mbinu sahihi katika kukusanya data kutoka vyanzo mbalimbali vya maarifa huchagiza utafiti kuaminika zaidi. Hivyo basi kutokana na mbinu tuliyotumia katika utafiti huu tunakiri kwamba matokeo tuliyopata ni dhahiri.

## 3. 10 Maadili ya Utafiti

Katika utafiti huu mtafiti aliomba ridhaa ya kupitia maktaba za taasisi mbalimbali ili kusoma matini mbalimbali katika utafiti huu. Vilevile maadili ya utafiti ya utunzwaji wa siri katika data zote za msingi yalizingatiwa popote tulipoingia na kutoka wakati

tukitafuta taarifa za utafiti huu. Matakwa ya maktaba katika taasisi za kitaaluma yalizingatiwa neno kwa neno.

Hali kadhalika utafiti tuliofanya ulikuwa wa maktaba. Hivyo mtafiti alizingatia maadili ya uandishi wa tasnifu hii. Data za utafiti kutoka katika tamthiliya teule zilikusanywa kwa makini hatimaye zikachambuliwa inavyopaswa akiongozwa na Nadharia ya Mwingilianomatini.

### 3. 11 Muhtasari

Kwa jumla, katika hii sura ya tatu, mtafiti amejadili mbinu za utafiti zilizotumika katika utafiti lengwa. Hapa ndani amejadili eneo la utafiti, usanifu wa utafiti, usampulishaji na vyanzo vya data. Hali kadhalika mtafiti ameeleza mbinu iliyotumika kukusanya data, usahihi wa mbinu za utafiti pamoja na uchambuzi wa data za utafiti. Pamoja nazo mtafiti ameeleza kuaminika kwa matokeo ya utafiti na maadili ya utafiti.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI WA DATA, UCHAMBUZI NA MJADALA WA MATOKEO

## 4. 1 Utangulizi

Sura ya nne katika utafifi huu ndiyo kiini cha utafiti. Mtafiti amewasilisha, kuchambua na kujadili data na matokeo ya utafiti uliofanyika. Katika sura hii mtafiti amefanya uchambuzi wa malengo mahsusi yote matatu ya utafiti huu kupitia Nadharia ya Mwingilianomatini.

Malengo mahsusi mawili; lengo mahsusi la kwanza na lengo mahsusi la pili yamechambuliwa kwa mtindo mtawalia kwa sababu yanaelekeana kimantiki. Mtafiti amebainisha fani za Biblia katika tamthiliya teule sambamba na kufanya mjadala kuhusu sababu za kutokea kwa fani hizo katika tamthiliya za Emmanuel Mbogo. Lengo mahsusi la tatu limechambuliwa pekee. Katika kuchambua lengo hili, mtafiti ameeleza dhamira zilizodhihirika kutokana na fani za Biblia zilizojitokeza ndani ya tamthiliya teule.

## 4. 2 Fani za Biblia na Sababu za Kujitokeza kwake katika Tamthiliya Teule

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa kuchunguza fani za Biblia katika fasihi ya Kiswahili, tukiegama katika tamthiliya za Emmanuel Mbogo. Malengo mahsusi yalikuwa matatu: kubainisha fani za Biblia katika tamthiliya teule, kujadili sababu za kujitokeza kwa fani za Biblia katika tamthiliya na teule hatimaye tukabainisha dhamira zinazowasilishwa kutokana na fani hizo. Tulitumia mbinu moja ili kukusanya data hizo; mbinu ya usomaji matini.

Katika utafiti uliofanyika, mtafiti amebaini kwamba, fani za Biblia katika tamthiliya teule za Emmanuel Mbogo zimejitokeza kwa namna mbalimbali. Katika kuwasilisha

fani hizi, mtafiti amewasilisha fani za Biblia zilizojitokeza katika tamthiliya teule zote sita. Vilevile, katika sehemu hii mtafiti ameeleza sababu za kujitokeza kwa kila fani ya Biblia katika tamthiliya teule.

Kimsingi, lengo mahsusi la kwanza na la pili, yamewasilishwa pamoja kwa kila hoja kwa sababu yanaendana kimantiki. Lengo mahsusi la tatu limechambuliwa pweke kuonyesha dhamira zinazoibuliwa kutokana na fani za Biblia zilizojitokeza katika tamthiliya teule

Mihimili ya Nadharia ya Mwingilianomatini iliyotuongoza katika kufanikisha malengo mawili mahsusi ya mwanzo; kubainisha fani za Biblia na kueleza sababu za kujitokeza kwa fani za Biblia katika tamthiliya teule ni hii ifuatayo:

- Hamna matini yoyote ile ya kifasihi ambayo inaweza kuangaliwa kivyake au kujitegemea.
- Matini yoyote ile ni mabadiliko ya mpangilio wa matini nyingine tangulizi.
- Kazi za kifasihi huundwa kutokana na mifumo ya kanuni na tamaduni mbalimbali zilizowekwa na kazi tangulizi za kifasihi ambapo taswira za maisha ya kawaida na uhusiano wa kimaana huunganishwa na kubadilishwa.

Kimsingi, fani ya Biblia yoyote iliyobainishwa, imechambuliwa pweke kwa kuhusisha tamthiliya zote teule kabla ya kuhamia fani nyingine. Mtafiti kupitia mbinu ya usomaji matini alibaini fani za Biblia zilizojitokeza katika tamthiliya teule za Emmanuel Mbogo kama inavyoonyeshwa katika jedwali hapa chini.

**Jedwali Na. 4. 1 Fani za Biblia Zilizojitokeza katika Tamthiliya Teule**

| **Na.** | **Fani ya Biblia Iliyotumika** |
|---|---|
| 1 | Nukuu za Biblia |
| 2 | Wahusika wa Biblia |
| 3 | Hadithi za Biblia |
| 4 | Sajili ya Biblia |
| 5 | Mandhari ya Biblia |

**Chanzo: Data za utafiti katika tamthiliya teule**

Kimsingi, hizo ndiyo fani mbalimbali za Biblia zilizotumika katika kuchambua data za utafiti huu. Fani hizi zinachambuliwa katika sehemu inayofuata hapa chini.

### 4. 2. 1 Nukuu za Biblia katika Tamthiliya Teule

Nukuu ni maandishi yaliyonakiliwa na kuingizwa katika hati nyingine au katika maneno ya mtu mwingine (BAKITA, 2022). Kupitia baraza hili tunabaini kwamba, mtindo wa kunakili, kuchukua maneno ya chanzo kingine, mtu mwingine kwa lengo la kushadidia jambo au kueleza jambo unalowasilisha katika maandishi ndiyo kunukuu. Nukuu zinaweza kuwa moja kwa moja au kurejea sehemu tungo mahsusi.

Mtafiti amebaini kwamba katika tamthiliya teule, Emmanuel Mbogo ametumia nukuu mbalimbali kutoka katika Biblia. Nukuu hizo hazikurejewa kibubusa. Ifahamike kwamba, watu wanapotumia nukuu kutoka katika vyanzo vingine huwa na

lengo mahsusi. Wakilenga zaidi kudhihirisha ukweli juu ya jambo wanaloandika au kuwasilisha kwa hadhira.

Mtunzi amewasilisha hili kupitia mazungumzo baina ya wahusika katika drama teule. Kujitokeza kwa fani hii kunathibitisha mhimili wa Nadharia ya Mwingilianomatini, unaoeleza kwamba kazi za fasihi ni zao la matini nyingine tangulizi hivyo athari ya kazi zilizotangulia huonekana katika kazi mpya zinazofuata baada yake (Kristeva, 1986). Katika sehemu inayofuata hapa chini, tumebainisha nukuu za Biblia kutoka katika tamthiliya teule zote.

#### 4. 2. 1. 1 Nukuu za Biblia katika Tamthiliya ya Mondlane na Samora

Mtunzi teule amenukuu Biblia katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora* (2016). Wahusika mbalimbali wametumika kuwasilisha nukuu hizo mathalan, Mhusika Nyerere akizungumza na wenzake kuhusu ukombozi wa fikra. Nukuu hiyo imedhihirika namna hii,

> NYERERE: ...*Inasemwa: Imani huja kwa kusikia*
> *Na kusikia, na kusikia...*
> *Uongo, ukweli ama uzandiki wa mtu ...*
> (Uk. 61)

Tungo, ‘Imani huja kwa kusikia’ katika mazungumzo ya Nyerere imechotwa kutoka katika kitabu cha Biblia. Ndani ya Biblia maneno haya yalitumiwa na Mtume Paulo katika waraka wake kwa Warumi akizungumza kuhusu imani. Katika Biblia tungo hiyo inasomeka hivi;

> “Basi *imani chanzo chake ni kusikia* na kusikia huja kwa neno la Kristo.” (Warumi 10:17)

Kimsingi, matokeo ya utafiti yamebaini kuwa kuna nukuu za Biblia katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora* (2016). Nukuu hizo zimenakiriwa waziwazi au kwa sehemu kama tulivyowasilisha. Bakhtin (1981) katika Nadharia ya Mwingilianomatini anaeleza kuwa, kazi za fasihi zinahusiana kifani na kimaudhui. Hivyo basi si ajabu kuona athari za matini moja iliyobuniwa awali katika matini nyingine iliyobuniwa baadaye. Hivyo ni dhahiri shayini kwamba nukuu za Biblia katika tamthiliya teule ni athari ya kitabu hicho kilichoandikwa hapo kwanza.

#### 4. 2. 1. 2 Nukuu za Biblia katika Tamthiliya ya Wangari Maathai

Hali kadhalika utafiti huu ulibaini nukuu za Biblia katika tamthiliya ya Wangari Maathai (2015). Nukuu hizo zimewasilishwa kupitia majibizano ya wahusika katika maonyesho aliyoandaa mtunzi. Katika tamthiliya ya Wangari Maathai, Emmanuel Mbogo amenukuu maandiko kutoka kwenye kitabu cha Biblia namna hii;

1) MKE 1: Wasije Makachero wake wakakuswaga Nyayo House
Nasikia huko wanaume wanateswa,
*Wanalia machozi na kusaga meno.*
*Ni kama Jehanam, Inatisha*.
(Uk. 10)

Kupitia mazungumzo ya mhusika MKE 1, mtafiti alibaini nukuu ya Biblia ndani yake. Mhusika huyu amenasibisha *Nyayo House* na *Jehanamu*, gereza ya watu wote watenda maovu kama inavyobainishwa kwenye Biblia. Biblia inaeleza katika gereza hilo la Jehanam kutakuwa na mateso makali. Watu watalia na kusaga meno.

> Hivi ndivyo itakavyokuwa wakati wa mwisho wa dunia.
> Malaika watakuja na kuwatenganisha watu waovu na watu wenye haki.
> Nao watawatupa hao waovu katika *tanuru la moto*
> *Ambako kutakuwa na kilio na kusaga meno*.

(Mathayo 13:49-50)

Vilevile nukuu ya Biblia imebainika kupitia mhusika mkuu wa tamthiliya hii, Wangari Maathai, katika onesho la sita.

2) WANGARI: Tumekwisha kubaliana juu ya kuweka kambi Uhuru Park.
Hapo *tutafunga na kumuomba Mwenyezi Mungu*;
Skycraper aslani haitajengwa Uhuru Park.
Watu walioko kizuizini lazima watoke...”
(Uk. 38)

Habari kuhusu dua za kufunga na kuomba baina ya matini za utafiti, zilitumika awali katika Biblia, kitabu cha waamini wa Kikristo. Mara ya pili ndipo zimesikika katika tamthiliya teule. Biblia inaeleza kuwa Mtume Yesu Kristo alikuwa akifundisha wafuasi wake kuhusu dua za kufunga na kuomba ili waweze kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazowasibu katika maisha kila uchao. Maombi hayo yalionekana kuwa suluhu ya changamoto zote.

Biblia imeandika hivi;

“Lakini namna hii haitoki ila kwa *kufunga na kuomba*.”
(Mathayo 17:21)

Kwa hivyo, Emmanuel Mbogo kupitia mhusika Wangari, amenukuu sehemu ya mstari huo. Wangari akiwahamasisha wanaharakati wenzake kupambana na wanaotaka kutumia mazingira isivyostahiki. Wanaharakati wanaelezwa kwamba wakifunga na kuomba, watashinda vita wanayoiendea. Msingi wa mwingilianomatini umethibitishwa hapa. Kazi awali ya Biblia inaonekana kuathiri tamthiliya teule iliyotungwa baada yake.

Kwa jumla, matokeo ya utafiti yamebaini nukuu za Biblia katika tamthiliya ya *Wangari Maathai* (2015). Sababu ya kutokea kwa nukuu hizo inachagizwa na dai la

wanamwingilianomatini kwamba, mtunzi wa fasihi huchota matini ya kazi moja ya fasihi iliyotangulia na kuihamishia kwenye matini nyingine, mpya inayobuniwa (Senkoro, 2011). Hivyo basi, Mbogo amechota matini ya Biblia na kuihamishia kwenye tamthiliya hii tuliyotafiti kama tulivyobainisha kupitia nukuu mbalimbali.

#### 4. 2. 1. 3 Nukuu za Biblia katika Tamthiliya ya Nyota ya Tom Mboya

Vilevile katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya* (2016) mtunzi amenukuu Biblia katika sehemu mbalimbali. Mathalani;

3) PAMELA: Endelea kukumbatia huyu mke mwenza
*Nami niko pamoja nawe*
*Kwa Mvua*
*Kwa Jua*
*Hadi mwisho wa dunia*
(Uk. 38)

Sehemu ya maandiko anayorejea Pamela hapo juu akizungumza na mume wake yalitumika katika Biblia, katika mafundisho ya ndoa. Biblia inaeleza kuwa, mume na mke wakishaoana hawatakiwi kuachana, kutenganishwa kwa tatizo lolote. Wanandoa wanapaswa kuishi pamoja katika shida na raha hadi mauti yamkute mmoja kati yao. Biblia inaandika hivi;

> "Lakini tangu mwanzo wa kuumbwa ulimwengu, aliwafanya mume na mume na mke. Kwa sababu hiyo mtu atamwacha babaye na mamaye, ataambatana na mkewe; na hao wawili watakuwa si wawili tena bali mwili mmoja. *Basi alichokiunganisha Mungu, mwanadamu asikitenganishe*."
> (Marko 10:6-9)

Emmanuel Mbogo kupitia mhusika Pamela ametumia dhana ya Jua kuashiria nuru katika ndoa yaani wakati wa furaha, shangwe na mafanikio. Mwezi umetumiwa kuashiria wakati wa giza, mateso, dhiki na mapambano katika ndoa. Pamela amekiri kusimama imara katika nyakati zote zitakazoikumba ndoa yake. Hatakuwa tayari

kumpoteza mume wake ingawa amebaini kwamba anamfanyia ulaghai. Hii inadhihirisha kuwa Emmanuel Mbogo amenukuu sehemu ya maandiko kuhusu mafundisho ya ndoa.

Kimsingi, matokeo ya utafiti yamebaini nukuu za Biblia katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya* (2016). Nukuu hizo zilitumika awali kutoka kwenye matini ya Biblia na sasa zimetumika kwa mara nyingine katika kazi hii teule tuliyoitafiti. Waasisi wa Nadharia ya Mwingilianomatini wanasema kuwa hakuna matini asili asilimia mia moja, matini za fasihi nyingi huwa ni mageuzi ya matini nyingine za kale alizopata kukutana nazo mtunzi kabla ya matini anayoandaa (Bakhtin, 1981). Kwa hali hiyo tunasema, Emmanuel Mbogo amenukuu sehemu ya maandiko kuhusu mafundisho ya ndoa kutoka kwenye Biblia. Mtunzi huyu teule amegeuza matini aliyokutana nayo hapo kale, *Biblia* katika kuumba tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya* ya zama hizi.

#### 4. 2. 1. 4 Nukuu za Biblia katika Tamthiliya ya Tanzia ya Patrice Lumumba

Vilevile nukuu za Biblia zimejitokeza katika tamthiliya *Tanzia ya Patrice Lumumba* (2015). Mtunzi amerejea nukuu hizo namna hii;

4) MOBUTU: Wacha na mimi niwaambie siri.
Lumumba maisha yake yatakuwa mafupi sana kwani leo Patrice amevunja *amri ya nne isemayo:*
*Waheshimu baba na mama yako ili upate kuishi miaka mingi...* (Uk. 12)

Amri inayorejewa na mhusika Mobutu katika mazungumzo haya imenukuliwa kutoka katika Biblia awali kabisa katika kitabu cha Mwanzo. Katika simulizi za Wana wa Israel, Mungu aliwapa amri kumi kupitia Nabii Musa. Amri hizo zilitolewa ili ziwe dira ya kuishi nchini kwao Kanaani, mara baada ya kukombolewa kutoka

utumwani Misri. Amri kumi za Mungu katika Biblia zinapatikana katika kitabu cha Kutoka 20: 2 – 16. Katika mfululizo wa amri hizo, amri ya nne inasomeka hivi;

> "*Waheshimu Baba na Mama yako, siku zako zipate kuwa nyingi*..."
> (Kutoka 20:12)

Hali kadhalika mtunzi amenukuu andiko lingine la Biblia ndani ya tamthiliya hii kama inavyobainika kupitia mazungumzo ya mhusika, Tshombe kama hivi;

5) TSHOMBE: Haya Mpolo! Una la kusema?
Kabla hujaungana na wafu wenzako?
*Padri* wetu alizoea kusema:
*Ulitoka kwa udongo, utarudi kwa udongo*;
Majivu kwa majivu; makaburi kwa makaburi. Sema!"
(Uk. 51)

Maneno yaliyonukuliwa kutoka katika Biblia ni haya *'ulitoka kwa udongo, utarudi kwa udongo; majivu kwa majivu; makaburi kwa makaburi*.' Mtafiti alibaini kwamba yalinukuliwa kwenye Biblia katika kitabu cha Mwanzo. Katika Biblia maneno hayo yalitumiwa na Mwenyezi Mungu alipokuwa akitoa laana ya kifo kwa mwanadamu baada ya kufanya uovu katika bustani ya Edeni. Biblia imeandika hivi;

> "Kwa jasho la uso wako utakula chakula, hata utakapoirudia ardhi,
> ambayo kwa hiyo ulitwaliwa;
> *Kwa maana u mavumbi wewe, nawe mavumbini utarudi*."
> (Mwanzo 3:19)

Kwa jumla, matokeo ya utafiti yamebaini nukuu za Biblia katika tamthiliya teule ya *Tanzia ya Patrice Lumumba* (2015). Mhimili mmojawapo wa mwingilianomatini unaeleza kwamba, matini za fasihi huwa zimechota, kunukuu, kugeuza, kuiga au kurejelea kwa njia moja ama nyingine matini nyingine zilizotangulia awali (Kristeva, 1980). Kuhusishwa nukuu za Biblia kupitia wahusika Mobutu na Tshombe katika

tamthiliya teule ya *Tanzia ya Patrice Lumumba* ni ithibati ya mhimili huo. Kwamba hiyo ndiyo sababu inayofanya tuone nukuu za Biblia, matini iliyotungwa awali kwenye matini mpya, tamthiliya ya *Tanzia ya Patrice Lumumba*.

#### 4. 2. 1. 5 Nukuu za Biblia katika Tamthiliya ya Mtumwa hadi Siti Binti Saad

Mtunzi teule amehusisha pia nukuu za Biblia kwa jinsi mbalimbali. Kwa mfano katika onesho la kwanza nukuu ya Biblia imebainika namna hii;

6) KHAMIS: ...Tafadhali kimwana, likubali ombi la penzi langu.
Tuoane; tuwe mume na mke.
*Mola akitujaalia tuzae watoto na tuijaze dunia*."
(Uk. 7)

Nukuu ya Biblia iliyotumika inahusu mafundisho ya ndoa. Mungu aliagiza mume na mke waoane kisha wazae na kuijaza dunia. Tazama;

"... Mungu akawabariki na kuwaambia;
*Zaeni mkaongezeke, mkaijaze nchi na kuimiliki*..."
(Mwanzo 1:28)

Vilevile utafiti ulibaini kwamba, Emmanuel Mbogo ametumia nukuu za Biblia katika onesho la nne la tamthiliya hii, *Mtumwa hadi Siti Binti Saad*. Nukuu hiyo imedhihirika kupitia mhusika Nongwa. Fani hiyo iliwasilishwa hivi;

7) NONGWA: '*Adui wa mtu ni mtu wa nyumbani mwake mwenyewe*.'
(Uk. 23)

Katika maelezo ya mhusika huyu, Emmanuel Mbogo amenukuu tungo hiyo kutoka katika Biblia. Mtume Yesu Kristo alizungumza maneno hayo akiwahubiria makutano mafundisho yake kama ilivyoelezwa katika kitabu cha Mathayo Mtakatifu. Biblia inaandika;

"Kwa maana nalikuja kumfitini mtu na babaye, na binti na mamaye,
na mkwe na mtu; *na adui za mtu ni wale wa nyumbani mwake*."
(Mathayo Mt. 10: 35 – 36)

Pamoja na hayo mtunzi amenukuu pia maneno kutoka kwenye Biblia katika onesho la kumi na tatu katika tamthiliya ya *Mtumwa hadi Siti Binti Saad*. Mtunzi ametumia maneno hayo kupitia mhusika Bonga. Mhusika huyu alikuwa akishangaa kuinuliwa kwa binti maskini, Mtumwa Siti kupitia muziki wa taarabu. Nukuu inasomeka hivi;

8) BONGA: Ama kweli, *Mwenyezi Mungu anaweza kumtoa mtu kwenye matope na kumwinua juu katika utukufu na enzi*."
(Uk. 79)

Katika Biblia, maneno hayo kuhusu kuinuliwa kwa mtu duni hadi kufanikiwa yametumika katika kitabu cha Nabii Samweli. Nabii huyu alikuwa akifundisha wafuasi wa Mwenyezi Mungu kuishi kwa matumaini, kwamba wanaweza kufanikiwa hata kama wanatoka katika mazingira au familia duni. Biblia inaeleza;

"Bwana…*humwinua mnyonge toka mavumbini, humpandisha mhitaji kutoka jaani, ili awaketishe pamoja na wakuu*."
(1Samwel 2: 7 – 8)

Kimsingi, utafiti huu umebaini nukuu za Biblia katika tamthiliya ya *Mtumwa hadi Siti Binti Saad* (2016). Nukuu hizo zimebainishwa kupitia mijadala ya wahusika katika maonyesho mbalimbali. Jilala (2018) akiandika kuhusu Nadharia ya Mwingilianomatini anasema kuwa, matini za fasihi ni zao la matini tangulizi. Mwanazuoni huyo anaendelea kushadidia kuwa, athari za matini tangulizi huonekana kwa jinsi moja ama nyingine katika matini mpya. Hivyo basi, nukuu za Biblia zilizorejewa na Emmanuel Mbogo katika kuandika drama hii ya kihistoria, inayozungumza kuhusu maisha ya Siti Binti Saad aliyekuwa mwimbaji maarufu wa muziki wa taarabu; nchini Zanzibar na Upwa wa Afrika Mashariki zinathibitisha mhimili wa nadharia hii. Matini za fasihi zinakamilishana. Ndipo sasa kaida za matini tangulizi (Biblia) huonekana tena katika matini fuatizi (tamthiliya) hapo baadaye kama tulivyobainisha.

#### 4. 2. 1. 6 Nukuu za Biblia katika Tamthiliya ya Malkia Bibi Titi Mohamed

Katika tamthiliya teule ya *Malkia Bibi Titi Mohamed* (2016) nukuu za Biblia zimebainishwa namna hii;

9) BIBITITI: Kwa jina la Mwenyezi Mungu; *Yeye mwenyewe Labana aliyeniumba ndiye atakuwa mtetezi wangu*. Yeye Mola wangu ajuaye siri na mafumbo yaliyo chini ya vilindi vya bahari, ndiye Wakili na Hakimu wangu. (Uk. 3)

Mhusika Bibi Titi ametumika kunukuu sehemu ya maneno kutoka kwenye Biblia akijitetea mbele ya mume wake dhidi ya tuhuma za usaliti. Katika kitabu cha Biblia manabii wamezungumza maneno kama hayo jinsi mbalimbali. Kwamba, mtu anayeonewa anastahili kumwachia Mola jukumu la kumtetea. Mtendwa hapaswi kukata tamaa kwa dhuluma mbalimbali anazokabiliana nazo kwenye maisha. Biblia inaeleza;

> "Tazama wote walioona hasira juu yako watatahayarika na kufadhaika; watu washindao nawe watakuwa si kitu, na kuangamia. Utawatafuta wala hutawaona wale wapiganao nawe; watakuwa si kitu; watakuwa kama kitu kisichokuwa wale waliofanya vita juu yako. *Kwa maana mimi Bwana, Mungu wako nitakushika mkono wako wa kuume, nikikuambia, Usiogope; mimi nitakusaidia*"
> (Isaya 41:11 – 13)

Pamoja na hayo, katika onesho la sita la tamthiliya hii mtafiti alibaini nukuu za Biblia. Mtunzi amewasilisha maneno hayo kupitia mhusika mkuu wa tamthiliya hii, BIBITITI. Nukuu hiyo inadhihirika namna hii;

10) BIBITITI: … Lakini sasa hakuna kulala
Hakuna kupumzika
*Yale makusudi ya Mola wangu*
*Kuniumba na kunileta duniani* ili
Niupiganie uhuru wa Tanganyika
Ima faima lazima yatimie.
(Uk. 49)

Nukuu kuhusu kusudi la Mungu kumuumba mwanadamu zilielezwa kwa mara ya kwanza na Mfalme Suleiman katika kitabu teule cha Biblia. Mfalme Suleiman kwa masimulizi ya Wayahudi, alikuwa mashuhuri sana katika Ufalme wa Yuda huko Israel. Mfalme huyo katika kitabu alichoandika aliwajulisha watu kwamba, kila mtu hapa ulimwenguni ameletwa na Mola kwa kusudi maalum. Mola amemleta afanye wajibu fulani. Kwa hivyo, watu wawajibike na kuthaminiana katika jamii. Biblia imeandika haya;

> "Bwana amefanya kila kitu kwa kusudi lake; Naam hata wabaya kwa siku ya ubaya..."
> (Mithali 16:4)

Kimsingi, matokeo ya utafiti yamebaini nukuu za Biblia katika tamthiliya ya *Malkia Bibi Titi Mohamed.* Mtunzi wa tamthiliya hii amenukuu mistari mbalimbali kutoka kwenye Biblia katika tamthiliya hii kama tulivyobainisha. Bakhtin (1981) na Kristeva (1986) waasisi wa Nadharia ya Mwingilianomatini wanasema, matini nyingi za fasihi uhusiana kifani na kimaudhui. Waasisi hawa wanaamini hakuna matini ya kazi ya fasihi isiyohusiana na kazi nyingine iliyopata kuwapo kuwako kabla yake. Kwa hivyo kujitokeza kwa nukuu hizi za Biblia katika tamthiliya ya *Malkia Bibi Titi Mohamed* ni zao la athari ya matini ya Biblia iliyoandikwa hapo kale kabla ya kazi hii tuliyoisoma sasa.

### 4. 2. 1. 7 Muhtasari

Kimsingi, matokeo ya utafiti yamebaini nukuu za Biblia katika tamthiliya teule zote kama tulivyowasilisha. Kuna mahusiano baina ya Biblia na tamthiliya teule kupitia kipengele hiki cha kifani, nukuu za Biblia. Biblia iliandikwa karne ya 8 hadi 6 K.W.K. (Soma Biblia Tanzania, 2011). Miaka kama 3,500 hivi iliyopita. Lakini sasa

inaonekana tena kwenye kazi za fasihi ya Kiswahili miaka 2022 B.K. Kazi teule ni zao ama tokeo la Biblia kama wanamwingilianomatini wanavyoeleza kwamba, hakuna matini asili katika fasihi, matini nyingi huwa zimetokana na matini nyingine ambazo watunzi wamewahi kukutana nazo kabla ya kuumba bunilizi zao. Athari hizo zinaweza kuwa za kifani au kimaudhui. Tamthiliya teule na Biblia zinahusiana kwenye kipengele cha kifani; nukuu za Biblia. Mtafiti anatanabaisha kuwa, mazungumzo baina ya wahusika katika bunilizi yametumika kuwakilisha nukuu za Biblia katika tamthiliya teule. Hivyo nukuu za Biblia katika tamthiliya teule zimebainika kupitia mazungumzo baina ya wahusika.

### 4. 2. 2 Simulizi za Biblia katika Tamthiliya Teule

Hadithi ni masimulizi kuhusu matukio yaliyopita; habari; visa, hekaya, ngano n.k. (BAKITA, 2022). Fasili hii inayotolewa kuhusu dhana ya hadithi na wanazuoni hawa imetusaidia katika utafiti huu tuliofanya. Wanazuoni hawa wanatuelekeza kwamba, hadithi uhusu matukio, mambo yaliyopita, yaliyotokea kale. Masimulizi hayo yanaweza kuhusu mtu, jamii au uga fulani. Taasisi hii inaendelea kueleza kwamba, masimulizi yanapotolewa yanaweza kutumia mtindo wa lugha ya mazungumzo au maandishi.

Simulizi ni hadithi za matukio halisi au za kubuni zinazohusu hali halisi ya maisha. Neno hili ‘simulizi’ lina usuli kutoka lugha ya Kiarabu (TATAKI, 2014). Taasisi ya taaluma za Kiswahili, inafasili dhana ya simulizi kama hadithi zenye usuli katika halisi halisi ya maisha. Wanachobainisha wanazuoni hawa ni kwamba, vyote iwavyo simulizi inapowasilishwa, ni lazima ihusiane na tukio, halisi katika jamii.

Wamitila (2008) anafasili simulizi au hadithi kama utungo wenye visa vya kubuni au halisi unaowasilishwa kwa lugha ya nathari kwa kusudi la kufundisha, kukuza maadili na kuunganisha jamii. Mwanazuoni huyu anashadidia kwamba, katika usimuliaji wa hadithi fanani hulenga kufikisha dhamira fulani kwa hadithi. Vilevile Wamitila (Ktj) anaendelea kueleza kuwa, katika usimuliaji wa hadithi fanani huwa mbunifu ili asiwachushe hadhira yake.

Kimsingi, hadithi au simulizi inaweza kufasiliwa kama utanzu wa fasihi unaotumia lugha ya nathari katika kufikisha ujumbe kwa hadhira. Utanzu huu wa kinathari uhusu matukio halisi yaliyowahi kutokea katika jamii ama yanayobuniwa na fanani ili kufikisha dhamira fulani kwa jamii.

Katika utafiti tuliofanya, lengo mahsusi mojawapo lilikuwa kubainisha fani za Biblia katika tamthiliya teule. Matokeo ya utafiti yamebaini kwamba, Emmanuel Mbogo ametumia simulizi za Biblia, zilizotumika awali kutoka kwenye Biblia katika kuumba kazi zake.

Katika sehemu inayofuata tumebainisha simulizi za kibiblia zilizojitokeza katika tamthiliya teule zote. Halikadhalka tumeeleza sababu za kutokea kwa simulizi hizo kwa kuegema kwenye Nadharia ya Mwingilianomatini. Tumebainisha fani hizi katika tamthiliya teule hapa chini sehemu inayofuata.

#### 4. 2. 2. 1 Simulizi za Biblia katika Tamthiliya ya Mondlane na Samora

Simulizi za Biblia nimehusishwa katika tamthiliya teule ya *Mondlane na Samora* (2016). Mtunzi teule amedhihirisha hili kupitia mazungumzo baina ya wahusika ndani ya tamthiliya. Simulizi ya ukombozi wa Israel kupitia Nabii Musa, aliyewatoa

utumwani Misri imepiga mwangwi ndani ya drama hii. Simulizi ya Biblia imehusishwa kwa jinsi hii;

11) NESI: Aaah! Ajabu ya Mungu hii!
Nasikia ile *fimbo alipewa na mamaake*.
Ni *fimbo iliyojaa ishara na miujiza*.
JANET: Kabisa! Nasikia ni kama ile *fimbo ya Nabii Musa*
iliyogawa bahari ya Shamu
NESI: [akicheka] Unajua hata hapa Dar watu wamembatiza;
*Wanamwita Nyerere, Nabii Musa*.
*Anatupeleka Kanaani, nchi ya Asali na Maziwa*.
(Uk. 88)

Katika simulizi za Biblia, Nabii Musa anaelezwa kama kiongozi wa kwanza, aliyewasaidia wana wa Israel kukombolewa kutoka uonevu wa kitumwa huko Misri, kwa Farao. Ajenda yake kuu, ama kusudi lake kuu lilikuwa hilo, kupigania ukombozi wa Israel. Watoke utumwani Misri, na kurejea kwenye nchi yao waliyoahidiwa na Mungu, Kanaani. Katika mapambano hayo, Mola alimpa msaidizi wake, Haruni. Huyo Haruni ndiye aliyeandamana na Nabii Musa katika harakati, mikutano mbalimbali ya kuikomboa Israel, huko Misri.

Simulizi za Biblia zinatanabaisha kwamba, katika harakati za ukombozi Nabii Musa alikuwa akitembea na fimbo. Fimbo hiyo ilimsaidia kufanya miujiza, ishara, maajabu mbalimbali. Jambo lolote alilotaka kulifanya kupitia fimbo hiyo, lilitimizwa. Biblia (2022) inaeleza;

> "*Musa, akanyoosha mkono wake juu ya bahari; BWANA akaifanya bahari irudi nyuma kwa upepo wa nguvu utokao Mashariki;* usiku kucha akafanya bahari kuwa nchi kavu, maji yakagawanyika. Wana wa Israel wakaenda ndani kati ya bahari katika nchi kavu..."
> (Kutoka 14:21)

> "Musa akamlilia Bwana akisema, Niwatendee nini watu hawa? Bado kidogo nao watanipiga kwa mawe. Bwana akamwambia

> Musa, pita mbele ya watu, ukawachukue baadhi ya wazee wa Israel pamoja nawe; *na ile fimbo yako* ambayo uliupiga mto kwayo, itwae mikononi mwako, ukaende. Tazama nitasimama mbele yako, juu ya lile jabali na maji yatatoka, watu wapate kunywa. Musa akafanya hivyo mbele ya wazee wa Israel."
> (Mwanzo 17: 4 – 6)

Simulizi zilizotumika awali katika Biblia zimetumika sasa katika tamthiliya teule, *Mondlane na Samora*. Musa kiongozi wa taifa la Israel aliyepambana hata taifa lake likakombolewa kutoka utumwani, Misri kwa Farao amenasibishwa na Mwalimu Nyerere, kiongozi wa kwanza wa taifa la Tanganyika (sasa Tanzania).

Nabii Musa katika jitihada za ukombozi wa taifa la Israel, alichorwa kama kiongozi anayetembea na fimbo inayofanya miujiza. Mwalimu Nyerere, mkombozi wa Tanganyika na Afrika kwa jumla, amechorwa hivyo katika tamthiliya hii ya *Mondlane* na *Samora.* Fimbo ya Mwalimu Nyerere ina uwezo wa kufanya maajabu kama fimbo aliyokuwa nayo Nabii Musa. Mbogo ameeleza hivi;

12) JANET: Sijui. Ila Samora alininong'oneza kuwa; baada ya mashambulizi yale ghafla, *Nyerere alimshika Samito, akainua kafimbo kake juu na mara wakayeyuka.* (Uk. 86)

Vilevile katika tamthiliya hii, kuna simulizi ya Biblia kuhusu taifa la Israel kukaa utumwani, Misri kwa zaidi ya miaka 400. Mtunzi ametumia maelezo yanayoakisi simulizi hiyo. Emmanuel Mbogo amenasibisha kutawaliwa kwa taifa la Msumbiji na Wareno muda wa miaka 400 kama ilivyotukia kwa Israel kukaa utumwani Misri katika Biblia. Mtunzi teule ameakisi simulizi hiyo ya Biblia namna hii;

13) BBC 2: Usisahau BBC 1 kwamba: *Wareno wameitawala Msumbiji kwa takribani miaka 400...* (Uk. 95)

Katika Biblia simulizi kuhusu Israel kutawaliwa miaka 400 na Misri, wakiwa watumwa huko ugenini imeelezwa katika kitabu cha Mwanzo. Biblia inaandika;

> "Basi wana wa Israel kukaa kwao, maana, muda waliokaa ndani ya Misri, ulikuwa ni *miaka mia nne na thelathini*."
> (Mwanzo 12: 40)

Simulizi ya Israel (katika Biblia) kutawaliwa miaka mia nne na Misri inarandana na simulizi ya Msumbiji kutawaliwa na miaka mia nne na Ureno. Hata hivyo pamoja na nchi hizo kutawaliwa miaka mia nne na wageni, siku ilifika zikapambana na hatimaye zikawa huru na kujitawala zenyewe.

Pamoja na hiyo, mtunzi amehusisha pia simulizi ya wanadamu wa kwanza katika Biblia; Adam na Eva. Wanadamu hawa waliasi agizo la Mwenyezi Mungu alilolitoa, kwamba wasile tunda fulani ndani ya bustani ya Edeni waliyokuwa wamewekwa, waitunze. Simulizi inaandika kwamba mwanamume Adam kwa kufuata ushauri wa mke wake Eva, aliakaidi agizo la Mungu. Adam akachukua tunda ale huku akijua kwamba akila tu hilo, atakufa. Emmanuel Mbogo amehusisha simulizi hii katika akimtumia mwanamke Pauline kumshauri mume wake Tshombe akaidi maagizo ya kiongozi wake ndani ya tamthiliya teule. Tshombe, mume wa Pauline hakubaliana na ushauri huo kutoka kwa mke wake akirejea simulizi ya Adam na Eva akisema;

14) TSHOMBE: *Pauline mimi siko tayari kufa kama Adam.*
*Adam alijua fika kuwa tunda lile lilikuwa sumu,*
*Lakini kwa ushawishi na ulaghai wa mwanamke,*
*Adam alichukua ufu, akautafuna, akaumeza,*
*akafa...!*
(Uk. 54)

Katika matini ya Biblia simulizi hiyo imeandikwa namna hii;

> "Bwana Mungu akamwagiza huyo mtu, akisema,
> Matunda ya kila mti wa bustani waweza kula, *walakini matunda ya mti*

> *wa ujuzi wa mema na mabaya usile, kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika*."
> (Mwanzo 2:16 – 17)

> "*Mwanamke alipoona ule mti wafaa kwa chakula, wapendeza macho, nao ni mti wa kutamanika kwa maarifa, alitwaa katika matunda yake, akala, akampa mumewe naye akala*."
> (Mwanzo 3: 6)

Kimsingi, kuna simulizi za Biblia katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora* (2016) kama tulivyowasilisha. Msomaji wa kitabu cha Biblia akikutana na mazungumzo ya Tshombe na Pauline kuhusu asili ya kifo, anakumbuka kisa cha Adam na Eva kwa ukaidi waliofanya mbele ya Mwenyezi Mungu. Ukaidi huo, ulifanya Adam, Eva na vizazi vyao waanze kuangamia kw amauti hata leo. Nadharia ya Mwingilianomatini inadai kuwa, mbunifu wa kazi ya fasihi huchukua matini moja ya fasihi na kuihamisha kwenye matini nyingine (Wamitila, 2003 na Senkoro, 2011). Emmanuel Mbogo ametumia simulizi za Biblia katika bunilizi zake. Hadithi mbalimbali zilizosimuliwa ndani ya Biblia awali, zinasikika pia katika tamthiliya teule kama tulivyobainisha. Msomaji wa Biblia anapozisoma tamthiliya teule, basi hadithi hizo nyingi alizowahi kukutana nazo humo zinabisha hodi kwenye ufahamu wake.

Biblia ni chipukizi la fasihi ya Wayahudi huko Mashariki ya Kati. Tamthiliya teule ni chipukizi la fasihi ya Waswahili, Afrika Mashariki. Lakini kazi hizi zimehusiana katika simulizi. Visa vinavyoelezwa katika tamthiliya teule za Kiswahili, vinanasibishwa na vile vilivyomo katika Biblia, kutoka jamii ya Wayahudi, Mashariki ya Kati. Masimulizi ya Ukombozi wa Israel wakiwa utumwani Misri, Maajabu ya Nabii Musa, Visa vya akina Adam na Eva n.k yanaonekana katika kazi hizi za fasihi ya Kiswahili. Musa, na kifimbo chake kuna pahala amenasibishwa na

Nyerere, na fimbo yake ya maajabu. Hakika mtunzi amechukua matini ya Biblia na kuihamishia katika matini teule kama mwingilianomatini unavyoeleza.

**4. 2. 2. 2. Simulizi za Biblia katika Tamthiliya ya Wangari Maathai**

Pamoja na hayo, simulizi za Biblia zimehusishwa katika tamthiliya ya *Wangari Maathai* (2015). Katika sehemu inayofuata tumebainisha simulizi za Biblia zilizojitokeza katika tamthiliya ya *Wangari Maathai*. Simulizi hizo zimedhihirika kama hivi;

15) WANGARI: Dunia yote lazima ijue kuwa,
Kenya hatutaiharibu ardhi kamwe,
*Ni wajibu wangu mimi na wewe,*
*Tuitunze misitu, miti tusiing'oweng'owe,*
Mazingira tutayabembeleza.
(Uk. 26)

Katika hotuba hiyo anayofanya Wangari, kuna mwangwi wa simulizi kuhusu mazingira kutoka katika Biblia. Biblia inasimulia kwamba, Mungu alipomuumba mwanadamu alimuweka kwenye bustani ya Edeni, alimpa jukumu la kuilima na kuitunza. Kwa hivyo jukumu la kutunza misitu nchini Kenya wanalopewa wananchi wa Kenya na Wangari ni chipukizi la simulizi ya Biblia. Kwamba wajibu wa kutunza mazingira ni wa kila mtu katika jamii. Biblia kuhusu wajibu wa mwanadamu kutunza mazingira imeeleza namna hii;

> "… *Mungu akapanda bustani upande wa Mashariki wa Edeni, akamweka ndani yake huyo mtu aliyemfanya*…"
> (Mwanzo 2: 7 - 8)
>
> "Bwana Mungu akamtwaa huyo mtu, *akamweka katika bustani ya Edeni, ailime na kuitunza."* (Mwanzo 2: 15)

Kimsingi, utafiti huu umebaini simulizi za Biblia katika tamthiliya ya *Wangari Maathai* (20015). Mathalani simulizi kuhusu wajibu wa mwanadamu kutunza

mazingira yake imechukuliwa kwenye Biblia ikatumika kwenye tamthiliya ya *Wangari Maathai*. Katika tamthiliya hii raia wa Kenya walikuwa wanakumbushwa kuhusu wajibu wao wa kutunza mazingira yanayowazunguka. Raia hao walikuwa wanaelezwa kuwa, ili Dunia iwe pahala pazuri pa kuishi mazingira yanatakiwa kuwa safi na salama.

Wafuasi wa Nadharia ya Mwingilianomatini (Mikhail Bakhtin na Julia Kristeva) wanasema, matini ya kifasihi inaweza kujidhihirisha, au kujihusisha na matini nyingine waziwazi, kwa kunukuu, kudondoa, kutaja, kurejelea au kusilimisha sifa za matini za awali; au kuwa katika mkumbo mmoja wa kifasihi (Wafula, 2015). Utafiti ulibaini kwamba, kuandikwa kwa tamthiliya teule kulichagizwa na simulizi za Biblia kutoka kitabu cha Mwanzo (Biblia) kama tulivyowasilisha. Mwandishi aliandika tamthiliya ya *Wangari Maathai* akihusisha simulizi mbalimbali za Biblia kuhusu mwanadamu na mazingira. Hivyo basi, Mbogo amesilimisha simulizi ya Biblia katika kuumba tamthiliya teule teule tuliyotafiti.

#### 4. 2. 2. 3 Simulizi za Biblia katika Tamthiliya ya Nyota ya Tom Mboya

Vilevile katika tamthiliya teule iliyoandwa na Emmanuel Mbogo, *Nyota ya Tom Mboya* (2016) kuna mwangwi wa simulizi za Biblia. Simulizi hizo zilisikika awali kwenye Biblia na sasa zimerejelewa tena katika tamthiliya teule. Simulizi za Biblia zilibainika kama ifuatavyo;

16) NDIEGE: [Anakunywa... Kilio cha utungu ndani (Ghafla inasikika radi;
wote wawili wanashtuka; na papo kwa papo, wakiwa
wanaangalia angani
*Inatokeza nyota* yenye mng’aro wa ajabu]
(Uk. 7)

Hadithi hii ya kuzaliwa kwa Tom Mboya, kwamba wakati akizaliwa ilitokea nyota angani, yenye mng'aro mkali inahusiana na simulizi ya kuzaliwa kwa Yesu Kristo kama inavyoelezwa kwenye Biblia. Simulizi ya Biblia inaeleza kwamba kuzaliwa kwa Yesu Kristo kuliambatana na kutukia kwa nyota yenye mng'aro mkali angani hata Mamajusi, Wataalam wa nyota huko Mashariki ya mbali wakaulizana kuhusu nyota hiyo. Jambo hilo hawakuwahi kuliona kabla katika kipindi chote cha utafiti wao. Habari za kuzaliwa kwa Yesu Kristo katika Biblia (1997) zimeeelezwa hivi;

> "Yesu alipozaliwa katika Bethelehem ya Uyahudi zamani za Mfalme Herode, tazama Mamajusi wa Mashariki walifika Yerusalem wakisema, *Yuko wapi yeye aliyezaliwa Mfalme wa Wayahudi? Kwa maana tuliiona nyota yake Mashariki*, nasi tumekuja kumsujudia." (Mathayo 2: 1-2)

Simulizi hii inamtambulisha Yesu kama mkombozi wa wanadamu ulimwenguni katika Biblia. Jinsi mkombozi huyo alivyozaliwa kumenasibishwa na kuzaliwa kwa mhusika Thomas (Tom Mboya) katika tamthiliya hii teule, *Nyota ya Tom Mboya*. Mhusika Thomas amechorwa kama mkombozi wa kweli wa taifa la Kenya dhidi ya ukoloni kutoka kwa Waingereza, wakoloni kutoka Ulaya. Thomas alikuwa akiwaongoza raia wa Kenya kupigania uhuru wao.

Hali kadhalika simulizi za Biblia katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya* zilibainika kupitia mazungumzo ya wahusika hawa; Wairimu na Mboya. Utafiti ulibaini kwamba, simulizi kuhusu maisha ya kijana mmoja, Yusufu mwana wa Yakobo kama inavyoelezwa kwenye Biblia imetumiwa katika kazi teule. Simulizi ya Biblia katika tamthiliya hii imeakisiwa namna hii;

17) WAIRIMU: Tom, *I admire your guts*.
*We ni muota ndoto kama Yusufu mwana wa Yakobo*.
MBOYA: Hiyo ni ndoto yangu. Ni mimba iliyo ndani ya Ubongo wangu...
(Uk. 49)

Kitabu cha Biblia kimesimulia hadithi ya kijana mmoja aliyeitwa Yusufu mwana wa Yakobo kutoka taifa la Israel. Yusufu mwana wa Yakobo amechorwa kama kijana mwenye uwezo mkubwa wa kuota na kufasili ndoto. Kipaji hicho kilimuwezesha hata siku moja akiwa nchi ya kigeni, Misri kuteuliwa kama Waziri Mkuu. Mfalme wa Misri, Bw. Faraoh, alimteua Yusufu kuongoza nchi baada yake baada ya kutafsiriwa ndoto aliyoiota. Simulizi za Yusufu zinapatikana katika Biblia, kitabu cha Mwanzo 37 – 50. Kuhusu uwezo wa Yusufu kuota ndoto Biblia imeeleza kwamba;

> "*Yusufu akaota ndoto, akawapa ndugu zake habari nao wakazidi kumchukia*."
> (Mwanzo 37:5)

Watheolojia wanaeleza kwamba, Biblia ilimtumia Yusufu kijana wa Yakobo kueleza nafasi ya maono katika mafanikio (Kimaro, 2015). Ndoto huanza kwanza ndani ya moyo wa mtu kisha baadaye inadhihirika waziwazi. Uwezo wa maono aliyokuwa nayo Yusufu umenasibishwa na maono yaliyoujaza mtima wa Tom Mboya, katika drama hii aliyoandika Emmanuel Mbogo. Hivyo simulizi hizi zinanasibiana.

Pamoja na hiyo, mtunzi katika tamthiliya ya Nyota ya Tom Mboya ametumia simulizi nyingine ya Biblia akimhusisha Nabii Musa. Simulizi za Nabii Musa zimerejewa namna hii;

> 18) NABII: *Naona maajab ya Musa*: Jeneza limeota mbawa.
> Jeneza limewaponyoka waombolezaji.
> Kwa mbawa imara kama Tai, Jeneza linapaa! Linapaa...
> (Uk. 55)

Maajabu ya Musa yanayorejewa na mhusika Nabii katika tamthiliya hii yamesimuliwa awali katika *Biblia* (Kutoka 6:28 – 7:7). Musa, alikuwa kiongozi wa taifa la Israel aliyeliongoza taifa kutoka utumwani Misri kurudi Kanaani, nchi

waliyoahidiwa na Bwana, Mungu wao. Katika harakati za ukombozi wa taifa hilo mikononi mwa Faraoh, mtawala wa Misri yalitokea maajabu mengi. Pia simulizi hizo zinaeleza kwamba, Israel wakiwa njiani, kurejea nchini kwao walikumbana na miujiza mbalimbali hata wakafika nchini mwao.

Baadhi ya maajabu ya Musa yanayoelezwa kutukia katika Biblia ni haya yafuatayo; Maji ya Mto Naili kugeuka rangi, kuwa mekundu, Vyura kujaa nchi yote ya Misri, Chawa kujaa nchi yote ya Misri, Nzi, Tauni kujaa nchi nzima. Wamisri wote kutoka majipu, kunyesha Mvua ya mawe, Nzige kujaa nchi nzima. Giza kukaa nchini Misri zaidi ya muda wa kawaida na kufa kwa watoto wa kwanza wa Wamisri, kila familia ikapata msiba. Katika Biblia simulizi kuhusu maajabu ya nabii Musa zimebainika namna hii;

> "Bwana akamwambia *Musa, ingia kwa Farao, ukamwambie Bwana asema hivi, Wape watu wangu ruhusa ili wapate kunitumikia. Tena kama akikataakuwapa ruhusa nitaipiga mipaka yako yote kwa kuleta Vyura; …*
> *Basi Haruni akanyoosha mkono wake juu ya Maji yote ya Misri, na hao Vyura wakakwea juu wakaifunika nchi ya Misri*"
> (Kutoka 8: 5 - 6)

Kimsingi, utafiti umebaini kuhusishwa kwa simulizi za Biblia katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya* (2016). Simulizi baina ya matini hizi teule zinahusiana. Kudhihirika kwa simulizi za Biblia katika tamthiliya teule ya *Nyota ya Tom Mboya* aliyotunga Emmanuel Mbogo kunathibitisha dai la Nadharia ya Mwingilianomatini kwamba, waandishi wa fasihi hutunga rnatini zao kutokana na matini za awali na wala hawaziandiki kutoka katika mawazo yao (Wafula, 2015). Kutokana na hili, matini mpya uhusisha kauli na tanzu kutoka matini nyingine za awali. Hivyo basi, matini zinaingiliana na kuathiriana pakubwa mathalani Biblia na tamthiliya ya Nyota ya Tom Mboya kama tulivyobainisha.

### 4. 2. 2. 4 Simulizi za Biblia katika Tamthiliya ya Tanzia ya Patrice Lumumba

Hali kadhalika katika matini teule tuliyotafiti, *Tanzia ya Patrice Lumumba* (2015) simulizi za Biblia zimerejewa na mtunzi. Tamthiliya hii inaeleza kuhusu ukombozi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Ukombozi wa taifa hilo unaelezwa kufanikiwa kupitia mauti ya mtu mmoja, aliyetoa maisha yake muhanga kuipigania Kongo, Patrice Lumumba. Mtunzi anaeleza kwamba, Patrice Lumumba aliutoa uhai wake, alimwaga damu yake ili nchi ya Kongo ipone. Simulizi ya Biblia kuhusiana na ukombozi wa kisiasa katika taifa la Msumbiji inasomeka hivi;

19) MOBUTU: Lumumba! Nimekuja kukuona kwa mara ya mwisho... *Imebidi mtu mmoja fedhuli afe kwa faida ya Wakongomani wote*..."
(Uk. 41)

Simulizi ya ukombozi wa Msumbiji kisiasa, inahusishwa na kisa cha ukombozi wa mwanadamu katika dini ya Wakristo hapa ulimwenguni. Mtunzi ameandika kuwa,

*"Imebidi mtu mmoja fedhuli afe kwa faida ya Wakongomani wote …"*

(Data Na. 20).

Tukisomwa kitabu cha Biblia, waandishi wameandika kwamba, hapo kale ili mwanadamu akombolewe kutoka kwenye dhambi zake ilipasa mtu mmoja afe kwa kuutoa uhai wake sadaka, asulubiwe hadi mauti. Mkombozi huyo ametambulishwa kama Yesu Kristo ndani ya kitabu cha Biblia. Mwandishi mmoja katika Biblia anaeleza hivi;

> "Mtu mmoja miongoni mwao, Kayafa, aliyekuwa Kuhani Mkuu mwaka ule, akawaambia, *Ninyi hamjui neno lo lote; wala hamfikiri ya kwamba yafaa mtu mmoja afe kwa ajili ya watu, wala lisiangamie*

> *taifa zima…*
> Wala si kwa ajili ya taifa hilo tu; lakini pamoja na hayo awakusanye watoto wa Mungu waliotawanyika, ili wawe wamoja. Basi tangu siku ile walifanya shauri la kumwua."
> (Yohana Mt. 11: 45 – 53)

Kwa jumla, matokeo yamebaini simulizi ya Biblia katika tamthiliya ya *Tanzia ya Patrice Lumumba*. Habari za ukombozi wa jamii kutaka mtu mmoja ajitoe muhanga, kutoa uhai wake ili kupambana kwa ajili ya jamii zimegeuzwa kutoka kwenye Biblia na kuingizwa na mtunzi katika tamthiliya teule tuliyotafiti. *Biblia* inaeleza kuwa Yesu Kristo alikufa kwa ajili ya kuwakomboa wanadamu wote ulimwengu mzima. Ukombozi wa Kongo unahusishwa na mauti ya Patrice Lumumba. Matini hizi zimehusiana katika kipengele hiki cha kifani, simulizi kuhusu ukombozi wa jamii za jamii za wahusika waliorejewa. Wahusika wote wawili walikufa kwa ajili ya kukomboa watu wa mataifa yao. Ni dhahiri kwamba, matini za fasihi ni mageuzi ya matini nyingine zilizotangulia. Mchakato huu hupelekea sifa za matini tangulizi kuonekana kwenye matini mpya.

### 4. 2. 2. 5 Simulizi za Biblia katika Tamthiliya ya Mtumwa hadi Siti Binti Saad

Vilevile mtunzi amerejea simulizi za Biblia katika tamthiliya ya *Mtumwa hadi Siti Binti Saad* (2016). Simulizi hizo zimebainishwa katika maonyesho mbalimbali katika tamthiliya teule. Katika tamthiliya ya Mtumwa hadi Siti Binti Saad, simulizi za Biblia zinadhihirika namna hii;

20) NONGWA: *Mungu kaliumba Jua lichomoze Mashariki lizame Magharibi; na wewe...*
(Uk. 39)

21) SITI: ... Lakini sina shaka kuwa;
*Mwenyewe Mwenyezi Mungu*
*Aijua thamani na kusudi la kumuumba mwanamke*
*Ni mwenyewe Mola wetu...*
(Uk. 56)

Tukirejea mazungumzo ya wahusika hawa; Nongwa na Siti tunabaini simulizi kuhusu uumbaji wa mwanadamu na vitu vyote vilivyomo humu ulimwenguni kutoka kwenye Biblia (Data Na. 21 & 22). Biblia inasimulia kwamba, mwanadamu aliumbwa na Mungu. Vitu vyote chini ya Jua viliumbwa na Mwenyezi Mungu. Kwa hivyo, Mungu ndiye mtengenezaji wa kila kitu. Simulizi kuhusu uumbaji wa mwanadamu inaeleza kuwa, kila mwanadamu aliyeumbwa na Mungu aliumbwa kwa kusudi maalum, wajibu maalum hapa duniani. Biblia imeeleza hivi;

> "*Hapo mwanzo Mungu aliumba mbingu na dunia. Dunia ilikuwa haina umbo tena ilikuwa tupu, giza lilikuwa juu ya uso wa vilindi vya maji, naye Roho wa Mungu alikuwa ametanda juu ya maji. Mungu akasema, "Iwepo nuru'' nayo nuru ikawepo. Mungu akaona ya kuwa nuru ni njema, ndipo Mungu akatenganisha nuru na giza. Mungu akaiita nuru "mchana'' na giza akaliita "usiku.'' Ikawa jioni ikawa asubuhi, siku ya kwanza*." (Mwanzo 1: 1 – 5)

> "*Mungu akasema na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakatawale Samaki baharini, na Ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila kitambaacho juu ya nchi. Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mkono wa Mungu alimuumba, mwanamume na mwanamke aliwaumba*."
> (Mwanzo 1:26 – 27)

Kimsingi, matokeo ya utafiti yamebaini simulizi za Biblia katika matini hizi teule. Simulizi kwenye Biblia, zinahusishwa na simulizi katika tamthiliya hii. Mtunzi anatujulisha kwamba Jua (Nyota kubwa inayowaka Mchana) na mwanamke (mwanadamu) muumbaji wake ni Mwenyezi Mungu. Hapana shaka tamthiliya hiyo na hayo yanayosemwa kuhusu uumbaji ni chipukizi la simulizi hizo katika Biblia.

Kujitokeza kwa simulizi hizo katika tamthiliya teule, kunathibitisha mhimili wa Nadharia ya Mwingilianomatini kwamba kazi za fasihi uhusiana kwa namna mbalimbali (Malugu, 2015). Biblia ilikuwepo kwanza kabla ya tamthiliya hii, mtunzi

akaihusisha katika imani yake. Katika uga huu wa utunzi wa kazi za fasihi, Biblia imejitokeza kwa namna nyingine katika tamthiliya teule kupitia kipengele hiki cha simulizi za Biblia kama tulivyowasilisha.

**4. 2. 2. 6 Simulizi za Biblia katika Tamthiliya ya Malkia Bibi Titi Mohamed**

Vilevile katika tamthiliya ya *Malkia ya Bibi Titi Mohamed* (2016) simulizi za Biblia zimerejewa ndani yake. Mtunzi amehusisha simulizi hizo kupitia mhusika mkuu. Mbogo akimtumia mhusika Bibititi anasema;

22) BIBITITI: Tunadai uhuru wetu kwa njia ya amani,
Hatutaki vita.
*Hatutuki umwagaji wa damu*.
Babu zetu mashujaa, akina Kinjeketile, walidai uhuru kwa vita vya Majimaji.
Babu zetu mashujaa, akina Mkwava, walidai uhuru kwa njia ya vita.
Nasi leo tunaitukuza na kuikumbuka damu yao iliyomwagika ili Mwafrika awe huru...
(Uk. 38)

Katika hotuba hii ya Bibi Titi, kuhusu kumwagika kwa damu ya babu zao, mashujaa iliyomwagika ili wakombolewe kutoka ukoloni mkongwe inanasibiana na simulizi za ukombozi wa taifa la Israel katika Biblia (Data Na. 23).

Ndani ya Biblia kuna simulizi imeelezwa kuhusu ukombozi wa mwanadamu hapa ulimwenguni. Simulizi inaeleza kuwa ili mwanadamu kukombolewa kutoka vifungo vya uovu ilipaswa mtu mmoja autoe uhai wake, afe. Mtu mmoja amwage damu yake kwa ajili ya wengi. Yesu Kristo ndiye aliutoa uhai wake, akamwaga damu yake, akafa kwa ajili ya wengi. Wayahudi wote wakahesabiwa kukombolewa huko Israel. Simulizi inasomeka namna hii katika Biblia;

> "Bali Mungu alionyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, *kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu*, tulipokuwa tungali wenye dhambi. Kwa maana ikiwa tulipokuwa adui, tulipokutanishwa na Mungu kwa mauti ya mwana wake; zaidi sana baada ya kupatanishwa tukaokolewa katika uzima wake."
> (Warumi 5: 8 – 11)

Kimsingi utafiti umebaini simulizi za Biblia katika tamthiliya hii. Mhimili wa Nadharia ya Mwingilianomatini unachagiza tubaini sababu za kujitokeza ama kuhusuiana simulizi katika matini teule tulizotafiti, Biblia na tamthiliya teule za Emmanuel Mbogo. Bakhtin (1895-1975) akirejelewa na Wafula (2015) anaeleza kuwa matini za fasihi uhusiana na matini nyingine za fasihi na hata watunzi tangulizi. Hivyo, matini moja inaweza kuwa inajibu ama kuendeleza matini za awali, matini za watunzi waliotangulia. Kazi za fasihi zinawasiliana na fasihi nyinginezo. Hivyo basi matini za mwanzo na sasa zinahusiana na zinaendelea kuathiriana. Kudhihirika kwa matumizi ya simulizi za Biblia, kuhusu ukombozi wa mwanadamu katika tamthiliya hii, *Malkia Bibi Titi Mohamed* kunathibitisha mhimili wa hii Nadharia ya Mwingilianomatini kama ulivyoelezwa na Bhaktin (1981).

### 4. 2. 2. 7 Muhtasari

Kimsingi, matokeo ya utafiti huu yamebaini kuwa, hakika kuna masimulizi ya Biblia katika tamthiliya teule zote kama tulivyobainisha. Tamthiliya teule za Emmanuel Mbogo zimeathiriwa na Biblia iliyoandikwa awali. Masimulizi yaliyoelezwa kwenye Biblia kuhusu uumbaji, ukombozi wa Israel (Wanadamu), usaliti, mapenzi na ndoa n.k. yanasikika pia katika tamthiliya teule. Emmanuel Mbogo ametumia simulizi za Biblia kuumba kazi zake. Kwa jumla, Biblia ni mama na tamthiliya teule ni watoto ndiyo maana simulizi zake zinanasibiana kama mhimili wa Nadharia ya Mwingilianomatini unavyoeleza.

### 4. 2. 3 Sajili ya Biblia katika Tamthiliya Teule

Katika taaluma ya isimu jamii, Sajili ni dhana inayorejea mitindo maalum ya lugha katika miktadha au hali mbalimbali (EasyElimu, 2022). Dhana hii inanasibishwa na rejesta, matumizi maalum ya lugha kuendana na shughuli pamoja na muktadha husika.

BAKITA (2022) wanaifasili dhana ya rejesta kama mtindo wa lugha yenye sifa na istilahi maalum kulingana na nyanja husika kama vile siasa, uchumi, tiba, umri, jinsi au kiwango cha elimu. Wanachosisitiza wanazuoni hawa ni kuwa matumizi ya lugha huathiriwa na mambo mbalimbali katika jamii. Mtindo wa lugha inayotumika mahakamani ni tofauti na mtindo wa lugha inayotumika kanisani ama msikitini kwenye nyumba za ibada.

Katika utafiti tuliofanya, tulitumia dhana ya sajili kurejea mitindo mbalimbali ya lugha iliyotumika katika kazi teule. Kwa hivyo, sajili ya Biblia imechukuliwa kama lugha inayozungumzwa na wahusika wa imani ya Kikristo, wanaotumia kitabu cha Biblia. Lugha hiyo huzungumzwa wakati wa ibada, sala katika nyumba za ibada au pahala pengine popote wanapozungumza mambo yanayorejea imani yao.

Amando (2022) akizungumza kuhusu dhana ya sajili ya Biblia anashadidia kwamba, lugha ya Biblia huwa na sifa zifuatazo;

- Misamiati ya Biblia
- Lugha ya upole
- Lugha sanifu
- Lugha ya matumaini

- Lugha iliyojaa sifa na tukuzo kwa Mungu
- Lugha ya shukrani kwa Mungu
- Taswira za Biblia (Dhahiri, Hisi au Mawazo)

Katika utafiti tuliofanya tulikuwa na lengo la kubainisha fani za Biblia katika tamthiliya za Kiswahili, tukitumia mifano kutoka tamthiliya za Emmanuel Mbogo. Hivyo, sajili ya Biblia, lugha ya Biblia ni kipengele kimojawapo tulichotafiti katika utafiti huu. Matokeo ya utafiti yamedhihirisha kwamba, Emmanuel Mbogo ametumia sajili ya Biblia katika kazi teule. Katika sehemu inayofuata, tumebainisha sajili ya Biblia ilivyojitokeza katika tamthiliya teule.

### 4. 2. 3. 1 Sajili ya Biblia katika Tamthiliya ya Mondlane na Samora

Katika utafiti huu, tulichunguza sajili ya Biblia katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora*, (2016). Mtunzi wa tamthiliya hiyo alitumia sajili ya Biblia kupitia mazungumzo ya wahusika wa drama hii. Lugha ya shukrani kwa Mungu na uteuzi wa misamiati yenye taswira za Biblia imebainika katika tamthiliya teule namna hii;

23) MONDLANE: ... Lakini huwezi kumuua binadamu *milele*.
Huwezi!
Lazima kuna siku *atafufuka*.
(Uk. 6)

Katika mazungumzo hayo, mhusika Mondlane anatumia lugha ya ushindi dhidi ya adui zake, Wakoloni wa Kireno (Data Na. 24). Wakoloni hao wanaangamiza watu wote wanaopigania uhuru wa jamii yao. Hata hivyo, mpigania uhuru Mondlane ametumia lugha ya tumaini na ushindi kuhusu kadhia inayomsibu. Kwamba, hata mpigania uhuru akiuawa, kuna siku ‘atafufuka’. Mtetezi huyo atapigana hadi ashinde na kuaza kujitawala mwenyewe, kama mzawa, mtu mweusi Afrika.

Katika Biblia kuna sajili zinazoeleza kuhusu kufufuka kwa mwanadamu, Yesu Kristo. Kwamba, Yesu Kristo alishuka kuwaokoa wanadamu. Katika simulizi hiyo, ilifika pahala akauawa na kuzikwa. Siku ya tatu alifufuka. Akawa hai. Biblia inaeleza;

> "*Lakini, ndugu, hatutaki msijue habari zao waliolala mauti, msije mkahuzunika kama na wengine wasio na matumaini. Maana, ikiwa twaamini ya kwamba Yesu alikufa akafufuka, vivyo hivyo na hao waliolala katika Yesu, Mungu atawaleta pamoja naye. ...*"
> (1Thesalonike 4: 13 – 17)

Mtunzi anaakisi taswira hiyo ya ufufuo kwa wapambanaji wote wanazipigania nchi zao. Dhana ya kufufuka, iliyosikika awali katika Biblia imehusishwa pia katika kazi hii teule ya Emmanuel Mbogo. Yesu Kristo, nabii wa Wakristo aliteswa na kuuawa lakini alifufuka siku ya tatu. Taswira za ufufuo zimehusishwa katika tamthiliya hii kama tulivyobainisha.

Pia mtunzi ametumia sajili zenye taswira ya Biblia akizungumza kuhusu ndoa. Mtunzi amenukuu maneno kutoka katika Biblia katika mazungumzo ya wahusika. Sajili za ndoa zimebainishwa hivi;

24) MONDLANE: *... arusi ya kuwaunganisha hawa wawili; Samora na Mondlane wawe mwili mmoja* itafanyika wiki ijayo hapa hapa msituni.
(Uk. 16)

Katika mazungumzo ya mhusika Mondlane hapo juu, mtunzi amejenga taswira ya ndoa kama inavyoelezwa katika Biblia (Data Na. 25). Watu wanaoona, huelezwa kuwa wamekuwa mwili mmoja. Taswira hiyo imeonekana kupitia mazungumzo ya Mondlane. Katika Biblia taswira hii imewasilishwa namna hii;

> "Kwa sababu hiyo mtu atamwacha babaye na mamaye, ataambatana na mkewe; na hao wawili watakuwa mwili mmoja; hata wamekuwa si wawili tena, bali mwili mmoja."
> (Marko 10: 7 – 8)

Hali kadhalika mtunzi ametumia misamiati yenye mwangwi wa Biblia katika bunilizi hii. Baadhi ya msamiati uliotumiwa ni Injili. Msamiati huu umetumiwa namna hii;

25) NUNGO: ... Ulimsikia Samora alivyoitetea *Injili* ya Ki-max kwa hamaki na jazba!?
(Uk. 25)

Katika mazungumzo baina ya wahusika wawili; Mondlane na Nungo kuna mwangwi wa Biblia (Data Na. 26). Mathalani dhana ya 'Injili' ya Ki-max. Katika Biblia dhana hii, Injili inaelezwa kama maandishi yenye mafunzo ya kidini katika sehemu ya Biblia yaliyoandikwa na wanafunzi waliokuwa wanaandamana na Yesu Kristo (Kamusi Kuu Karne 21, 2022). Baadhi ya vitabu vya injili katika Biblia ni injili ya; Mathayo Mtakatifu, Marko Mtakatifu, Yohana Mtakatifu na Luka Mtakatifu. Hivyo msamiati 'injili' una mwangwi wa Biblia.

Hali kadhalika mtunzi teule ametumia misamiati; shetani na kuzimu. Sajili hizo ni chipukizi la matini ya Biblia. Sajili hizi zimehusishwa namna hii;

26) NYERERE: Mkoloni, bila kukoma
Usiku hata mchana
Aliendelea, masikioni sumbu
Kututapikia: Wewe ni bwege. Wewe!
Si mtu
Ni kijitu
Ni kima
Ni panzi
Mnyoo
Jongoo!
...
Usimsikilize
Usimwamini
Ana shahada ya uongo
...
*Ni shetani toka kuzimu*
Ni nguruwe wa shamba la wanyama.
(Uk. 61 & 62)

Msamiati ‘kuzimu’ katika Biblia unaelezwa kama rumande ya watenda dhambi wote (Data Na. 27). Simulizi za Biblia zinaeleza kwamba, shetani alipofanya dhambi, kukiuka maagizo ya Mwenyezi Mungu huko Mbinguni alitupwa kuzimu, Jehanamu. Biblia inaeleza kwamba, kuzimu ndiko watakapotupwa wanadamu wote wanaovunja sheria za Mwenyezi Mungu wakiwa hapa duniani. Dhana ya kuzimu imeelezwa hivi katika Biblia;

> “Kisha nikaona Malaika akishuka kutoka Mbinguni, mwenye ufunguo wa kuzimu na minyororo mkubwa mkononi mwake. Akamshika yule *Joka, yule nyoka wa zamani ambaye ni Ibilisi na shetani,* akamfunga miaka elfu; akamtumpa *kuzimu,* akamfunga, akatia muhuri juu yake, asipate kuwadanganya mataifa tena, hata ile miaka elfu itimie na baada ya hapo yapasa afunguliwe muda mchache.”
> (Ufunuo 20: 1 – 3)

Kimsingi, matokeo ya utafiti yamebaini sajili za Biblia katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora* (2016). Nadharia ya Mwingilianomatini inaeleza kwamba, kazi za fasihi ni zao la matini nyingine zilizotangulia (Ponera, 2014). Kwa hivyo, kuonekana kwa sajili ya Biblia katika tamthiliya hiyo ni ithibati ya mhimili huu. Kwamba, tamthiliya hii ya *Mondlane na Samora* ni tokeo la matini ya Biblia iliyotangulia kabla kazi haijaumbwa. Mbogo, mtunzi teule katika utafiti huu alikutana na Biblia kwanza, kabla ya kubuni kazi yake. Hivyo tunaweza kuhitimisha kwamba, tamthiliya hii ni zao la matini ya Biblia kwa kupitia athari za sajili ya Biblia zilizobainika katika kazi teule tuliyotafiti.

#### 4. 2. 3. 2 Sajili ya Biblia katika Tamthiliya ya Wangari Maathai

Hali kadhalika katika kubainisha fani ya Biblia katika tamthiliya teule za Emmanuel Mbogo, utafiti huu ulichunguza pia sajili ya Biblia katika tamthiliya ya *Wangari Maathai* (2015). Mwandishi mteule ametumia sajili zenye mwangwi wa Biblia katika

tamthiliya hii. Sajili ya Biblia imehusishwa na misamiati ya Biblia, sajili za shukrani, sajili za matumaini n.k. Sajili hizo zimebainishwa hivi;

27) MWANGII: *You see!*
Uprofesa wako ndio unaokupa kiburi...
Mwanamume yeyote anahitaji *neema ya Mungu* ili kuyakumbatia mapenzi kama haya"
(Uk. 7)

Dhana 'Neema ya Mungu' katika maongezi ya mume wa Wangari, Bw. Mwangii inaakisi sajili ya Biblia. Msamiati 'neema' umetumika awali katika kitabu cha Biblia. Dhana hiyo huelezwa kama zawadi, kibali ambacho Mungu amempa mwanadamu bila kustahili kwa kumpatia msaada, wokovu kwa njia ya imani katika Kristo Yesu. Kwamba mwana huyo wa Mungu, Yesu Kristo aliutoa uhai wake kwa ajili ya wanadamu wote, wakombolewe kutoka utumwa wa dhambi zao. Kuhusu mafundisho ya neema ya Mungu, Biblia imeeleza kuwa;

> "*Basi tena, kama kwa kosa moja watu wote walihukumiwa adhabu, kadhalika kwa tendo moja la haki watu wote walihesabiwa haki yenye uzima.* Kwa sababu kama kwa kuasi kwake mtu mmoja watu wengi waliingizwa katika hali ya wenye dhambi, kadhalika kwa kutii kwake mmoja watu wengi wameingizwa katika hali ya wenye haki. Lakini sheria iliingia ili kosa lile liwe kubwa sana; na dhambi ilipozidi, neema ilikuwa nyingi zaidi; ili kwamba, kama vile dhambi ilivyotawala katika mauti, *vivyo hivyo kwa njia ya haki neema itawale hata uzima wa milele kwa Yesu Kristo Bwana wetu*."
> (Warumi 5: 18 – 21)

Msamiati 'neema' unaoelezwa katika tamthiliya teule ulitumika awali katika Biblia kueleza upendo mkuu wa Mungu kwa wanadamu (Data Na. 28). Mwandishi wa kitabu cha Warumi, Mtume Paulo anaeleza kuwa Mungu alimpendelea mwanadamu kitu kikubwa ingawa alikuwa muasi (Mastai, 2023). Hivyo dhana hii kuonekana kwenye tamthiliya sasa ni ithibati kwamba usuli wake umeanzia kwenye Biblia, kitabu kikongwe kabla ya tamthiliya teule.

Pia katika tamthiliya hii kuna sajili ya Biblia. Mtunzi ametumia lugha ya sifa na tukuzo kwa Mtume wa Wakristo, Yesu Kristo. Mtindo huo wa lugha umeakisi taswira ya Biblia ndani yake. Sajili hiyo imejitokeza nama hii;

28) WANGARI: *Tumsifu Yesu Kristo*!
ANGEL: Amina! Una shida gani na *sister*? ...
WANGARI: Alipokuja kusali leo Kanisani kwetu, nilimweleza shida yetu. Akasema nije leo. {KIMYA}
(Uk. 14)

Mtindo wa salamu wanaotumia wahusika katika salamu tajwa 'Tumsifu Yesu Kristo' hapo juu inaakisi tukuzo kwa Yesu Kristo, mtume wa waamini wa Kikristo (Data Na. 29). Sajili hiyo ni zao la Biblia. Waamini wa Kikristo, hasa wale wa Kanisa Romani Katoliki hutumia mtindo huo kusabahiana kwa namna hiyo kisha kufungua mazungumzo. Sajili hiyo inamsifu Yesu Kristo kwa matendo makuu mbalimbali aliyoyatenda kama waamini wanavyoelezwa katika Biblia. Mathalani kufanya miujiza mbalimbali kama vile, kuponya vipofu, viwete, viziwi, kufufua wafu, kufufuka kaburini n.k. Mfano. Yesu amponya kipofu Bartimayo. Biblia imeeleza;

> 'Wakafika Yeriko. Na Yesu alipokuwa akiondoka pamoja na Wanafunzi wake na umati wa watu, kipofu mmoja, jina lake Bartmayo, mwana wa Timayo, alikuwa ameketi kando ya njia akiomba…akaanza kupiga kelele, "Yesu, Mwana wa Daudi, nionee huruma!" …
> Yesu akasimama akawaambia,
> "Mwiteni." Wakamwita…
> Yesu akamuuliza, *"Unataka nikufanyie nini?"* Yule kipofu akajibu, "Mwalimu, nataka kuona tena."
> Yesu akamwambia, "*Nenda, imani yako imekuponya.*"
> Wakati huo huo akaweza kuona, akamfuate Yesu njiani.
> (Marko 10: 46 – 52)

Vilevile sajili ya Biblia kuhusu sifa na tukuzo kwa Mwenyezi Mungu imejitikoza katika onyesho lingine la tamthiliya ya *Wangari Maathai* . Mhusika mkuu, Wangari anamsifu na kumtukuza Mungu wake kwa uweza alionao. Wangari anajigamba

kwamba, Mola atawaponya watumwa wote. Huyo Mola anasifiwa kwamba, hasinzii wala halali. Yuko macho wakati wote kutazama wana wake. Wangari anasema;

29) WANGARI: ...
*Naye Mwenyezi Mungu atatenda makuu.*
Atazivunja nira zao za utumwa ...
Ndipo watakapotambua kuwa,
*Mungu wa Profesa Wangari Maathai*
*Halali wala hasinzii!*
(Uk. 53)

Sajili aliyotumia Wangari ilitumika awali kwenye Biblia (Data Na. 30). Kitabu cha Zaburi, alichoandika Mfalme Daudi (Mastai, 2023) kimehusisha sajili hizo za sifa na tukuzo kwa Mungu Mwenyezi. Mfalme Daudi ameonekana pahala pengi akimsifu Mwenyezi Mungu kwa matendo makuu aliyomtendea kwenye maisha yake. Muimbaji huyo, kama mtawala wa Wayahudi hapo kale kila anaposhinda vitani alisimama kuimba nyimbo za sifa na tukuzo kwa Mungu wao. Kwamba, kwa msaada wa huyo Mungu ndiyo wamefanikiwa kumshinda adui vitani. Daudi katika kitabu cha Zaburi ndani ya Biblia anasema;

"Msaada wangu utatoka wapi?...
*Asisinziye akulindaye;*
*Naam, hatasinzia wala kulala usingizi*,
Yeye aliye mlinzi wa Israel."
(Zaburi 121: 2 – 4)

Mungu wa Profesa Wangari Maathai, hasinzii wala halali. Muda wote yuko macho kulinda watu wake. Mungu wa Mfalme Daudi katika Biblia naye vivyo hivyo. Mungu Mwenyezi anayerejewa kwa ajili ya kulinda watu wake, yuko macho daima. Sajili hizi zinahusiana, kumpa Mungu sifa na tukuzo kwa ukuu na uweza wake kwa wanadamu aliowaumba.

Pamoja na hiyo mtunzi ametumia sajili ya shukrani kwa Mwenyezi Mungu katika tamthiliya hii ya *Wangari Maathai*. Sajili hii imedhihirika kupitia mazungumzo ya wahusika katika tamthiliya teule. Mathalani semi, “Asante Yesu”. Inaonyesha shukrani kwa Yesu Kristo, mtume wa waamini wanaotumia kitabu cha Biblia katika imani yao, Wakristo. Sajili hiyo imebainishwa hivi;

30) WANGARI: Asante. Vipi Muta?
MWANGII: Yuko salama na Njeri.
WANGARI: *Asante Yesu.*
(Uk. 32)

Katika tamthiliya ya *Wangari Maathai*, mtunzi amemchora mhusika Wangari kama mwanadamu mwenye kurudisha shukrani kwa Mola wake, Yesu Kristo kwa kuwaponya vijana wake, Muta na Njeri (Data Na. 31). Kitabu cha Biblia kinawaagiza waamini kurejesha shukrani kwa Mola wao kwa mambo mema mbalimbali anayowatendea kila uchao. Mafundisho kuhusu shukrani kwa Mola ndani ya Biblia yanaelezwa hivi;

> “*Ni neno jema kumshukuru BWANA*
> *Na kuliimbia jina lako, Ee uliye juu*
> *Kuzitangaza rehema zako asubuhi* ...”
> (Zaburi 29: 1 – 2)

Pamoja nazo, mtunzi wa tamthiliya hii ya *Wangari Maathai* (2015), Emmanuel Mbogo ametumia lugha ya kumtumaini Mola. Wahusika katika mazungumzo yao wanasawiri mtindo wa lugha hiyo. Mbogo anaeleza jamii kwamba, mwanadamu kila uchao hukumbana na changamoto mbalimbali maishani. Hata hivyo, anapaswa kuweka tumaini kwa Mola kwani ndiye huwa msaada kwa wanadamu dhidi ya kadhia mbalimbali wanazokabiliana nazo.

Mhusika mkuu Wangari, katika tamthiliya teule amechorwa kuwapa wanajumuiya wenzake moyo kwamba watashinda katika harakati zao za kupigania mazingira. Tumaini hilo limehusishwa na kufanya dua na sala za mfungo kwa Mola. Waumini wakiamini kwamba, Mola amewasikia na hivyo watashinda katika zoezi lililoko mbele yao. Wangari, kuhusu kuweka tumaini kwa Mola anasema;

31) WANGARI: "...
*Tutafunga kula na kunywa hata kama ni mwaka mzima.* Hadi tuusambaratishe mpango wa kujenga Skycraper pale Uhuru Park..."
(Uk. 37)

Sajili ya kumtumaini Mola imeelezwa pia katika vitabu mbalimbali ndani ya Biblia (Data Na. 32). Waumini wa dini ya Kikristo wanaotumia Biblia, wamefundishwa kufunga na kuomba kama ngazi ya kuwatoa kwenye teso, tatizo maishani. Waamini wanaelezwa kwamba, wakishafanya dua na sala, waishi kwa amani. Wakitumaini kwamba, Mola atawasaidia waondokane na dhiki hizo. Waandishi wa Biblia wameeleza hivi ujumbe wa kuweka tumaini kwa Mungu;

> Akawajibu, ''Kwa sababu ya imani yenu ndogo. Ninawaambia kweli, mkiwa na imani kama punje ndogo ya haradali, mtauambia mlima huu, 'Ondoka hapa uende pale' nao utaondoka. Wala hakutakuwa na jambo lisilowezekana kwenu.''
> *''Lakini hali kama hii haitoki ila kwa kuomba na kufunga.*''
> (Mathayo 17: 20 – 21)

Mtume Yesu Kristo hapo ameonekana kufundisha wafuasi wake kufanya dua na sala kwa Mwenyezi Mungu. Wafuasi wake wanaelezwa kwamba, hata mateso yawe magumu kwa uzito mkubwa kiasi gani, wafuasi wa Mwenyezi Mungu wakifanya dua na sala za kufunga watazipata suluhu.

Kimsingi, utafiti huu umebaini kuwa sajili ya Biblia imejitokeza katika tamthiliya ya *Wangari Maathai* (2015). Kwa nini sajili hizo zimejitokeza kwenye matini hii?

Nadharia ya Mwingilianomatini ina mhimili unaoeleza kuwa, matini za kifasihi hutokana na muathiriano wa kazi za kifasihi zilizotangulia na kusaidia katika uashiriaji wa kazi za baadaye (Senkoro, 2011). Hii ina maana kwamba, kazi zilizotangulia huathiri bunilizi mpya pia kazi hizo za fasihi zinaweza kutoa dira kwa kazi zinazofuata baadaye. Watunzi hukutana na kazi tangulizi kabla ya kuandika bunilizi zao. Hivyo vipengele vya kifani au kimaudhui vya matini hizo za awali, vinaweza vikajitokeza kwenye andiko wanalobuni. Mbogo aliisoma Biblia kwanza kabla ya kuandika kazi yake. Ndipo sasa watunzi wa kitabu hicho cha dini wamemuathiri kifani kupitia kipengele hiki cha simulizi kama alivyozirejea.

#### 4. 2. 3. 3 Sajili ya Biblia katika Tamthiliya ya Nyota ya Tom Mboya

Hali kadhalika mtunzi teule amerejea sajili za Biblia katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya* (2016). Sajili hizo zimewasilishwa kupitia mazungumzo ya wahusika a katika tamthiliya hii. Sajili za Biblia katika tamthiliya ya Nyota ya Tom Mboya zimedhihirika kwa namna mbalimbali kama ifuatavyo;

32) KANOGA: Wanjiru! Nimenusurika kifo pale ulipopiga kelele *“THE BLOOD OF JESUS”*
WANJIRU: *Ndiyo! Blood of Jesus!*
KANOGA: *Ghafla, kama mvuke, ule mzuka ukatoweka hewani.* (Uk. 46)

33) WANJIRU: {Anaingia ghafla. Kavaa nightdress. Kwa sauti ya kukemea}:
*BLOOD OF JESUS!!*
(Kufumba na kufumbua: Mzuka wa Abdulla unakimbia; muziki wa Kihindi unanyamaza na wote watatu wanamtazama Wanjiru kwa mshangao...
Ooh! Darling! (Uk. 59)

Mazungumzo baina ya wahusika tajwa; Kanoga na Wanjiru hapo juu katika tamthiliya teule, yana mwangwi wa sajili ya Biblia (Data Na. 33 & 34). Mtunzi ametumia lugha hii, *‘The Blood of Jesus’* yaani ‘Damu ya Yesu’ (TY) kama ishara ya

ushindi dhidi ya dhiki aliyokuwa ikimkabili mhusika, Kanoga. Ushindi huo umenasibishwa na sajili 'Blood of Jesus' kama kinga dhidi ya mzuka uliomtokea mhusika Kanoga.

Fauka ya hayo dhana ya *'Damu ya Yesu'* katika tamthiliya hii imetumiwa kama tashihisi. Katika Kiswahili, wanaisimu huifasili tashihisi kama tamathali ya semi inayorejea vitu visivyo na uhai kutenda kama wanadamu (Lyimbo, 2023). Katika Biblia, damu hiyo imepewa uwezo wa kutenda kama mwanadamu. Biblia imeeleza damu ya Yesu kama silaha dhidi ya magumu, vita yoyote wanayopitia wanadamu. Uweza wa damu ya Yesu unaelezwa hivi katika Biblia;

> "*Nao wakamshinda kwa Damu ya Mwanakondoo, na kwa neno la ushuhuda wao; ambao hakupenda maisha yao hata kufa*."
> (Ufunuo 12:11)

Fundisho kuhusu damu ya Yesu hapo juu katika Biblia, linahusisha habari za ndugu waliokuwa katika mapambano na Ibilisi shetani. Wapambanaji hao walipoiita damu ya Mwanakondoo yaani Yesu Kristo, huko vitani wakashinda.

Hivyo basi, sajili hizo kutokea kwenye tamthiliya hii ya Emmanuel Mbogo, ni tokeo la mafundisho hayo yanayopatikana katika Biblia. Mhusika anakiri ameushinda Mzuka baada ya mke wake kutamka 'The Blood of Jesus' (Data Na. 34) alipotokea wakati wa mapambano.

Vilevile sajili ya Biblia katika tamthiliya ya *'Nyota ya Tom Mboya'* imejitokeza kupitia mhusika, NABII. Mhusika huyu ametumia taswira, lugha ya picha lenye mwangwi wa Biblia ndani kwa kumtaja 'Nabii Musa' na 'Maajab ya Musa' kama wanavyoelezwa kwenye Biblia. Sajili imedhihirika hivi;

34) NABII: Naona maajabu ya Musa: Jeneza limeota mbawa. Jeneza
limewaponyoka waombolezaji.
Kwa mbawa imara kama Tai, Jeneza linapaa! Linapaa!
(Uk. 55)

Mazungumzo ya mhusika Nabii, yanadhihirisha sajili ya Biblia aliyotumia mtunzi katika tamthiliya teule (Data Na. 35). Mtunzi ametumia taswira 'Maajab ya Musa' inayojenga picha kuhusu maajabu ya Nabii Musa anayeelezwa kwenye kitabu cha Biblia. Biblia inaeleza kuwa Nabii Musa, alikuwa kiongozi wa Wayahudi hapo kale. Kupitia simulizi mbalimbali, Biblia inabainisha maajabu, miujiza lukuki iliyofanywa na Nabii Musa akiliongoza taifa la Israel. Ishara na maajabu ya Musa yalianzia katika harakati za kuwakomboa Wayahudi huko utumwani Misri ili warejea kwao Kanaani. Baadhi ya maajabu yanayoelezwa kutokea chini ya Nabii Musa ni haya yafuatayo;

**Jedwali Na. 4. 2: Kuonyesha Maajabu ya Nabii Musa huko nchini Misri**

| Ajabu la Musa | Kitabu cha Biblia |
|---|---|
| Maji ya Mto Naili kubadilika rangi na kuwa mekundu | Kutoka 6: 19 – 21 |
| Vyura kujaa nchi nzima | Kutoka 8: 1 – 8 |
| Chawa kujaa nchi nzima | Kutoka 8: 16 – 18 |
| Nzi kujaa nchi nzima | Kutoka 8: 20 – 24 |
| Vifo vya mifugo kwa ugonjwa wa Tauni | Kutoka 9: 1 – 7 |
| Raia wote wa Misri kutokwa na majipu | Kutoka 9: 8 – 12 |
| Mvua ya mawe kunyesha mfululizo | Kutoka 9: 13 – 26 |
| Nzige kujaa nchi nzima | Kutoka 10: 1 – 6 |
| Watoto wa kwanza kwa Wamisri wote kufariki | Kutoka 11: 1 – 9 |

**Chanzo: Biblia Takatifu – Tafsiri ya Ulimwengu Mpya (2017)**

Musa anayerejewa katuika tamthiliya hii teule, anahusianishwa na Musa aliyesimuliwa katika Biblia. Mtunzi ameakisi ushujaa wa Musa aliyetumiwa katika Biblia ndani ya tamthiliya hii (Data. 35).

Kimsingi, utafiti umebaini sajili za Biblia katika tamthiliya *Nyota ya Tom Mboya* kama tulivyowasilisha. Wahakiki wa Nadharia ya Mwingilianomatini wakiongozwa na Kristeva (1980) wanaeleza kuwa matini za fasihi zilizopita huathiri matini za fasihi zijazo kifani na kimaudhui. Hali hiyo ndiyo inakuwa ngazi kwa sajili ya matini moja kuonekana katika matini nyingine. Hivyo basi Biblia imetumiwa kuumba sajili mbalimbali katika tamthiliya teule. Kusikika kwa sajili ya Biblia 'Damu ya Yesu' iliyotumika awali katika Biblia na sasa kuonekana tena katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya* ni ithibati ya athari za kazi zilizopita kwa kazi zilizofuata baada yake**.**

#### 4. 2. 3. 4 Sajili ya Biblia katika Tamthiliya ya Tanzia ya Patrice Lumumba

Hali kadhalika mtafiti alichunguza tamthiliya ya *Tanzia ya Patrice Lumumba* (2015) ili kubaini sajili ya Biblia ndani yake. Matokeo ya utafiti huu yamebaini kwamba, mitindo ya lugha ya Biblia katika tamthiliya hii imejitokeza kwa jinsi mbalimbali. Mathalani; lugha ya sala na lugha ya matumaini. Sajili za Biblia zimedhihirika kwa namna mbalimbali. Mathalani;

Lugha ya sala, sala ni mazungumzo baina ya Mungu na mwanadamu (Mwakasege, 2018). Mwalimu huyo wa mafunzo ya Biblia anaendelea kutanabaisha kwamba, dhana ya 'sala' hutambulika pia kama maombi kwa Mwenyezi Mungu. Sala ndiyo njia anayotumia mwanadamu kuwasiliana na Mola wake huko Mbinguni. Katika kipindi cha sala au maombi, mtu hueleza mahitaji yake mbele za Mwenyezi Mungu. Sala huweza kufanywa pahala pa jumuiya (nyumba za ibada) ama sehemu ya pekee.

Lugha ya imetumiwa katika tamthiliya ya *Tanzia ya Patrice Lumumba*. Emmanuel Mbogo akimtumia mhusika Pauline ametumia sajili hiyo. Sajili hiyo imehusishwa namna hii;

35) PAULINE: *Fuzu la Kichwa cha Bikira Maria tuombe saa za uzima na saa za kufa kwetu.*
(Uk. 20)

Mazungumzo ya mhusika Pauline ni tokeo la sala ya waumini wa dini ya Kikristo (Data Na. 36). 'Fuzu la Bikira Maria' limepambwa katika nyumba za ibada na makazi kutani. Wafuasi wa dini huamini Maria ni mama mtakatifu asiye na doa wala waa lolote mbele ya Mwenyezi Mungu. Ndiyo maana wanamtumia awaombee.

Biblia inamweleza Bikira Maria kama mama wa Yesu Kristo, mtoto wa pekee wa Mwenyezi Mungu. Wafuasi wa dini ya Kikristo wamempa nafasi kubwa mhusika huyu kuwaombea mbele za Mungu kwani anaweza kuwasiliana na Mungu ana kwa ana. Vilevile Biblia inaeleza kuwa Mungu huwasiliana na Mariam, kupitia Malaika zake. Kwa mfano: Malaika Gabriel. Juu ya hayo Biblia imeandika hivi;

> "*Mariam akasema,*
> *Moyo wangu wamwadhimisha Bwana.*
> *Na roho yangu imemfurahia Mungu, Mwokozi wangu*
> *Kwa kuwa Bwana ameutazama unyonge wa mjakazi wake.*
> *Kwa maana tazama tokea sasa vizazi vyote vitaniita mbarikiwa*" (Luka 1: 46 – 48)

Kimsingi, sala anayofanya Pauline inawarejesha hadhira kwenye kitabu cha Biblia kukumbuka jinsi ya kufanya sala. Vilevile hadhira wanaweza kukumbuka namna ambavyo Mungu huwasiliana na waja wake kupitia Malaika kama vile Malaika Gabriel waliyemsoma kwenye Biblia. Hilo lilidhihirika Malaika Gabriel alipomtembelea Mariam huko Uyahudi ili kumjulisha habari za kumzaa mtoto wake, Yesu Kristo.

Zaidi ya hiyo mtunzi teule ametumia pia sajili ya lugha ya matumaini pia katika tamthiliya hii. Matumaini ni matarajio yenye furaha ya mambo mema yatakayotukia

baadaye (Meyer, 1967). Mhusika Pauline katika tamthiliya ya *Tanzia ya Patrice Lumumba* amechorwa kutangaza ushindi kwani amepewa nguvu mpya ya kupambana na maadui wote wa Kongo, wanaomtesa mume wake, Patrice. Pauline anajipa moyo kwamba atashinda harakati hizo za ukombozi wa nchi yake kwa kuwa, Bikira Maria, mama wa Mungu amesikia dua zake na kumwongezea nguvu ya mapambano. Sajili ya matumaini kwa Mola inasikika hivi;

36) PAULINE: *Nimeshamuomba Bikira Maria,*
*Naye amenivuvia moyoni mwangu roho saba mara sabini za*
*Simba wa Yuda.*
*Ujasiri na ushujaa wa kujitoa mhanga ili kumuokoa Baba wa watoto wangu, ninao*!!
(Uk. 44)

37) MAPANGALA: *{Akimtazama Pauline} Mungu akujaalie Mama.*
*Bila shaka Bikira Maria yupo pamoja nawe*
(Uk. 51)

38) PAULINE: ... Kwamba, kwa agano la damu hii ya Lumumba iliyotapakaa kote mwilini; *kwa kiapo changu kwa Mwenyezi Mungu na kwa Bikira Maria kwamba; huko uhamishoni tutakapohamia, hatutarejea tena na kukanyaga ardhi ya Kongo*.
(Uk. 53)

Lugha ya ushindi na matumaini ni chipukizi la Biblia. Mhusika Pauline na mwenzake Mapangala wamedhihirisha hilo (Data Na. 37, 38 & 39). Wao wanaamini kwamba, kwa kuwa wamefanya sala kwa Mwenyezi Mungu, 'Bikira Maria' akiwa pamoja nao basi watashinda vita iliyo mbele yao.

Biblia imehusisha sajili hii pia katika vitabu vyake. Wahusika mbalimbali waliokwenda vitani waliweka tumaini kwa Mwenyezi Mungu. Wapambanaji hao kabla ya kuiendea vita yoyote, katika taifa la Wayahudi walifanya kwanza sala, dua kwa Mwenyezi Mungu. Walimuomba Mola awafanikishe washinde vita iliyo mbele

yao. Wayahudi walipofanya hivyo, walishinda hizo vita. 'Simba wa Yuda' (Data Na. 73) ambaye Pauline anajigamba kumpelekea dua zake ili ampiganie amebainishwa kwenye kitabu cha Bilia namna hii;

> "Na mmoja wapo wa wale wazee akamwambia usilie. Tazama, *Simba aliye wa kabila la Yuda*, *Shina la Daudi*, yeye ameshinda apate kukifungua kile kitabu, na zile muhuri zake saba."
> (Ufunuo 5:5)

Simba wa Yuda anayerejewa katika Biblia anaelezwa kuwa mshindi dhidi ya vita iliyokuwa inamkabili Simba huyo amepambana hadi akachukua kitabu na muhuri saba kutoka kwa mpinzani wake. Kwa hivyo, anaonekana kama mpambanaji jasiri na shujaa katika vita zote ziwazo.

Kimsingi, utafiti umebaini sajili za Biblia katika tamthiliya *Tanzia ya Patrice Lumumba* (2015) kama tulivyobainisha. Lugha ya sala na lugha ya matumaini iliyotumika katika matini teule; *Tanzia ya Patrice Lumumba* na *Biblia* inathibitisha mahusiano baina ya matini hizi. Sajili ya Biblia iliyojitokeza awali kwenye matini ya Biblia imetumika tena kwenye tamthiliya teule. Bakhtin na Kristeva katika Nadharia ya Mwingilianomatini wanaeleza kwamba, ni kaida ya kazi za fasihi tangulizi kuathiri kazi zinazofuata kifani na kimaudhui. Mhimili huo umetusaidia kubaini sajili za Biblia katika tamthiliya teule. Pamoja na hayo tumeweza kueleza sababu za kutukia kwa sajili za Bibli, kazi tangulizi katika tamthiliya teule, kazi iliyofuata baadaye.

#### 4. 2. 3. 5 Sajili ya Biblia katika Tamthiliya ya Mtumwa hadi Siti Binti Saad

Vilevile sajili ya Biblia imeonekana katika tamthiliya teule ya *'Mtumwa hadi Siti Binti Saad' (2016).* Mtunzi ametumia sajili ya lugha ya matumaini, mhusika kutaraji

ushindi katika kadhia mbalimbali anazokutana nazo mwanadamu katika maisha. Vipengele vya lugha kama vile tamathali na misamiti yenye mwangwi wa Biblia ndani yake imetumika kuakisi hilo, watu wasikate tamaa katika maisha. Sajili hizo zimebainishwa namna hii;

39) ALI: *Sikiliza Mtumwa, Sauti unayo tena sauti* ya *Malaika ...*
(Uk. 28)

Katika mazungumzo ya mhusika huyu, mtunzi ameteua msamiati unaoakisi sajili ya Biblia, 'Malaika' (Data Na. 40). Mhusika Ali anamtia moyo mwenzake Siti kuhusu sauti aliyonayo. Sauti hiyo inanasibishwa na sauti ya malaika, kwa namna ilivyo nzuri na anavyoimba vizuri. Malaika wanaelezwa kama viumbe wa Mwenyezi Mungu wasioonekana (Kamusi Kuu Karne ya 21).

Katika Biblia, Malaika - Maserafi ni viumbe wa Mwenyezi Mungu ambao kazi yao ni kumwimbia Mungu muda wote, saa ishirini na nne. Biblia inaeleza kuwa, Malaika hao humwimbia Mungu kwa kupaza sauti zao bila kukoma wakisema;

> *"Katika mwaka ule aliokufa mfalme Uzia nalimwona Bwana ameketi katika kiti cha enzi, kilicho juu sana na kuinuliwa sana, na pindo za vazi lake zikalijaza hekalu. Juu yake walisimama maserafi; kila mmoja alikuwa na mabawa sita; kwa mawili alifunika uso wake, na kwa mawili alifunika miguu yake, na kwa mawili aliruka. Wakaitana, kila mmoja na mwenzake, wakisema, Mtakatifu Mtakatifu, Mtakatifu, ni Bwana wa majeshi, dunia yote imejaa utukufu wake".*
> (Isaya 1: 1 - 3)

Katika dini ya Kikristo kuna mapokeo kwamba, Maserafi ni malaika wenye sauti nzuri sana. Hivyo jamii inamnasibisha mtu yeyote anayeimba vizuri, kwa sauti nzuri na viumbe hao wa Mwenyezi Mungu. Nabii Isaya katika kitabu cha Biblia ametumiwa kushadidia hilo kama tulivyoona rejea kwenye kitabu chake.

Pamoja na hayo, mtunzi Emmanuel Mbogo ametumia pia lugha yenye sifa za Biblia, lugha ya matumaini kwa Mola. Mhusika mkuu katika tamthiliya hii, Siti binti Saad anapokumbana na mgogoro mkubwa katika ndoa yake, amechorwa kumtegemea Mola ama kumuita Mola ili amfae katika dhoruba hiyo. Siti anashutumiwa na mume wake kwamba alifanya zinaa wakati mume wake akiwa safarini. Siti akifahamu fika kwamba, dai hilo ni uongo anamhusisha Mola amsaidie, amtetee katika dhiki hiyo ili mume wake aamini anachosema. Sajili ya matumaini kwa Mola imebainika hivi;

40) SITI: *Nataka kumuomba Mola ombi la kipumbavu kuwa; Azitie pumzi za uhai kuta hizi ziseme, zinisute, zishuhudie juu ya unajisi na ukware wangu.*
*Kama kweli niliacha maua ya mume wangu yakatafunwa na wadudu wa mjini, ama kumeng'enywa na Ngedere wa mwituni.*
(Uk. 56)

Sajili ya Biblia uhusisha lugha ya matumaini kwa Mola, kwamba jambo jema lilatukia hapo baadaye kwa msaada wa Mola (Data Na. 41). Lugha ya namna hiyo imetumika katika vitabu vingi, kati ya vitabu vingi vilivyomo ndani ya Biblia. Waandishi wengi wanaweka bayana kuwa Mola ndiye muweza wa yote na anaweza kumtetea mtu katika shtaka lolote lililo mbele yake. Katika kufanya hilo, Mola anaweza kutumia kitu chochote. Mtunzi ametumia tashihisi 'kuta kuongea' kuakisi hilo. Mhusika mkuu, Siti anaamini kuwa, Mwenyezi Mungu anaweza kuzitumia kuta kumtetea, kuongea mbele za mume wake kwamba hakuwahi kufanya zinaa (Data Na. 41).

Katika Biblia kuna kisa cha kuta za mji wa Yeriko kuvunjika zenyewe bila kuguswa na mtu ili Wayahudi, taifa la Israel liingie mjini Yeriko. Kuta hizo zilijengwa kuzunguka mji wa Yeriko. Israel wakiwa safarini kutoka Misri walipofika Yeriko

walishindwa kuingia katika mji. Biblia inaandika, walipomuomba Mola wao, walipewa agizo wauzunguke mji siku saba, kisha kuta zikaanguka zenyewe pasina kutumia kifaa chochote na wao wakaingia kwa salama. Sajili ya tumaini kwa Mola kupitia Wayahudi ilielezwa hivi katika Biblia;

> *"Siku ya saba mzunguke mji mara* saba. *Kisha mpige sauti ndefu ya tarumbeta zenu, na kila mtu apige yowe kuu ya vita. Kuta zitaanguka chini kabisa!"*
> (Yoshua 6: 1 – 25)
>
> "*Na kuta za Yeriko zilianguka kwa ajili ya imani ya watu wa Mungu. Walitembea kuuzunguka ukuta kwa siku saba; na kisha kuta zikaanguka."*
> (Ebrania 11:30)

Biblia inaeleza kuhusu mapambano waliyopitia Wayahudi waliposhindwa kuingia katika mji wa Yeriko. Hata hivyo walipomuomba Mola, walipewa maelekezo na suluhu ya shida yao ikapatikana. Kuta za mji zikavunjika nao wakaingia. Kumbe tumaini lao kwa Mola liliwasaidia.

Vilevile mtunzi ametumia misamiati yenye taswira za Biblia ndani ya tamthiliya ya *Mtumwa hadi Siti Binti Saad* (2016). Mathalani neno 'dhambi' ni dhana inayorejea tendo au wazo lolote linalopingana na maagizo ya Mwenyezi Mungu (Mhombo, 2023). Dhana hii imebainishwa kupitia mazungumzo ya mhusika Khamis. Sajili yenye taswira za Biblia katika matini hii imehusishwa hivi;

41) KHAMIS: *Siwezi!... kwa viapo vyako batili na kulitaja jina la Mwenyezi Mungu: Waweza kufuta dhambi za uhayawani wako?*
(Uk. 56)

Msamiati 'dhambi' una taswira ya Biblia. Katika Biblia dhana hii 'dhambi' imefasiliwa kama uvunjaji ama ukiukaji wa maagizo ya Mwenyezi Mungu (Biblica, 1989). Dhana hii imetumika awali katika kitabu cha Biblia, sasa imeonekana katika

tamthiliya teule tuliyotafiti, *Mtumwa hadi Siti Binti Saad*. Biblia inaieleza dhambi hivi;

> *"Kila atendaye dhambi afanya uasi"*
> (1 Yohana 3: 4)
>
> "*Kila lisilo haki ni dhambi na dhambi ipo isiyo ya mauti"*
> (1Yohana 5: 17)

Dhana 'Dhambi' inavyorejewa katika tamthiliya teule (Data Na. 43) na Biblia (Data Na. 83) inahusiana. Dhana hii imepewa taswira ya uasi, uovu katika matini zote teule. Biblia ndiyo mzaliwa wa kwanza, tamthiliya teule ni mzaliwa wa pili. Hivyo basi mtunzi teule aliichota dhana hiyo kutoka kwenye Biblia akaitumia katika kuumba kazi yake.

Kimsingi, matokeo ya utafiti yamebaini sajili za Biblia katika tamthiliya ya *Mtumwa hadi Siti Binti Saad* (2016). Nadharia ya Mwingilianomatini ina mhimili unaoeleza mahusiano baina ya kazi za fasihi kifani na kimaudhui. Wahakiki hawa wanaaamini kuwa matini za fasihi zilizopita zinaingiliana na kuchagizana na matini mpya, hivyo kuamini kuwa matini ya kifasihi inajitegemea ni kupotoka (Kristeva, 1960). Wahakiki hawa wanaendelea kueleza kuwa, matini mpya hufaidi kutoka kwenye matini zilizotangulia. Kwamba, watunzi huchukua vipengele vingi vya kifani na kimaudhui katika kazi tanguzi na kuvitumia katika kuumba kazi zao mpya. Kwa sababu ya mchakato usemezano baina ya matini za kifasihi haukwepeki. Wafuasi wa Nadharia ya Mwingilianomatini wametusaidia kubainisha sajili za Biblia na sababu za kujitokeza kwake katika tamthiliya teule tuliyowasilisha.

#### 4. 2. 3. 6 Sajili ya Biblia katika Tamthiliya ya Malkia Bibi Titi Mohamed

Vilevile katika utafiti huu tulichunguza tamthiliya ya *Malkia Bibi Titi Mohamed* (2016) ili kubaini sajili ya Biblia. Katika tamthiliya hii teule, sajili ya Biblia imejitokeza katika mitindo mbalimbali kama vile lugha ya matumaini na taswira ya mwanamke. Lugha ya matumaini kwa Mwenyezi Mungu ni mazungumzo yenye taswira ya faraja anayokuwa mwanadamu kwa dhiki anayopitia akitumaini kwamba, iko siku atapata suluhu dhidi ya teso hilo linalomsibu katika maisha yake (Mangare, 2023).

Katika tamthiliya hii, mtindo huu umedhihirika kupitia mazungumzo ya mhusika Bibi Titi. Mhusika huyo katika jitihada za kupigania ndoa yake kuzama anamsihi Mola amwokoe na teso hilo. Vilevile Bibi Titi anatangaza kwamba, huyo Mola anayemuomba atamtetea na shida inayomkabili kwenye ndoa itaisha. Sajili hii ya Biblia imebainika hivi;

42) BIBI TITI: *Kwa Jina la Mwenyezi Mungu*;
*Yeye mwenyewe Rabana aliyeniumba ndiye atakuwa mtetezi wangu*.
*Yeye Mola wangu ajuaye siri na mafumbo yaliyoko chini ya vilindi vya bahari, ndiye wakili na Hakimu wangu.*
(Uk. 3)

Bibi Titi katika teso lake anaamini kwa mkono wa Mola atashinda (Data Na. 43). Mhusika huyo anaamini Mwenyezi Mungu, aliyemuumba yeye ndiye atamtetea katika kesi zinazomkabili hapa ulimwenguni. Mbogo anafundisha watu kuweka tumaini kwa Mwenyezi Mungu.

Katika Biblia sajili kama hii inajitokeza katika vitabu mbalimbali. Wanadamu mbalimbali wamechorwa kuwasilisha tumaini lao kwa Mwenyezi Mungu. Mtu mmoja, Ayubu alipita kwenye mahangaiko mengi ya maisha, magonjwa n.k. lakini akaweka tumaini kwa Mwenyezi Mungu hadi akashinda na kurejea kwenye hali ya maisha ya kawaida, yenye furaha na amani. Biblia inaandika;

> "Lakini mimi najua ya kuwa *Mteteaji wangu yu hai, Na ya kuwa hatimaye atasimama juu ya nchi. Na baada ya ngozi yangu kuharibiwa hivi, Lakini, pasipokuwa na mwili wangu nitamuona Mungu*."
> (Ayubu 19:25 – 26)

Pamoja na hayo katika tamthiliya hii, sajili ya lugha ya matumaini katika tamthiliya teule inadhihirika. Bibi Titi anaeleza thamani ya wanawake waliotumaini Mungu katika maisha yao. Wanawake hao walipewa fursa ya kutenda mambo makubwa katika jamii zao. Bibi Titi anawatia moyo wanaharakati wenzake kwamba, kwa kuwa Mungu amewakirimia vitu vingi vizuri, basi hata nchi yao kukombolewa kupitia wao inawezekana. Wamtumaini tu Mola wao. Bibi Titi anasema;

43) BIBITITI: ...
*Mungu ametupa wanawake mamlaka*
*Mungu ametupa matumbo ya kutunza uhai, vifaa vya kuwanyonyeshea*
*Na migongo ya kuwabeba wana*"
(Uk. 31)

BIBITITI: Mungu amepanda mbegu ndani mwetu
Natazama: Mbegu imeota
*Mungu ametupa uwezo huu*,
Bila ushirikiano wetu, hatutapata uhuru."
(Uk. 31)

Wanawake wanaomsikiliza Bibi Titi wanatiwa moyo mkuu, wainuke kuipambania nchi yao (Data Na. 44). Hilo linachagizwa na wajibu mkubwa aliowapa Mwenyezi Mungu kufanya shughuli mbalimbali katika maisha. Mfano, kuzaa na kulea watoto.

Yote hayo yanaelezwa kutolewa na Mungu kwa vile anamthamini na kumwamini mwanamke. Hivyo wamtumaini Mola, wainuke wapambane nchi yao ipate uhuru.

Biblia inawatambulisha wanawake kama jeshi kubwa, ambao wakishikamana wanaweza kufanikisha nia yoyote waliyonayo. Mfalme Daudi katika utawala wa Wayahudi huko Israel, anadhihirisha hilo katika kitabu cha Zaburi akisema,

> *"Wanawake watangazao habari njema, ni jeshi kubwa."*
> (Zaburi 68:11)

Katika Biblia kumeelezwa wanawake mbalimbali walioshiriki katika jitihada za ukombozi katika jamii zao. Wanawake waliaminika kama wapambanaji ambao wakitia nia, hawageuki nia. Kielelezo kifuatacho kimeeleza habari za wanawake katika Biblia na mambo waliyoyafanya katika jamii zao.

**Jedwali Na. 4. 3 Wanawake Waliotumika Kufanya Mambo Makubwa Katika Jamii Zao Katika Biblia**

| **Jina la Mwanamke** | **Kitabu katika Biblia** | **Wajibu Aliofanya** |
|---|---|---|
| Mariam Magdalena | Luka 8:1-3 | Kutegemeza kazi ya Yesu Kristo duniani |
| Sarah | Mwanzo 17:17; 21:2-5 | Kumzalia Ibrahim, Baba wa Imani ya Kikristo, mtoto Isaka. |
| Malkia Esta | Esta 3:13-15; 4:1, 5<br>Esta 4:10-16; 7:1-10 | Kulikomboa taifa la Israel |
| Rahabu | Yoshua 2:1-24;<br>Waebrania 11:31. | Kuhifadhi Wapelelezi wa Israel |
| Debora | Waamuzi 4:24; 5:31 | Unabii na Ulinzi wa Israel |

**Chanzo: Biblia Takatifu – Tafsiri ya Ulimwengu Mpya (2017)**

Kwa jumla, matokeo ya utafiti yamebaini sajili za Biblia katika tamthiliya ya *Malkia Bibi Titi Mohamed* (2016). Mhimili wa Nadharia ya Mwingilianomatini unaeleza kuwa, watunzi wa kazi za fasihi hugeuza matini tangulizi ili kuumba kazi zao mpya (Kristeva, 1960). Matokeo ya utafiti yamebaini kwamba, mtindo wa lugha iliyotumika katika tamthiliya ya *Malkia Bibi Titi Mohamed* unahusiana na mtindo uliotumika katika Biblia, hapo kwanza. Wahusika Bibi Titi na Mfalme Daudi katika vitabu teule, wanafanya jambo moja kuhusu mwanamke. Wanamtia moyo kupambana katika vita inayomsibu, kwamba siku moja ushindi upo! Asikubali kurudi nyuma bali asonge mbele na mapambano hadi ashinde vita yake.

#### 4. 2. 3. 7 Muhtasari

Kimsingi, utafiti huu umebaini kwamba, sajili ya Biblia katika tamthiliya teule zote tulizotafiti. Mtunzi teule kwa jinsi moja ama nyingine amerejea sajili hizo kama zinavyotumika awali katika Biblia. Wahakiki wa Nadharia ya Mwingilianomatini wanaeleza kuwa, matini za fasihi huchota ama kugeuza matini tangulizi wakati zinapobuniwa na watunzi kipindi kinachofuata. Mageuzi hayo uhusianisha na muktadha wa jamii mpya walizomo watunzi mahsusi. Mwandishi teule, Emmanuel Mbogo aliisoma Biblia awali, ndipo akaandika kazi zake. Hivyo, anaigeuza matini asili Biblia kwa namna mbalimbali ili kuzipata matini mpya, tamthiliya teule zinazoendana na jamii aliyomo sasa.

### 4. 2. 4 Wahusika wa Biblia katika Tamthiliya Teule

Njogu & Chimerah (2011) wanafasili wahusika kama viumbe wa sanaa wanaobuniwa kutokana na mazingira ya msanii. Pamoja na hayo kipengele hiki

hutambulishwa kama sehemu ya fani katika sanaa. Wanazuoni hawa wanaendelea kueleza kuwa mtunzi hubuni wahusika kutokana na dhamira anazotaka kufikisha kwa hadhira. Hivyo basi wahusika wanafasiliwa kama viumbe katika kazi ya fasihi ambao wanatokana na mawazo ya mwandishi au mtunzi wa kazi ya fasihi. Viumbe hao huumbwa kwa lengo la kufikisha ujumbe wa mtunzi kwa hadhira yake.

Mulokozi (2017) anafasili wahusika katika bunilizi za fasihi kama binadamu na viumbe wa aina nyingine au vitu visivyo na uhai ambavyo hutumika katika kazi za fasihi kutokana na fani husika na lengo la mtunzi. Mwanazuoni huyu anazidi kushadidia kwamba, wahusika ndiyo watendaji wakuu katika kazi za fasihi. Ili kazi ya fasihi iweze kuibuka, kusonga mbele na kufika hatma, inahitaji wahusika katika kufanikisha hilo. Kupitia mwanazuoni huyu tumebaini kwamba, wahusika ni kipengele muhimu cha kifani katika kazi za fasihi.

Lyimo (2018) anaeleza dhana ya wahusika wa kifasihi namna hii, "Wahusika wa kifasihi ni watendaji au watendwaji wa kazi ya fasihi. Hawa wanaweza kuwa binadamu, wanyama wengine wasio na urazini, ndege, wadudu, mimea, mawe, upepo na kadhalika. Kimsingi, wahusika katika fasihi wanaweza kuwa viumbe wenye uhai au wafu ambao katika fasihi uhaishwa ili kutumiwa katika kazi za fasihi kwa lengo fulani.

Vilevile mwanazuoni huyo anaendelea kueleza kwamba, wahusika hupewa uhusika kulingana na kile alichokusudia kuwasilisha mtunzi. Mtunzi ndiye huamua awatumie kwa jinsi gani wahusika katika kazi yake kulingana na kile anachotaka kuwasilisha kwa hadhira husika.

Mboka (2018) anamueleza mhusika kama mtendaji au kiumbe katika kazi za fasihi. Mhusika ndiyo nguzo msingi ya dhamira za kazi ya fasihi. Kupitia wahusika, mtunzi hufikisha dhamira zake alizokusudia kwa hadhira lengwa. Mwanazuoni huyu anaendelea kudadavua kuwa, wahusika hutumika kuwasilisha hali halisi za maisa ya binadamu katika jamii mahsusi.

Kimsingi, dhana ya wahusika tunaweza kuifasili kama binadamu, wanyama, ndege au viumbe mbalimbali ambao hubuniwa na mtunzi wa fasihi ili kubeba ama kuwasilisha dhamira fulani kwa jamii lengwa. Binadamu, wanyama au viumbe hao hutumika kama kioo tu, kwamba huwakilisha binadamu halisi katika jamii. Hivyo, mtunzi anaweza kuwabuni ama kuwapanga apendavyo kutoka na lengo alilokusudia hadhira yake ilipate. Wahusika ndiyo watendaji wa matukio yote katika simulizi bunilizi za mdomo au maandishi.

Utafiti huu ulikuwa na malengo mahsusi ya kubainisha fani za Biblia katika tamthiliya teule na kueleza sababu za kujitokeza katika bunilizi hizo. Matokeo yalibaini kwamba wahusika wa Biblia wametumika kujenga wahusika katika tamthiliya teule, yaani binadamu au viumbe watendaji waliotumika awali katika kitabu cha Biblia katika vitabu vyake vidogo vidogo 66. Zama hizi watendaji hao wa Biblia wanaonekana tena katika bunilizi teule.

Utafiti umebaini kwamba Emmanuel Mbogo, mtunzi teule ametumia wahusika wa kibiblia katika kuumba kazi zake tulizotafiti. Katika maonyesho na sehemu za tamthiliya hizi teule, fani hii inadhihirika. Kuna kufanana kwa sehemu kubwa kwa wahusika waliotumika katika Biblia na hawa waliotumika sasa katika tamthiliya

teule. Katika sehemu inayofuata tunabaisha wahusika mbalimbali wa Biblia waliojitokeza katika tamthiliya teule.

### 4. 2. 4. 1 Wahusika wa Biblia katika Tamthiliya ya Mondlane na Samora

Fani ya wahusika wa Biblia katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora* (2016) ihusishwa pia. Wahusika wenye mwangwi wa wahusika kutoka katika vitabu mbalimbali kutoka katika Biblia wamebainishwa katika tamthiliya hii. Katika sehemu inayofuata tumebainisha wahusika hao, waliotumika awali katika Biblia na sasa wamejitokeza tena katika drama hii aliyoandika Mbogo miaka 3000 baadaye tangu Biblia iandikwe.

Katika tamthiliya hii, mhusika mkuu, Nyerere, rais wa kwanza wa Tanganyika (sasa Tanzania) ametumika kwa taswira ya Nabii Musa. Nabii huyo alikuwa kiongozi wa taifa la Israel aliyewaongoza kutoka utumwani Misri kurejea katika nchi yao Kanaani. Mhusika Nyerere aliiongoza Tanzania kupata uhuru kutoka kwa Wakoloni, Waingereza mwaka 1961. Mtunzi teule ameandika hivi;

44) NYERERE: *Tunaapa bila ajizi!*
*Tutapambana na Walowezi*
*Kwa ajili ya chetu kizazi*
*Kuishi kwa utukufu na enzi.* (Uk. 61)

45) NESI: *[akicheka] Unajua hata hapa Dar watu wamembatiza;*
*Wanamwita Nyerere Nabii Musa.*
*Anatupeleka Kanaani, nchi ya asali na maziwa.*
(Uk. 88)

Mhusika maarufu katika jamii ya Wayahudi, Nabii Musa amerejewa katika mazungumzo ya wahusika katika tamthiliya teule (Data Na. 45 & 46). Musa, amenasibishwa na Nyerere, kiongozi wa kwanza wa taifa la Tanganyika, sasa Tanzania.

Katika Biblia, mhusika Nabii Musa ni kiongozi mashuhuri wa Wayahudi huko Israel. Kiongozi huyo ametumika zaidi katika Biblia, vitabu vya Agano la Kale. Musa alichaguliwa na Mungu kuwaokoa Waisrael kutoka utumwani Misri. Taifa hilo la Wayahudi lilichukuliwa utumwani Misri baada ya kukumbwa na janga kubwa la njaa katika nchi yao, hivyo wakakimbilia Misri kupata vyakula kuokoa maisha yao.

Biblia inaeleza kuwa, Waisrael walikaa utumwani Misri miaka 430 (Kutoka 12:40). Baadaye Mwenyezi Mungu alimsimamisha kiongozi kati yao, Nabii Musa awaongoze Israel kupambana na mtawala wa Misri, Farao. Vita yao ilifanikiwa baada ya mapambano mbalimbali yaliyochukua kitambo kikubwa. Biblia imeeleza kuwa;

> "*Bwana akasema na Musa, akamwambia, Ingia ndani useme na Farao, Mfalme wa Misri, ili awape ruhusa wana wa Israel watoke nchi yake."*
> (Kutoka 6: 10 – 11)
>
> "*Farao akaondoka usiku, yeye na watumishi wake wote; na Wamisri wote... Akawaita Musa na Haruni usiku, akasema, Ondokeni tokeni katika watu wangu, ninyi na wana wa Israel, enendeni mkamtumikie Bwana kama mlivyosema.*"
> (Kutoka 12: 30 – 31)

Nabii Musa katika Biblia hapo juu anaelezwa kama kiongozi taifa la Israel ayeshirikiana na wenzake; Haruni, Yoshua na Kalebu kulikomboa taifa hilo kutoka utumwani. Viongozi hao walipambana hata taifa lao likakombolewa kutoka pingu za utumwa Misri. Hatimaye wakarejea nchini kwao, Kanaani nchi iliyojaa asali na maziwa.

Kimsingi, nafasi aliyocheza mhusika Nyerere katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora* inahusiana na uhusika wa Nabii Musa katika Biblia. Katika tamthiliya teule

mtunzi amebainisha hata baadhi ya zana alizokuwa akitumia Nabii Musa kupambana na Farao, Mtawala wa Misri ambazo Nyerere naye anazitumia anapopambana na Waingereza akidai uhuru wa Tanganyika. Mfano: ‘Fimbo ya miujiza’.

Mhusika Nyerere pia amechorwa kuwa na fimbo mkononi yenye uwezo wa kutenda ishara, maajabu mbalimbali. Wahusika hawa wanashabibiana kifani na kimaudhui. Wote wamechorwa kama waasisi wa ukombozi wa kisiasa katika mataifa yao. Tazama mizungu ya fimbo ya Mwalimu Nyerere;

46) *“…Nyerere alimshika Samito, akainua kafimbo kake juu na mara wakayeyuka.”*
(Uk. 86)

Fimbo ya mhusika Nyerere inamsaidia kupona maangamizi yaliyoko mbele yake kwa kumyeyusha yeye na jamaa yake, Samito (Data Na. 47). Uwezo wa fimbo ya Nyerere katika tamthiliya teule unashabihiana na fimbo ya Nabii Musa, katika Biblia.

Kimsingi, matokeo ya utafiti yamebaini wahusika wa Biblia katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora*. Mwingilianomatini ni mbinu, stadi ama taaluma na mwongozo wa uchunguzi wa matini kisayansi, hususani kazi za kisanaa na zisizo za kisanaa ili kubaini kuwepo kwa athari ya uchopekaji ama usemezano; yaani kufanana kifani, kimaudhui na kimbinu kati ya matini moja na nyingine (Masatu na wenzake, 2020). Watafiti hawa wanaendelea kueleza kwamba, ufanano huo huweza kuwa wa moja kwa moja au kuwapo kwa ukaribiano. Mwingiliano huo hutambulika pia kama mwangwi wa kazi tangulizi katika kazi mpya iliyobuniwa baadaye. Hivyo mahusiano ya wahusika wa fasihi katika Biblia na tamthiliya teule tulizotafiti katika utafiti huu ni athari ya kitabu cha Biblia katika tamthiliya teule.

**4. 2. 4. 2 Wahusika wa Biblia katika Tamthiliya ya Wangari Maathai**

Hali kadhalika wahusika wa kibiblia wamerejewa katika tamthiliya ya *Wangari Maathai* (2015). Katika sehemu hii tumebainisha wahusika wa Biblia waliohusishwa katika tamthiliya teule. Pia tumeeleza sababu za kujitokeza kwa wahusika hao katika hiyo.

Mtunzi wa tamthiliya ya *Wangari Maathai*, amemtumia mhusika Pastor Njoya kwa nafasi ya Nabii Samweli (*Biblia*). Nabii Samweli ametumiwa kwenye Biblia katika jamii ya Wayahudi katika kusimika viongozi wapya wanapoingia katika nafasi zao. Katika tamthiliya hii, Pastor Njoya anacheza namna hiyo pia. Mwangwi wa Nabii Samweli unasikika namna hii;

47) MUITE: ...
*Hivyo tunamuomba aje akalie kiti chake.*
*[Wangari anakuja. Anakaa. Pastor Njoya anasimama mbele yake...]*
*Sasa tunamuomba Pasta Timothy Njoya aje hapa ili akamilishe halfa hii ya leo. [Pastor anaendda mbele]*
(Uk. 5)

48) NJOYA: *Wakati wa kumuenzi binti wa Afrika, sasa umewadia [Vitendo vifuatavyo vimeandamana na ukimya isipokuwa muziki wa jadi kwa sauti ya chini.*
*Wangari anasimama.*
*Pasta anamvika ngolole.*
*Kisha taji; kisha anapewa mkuki na Biblia]*
(Uk. 51)

Emmanuel Mbogo amemchora mhusika huyu, Pastor Njoya kumvika taji ya ushindi, Wangari Maathai (Data Na. 48 & 49). Heshima hiyo anatunukiwa Wangari na uongozi wa Kenya kwa heshima kubwa aliyoileta katika taifa hilo, baada ya kupewa tuzo ya kimataifa ya amani ‘Noble Peace Prize’. Mhusika Njoya na uhusika wake unashabihiana na ule mhusika Nabii Samweli na uhusika wake katika Biblia. Nabii

huyo Samweli amechorwa kushiriki katika shughuli za kutunuku au kusimika viongozi wa taifa la Israel. Samweli amehusika namna hii katika Biblia;

> "*Ndipo Samweli akaitwaa Pembe yenye mafuta, akamtia mafuta kati ya ndugu zake; na roho ya Bwana ikamjia Daudi kwa nguvu, tangu siku ile. Basi, Samweli akaondoka, akaenda zake Rama."* (1Samweli 16:13)

Nabii Samwel katika Biblia alikuwa mjumbe wa Mungu huko Uyahudi. Mtumwa huyo wa Mwenyezi Mungu alitumwa na Mola kwenda katika familia ya Mzee Yese, ili kumpaka, kumsimika Mfalme mpya wa Israel. Alipofika katika huko, alifanya kama Mungu alivyomwelekeza; kumpaka mfalme mpya mafuta. Mfalme aliyechaguliwa na Mungu aliitwa, Daudi. Huyu kijana alikuwa mtoto wa mwisho katika familia ya Mzee Yese. Basi, Nabii Samweli akamchukua kijana Daudi na kumpaka mafuta. Vifaa vya jadi vilitumiwa katika kufanya zoezi hilo mf. Pembe za mnyama n.k. Mhusika Njoya naye ametumia vifaa vya jadi pia katika kufanya tendo kama hilo kama tulivyoona. Mf. Mkuki, Ngolole n.k.

Kimsingi, matokeo ya utafiti yamebaini wahusika wa Biblia katika tamthiliya ya *Wangari Maathai* mathalani Nabii Samweli. Mhusika Pastor Njoya kutoka katika tamthiliya teule ananasibishwa na mhusika Nabii Samweli kutoka katika Biblia. Wahusika hao wamecheza nafasi sawia katika matini teule. Dai la Kristeva (1980) kwamba, watunzi wa fasihi hawatungi kazi zao kutoka fikra zao wenyewe bali huathiriwa na matini tangulizi limedhihirika wazi namna hiyo. Mwandishi teule, Emmanuel Mbogo amechota uhusika wa Nabii Samweli kutoka kwenye Biblia akamvika mhusika Pastor Nyoya katika tamthiliya ya *Wangari Maathai*. Msomaji wa kazi za fasihi aliyewahi kuisoma Biblia awali kabla ya kukutana na kazi hii teule,

anaweza kuiona taswira ya Nabii Samweli na tukio la kumtawaza Mfalme Daudi huko Israel, kwenye taifa la Wayahudi.

#### 4. 2. 4. 3 Wahusika wa Biblia katika Tamthiliya ya Nyota ya Tom Mboya

Wahusika wenye mwangwi wa Biblia wamejitokeza katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya* (2016). Wahusika hao walitumika awali kwenye Biblia na sasa mtunzi teule, Emmanuel Mbogo amewahusisha katika tamthiliya hii tuliyotafiti. Kwa mfano, Mhusika Nabii Eglon, aliyecheza kama nabii katika tamthiliya hii anapiga mwangwi wa wahusika mbalimbali waliotumiwa katika Biblia. Mwangwi wa wahusika wa Biblia umebainika hivi;

49) MBOYA: *Bwana Tuta unanishangaza sana.*
*Mimi sikujua kama wewe ni nabii.*
*Unayo elimu ya unajimu.*
*Yamkini, roho yako yaweza kubashiri kuwa Mtukufu Rais ataiaga dunia siku ya karibuni?* (Uk. 30)

50) NABII: *Naona maajabu ya Musa;*
*Jeneza limeota mbawa. Jeneza limewaponyoka Waombolezaji.*
*Kwa mbawa imara kama Tai, Jeneza linapaa!*
*Linapaa!!!!...*
(Uk. 55)

Wahusika manabii, ni mashuhuri mno katika kitabu cha Biblia (Data Na. 50 & 51). Theolojia inamweleza nabii kama binadamu anayesema na wanadamu wenzake kwa niaba ya Mungu hasa kwa kuelekeza wenzake wafuate imani na maadili sahihi (Mwakasege, 2018). Mjumbe huyo hutoa taarifa kabla ya jambo kutokea. Baadhi ya manabii wanaotajwa zaidi katika Biblia ni hawa wafuatao: Nabii Isaya; Nabii Yeremia; Nabii Ezekiel; Nabii Hezekia.

Vilevile Biblia inamweleza nabii kama msemaji wa Mungu. Kwamba nabii ni mtu au mjumbe anayepeleka maneno ya Mungu kwa wanadamu. Mungu huwasiliana na nabii na kuweka maneno kinywani mwa nabii ili aende kuwaeleza wanadamu, katika jamii aliyokusudia (Ellen, 2021). Kwa mfano Nabii Yeremia aliambiwa na Mungu namna hii kuhusu wajibu aliompa kwa wanadamu hapa ulimwenguni. Kwa mfano Biblia inaandika, Mungu akiwasiliana na Nabii Yeremia alisema naye hivi;

> *"Kabla sijakuumba katika tumbo nalikujua...nalikutakasa; nimekuweka kuwa nabii wa mataifa...ukawaambie maneno yote niliyokuamuru."*
> (Yeremia 1:5)

Hali kadhalika, Nabii Isaya alitumiwa na Mungu kuleta habari za kuzaliwa kwa Yesu Kristo hapa duniani. Hivyo akatabiri tukio hilo miaka mingi kabla halijadhihirika katika ulimwengu halisi. Biblia inaandika,

> *"Kwa hiyo Bwana mwenyewe atawapa ishara. Tazama bikira atachukua mimba, atazaa mtoto mwanamume, naye ataitwa jina lake Immaniel".* (Isaya 7: 14 & Isaya 9:6)

Kimsingi, utafiti umebaini wahusika wa Biblia katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya*. Mhusika 'Nabii' (Data Na. 50 & 51) ni mwangwi wa manabii wanaotajwa kwenye Biblia kama tulivyobainisha. Wajibu wa nabii unavyobainishwa katika Biblia u sawia na ule aliorejea mtunzi teule katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya*. Mathalani Yeremia wa *Biblia* na Eglon wa *Nyota ya Tom Mboya* wana uwezo sawa wa kuota ndoto na kueleza matukio yatakayotukia baadaye kwa kuonyeshwa na Mwenyezi Mungu. Hivyo wahusika manabii kutoka kwenye Biblia wanahusiana na hawa wanaotumiwa katika kazi teule.

Masatu na wenzake (2020) wakimrejea Mningo (2015) wanasema kuwa, washadidi wa Nadharia ya Mwingilianomatini wanadai kazi yoyote ile ya fasihi huwa na sauti

mbalimbali zinazoingiliana na kupiga mwangwi kutoka kazi zilizotangulia kuumbwa. Hivyo basi, kila kazi inayotungwa sasa huwa na mwangwi wa kazi tangulizi. Mhimili huo umedhihirika katika utafiti tuliofanya. Matokeo ya utafiti yamebaini kwamba kuna mwangwi wa wahusika wa Biblia katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya* (2016).

#### 4. 2. 4. 4 Wahusika wa Biblia katika Tamthiliya ya Tanzia ya Patrice Lumumba

Pamoja na hayo, mtunzi teule katika tamthiliya ya *Tanzia ya Patrice Lumumba* (2015) hii amemtumia wahusika wa *Biblia*. Mhusika mkuu Pauline, ametumika kuwasilisha wahusika wa Biblia katika matini hiyo. Katika onesho la 11, Uk. 43 tulibaini haya;

51) PAULINE: *[Anaongea na Sanamu la Bikira Maria] ...*
*Ninaomba roho saba za ujasiri wa Simba wa Yuda...*
*Ninaomba roho saba za ujasiri wa Malkia Esther ziingie ndani ya maji haya ya baraka!*
*Naomba roho saba za mabinti wa Zelophehad...*
*Naomba roho saba za mamlaka ya Debora...*
*Ushujaa na werevu wa Yokebedi na Miriam* (Uk. 43)

Katika dua na sala hii mhusika Pauline anazungumza na taswira ya Bikira Maria (Data Na. 52). Sanamu la Bikira Maria katika tamthiliya *Tanzia ya Patrice Lumumba* limechorwa kumwakilisha Maria Mtakatifu, Mama wa Mungu (Biblia). Sanamu hilo limepewa uwezo wa kutenda kama binadamu. Ndiyo maana Pauline anapeleka dua zake mbele za Mungu kwa hilo.

Biblia inamweleza Bikira Maria kama mama mzazi wa Yesu Kristo. Kupewa wajibu wa kumzaa mwokozi wa ulimwengu, kumempa nafasi kubwa kwa waamini wa dini hiyo. Waumini wa dini ya Kikristo wanaotumia kitabu cha Biblia, mathalani

Wakatoliki wameamini hata kumuomba Mungu Mwenyezi kupitia yeye kwani Biblia imeeleza mama huyo huwasiliana hata na Mungu kupitia Malaika zake. Biblia inaeleza mawasiliano ya Mung una Bikira Maria namna hii;

> "Mwezi wa sita, malaika Gabrieli alitumwa na Mungu kwenda mpaka mji wa Galilaya, jina lake Nazareti, kwa mwanamwali bikira aliyekuwa ameposwa na mtu, jina lake Yusufu, wa mbari ya Daudi; *na jina lake bikira huyo ni Mariamu*. Akaingia nyumbani kwake akasema, Salamu, uliyepewa neema, Bwana yu pamoja nawe…
> *Malaika akamwambia, Usiogope, Mariamu, kwa maana umepata neema kwa Mungu.* Tazama, utachukua mimba na kuzaa mtoto mwanamume; na jina lake utamwita Yesu. Huyo atakuwa mkuu, ataitwa Mwana wa Aliye juu, na Bwana Mungu atampa kiti cha enzi cha Daudi, baba yake…"
> (Luka 1: 26 – 38)

Biblia katika maelezo hapo juu inamtambulisha Mariam kama mhusika aliyekuwa na uwezo wa kuzungumza na Malaika wa Mungu, Mf. Malaika Gabriel. Mahusiano haya ya karibu na Mungu katika Biblia yalipelekea Wayahudi kumuamini sana Mariam. Mawasiliano ya Bikira Mariam na Mungu kupitia Malaika Gabriel yanathibitisha utakatifu wa mwanamke huyo. Wayahudi waliamini Mungu huwasiliana na watu wema, wanaomcha na kumtegemea siku zote za maisha yao. Hivyo, maisha yake tukufu, ndiyo yalichagiza hata akapewa heshima ya kumzaa mkombozi wa wanadamu ulimwenguni, Yesu Kristo.

Vilevile katika tamthiliya hii mtunzi teule amemlinganisha mhusika Pauline na wahusika wanawake waliotumika kwenye Biblia. Wahusika wa Biblia waliotajwa humu walishiriki katika harakati mbalimbali za ukombozi wa jamii zao. Jedwali linalofuata limetusaidia kuwawakilisha wahusika hao vizuri.

**Jedwali Na. 4. 4: Kuonyesha Wahusika Waliorejewa kama Pauline katika Biblia**

| **Wahusika wa Tamthiliya** | **Wahusika wa Biblia** |
|---|---|
| Pauline | Malkia Esta (Esta 4:16)<br>Debora (Waamuzi 5:7)<br>Miriam (Mika 6: 4)<br>Yokebedi (Kutoka 15: 21) |
| Sanamu la Bikira Maria | Mariam – Mama wa Yesu Kristo<br>(Luka 1: 26 -38) |

**Chanzo: Biblia Takatifu – Tafsiri ya Ulimwengu Mpya (2017)**

Kimsingi, matokeo ya utafiti huu yamebaini kwamba, kuna wahusika wa Biblia waliojitokeza katika tamthiliya ya *Tanzia ya Patrice Lumumba*. Uhusiano kati ya wahusika waliojitokeza katika tamthiliya teule na Biblia unadhihirisha hilo. Wahusika waliowahi kujitokeza katika vitabu mbalimbali ndani ya Biblia, wamehusishwa na mtunzi teule katika tamthiliya ya Tanzia ya Patrice Lumumba.

Pauline, mhusika mwanamke anayeshiriki katika ukombozi wa taifa la Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo akishirikiana na mume wake Patrice Lumumba ananasibishwa na wanawake wa kwenye Biblia. Mathalani mhusika Miriam (Biblia), huyu alikuwa dada wa Nabii Musa. Mhusika huyo alishirikiana na kaka yake, Nabii Musa katika harakati za ukombozi wa taifa la Israel huko utumwani Misri hadi Israel ikakombolewa (Mika 6: 4).

Ponera na wenzake (2014) wakitafiti mihimili ya Nadharia ya Mwingilianomatini wanaeleza kuwa, siyo rahisi na haiwezekani kuiangalia matini kama zao yatima, katika upekee wake na kwa kujibagua, badala yake ni lazima tutambue kuwa kuna matini tangulizi yenye kuhusiana na matini mpya. Matokeo ya utafiti huu yamebaini

kwamba kuna matumizi ya wahusika wa Biblia katika tamthiliya ya *Tanzia ya Patrice Lumumba* (2015). Wahusika waliotumika awali katika matini tangulizi, Biblia wanahusiana na wahusika waliotumika katika matini mpya, tamthiliya teule. Hivyo basi, wahusika wa Biblia wanaojitokeza katika tamthiliya ya *Tanzia ya Patrice Lumumba*.

#### 4. 2. 4. 5 Wahusika wa Biblia katika Tamthiliya ya Mtumwa hadi Siti Binti Saad

Katika tamthiliya ya *Mtumwa hadi Siti Binti Saad* (2016) kuna mwangwi wa wahusika wa Biblia. Mhusika mkuu Siti binti Saad ananasibishwa na mhusika Yusufu mwana wa Yakobo kutoka kwenye Biblia huko katika nchi ya Wayahudi, Israel. Emmanuel Mbogo amemchora mhusika Siti Binti Saad kama mhusika aliyetoka katika familia duni, ya kitumwa. Hivyo alikuwa mtumwa katika nchi yake Unguja. Mhusika huyo japo alizaliwa katika familia ya kitumwa, amechorwa kufanya juhudi za maisha kupitia muziki hadi akafanikiwa kimaisha. Siti alipandishwa daraja, kutoka utumwani hadi kuketi na wakuu, watawala katika Kisiwa cha Unguja. Taz.

52) MALIKIA: *Mmh! Sasa kuna mwaliko. Mimi na mfalme tunataka Club yenu ije kutumbuiza Ikulu Jumamosi hii...* (Uk. 77)

53) MALIKIA: *Hiyo ni kwa ajili ya matayarisho ya shoo yenu. Mfalme amealika mabalozi na mawaziri...* (Uk. 77)

54) BONGA: *Ama kweli, Mwenyezi Mungu anaweza kumtoa mtu kutoka kwenye matope na kumwinua juu katika utukufu na enzi.* (Uk. 79)

55) NONGWA: *Nasikia Banji alienda kwa Siti na kumwambia, "Mimi iko peleka Siti India. Tafanya recording ya*

> *Akwaani Sofaa. Tena hiyo miezi ijayo Ummu Kulthum takuja India toka Misri. Mimi taka Siti Binti Saad fanya kolabo na Ummu..."*
> (Uk. 79)

Katika tamthiliya hii tunamwona mhusika Siti binti Saad akiinuliwa kutoka utumwani hadi kuwa Malkia wa Taarab, Unguja - Upwa wa Afrika Mashariki (Data Na. 53 – 56). Siti Binti Saad alikuwa mhusika kutoka tabaka duni, tabaka la chini la watumwa huko Unguja. Hata hivyo, kutokana na juhudi kubwa alizofanya katika tasnia ya muziki, aliweza kufanikiwa kimaisha. Siti amechorwa kupata heshima kubwa, hata akawa anaalikwa kwenye shughuli mbalimbali za Kiserikali.

Mhusika Siti anahusishwa na mhusika mmoja katika Biblia almaarufu kama Yusufu bin Yakobo. Biblia inamweleza mhusika Yusufu kama kijana wa Kiyahudi aliyeinuliwa na Mungu Mwenyezi kutoka utumwani hadi kuwa Waziri Mkuu nchini Misri. Yusufu alifika huko Misri akitoka Uyahudi kama mtumwa baada ya kuuzwa na kaka zake wa kuzaliwa kwa Wafanyabiashara wa Midiani, walioishia kumuuza kama mtumwa kwa Wamisri. Biblia inaandika hivi;

> *"Basi Yusufu akaletwa mpaka Misri naye Potifa akida wa Farao, mkuu wa askari, mtu wa Misri, akamnunua mikononi mwa hao Waishmael waliomleta huko. Bwana akawa pamoja na Yusufu, naye akastawi, Mmisri."* (Mwanzo 39: 1 – 2)

Katika Biblia Yusufu bin Yakobo aliuzwa Misri kama mtumwa. Kijana huyo alipokuwa huko ugenini, kwa kudra za Mwenyezi Mungu na jitihada zake katika wajibu mbalimbali aliopewa kufanya alifanikiwa sana. Siku moja mtawala wa Misri, Farao aliota ndoto ngumu. Watu wote katika taifa hilo wakashindwa kutambua maana ya ndoto hiyo.

Biblia inaeleza kuwa, mtumishi mmoja wa Mfalme huko Misri alimtaja Yusufu kama kijana mmoja mwenye uwezo wa kufasili ndoto, waliyemuacha gerezani. Mfalme akaagiza Yusufu aletwe. Alipofika Yusufu akajuzwa ndoto, naye akaifasili. Kwa hilo Farao aliitambua hekima kubwa ndani ya kijana huyo, basi akamteua awe waziri mkuu katika taifa hilo ili asimamie na kuratibu ndoto yote kama ilivyofumbuliwa mbele yake. Biblia inaeleza haya;

> *"Farao akawaambia watumwa wake, tupate wapi mtu kama huyu, Mwenye roho ya Mungu ndani yake? Farao akamwambia Yusufu, kwa kuwa Mungu amekufahamisha hayo yote, hapana mwenye akili na hekima kama wewe. Basi, wewe utakuwa juu ya nyumba yangu, na kwa neno lako watu wangu watatawaliwa. Katika kiti cha enzi tu nitakuwa mkuu kuliko wewe."*
> (Mwanzo 41: 38 – 40)

Wahusika hawa wawili; Siti binti Saad katika tamthiliya teule (tamthiliya teule Data Na. 53 - 56) na Yusufu bin Yakobo katika Biblia wanahusiana kifani na kimaudhui. Siti Binti Saad ameanza kucheza kama mtumwa katika tamthiliya teule, akaishia kwenye Umalkia wa Taarab. Daraja alilopo sasa anaalikwa hadi kwenda Ikulu kutumbuiza hafla mbalimbali za kiserikali. Anapelekwa hadi nchi za nje, India kwenda kurekodi muziki huko akishirikiana na wanamuziki wanawake maarufu nchini India. Ni mafanikio makubwa.

Pamoja naye Yusufu bin Yakobo, ndani ya Biblia alitoka utumwani, gerezani na kuishia kiti cha uwaziri mkuu. Yusufu aliteuliwa nafasi ya juu kabisa ya utawala tena akiwa ugenini, si raia asili wa Misri. Ni faraja kubwa aliipata, huenda aliwasamehe hata kaka zake waliomuuza kama mtumwa hata akapelekwa huko.

Kimsingi, matokeo ya utafiti yamebaini wahusika wa Biblia katika tamthiliya teule tuliyotafiti. Wafuasi wa Nadharia ya Mwingilianomatini unaeleza kuwa matini za

fasihi huingiliana na kukamilishana (Senkoro, 2011). Hivyo, tukizisoma kazi za fasihi kwa mwega wa Nadharia ya Mwingilianomatini tunaweza kutambua na kufafanua mahusiano yaliyopo kati ya matini moja na matini nyingine. Athari za kazi tangulizi zinaweza kuonekana katika kazi mpya. Athari hizo zinaweza kuwa za moja kwa moja au kimwangwi (Ndunguru, 2020).

Hivyo basi, sababu ya kutumiwa kwa wahusika kutoka matini nyingine iliyotungwa awali, Biblia katika tamthiliya teule iliyotungwa baadaye, inaelezwa kama kaida ya kazi za fasihi. Mhusika Yusuf katika Biblia ametumika kumuumba mhusika Siti binti Saad katika tamthiliya ya *Mtumwa hadi Siti Binti Saad*. Mtunzi anaeleza jamii kwamba ushindi maishani unawezekana hata kama mtu ametoka daraja la chini.

### 4. 2. 4. 6 Wahusika wa Biblia katika Tamthiliya ya Malkia Bibi Titi Mohamed

Pamoja na hayo, tulichunguza wahusika wa Biblia katika tamthiliya ya *Malkia Bibi Titi Mohamed* (2016). Maelezo ya mtangazaji wa kwanza na Bibi Titi katika tamthiliya hii yana mwangwi wa wahusika wa Biblia.

56) MTANGAZAJI 1: [Mwanamke]…
Tangazo! Tangazo! Tangazo!
Mabibi na mabwana.
Wakazi wa Mjini Dodoma.
*Malkia wa harakati za Uhuru wa Tanganyika*
*Bibi Titi Mohamed, tayari yupo Dodoma.*
Bibi Titi yupo Dodoma!
Yupo Dodoma!
Anahutubia mkutano wa hadhara katika viwanja vya mpira.
(Uk. 27)

57) BIBITITI: *Natazama mbegu imeota*
*Mungu ametupa uwezo huu,*
*Bila ushirikiano wetu hatutapata uhuru...*
(Uk. 31

Bibi Titi Mohamed katika tamthiliya teule amechorwa kama mwanamke, mwanaharakati aliyepambana kufa na kupona ili nchi ya Tanganyika na jirani zake, Afrika Mashariki zipate uhuru miaka ya 1960 (Data Na. 57 & 58). Kupitia data hizi tunaelezwa jinsi Bibi Titi alivyoshiriki katika mapambano ya ukombozi wa Tanganyika upitia tasnia ya muziki. Nyimbo alizokuwa akiimba zilikuwa zikiwainua, kuwahamasisha wanawake na Watanganyika wote ili washikamane na kupambana na Wakoloni hadi Tanganyika, Afrika ipate uhuru.

Kitabu cha Biblia kinamweleza mhusika mmoja mwanamke, mwenye jina la Malkia Esta. Mhusika huyo mwanamama alikuwa Myahudi, aliyeolewa na Mfalme Ahasuero, Ugenini nchini ya Shushani. Wayahudi walikuwa wageni, watumwa katika nchi hiyo. Hamani mtu mwenye cheo kikubwa katika nchi hiyo alitoa amri kwamba, kila mtu atakayekutana na Mfalme Ahasuero, ainame na kumsujudia. Wayahudi walipinga kufanya hilo, ukaandikwa waraka na akida huyu kwamba, Wayahudi wote wauawe.

Malkia Esta alisimama imara kuwaokoa ndugu zake Wayahudi dhidi ya tangazo hilo la kuuawa kwao. Esta alipambana na hatimaye waraka huo wa kuuawa Wayahudi ukabatilishwa na Mfalme Ahasuero. Wayahudi wakapona mauti kwa mkono wa binti yao, aliyekuwa ameolewa katika nyumba ya Mfalme Ahasuero. Mchango wa Malkia Esta unabainishwa namna hii katika Biblia;

> *"… Basi Esta akawatuma ili wamjibu Mordekai, Uende* ukawakusanye *Wayahudi wote waliopo hapa Shushani, mkafunge kwa ajili yangu; msile wala kunywa muda wa siku tatu, usiku wala mchana, nami na wajakazi wangu tutafunga vile vile; kisha nitaingia kwa mfalme, kinyume cha sheria; nami nikiangamia, na niangamie. Basi Mordekai akaenda zake, akafanya yote kama vile Esta alivyomwagiza."*
> (Esta 4: 12 – 17)

> "…*Ndipo malkia Esta alipojibu, akasema, Mfalme, ikiwa nimepata kibali machoni pako, na mfalme akiona vema, nipewe maisha yangu kuwa dua yangu, na watu wangu kuwa haja yangu. Maana tumeuzwa, mimi na watu wangu, ili tuharibiwe, na kuuawa, na kuangamia..."*
> (Esta 7: 1 – 7)

Kimsingi, matokeo ya utafiti yamebaini kutokea kwa wahusika wa Biblia katika tamthiliya hii. Wahusika waliorejewa katika matini teule wanahusiana kwa jinsi walivyoshiriki katika harakati za ukombozi wa jamii walizotokea. Malkia Bibi Titi Mohamed ameshiriki kuwakomboa Watanganyika na Afrika Mashariki kwa jumla (Data Na. 57 & 58). Malkia Esta katika Biblia ameshiriki kuwakomboa ndugu zake Wayahudi na mauti ya kitanzi waliyokuwa wameandikiwa katika ardhi za watu huko Shushani (Esta 7: 1 – 7). Uhusika wa wahusika hawa, unahusiana katika mambo waliyoyafanya katika mataifa yao. Huenda ndiyo maana wote wakatunukiwa wadhifa wa Umalkia katika matini teule tulizotafiti, kutokana na mchango wao katika kukomboa jamii zao.

Wafuasi wa Nadharia ya Mwingilianomatini wanaeleza kuwa, uhusiano wa matini katika tanzu za fasihi hujibainisha kwa njia ya urejeleaji wa vipengele vya matini tangulizi ndani ya matini mpya (Lemaster, 2012). Mhusika Malkia Esta (katika Biblia) kubainika katika tamthiliya teule kama Malkia Bibi Titi Mohamed ni ithibati ya mwingilianomatini baina ya matini teule tulizotafiti; Biblia (kazi tangulizi) na *Malkia Bibi Titi Mohamed* (matini mpya). Hivyo basi utafiti umebaini kuwa, Emmanuel Mbogo alimtumia mhusika Malkia Esta kutoka katika Biblia kumuumba Malkia Bibi Titi katika tamthiliya teule tuliyotafiti kama tulivyobainisha.

#### 4. 2. 4. 7 Muhtasari

Kimsingi, wahusika wa Biblia katika tamthiliya teule zote tulizotafiti wamejitokeza kwa taswira mbalimbali kama tulivyobainisha. Dai la washadidi wa Nadharia ya

Mwingilianomatini kwamba, kila kazi ya fasihi inahusiana na matini nyingine tangulizi ni yakinifu. Si sahihi kuitazama kazi ya fasihi kama zao yatima. Hii ndiyo sababu inayopelekea sifa za kazi tangulizi kuonekana kwenye matini mpya. Emmanuel Mbogo kuhusisha wahusika wa Biblia katika kazi yake kunathibitisha mhimili huo wa Nadharia ya Mwingilianomatini. Hivyo basi, kazi za kifasihi zinahusiana kwa namna mbalimbali na kazi zilizokuwapo kabla ya matini mpya kubuniwa. Mbogo aliisoma Biblia kwanza, ndipo akaunda kazi zake. Ndipo sasa athari za kitabu hicho katika bunilizi zake zikadhihirika kupitia wahusika wake kama tulivyobainisha.

### 4. 2. 5 Mandhari ya Biblia katika Tamthiliya Teule

Pengine kabla ya kubainisha mandhari ya Biblia katika tamthiliya teule za Emmanuel Mbogo, tunaona vema tueleze dhana ya mandhari. Mandhari ni nini? Itakuwa vema swali hili tukilijibu kisha tusonge mbele kubainisha kipengele tajwa katika kazi teule.

Lymo (2018) akimrejelea Wamitila (2008) anasema, “Mandhari ni wakati na mazingira ambayo ndiyo msingi katika uandishi wa kazi za fasihi.” Mtaalam huyu anazidi kudadavua kwamba, mandhari inaweza kuanishwa kwa namna mbalimbali. Mathalani; mandhari ya kijiografia (mandhari halisi), mandhari ya kihistoria (zinazokiuka masuala ya kihistoria), mandhari ya kidhanifu au kinjozi (zinazokiuka uhalisia), mandhari dokezi (mandhari zinazoishia kudokeza tu jambo) na mandhari ya kiajinabi (mandhari zinazokiuka sifa za kawaida). Pamoja na aina zote zilizoanishwa, mandhari zinaweza kuweka katika mafungu mawili; mandhari halisi na mandhari ya kinjozi. Kila mandhari huwa na lengo mahsusi katika uumbaji wake.

Gasper (2016) anaeleza kuwa, mandhari ni sehemu, mahali au mazingira ambayo matukio ya hadithi au masimulizi hutendeka, hufanyika ama kutokea. Kwa jumla, mandhari yanaweza kuwa halisi au ya kubuni. Mandhari halisi hujumuisha mazingira yanayoweza kudhihirika kikawaida. Mandhari ya kubuni, ni dhanifu si halisi. Mtaalam huyu anashadidia kwamba, mandhari katika fasihi ni muhimu kwani humsaidia mtunzi kuifikia hadhira inavyostahili. Mwanazuoni huyu anakiri kwamba, mandhari huwawezesha wahusika wa kazi za fasihi na kusaidia ujenzi wa dhamira za fasihi.

Mwavali, Nyandoro na Onyango (2020) wanafasihi mandhari kama mahala au pahali ambapo kazi ya fasihi hutokea, hutendeka. Wanazuoni hawa wanasonga mbele zaidi kueleza kwamba, mandhari huwa ni sura ya mahali, hususani jinsi panavyoonekana katika hali halisi ya maisha. Vilevile wanazuoni hawa wanadadavua kwamba, mandhari hujumuisha vipengele vya wakati, mahali na mazingira ambayo wanajamii hutangamana.

Vipengele vya wakati, mahali na mazingira ni muhimu katika ujenzi wa mandhari (Mwavali, Nyandoro na Onyango, 2020). Magwiji hawa wa fasihi kutoka nchini Kenya, wanashadidia kwamba kipengele cha wakati haswa humuelekeza msomaji kuelewa nyakati palimotokea matukio na mazingira husika kama vile hali ya utamaduni, kisiasa na kiuchumi katika jamii.

Kimsingi, mandhari katika kazi za fasihi inaweza kuelezwa kama mahali au wakati ambao tukio la fasihi hubuniwa na kutendeka. Wamitila (2002) anaeleza kwamba, mandhari hufanikisha ujenzi wa hisia za msomaji na msikilizaji au mtazamaji kwa

msingi wa kazi ya fasihi iliyowasilishwa mbele yake. Vilevile mandhari inafasiliwa kama mahali ambapo kazi ya fasihi ilitendeka, inatendeka au itatendeka. Kazi yoyote ya fasihi ni lazima iwe na mahali au sehemu panapotokea matukio ya bunilizi. Mandhari ni kipengele muhimu cha kifani katika fasihi; simulizi na andishi.

Katika utafiti tuliofanya, dhana hii 'Mandhari ya Biblia' ilitumika kurejea sehemu au mahali ambapo matukio mbalimbali yalitendeka ndani ya vitabu vya Biblia. Utafiti huu ulilenga kubainisha mandhari hizo na kueleza sababu za kujitokeza kwake katika tamthiliya teule. Nadharia ya Mwingilianomatini ndiyo ilikuwa kiunzi cha kueleza sababu ya kujitokeza kwa fani hii katika tamthiliya teule.

Uchambuzi wa mwangwi wa Biblia katika matini umefanyika kwa kuzingatia malengo mahsusi mawili mtawalia. Mosi, mtafiti amebainisha mandhari ya Biblia katika tamthiliya teule. Pili, usuli wa mandhari hiyo kutoka kwenye Biblia umewekwa bayana. Mwisho, tukahitimisha kwa kueleza sababu za kujitokeza kwa mandhari za Biblia katika tamthiliya teule tulizotafiti tukiegemea mihimili ya Nadharia ya Mwingilianomatini.

### 4. 2. 5. 1 Mandhari ya Biblia katika Tamthiliya ya Mondlane na Samora

Mandhari za *Biblia* katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora* (2016) zimehusishwa kwa taswira mbalimbali. Mandhari hizo zilitumika awali katika kitabu cha Biblia, wakati huu zimetumiwa katika tamthiliya teule kwa mfano: 'Bahari ya Shamu'. Taz.

58) JANET: *Kabisa! Nasikia ni kama ile fimbo ya Nabii Musa iliyogawa "Bahari ya Shamu".*
(Uk. 88)

Maelezo ya mhusika JANET yamedokezwa mandhari yenye mwangwi wa Biblia, 'Bahari ya Shamu' (Data Na. 59). Bahari ya Shamu, sasa Bahari Nyekundu (Red Sea) inayotajwa kwenye tamthiliya ya *Mondlane na Samora*, inaelekeana na ile inayotajwa kwenye Biblia. Kwa wasomaji wa Biblia, Bahari ya Shamu ni mahali maarufu ambapo Israel wanadai Mwenyezi Mungu aliwatendea mambo makubwa walipokuwa safarini kutoka utumwani, Misri kurejea nchini kwao, Kanaani nchi ya asali na maziwa.

Biblia inaeleza kwamba, Israel wakiwa safarini kutoka utumwani, Misri kurejea nchini kwao walikutana na Bahari ya Shamu. Hivyo Israel wakashindwa kuvuka kwenda upande wa pili wa Bahari ya Shamu. Ndipo Israel wakafanya dua na sala, Mwenyezi Mungu akawatengenezea njia katika ya Bahari ya Shamu, kwa kugawanya bahari hiyo pande mbili. Wakapata njia. Israel wakapita nchi kavu, wakavuka na kusonga na safari. Bahari ya Shamu imeelezwa hivi kwenye Biblia;

> *"BWANA akamwambia Musa, mbona unanililia mimi? Waambie wana wa Israel waendelee mbele. Nawe inua fimbo yako, ukanyooshe mkono wako juu ya bahari, na kuigawanya; nao wana wa Israel watapita kati ya bahari katika nchi kavu."*
> (Kutoka 14: 15 – 16)
>
> *"Yeye aliyeigawa Bahari ya Shamu; kwa maana fadhili zake ni za milele."*
> (Zaburi 136: 13)

Kimsingi, matokeo ya utafiti yamebaini kujitokeza kwa mandhari ya Biblia katika tamthiliya teule. Bahari ya Shamu inayoelezwa katika Biblia hapo juu imetumika katika tamthiliya teule (Data Na. 59). Mandhari inayotumika katika matini moja ya fasihi inaweza kujitokeza kwenye matini nyingine hapo baadaye (Kristeva, 1980). Matumizi ya mandhari ya Bahari ya Shamu katika hii tamthiliya ya *Mondlane na Samora* yanathibitisha mhimili wa Nadharia ya Mwingilianomatini. Mandhari ya

'Bahari ya Shamu' iliyotumika awali katika Biblia imejitokeza kwa mara nyingine katika matini mpya, tamthiliya ya *Mondlane na Samora*. Hivyo, matini tangulizi na fuatizi zimeathiriana kifani, tukiegema kwenye kipengele cha mandhari ya Bahari ya Shamu.

### 4. 2. 5. 2 Mandhari ya Biblia katika Tamthiliya ya Wangari Maathai

Mwangwi wa mandhari ya Biblia katika tamthiliya ya *Wangari Maathai* (2015) umedhihirika kupitia mazungumzo ya wahusika kuakisi mahali ambapo palifanyika matukio fulani katika Biblia. Katika utafiti huu tulibaini mandhari ya Biblia, 'Bustani ya Edeni' kama ifuatavyo;

59) AKINYI: ...
*Waligwala hata msitu wa Malaika uliokuwa*
*unatembea bustani ya Edeni.*
(Uk. 1)

60) WANGARI: ...
*Ni taswira ya bustani ya Edeni kwa ajili ya vizazi vijavyo*
*katika sayari hii tuishiyo...*
(Uk. 1)

Utafiti tuliofanya ulibaini kwamba, Bustani ya Edeni inayorejewa na wahusika Akinyi pamoja na Wangari inahusiana na Bustani ya Edeni inayoelezwa kwenye Biblia (Data Na. 60 & 61). Wangari akishirikiana na wanawake wenzake wanapambana kadri wanavyoweza kuifanya nchi ya Kenya iwe na mazingira bora na salama kwa viumbe vyote kuishi. Wanatamani nchi ya Kenya iwe na mandhari nzuri kama ile iliyokuwa bustani ya Edeni, katika Biblia iliyopandwa na Mungu Mwenyezi alipoumba dunia.

Biblia inaeleza Bustani ya Edeni kama mahala alipopatengeneza Mwenyezi Mungu hapa Ulimwenguni kisha akawaweka wanadamu wa kwanza, Adam na Eva waishi na kupatunza. Hiyo bustani ilikuwa eneo la furaha kuu, utulivu na paradiso ya Mungu. Nyakati za jioni Mwenyezi Mungu alishuka hapo kupumzika, kupunga upepo baada ya kazi. Biblia inaandika hivi;

> "*BWANA Mungu akapanda bustani upande wa mashariki wa Edeni,* akamweka ndani yake huyo mtu aliyemfanya. BWANA *Mungu akachipusha katika ardhi kila mti unaotamanika kwa macho na kufaa kwa kuliwa; na mti wa uzima katikati ya bustani*, na mti wa ujuzi wa mema na mabaya. *Ukatoka mto katika Edeni wa kuitilia bustani maji,* na kutokea hapo ukagawanyika kuwa vichwa vinne... BWANA Mungu akamtwaa huyo mtu, akamweka katika *bustani ya Edeni*, ailime na kuitunza."
> (Mwanzo 2: 8 – 10/15)

Wangari Maathai, mhusika mkuu katika tamthiliya teule ana hamu ardhi yote ya Kenya ifanane na 'Bustani ya Edeni' (Data Na. 61). Kenya iwe na mazingira bora na salama kwa wanadamu na kila kiumbe kuishi ndani ya viunga vyake kama ilivyokuwa 'Bustani ya Edeni' katika Biblia walipokaa wanadamu wa kwanza, Adam na Eva kama ilivyobainika katika Biblia.

Kimsingi, matokeo ya utafiti huu yalibaini kuwa kuna mandhari ya Biblia katika tamthiliya teule, *Wangari Maathai* (2015). Tamthiliya hii imehusisha mandhari inayohusiana na mandhari iliyojitokeza katika kazi tangulizi, Biblia. Hii ni ithibati kwamba matini za kisanaa uhusiana na kutegemeana kwa jinsi mbalimbali. Tamthiliya hii aliyoandika Emmanuel Mbogo haikuwa zao lake pekee, bali imehusiana na matini nyingine, Biblia. Kipengele cha mandhari ya Biblia kimetumika kuthibitisha mahusiano hayo.

Matumizi ya mandhari ya ‘Bustani ya Edeni’ katika tamthiliya teule yanabainisha mandhari ya ‘Bustani ya Edeni’ katika *Biblia*. Mahusiano baina ya mandhari hizi katika matini teule yanathibitisha mhimili wa Nadharia ya Mwingilianomatini tuliosoma kwamba, matini za kisanaa si zao la mwandishi pekee bali huchagizwa ama kufaidika kutoka kwa matini nyingine (Wanjiru, 2022). Kuchagizana kwa kazi za fasihi ndiyo kumechangia kujitokeza kwa mandhari za Biblia; ‘Bahari ya Shamu’ na ‘Bustani ya Edeni’ katika tamthiliya teule ya *Wangari Maathai*.

#### 4. 2. 5. 3 Mandhari ya Biblia katika Tamthiliya ya Nyota ya Tom Mboya

Pamoja na hayo mtafiti alibaini kwamba kuna mwangwi wa mandhari ya Bibilia katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya* (2016). Mwangwi huo ulibainishwa kupitia matumizi mbalimbali ya mandhari ya Biblia katika tamthiliya teule. Mtunzi teule amehusisha mandhari ya Biblia katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya*. Hilo limedhihirika kupitia mandhari katika maonesho na sehemu mbalimbali ndani ya tamthiliya teule kuhusiana na mandhari zilizojitokeza awali kwenye Biblia. Mathalani, mandhari ya ‘Kuzimu’. Mandhari hiyo inaelezwa hivi;

61) KANOGA: *“Na CIA ni zimwi toka Kuzimu, lenye uwezo wa kumng’oa Rais mmoja na kumsimika Rais wanayemtaka popote duniani...”*
(Uk. 42)

Dhana ‘Kuzimu’ iliyohusishwa katika mazungumzo ya mhusika huyu, Kanoga imenasibishwa na mandhari moja kutoka kwenye *Biblia* (Data Na. 62). Sabaji (2018) anatujulisha kwamba, Watheolojia wanafasili kuzimu kama mahali pa mateso ya muda mfupi huku watenda mabaya wakisubiri Parapanda ya Bwana Yesu ile siku ya mwisho. Ambapo, watu wote wenye dhambi watatupwa katika ziwa la moto almaarufu kama Jehanamu ili waangamizwe.

Biblia inaeleza ‘Kuzimu’ kama makazi ya Ibilisi, Shetani na watenda kazi wake. Sehemu hiyo imetengenezwa na Mwenyezi Mungu kama gereza la wanadamu wote wanaotenda maasi humu ulimwenguni. Kuzimu inaelezwa hivi;

> “*Kuzimu chini kumetaharuki kwa ajili yako, ili kukulaki utakapokuja. Huwaamsha waliokufa kwa ajili yako. Naam walio wakuu wote wa dunia...”*
> (Isaya 14: 9 – 11)
>
> *“Kwa hiyo kuzimu kumeongeza tamaa yake, kumefunua kinywa chake bila kiasi; na utukufu wao, na wingi wao, na ghasia yao, naye pia afurahiaye miongoni mwao, hushuka na kuingia humo.”*
> (Isaya 5:14)

Mtafiti amebaini kwamba mandhari ya ‘Kuzimu’ iliyotumika awali kwenye Biblia kama tulivyobainisha imetumika kwa mara nyingine katika tamthiliya teule, *Nyota ya Tom Mboya* (Data Na. 62). Mandhari ya Kuzimu katika hizi teule imetumika kurejea mandhari hasi wanakowekwa watu waliofanya maovu, mambo mabaya katika jamii.

Kwa jumla matokeo ya utafiti yamebaini kujitokeza kwa mandhari ya Biblia katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya*. Kujitokeza kwa mandhari ya ‘Kuzimu’ katika tamthiliya tuliyosoma, kunathibitisha mhimili wa nadharia ya mwingilionatini unaoeleza kwamba matini mpya ni mabadiliko ya matini nyingine tangulizi iliyoandikwa kabla ya kazi mpya kubuniwa. Kuhusiana kwa mandhari hii ya ‘Kuzimu’ katika kazi teule tulizotafiti, kumethibitisha hilo. Emmanuel Mbogo ameitumia matini ya Biblia kujenga mandhari ya ‘Kuzimu’ katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya*.

#### 4. 2. 5. 4 Mandhari ya Biblia katika Tamthiliya ya Tanzia ya Patrice Lumumba

Hali kadhalika utafiti umebaini mandhari ya Biblia katika tamthiliya ya *Tanzia ya Patrice Lumumba* (2015). Mtunzi teule ametumia mandhari ya 'Kuzimu' kutoka katika Biblia, matini tangulizi kisha kuiambatisha na muktadha mwingine wa jamii ya Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo. Mhusika Pauline, Mke wa Lumumba ametumiwa kudokeza mandhari ya Kuzimu kama ifuatavyo;

62) PAULINE: ...
*Mashetani! Vibwengo!! Mazimwi toka kuzimu nyie!*
(Uk. 38)

Mandhari ya kuzimu inayorejewa katika tamthiliya teule ni taswira ya sehemu mbaya kwa mujibu wa kitabu cha Biblia (Data Na. 63). Kuzimu siyo mahali pazuri pa mtu kuishi. Kuzimu hakufai kwa makazi ya mwanadamu. Viumbe viliotajwa kuishi huko; Mashetani, Vibwengo na Mazimwi vyote vina uhusika wa uovu na uadui kwa wanadamu kama Biblia inavyoeleza.

Biblia pia inaeleza kuzimu kama Gereza la watenda dhambi. Waumini ya dini ya Kikristo wanaotumia kitabu cha Biblia huamini kwamba, watenda mabaya watahukumiwa na kuwekwa kwenye gereza hilo kuteswa (Hananja, 2011). Kuzimu inaelezwa hivi;

> *"Basi kule kuzimu aliyainua macho yake, alipokuwa katika mateso, akamwona Ibrahim kwa mbali, na Lazaro kifuani mwake.*"
> (Luka 16:23)

Kimsingi, mtunzi wa tamthiliya ya *Tanzia ya Patrice Lumumba* kunasibisha mandhari ya kuzimu na makazi ya Wakoloni kunaibua taswira hasi waliyokuwanayo Waafrika kutoka Kongo dhidi ya jeshi la Marekani. Mhusika Pauline katika tamthiliya ya *Tanzia ya Patrice Lumumba* kunasibisha makazi ya watu wanaomtesa

mume wake, Patrice na kuzimu kunajenga taswira hasi kuhusu makazi hayo ya Ibilisi na watu wake kama Biblia inavyoeleza. Mbogo ameitumia mandhari iliyotumika katika Biblia, ‘Kuzimu’ na kuiambatisha katika bunilizi yake ili aweze kufikisha ujumbe aliokusudia kwa hadhira lengwa.

Washadidi wa Nadharia ya Mwingilianomatini wanaeleza katika mhimili mmoja kuwa, kila uumbaji wa matini huwa ni kijalizo cha matini tangulizi, na hivyo basi huigeuza kwa kiwango (Macha, 2013). Kwa jumla kauli inayonukuliwa hubadilika na kuelezea upya kauli asilia kwa kuiambatisha na muktadha mwingine wa kiisimu na kijamii. Mandhari ya kuzimu iliyotumika kwenye Biblia, kitabu tangulizi imegeuzwa tena ikatumika katika tamthiliya ya Kiswahili kuendana na muktadha wa nchi ya Kongo. Hivyo kuna mwangwi wa mandhari ya Biblia katika tamthilia ya *Tanzia ya Patrice Lumumba.*

4. 2. 5. 5 Mandhari ya Biblia katika Tamthiliya ya Malkia Bibi Titi Mohamed

Mtunzi teule amemtumia mhusika mkuu Bibi Titi katika kudhihirisha mandhari ya Biblia katika matini hii. Bibi Titi akizungumza na jamii kuhusu mpango wake wa kupigania uhuru wa Tanganyika anadokeza mandhari ya Biblia. Mhusika mkuu huyo anatambulisha ‘Dunia’ kama mahala ambapo Mungu Mwenyezi kwa makusudi yake alipaumba kisha akamuweka mwanadamu aishi humo. Bibi Titi anaendelea kudai kwamba, kuwekwa kwake hapa duniani, Tanganyika kulikuwa na kusudi maalum, mojawapo likiwa kukomboa Watanganyika wenzake.

63) BIBITITI: ...
Yale *makusudi ya Mola wangu kuniumba na kunileta duniani ili niupiganie uhuru wa Tanganyika* lazima yatimie.
(Uk. 49)

'Dunia' katika Biblia ni sayari aliyoiumba Mwenyezi Mungu kama makazi ya mwanadamu. Katika matini ya Biblia kuna dai kwamba, dunia na vitu vyote vilivyomo ndani yake viliumbwa na Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu aliitengeneza Sayari ya Dunia, mahsusi kwa ajili ya kumfanya mwanadamu akae humo na kufanya shughuli zake mbalimbali.Taz.

> "*Hapo mwanzo, Mungu aliumba mbingu na dunia...*"
> (Mwanzo 1: 1/27-28)

Kimsingi, matokeo ya utafiti huu yalibaini matumizi ya mandhari ya Biblia katika tamthiliya teule ya *Malkia Bibi Titi Mohamed* (2016). Maguo na Rashid (2020) wakichunguza mtindo katika riwaya za Euphrase Kezilahabi na Mohamed Suleiman kwa mwega wa Nadharia ya Mwingilianomatini wanaandika hivi, "Bakhtin aliamini kwamba mwandishi anapoanza kuandika hujiingiza kwenye usemezano wa aina fulani na mwandishi aliyemtangulia. Kwa hivyo, panakuwako na sauti zinazojibizana."

Hivyo basi, matokeo ya utafiti yamebaini mandhari ya Biblia katika tamthiliya ya *Malkia Bibi Titi Mohamed* tukirejea Data Na. 64. Mandhari zilizotumika katika matini teule baina ya waandishi wa fasihi zinahusiana. Uhusiano huo hujitokeza kwa sababu, kila mtunzi anapoanza kuumba kazi yake uhusisha kazi fulani ya mwandishi aliyemtangulia. Hali hiyo huchagiza kutokeza kwa sifa za kifani au kimaudhui za kazi iliyotungwa awali katika matini mpya anayounda mwandishi sasa. Mandhari ya Biblia imejitokeza katika tamthiliya teule tuliyotafiti kama tulivyowasilisha. 'Dunia' anayoisema Bibi Titi katika tamthiliya teule inahusiana na 'Dunia' iliyozungumzwa kwenye *Biblia*. Bibi Titi anakiri kwamba, Mwenyezi Mungu amemuumba na kumleta duniani, katika nchi ya Tanganyika kwa lengo lake.

### 4. 2. 5. 6 Muhtasari

Kwa jumla, matokeo ya utafiti huu yamebaini kwamba mandhari za Biblia zimejitokeza katika tamthiliya teule tulizotafiti isipokuwa tamthiliya moja pekee, *Mtumwa hadi Siti Binti Saad.* Katika tamthiliya hiyo hatukubaini mandhari yoyote yenye mwangwi wa Biblia kama tulivyowasilisha.

Vilevile kwenye kipengele hiki tumebainisha fani za Biblia zilizojitokeza katika matini teule tulizotafiti, lengo mahsusi la kwanza. Matini za Biblia tulizobainisha katika tamthiliya teule tulizotafiti ni hizi zifuatazo: Nukuu za Biblia; Wahusika wa Biblia; Simulizi za Biblia; Sajili ya Biblia na Mandhari ya Biblia.

Hali kadhalika tumeeleza sababu za kujitokeza kwa fani za Biblia katika matini teule tulizotafiti kwa minajili ya kutimiza lengo mahsusi la pili la utafiti huu. Nadharia ya Mwingilianomatini ndiyo ilikuwa dira ya kukamilisha malengo mahsusi mawili tuliyoyawasilisha mtawalia. Mosi, kubainisha fani za Biblia katika matini teule. Pili, kueleza sababu za kujitokeza kwa fani za Biblia katika tamthiliya teule.

## 4. 3 Dhamira Zilizowasilishwa kupitia Fani za Biblia Zilizobainishwa katika Tamthiliya Teule

Lengo mahsusi la tatu katika utafiti huu tuliofanya lilikuwa kubainisha dhamira zinazodhihirika kutokana na fani za Biblia katika tamthiliya teule tulizotafiti. Lengo hili liliegema katika mihimili ya Nadharia ya Mwingilianomatini inayoeleza namna ya kubaini maana katika matini za fasihi. Mihimili mahsusi ya Nadharia ya Mwingilianomatini iliyotuongoza katika kuchambua dhamira hizi ni hii ifuatayo;

i. Maana ya matini haipatikani katika matini inayochunguzwa pekee, bali inajengwa na msomaji katika matini husika na mseto wa matini nyingine zinazotajwa na kurejelewa katika usomaji huo (Coyle, 1990). Mwanazuoni huyu anaeleza kuwa matini za fasihi ni zao la matini nyingi tangulizi. Hivyo hurejea matini nyingine. Hivyo basi, ili msomaji abaini maana ya matini anapaswa kuhusisha matini anayosoma na matini nyingine zinazorejelewa katika kazi teule.

ii. Matini ya fasihi yoyote imefumwa kama mseto wa unukuzi, na matini yoyote inahusiana na matini nyingine. Kwa vile matini hizo huhusiana na kuathiriana basi kuielewa matini kunachagizwa na matini nyingine aliyokutana nayo msomaji awali (Clayston na Rothstein, 1991). Wanazuoni hawa wanatanabaisha kuwa usukaji wa maana ya matini huchagizwa na matini nyingine tangulizi.

iii. Mawasiliano baina ya mwandishi na hadhira yake huambatana na mwingiliano uliopo baina ya maneno na namna yalivyokuwa yakitumika katika matini za awali (Wamitila, 2002). Mwanazuoni huyu amefanya tubaini kuwa, maneno yalivyokuwa yakitumika awali katika matini tangulizi kuwasilisha dhamira fulani, yakisikika tena katika matini fuatizi yanaweza kuwa dira kwa hadhira kubaini maana inayoelezwa katika matini iliyo mkononi mwa msomaji.

Matini yoyote hujumuisha ishara fulani ili kuzalisha maana katika matini lengwa (Kristeva,1980). Mwanafalsafa huyu anaendelea kueleza kuwa hadhira ikihusisha fani katika matini teule nje ya matini inayosomwa, itabaini dhamira mbalimbali anazowasilisha mtunzi wa matini.

Tumejulishwa na wanamwingilianomatini kwamba, ili hadhira ielewe kazi yoyote ni muhimu kuhusisha kazi hiyo na vipengele vingine nje ya muktadha wa usomaji huo au usimulizi (Wafula na Njogu, 2007). Tamthiliya teule tulizotafiti zimetumia fani za Biblia. Hadhira ikihusisha vipengele hivyo katika matini teule na jinsi vilivyotumika awali katika Biblia, nje ya muktadha itabaini dhamira lengwa. Utafiti umebaini kwamba, msomaji yeyote ambaye alishakutana na Biblia awali, akizisoma tamthiliya teule atabaini dhamira mbalimbali anazowasilisha mtunzi teule kupitia fani hizo.

Fani ni kibebeo cha maudhui (Ponera, 2019). Mtafiti huyo anaendelea kueleza kuwa matumizi ya fani yanaathiriwa na dhamira anazotaka kuwasilisha mtunzi kwa hadhira. Ponera (Ktj) anakubali kuwa fani anazotumia mtunzi wa matini ya fasihi hulenga kuwasilisha dhamira fulani mahsusi.

Hali kadhalika mwanazuoni huyo anaunga mkono dai la washadidi wa Nadharia ya Mwingilianomatini kuhusu athari ya matini tangulizi katika kubaini maana za matini fuatizi. Kwamba, hadhira ikihusisha vipengele vingine nje ya muktadha husika katika matini inayochunguzwa inaweza kubaini maana, dhamira katika matini inayosomwa.

Mningo (2015), anaeleza kwamba mtunzi teule wa fasihi hutumia fani kuwasilisha dhamira mbalimbmali kwa hadhira lengwa. Hivyo basi fani za Biblia zilizojitokeza katika tamthiliya teule ziliwasilishwa kama ngazi ya kufikisha dhamira kwa hadhira lengwa. Kila fani ya Biblia iliyotumika katika bunilizi teule ililenga kuwasilisha dhamira fulani kwa hadhira.

Maelezo anayotoa mwanazuoni huyu kuhusu uhusiano wa fani na maudhui yanadhihirisha kuwepo kwa fani za Biblia katika tamthiliya teule tulizotafiti. Washadidi wa mwingilianomatini wanasisitiza kwamba fani hizo zikihusishwa na msomaji wakati wa kupitia tamthiliya teule zinaweza kudhihirisha dhamira fulani mahsusi katika matini. Kimsingi hadhira ikizihusisha fani za Biblia zilizojitokeza katika tamthiliya inayosomwa au kuchezwa jukwaani, inaweza kubaini dhamira mbalimbali zinazodhihirika katika matini hiyo.

Fasihi ni sanaa inayotumia lugha na ambayo hujishughulisha na binadamu pamoja na maisha yake na huathiri, hugusa au kuacha athari fulani na hupatikana katika umbo ambalo hutambuliwa na jamii fulani (Wamitila, 2008). Kupitia mwanazuoni huyu tunabaini kwamba, fasihi ni zao ama tokeo la jamii. Hivyo, mambo mbalimbali yanayotendeka katika jamii, huakisiwa ndani ya kazi iliyobuniwa na mtunzi.

Vilevile tamaduni za jamii hudhihirika katika kazi za fasihi (Omukabe, 2020). Mila na desturi hudhihirika ndani ya kazi za fasihi. Katika kazi za fasihi tunaweza kukutana na habari za dini, mapenzi na ndoa, maadili, desturi/sheria, tabia, kazi za sanaa n.k.

Katika sehemu inayofuata tumetimiza lengo mahsusi la tatu katika utafiti huu tuliofanya. Mtafiti amebainisha dhamira mbalimbali zinazodhihirika kupitia fani za Biblia zilizojitokeza katika tamthiliya teule tulizotafiti. Dhamira hizo zimewasilishwa kwa kuhusisha fani za Biblia zilizojitokeza katika tamthiliya za mtunzi teule, Emmanuel Mbogo. Rejea za kushadidia hoja kwenye uchambuzi huu zimehusisha tamthiliya zote teule kadri zilivyojitokeza.

### 4. 3. 1 Nafasi ya Dua na Sala katika Jamii

Dini ni mfumo wa imani, mila na alama zilizoanzishwa karibu na wazo la alama la uungu au katika utakatifu (Sanchez, 2021). Kupitia maelezo ya mwanazuoni huyu tunabaini kuwa, dini ndiyo mafundisho ambayo yanamuunganisha Mungu na mwanadamu. Kupitia dini, mwanadamu huamini akifanya dua na sala ndiyo awasiliana na Mwenyezi Mungu.

Dhana ya dua ama sala inaelezwa kama njia mbalimbali anazotumia mwanadamu kuwasiliana na Mungu, miungu anayoamini (Katubayemo, 2022). Mwalimu huyo anaendelea kueleza, mwanadamu huamini kuwa anafanya mawasiliano na Mungu wake anayemuani. Mawasiliano baina ya Mungu na mwanadamu ndiyo hukamilishwa kwa njia ya dua au sala. Mwanadamu huamini kuwa Mungu anaweza kumuokoa katika kadhia, shida mbalimbali anazokumbana nazo katika safari ya maisha hapa Ulimwenguni kila uchao.

Fasihi kama kioo cha jamii hutuchorea taswira ya uhalisi wa maisha ya binadamu (Madumulla, 2009). Hali hii ndiyo inayochagiza tuone namna mila, desturi, imani, maadili, sanaa, sayansi na teknolojia zinavyotendwa katika jamii kupitia kazi za fasihi. Fasihi simulizi pamoja na fasihi andishi zote hujumuisha tamaduni za jamii fulani mahsusi. Dini kama sehemu ya utamaduni huonekana katika fasihi ya Kiswahili. Hivyo fasihi ya Kiswahili huonyesha pia shughuli za kidini zinavyofanywa kama vile dua na sala kwa waumini na dhamira nyingine mbalimbali zinazowasilishwa kuihusu (Wamitila, 2003).

Katika tamthiliya ya *Wangari Maathai* (2015) dhamira ya dua na sala kwa waumini wa dini inajitokeza kupitia fani za Biblia. Mtunzi ametumia sajili ya Biblia inayorejea dua na sala wanazofanya wanajamii kwa Mwenyezi Mungu. Mgogoro ulioibuliwa baina ya wahusika wawili katika tamthiliya hii; Mwangii na Wangari ambao ni mume na mke suluhu yake imeelekezwa kwenye imani za kidini. Mhusika anaweka bayana kuwa dua na sala ndiyo tiba ya shida inayomkabili mke wake, Wangari. Dhamira hiyo imehusishwa namna hii;

64) MWANGII: *Umepagawa na pepo Wangari.*
*Unahitaji maombi. Jini mahaba amekuingia*
(Uk.6)

Katika maelezo ya Mwangii, mtunzi ametumia maneno yenye mwangwi wa Biblia. Mathalani, 'kupagawa pepo', 'maombi' na 'jini mahaba'. Maneno haya yanadhihirisha dhamira ya kidini, kwamba dua kwa Mwenyezi Mungu ndiyo dawa dhidi ya mateso yote kwa mwanadamu. Mgogoro ulioko baina ya wanandoa hawa; Wangari na Mwangii suluhu yake imehusishwa na kutatuliwa kupitia kudra za Mwenyezi Mungu. Familia zinafundishwa kumwomba Mwenyezi Mungu ili ziwe salama. Mapepo, majini yanayosemwa na Mwangii dawa yake ni kufanya dua, sala kwa Mwenyezi Mungu.

Wasomaji wa tamthiliya ya *Wangari Maathai* waliowahi kukutana na Biblia wakihusisha maneno hayo na jinsi yalivyotumika katika matini tangulizi, Biblia wanaweza kubaini dhamira hii. Maneno hayo yalitumika awali katika Biblia mitume wakifundisha waamini wa Kiyahudi kuhusu nafasi ya maombi katika kupambana na mitihani ya maisha. Maombi katika Biblia yameelezwa kama silaha ya kupambana na maadui katika maisha.

Kwa mfano ndani ya Biblia, kuna kisa cha mtu mmoja, Mgerasi kuondolewa mapepo na majini alipoombewa na Yesu Kristo, mtume wa Wayahudi. Biblia inaandika;

> *"Na hapo palikuwa na mwanamke mmoja aliyekuwa mgonjwa kwa miaka kumi na minane kutokana na pepo aliyekuwa amempagaa. Kwa sababu hiyo, mwili wake ulikuwa umepindika vibaya hata asiweze kusimama wima. Yesu alipomwona, alimwita, akamwambia, "Mama, umeponywa ugonjwa wako."*
> *Akamwekea mikono, na mara mwili wake ukawa wima tena, akawa anamtukuza Mungu."*
> (Luka Mtakatifu 13: 11 – 13)

Hadhira iliyowahi kukutana na maneno ya '*maombi, mapepo na majini*' kwenye Biblia inaweza kubaini dhamira hii. Kwani maneno hayo yalitumika katika masomo ya kufundisha watu kumuomba Mwenyezi Mungu. Pia walifundishwa kwamba Mungu hana yanayomshinda hata akiamuru mapepo, majini yamtoke mtu, hufanya hivyo.

Wamitila (2002) anatambulisha mhimili wa Nadharia ya Mwingilianomatini unaosema, mawasiliano baina ya mwandishi na hadhira yake huambatana na mwingiliano uliopo baina ya maneno na namna yalivyokuwa yakitumika katika matini za awali. Kupitia mhimili huu tunabaini kuwa maana ya matini inaweza kubainika kwa hadhira kuhusisha maneno inayokutana nayo katika matini iliyo mkononi na jinsi yalivyotumika katika matini tangulizi. Misamiati ya Biblia iliyotumika katika tamthiliya hii ilitumika awali katika Biblia kuzungumza nafasi ya maombi kwa waamini wa Kikristo. Hivyo dhamira iliyoibuliwa awali inaweza kunasibishwa nah ii inayowasilishwa sasa.

Vilevile Sajili za Biblia alizotumia Mbogo katika tamthiliya ya *Wangari Maathai*: 'Umepagawa na pepo Wangari'; 'Jini Mahaba amekuingia' na 'Unahitaji maombi'

zinadhihirisha dhamira hii, umuhimu wa maombi kwa waamini. Sajili hizo zilitumika awali kwenye Biblia kudhihirisha dhamira hiyo. Hadhira ikihusisha sajili hizo na jinsi zilivyotumika awali katika Biblia, ikirejelea kisa cha Mgerasi aliyepagawa na mapepo, akaponywa majini kwa kuombewa na Mtume Yesu Kristo inabaini dhamira anayowasilisha mtunzi. Nafasi ya dini imeelezwa katika tamthiliya hii kama tulivyobainisha, tukiegema mhimili wa Nadharia ya Mwingilianomatini.

### 4. 3. 2 Nafasi ya Viongozi wa Dini katika Jamii

Hali kadhalika dhamira ya nafasi ya viongozi wa dini katika jamii imewasilishwa katika matini teule tulizotafiti. Japhet (2017) anasema, "Viongozi wa dini ni waumini wa dini walioitwa na Mungu kusimamia, kulinda, kufundisha na kuongoza waumini wengine." Mtafiti huyu anatusaidia kuelewa kwamba watu wanaoongoza na kuratibu shughuli za kiimani katika imani mbalimbali ndiyo hutambulika kama viongozi wa dini. Vilevile Japhet (Ktj) anaeleza kuwa viongozi wa dini hupatikana kwa njia ya kuitwa na Mungu moja kwa moja kama ilivyokuwa kwa manabii tangulizi hapo kale au kwa kuitwa na Mungu kupitia kuchaguliwa na waumini wenzao kama ilinavyofanyika kwa mashemasi, wazee wa kanisa katika zama hizi mpya.

Pamoja naye, Guterres (2022) anaeleza kuwa serikali nyingi katika mataifa mbalimbali zinashirikisha viongozi wa dini katika shughuli zake za utawala. Katibu huyo wa Umoja wa Mataifa sasa anaendelea kueleza kwamba pahala pengine viongozi wa dini wametumika katika kuimarisha amani, kutoa elimu, kutetea wanaoonewa, kutoa huduma za afya na harakati mbalimbali kuhusu haki za binadamu. Kiongozi huyu wa Umoja wa Mataifa (UN) anatujulisha kuwa yako

mahusiano baina ya viongozi wa kisiasa na viongozi wa dini. Kupitia andiko lake tunajifunza kwamba viongozi hawa hushirikiana katika shughuli mbalimbali ndani ya taifa kwa minajili ya maendeleo ya nchi zao.

Matokeo ya utafiti yamebaini dhamira ya nafasi ya viongozi katika jamii katika tamthiliya ya *Wangari Maathai* (2015). Katika jamii zetu hapa ulimwenguni, mathalani nchini Kenya na Afrika kwa ujumla viongozi wa dini hushirikishwa katika matukio mbalimbali ya kitaifa. Katika nchi nyingine viongozi wa dini hutambulika kama washauri wa rais, serikali kuu inayoongoza nchi (Mwamakula, 2022).

Katika tamthiliya ya *Wangari Maathai* (2015) mtunzi ameonyesha namna viongozi wa dini wanavyoshirikishwa na serikali zao katika matukio mbalimbali ya kitaifa. Mathalani matukio ya kusimika viongozi na kutoa tuzo za kitaifa kwa wananchi waliofanya mambo mazuri ndani ya nchi. Katika tamthiliya hii Mchungaji Nyoya 'Pasta Njoya' ametumika kuwasilisha dhamira hii, kuonyesha nafasi ya viongozi wa dini katika jamii. Kama ifuatavyo;

65) MUITE: *"...Sasa tunamuomba Pasta Timothy Njoya aje hapa ili akamilishe halfa hii ya leo. [Pastor anaenda mbele]* (Uk. 5)

Katika tamthiliya hii, Pasta Njoya amealikwa na serikali ya Kenya kwenye halfa ya kumpongeza Wangari kwa kutunukiwa tuzo ya kimataifa 'Nobel Peace Prize'. Nchi ya Kenya imeona fahari kubwa kwa tendo hilo. Taifa linaamua kumpongeza Wangari kwa heshima kubwa aliyoipa nchi. Katika kukamilisha tukio hilo, kiongozi wa dini, 'Pastor Njoya' amealikwa kushiriki. Matumizi ya mhusika huyo, kiongozi wa kanisa katika tukio hilo la kitaifa yamedhihirisha dhamira ya nafasi viongozi wa dini katika jamii. Kuanzia ngazi ya mtu binafsi hadi serikali kuu.

Mningo (2015) akimrejea Kristeva (1980) anasema, "Mwingilianomatini unahusishwa na jumla ya maarifa na mbinu zinazoifanya matini kuwa na maana, ambapo maana ya matini huangaliwa kama inayotegemea matini nyingine kwa kile kinachoitwa 'Mwanda wa Ki-mwingilianomatini'." Mwanazuoni huyu anashadidia kwamba ili matini ieleweke, inatakiwa ihusiane na matini nyingine. Hadhira ikihusisha fani zinazotumika katika matini inayowasilishwa na matini nyingine ndiyo hubaini dhamira za matini inayosomwa.

Waandishi wa Biblia wamejadili pia nafasi ya viongozi wa dini katika jamii wakihusisha zaidi taifa la Israel. Biblia inabainisha kuwa viongozi wa dini pia hushiriki katika shughuli za utawala, serikali. Katika taifa hilo viongozi wa kitaifa, Wafalme wanasimikwa na manabii, viongozi wa dini.

Kwa mfano, hapo kale ili mtu awe Mfalme wa Israel, kiongozi wa dini, nabii alitumwa na Mwenyezi Mungu kumuidhinisha kwamba, yeye ndiye Mfalme, mtawala mpya. Katika Biblia, Mfalme Daudi aliidhinishwa, alisimikwa na kiongozi wa dini, Nabii Samweli. Nabii huyo anatajwa kumpa uongozi Mfalme Daudi, kijana mdogo kutoka katika familia ya Mzee Yese huko Uyahudi. Biblia inaandika;

> *"... Basi Samweli akamwambia Yese, Tuma watu, wamlete; ... Ndipo Samweli akaitwaa pembe yenye mafuta, akamtia mafuta kati ya ndugu zake; na roho ya BWANA ikamjilia Daudi kwa nguvu tangu siku ile ..."*
>
> (1Samweli 16: 11 – 13)

Matumizi ya mhusika Pastor Njoya, kiongozi wa dini katika tamthiliya ya *Wangari Maathai* ndiyo yalibeba dhamira hii. Mtunzi amemtumia mhusika huyo kuonyesha

nafasi ya viongozi wa dini katika jamii. Kwamba, viongozi hao hawashiriki katika shughuli za misa pekee katika nyumba za ibada bali hushiriki pia katika shughuli mbalimbali za kitaifa au kiutawala nchini.

Hadhira ikihusisha uhusika wa Pastor Njoya katika tamthiliya ya *Wangari Maathai* na uhusika wa Nabii Samweli katika Biblia, inabaini dhamira inayoelezwa. Wajibu alioufanya Nabii Samweli kwa viongozi wa taifa la Israel, unadhihirisha nafasi ya viongozi wa dini katika jamii. Hadhira ikihusisha ilichoona awali katika Biblia kwa Nabii Samweli na mhusika Pastor Nyoja, katika tamthiliya hii inabaini nafasi ya viongozi wa dini katika taifa.

Kimsingi, matumizi ya mhusika Pastor Njoya yamedhihirisha dhamira ya nafsi ya viongozi wa dini katika jamii. Kwamba viongozi wa dini katika jamii wana wajibu mbalimbali zaidi ya kutumika tu katika nyumba za misa, ibada kwenye makutano ya waamini mbalimbali. Viongozi hao huweza kushirikishwa na watawala wa kisiasa katika shughuli mbalimbali za kisiasa kama tulivyobainisha.

### 4. 3. 3 Uadilifu na Unyenyekevu katika Jamii

Fauka ya hayo dhamira nyingine iliyojadiliwa kupitia fani za Biblia zilizojitokeza katika matini teule ni uadifu na unyenyekevu katika jamii. Uadilifu ni nini? Uadilifu ni uwezo wa mtumishi wa umma kuwa na maadili kama vile kuzingatia taaluma, kuwa mwaminifu na kuwa mwajibikaji (Mollel, 2006). Mama huyo aliyekuwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma miaka ya 2006 anaendelea kueleza kuwa, mambo hayo yote yakizingatiwa humfanya mtumishi kuwa mwadilifu. Kupitia maelezo ya kiongozi huyu tunajifunza kwamba, uadilifu ni

uwezo wa mtu kufanya kilicho sahihi, anachostahili mahali anapohudumu katika jamii.

Vilevile Bakize (2018) anaeleza kuwa maadili ni mwenendo mwema katika maisha. Mtu akifanya kilicho sahihi mbele za umma, hupewa anuani ya kuwa na maadili mema. Vilevile mtu akifanya kisicho sahihi katika jamii, hupewa anuani ya kuwa na maadili potofu.

Unyenyekevu ni nini? Tukijibu swali hili litakuwa nuru njema katika mjadala wa dhamira tunaouendea. Unyenyekevu ni hali ya kujishusha iliyo ndani ya moyo wa mtu licha ya hadhi aliyonayo au kiwango alichonacho mbele za watu (Myinga, 2019). Mtafiti huyu anaendelea kueleza dhana ya unyenyekevu kama hali ya mtu kuinua kiwango cha thamani ya watu wengine na kuwaleta katika hadhi au daraja aliloko. Kwamba, mnyenyekevu huwaona watu wengine kuwa na thamani na hadhi kubwa kama yake au hata zaidi yake.

Hivyo basi, dhana ya unyenyekevu inaweza kuelezwa kama hali ya kujishusha na kuwa tayari kutumika kwa daraja lisilostahili bila kiburi wala majivuno. Watu wanaoishi bila kiburi wala majivuno huweza kukubaliwa sana katika jamii. Watu hao huonekana kuwa wema.

Ni ndoto ya jamii nyingi ulimwenguni watu wake waishi kwa kufanya mambo sahihi, yanayopaswa ili jamii zao ziwe pahala pazuri pa kuishi. Jamii inatamani kuwa na watu wema wanaoishi bila kiburi na majivuno mtimani mwao. Watunzi wa fasihi ya Kiswahili katika tanzu za nathari na ushairi wamejadili dhamira ya uadilifu na unyenyekevu wa wanajamii kwa namna mbalimbali. Tunahitimisha kwamba dhamira

hii imejitokeza katika fasihi ya Kiswahili tangu kale. Baadhi ya waandishi wanaowasilisha dhamira hii katika bunilizi zao ni hawa; Kunemah (2008), Mnyagatwa (2015), Mbogo (2010) na wengine wengi.

Kupitia utafiti huu tulitumia tamthiliya ya *Malkia Bibi Titi Mohamed* (2016) kubainisha dhamira zinazodhihirika katika fani za Biblia zilizojitokeza ndani yake. Matokeo ya utafiti yamebaini dhamira ya uadilifu na unyenyekevu kwa wanajamii. Mtunzi teule amefundisha hadhira lengwa kuwa waadilifu na wanyenyekevu akiegema kwenye fani za Biblia.

Mbogo katika tamthiliya hii anaelekeza hadhira kuwa waadilifu na wanyenyekevu katika jamii. Wanajamii wanajifunza kuishi kwa kufuata kanuni zilizowekwa na mamlaka na kuthamini wenzao katika jumuiya mbalimbali wanazochangamana nazo. Katika kuwasilisha dhamira hii mtunzi ametumia sajili ya Biblia, akihusisha kipengele cha sitiari. Bibi Titi akifananishwa na Mungu, mwenye uwezo wa kila jambo.

Sitiari iliyotumika, kumfananisha Bibi Titi na Mwenyezi Mungu inadhihirisha dhamira ya uadilifu na unyenyekevu katika tamthiliya hii. Biblia inaelekeza waumini kuwa waadilifu na wanyenyekevu mbele za Mungu na jumuiya yote kwa kuwa Mungu Mwenyezi ndiye muweza wa yote.

Mazungumzo baina ya Christina na Bibi Titi yameakisi dhamira hii. Christina anamsihi Bibi Titi kuwa mwadilifu na mnyenyekevu mbele za wenzake, katika jamii. Bibi Titi anakumbushwa kwamba anapaswa kuwa mwadilifu na mnyenyekevu kwa

wenzake kwani hana uwezo wa kufanya mambo makubwa kama Mwenyezi Mungu alivyo. Sitiari yenye dhamira hii inawasilishwa namna hii;

66) CHRISTINA: *Mtakuwa mmeitoa wapi? Mliiumba?*
*Bibi Titi acha kujifanya Mungu.*
(Uk. 2)

Hali kadhalika katika kitabu cha Biblia, simulizi za Mwenyezi Mungu kumuumba mwanadamu na viumbe wote inasemwa katika kitabu cha Mwanzo (1: 1 - 25). Kitabu hicho kilichoandikwa na Nabii Musa kinaeleza habari zote kuhusu uumbaji wa mwanadamu, mbingu, nchi na viumbe wote kama jamii ya Wayahudi wanavyoamini. Biblia inaeleza;

> *"Hapo mwanzo Mungu aliumba mbingu na dunia. Dunia ilikuwa haina umbo tena ilikuwa tupu, giza lilikuwa juu ya uso wa vilindi vya maji, naye Roho wa Mungu alikuwa ametanda juu ya maji…''*
> *(Mwanzo 1: 1 – 5)*

Washadidi wa Nadharia ya Mwingilianomatini wanaeleza kuwa, uelewaji wa kazi ya fasihi; riwaya, tamthiliya au ushairi hutegemea kuwako kwa kazi nyingine kabla ya kazi maalum inayochunguzwa (Wamitila, 2002). Hivyo basi, matini tangulizi huchagiza uelewaji wa matini mpya anayokutana nayo hadhira mahsusi.

Hadhira iliyowahi kukutana na Biblia awali kisha ikakutana na simulizi za uumbaji katika tamthiliya hii inaweza kubaini dhamira ya uadilifu na unyenyekevu katika matini mpya. Sajili na simulizi ya Biblia zilizonukiliwa katika tamthiliya hii, zilitumika awali kwenye kitabu hicho kufundisha uadilifu na unyenyekevu mbele za Mungu na jamii yote kwa jumla.

Kimsingi, hadhira ikihusisha fani zilizojitokeza katika matini kuzungumza kuhusu dhamira ya uadilifu na unyenyekevu ndani ya jamii katika matini tangulizi ilizosoma,

itabaini dhamira inayowasilishwa na mtunzi. Mathalani simulizi za uumbaji wa mwanadamu na sajili ya Biblia. Hadhira watabaini kuwa wanapaswa kuishi kwa uadilifu na unyenyekevu. Dhamira hiyo imehusishwa na uweza wa Mwenyezi Mungu kufanya mambo yote. Bibi Titi anakumbushwa na Christina kujishusha mbele za wenzake. Mhusika Bibi Titi anaelezwa asijikweze kwani hana uwezo wa kufanya mambo makubwa kuliko Mwenyezi Mungu. Simulizi na Sajili za Biblia zilizojitokeza zinadhihirisha dhamira hii tuliyojadili, uadilifu na unyenyekevu kwa wanajamii.

### 4. 3. 4 Kutokukata Tamaa katika Maisha

Aidha matokeo ya utafiti huu yamebaini kuwa, mtunzi teule ameeleza dhamira ya kutokukata tamaa katika maisha katika tamthiliya tulizotafiti. Kukata tamaa ni nini? Kukata tamaa ni hali ya mtu kupoteza matumaini baada ya kushindwa kupata suluhu, njia ambayo ingeweza kumfanya atatue au ajitoe katika matatizo au changamoto inayomkabili (Fungavyema, 2020). Mtheolojia huyu anaeleza kuwa katika hali halisi, kukata tamaa ni hali ya kaida katika maisha na humtokea kila mwanadamu kwa namna moja au nyingine.

Fungavyema (2020) anaendelea kueleza kuwa, hali ya kukata tamaa huathiri sana watu wengine, hata kufikia pahala wakapoteza mwelekeo wa kitu wanachokipambania. Pamoja na hayo tunaelezwa pia kuwa wapo watu ambao huwa wastahimilivu katika dhiki wanazopitia. Watu hao hupambana hadi kupata suluhu ya hitaji lao hata wakaishia kupata ushindi.

Vilevile Mwananchi (2021) wanaeleza kuwa wanajamii katika maisha yao ya kila siku hukutana na mambo mazuri na kwa upande mwingine matatizo ambayo hukatisha tamaa. Matatizo yanayowakabili wananchi yanaweza kuwa; kifo, umaskini, magonjwa, vita, kufukuzwa kazi na kufilisika. Pamoja na hayo changamoto za kutengwa, kukataliwa, kunyanyapaliwa, migogoro ya ndoa, kuonewa, kunyanyaswa na kukandamizwa yanawakabili watu kila uchao katika uso wa ulimwengu. Changamoto hizo zinapotukia hupelekea watu kupata magonjwa yanayotokana na msongo wa mawazo kama vile kisukari, shinikizo la damu, matatizo ya moyo, magonjwa ya akili na kiharusi.

Fasihi ni mwarobaini wa matatizo ya kiafya (Mosha, 2021). Mwanazuoni huyu kutoka Taasisi ya Taaluma za Kiswahili – TATAKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam anaeleza kuwa, riwaya za Kiswahili zimeonekana kuwa tiba murua kwa watu wanaokabiliwa na changamoto za kiafya, hasa zinazohusu saikolojia. Kazi za fasihi zimeonekana kuhusisha fani mbalimbali ambazo msomaji akizisoma, anapata nguvu mpya ya kuendelea mbele na maisha. Kwa mfano matumizi ya wahusika ambao hupambana na vita kali lakini mwishoni wanapata ushindi. Matumizi ya visa vinavyoeleza habari za watu walivunjika moyo, lakini walipovumilia mwishoni wakapata suluhu ya mateso yao.

Riwaya za Kisaikolojia ni dawa njema kwa watu waliokata tamaa. Mosha (2021) anaeleza kuwa baadhi ya riwaya zinazoingia katika mkondo huu ni *Rosa Mistika*, *Kichwamaji* (E. Kezilahabi), *Nyota ya Rehema*, *Tata za Asumini* (S. Mohamed), *Msimu wa Vipepeo* (K. Wamitila) na nyingine nyingi.

Mosha (2021) alijadili dhamira ya kutokukata tamaa katika maisha kupitia riwaya za Kiswahili. Utafiti huu umechunguza dhamira hiyo katika tamthiliya za Kiswahili. Mwanazuoni huyo ametuwezesha kung'amua kuwa fasihi ya Kiswahili imeeleza dhamira hii ya kutokukata tamaa katika maisha kutokana na masaibu mbalimbali. Yeye alitazama utanzu wa riwaya, sisi tumetazama utanzu wa tamthiliya. Hili limeongeza maarifa katika uga wa fasihi ya Kiswahili kama tulivyowasilisha.

Matokeo ya utafiti huu yamebaini dhamira ya kutokukata tamaa katika maisha katika tamthiliya ya *Malkia Bibi Titi Mohamed* (2016). Fani za Biblia zilizojitokeza katika tamthiliya hii zinaelekeza watu kuishi kwa matumaini. Wanajamii kuweka tumaini kwa Mola katika changamoto mbalimbali wanazopitia humu ulimwenguni. Fani za Biblia zilizojitokeza katika tamthiliya hii zinawasilisha dhamira hiyo barabara.

Mtunzi anaeleza jamii kuwa, ikimtegemea Mola katika mateso inayopitia ipo siku itashinda changamoto zinazojili kila uchao kwenye maisha yao. Hali kadhalika jamii inafundishwa kuwa ili kufikia lengo maishani jamii inapaswa kujipa moyo, kwani changamoto ni sehemu ya maisha ya mwanadamu.

Mtunzi teule katika tamthiliya hii amemchorwa mhusika Bibi Titi akitamba mbele ya wenzake kwamba, kwa kuwa Mungu alimuumba na kumuweka Tanganyika basi lazima atapambana hadi Tanganyika ipate uhuru. Bibi Titi anashadidia kuwa, Mwenyezi Mungu alimleta Tanganyika ili awe ngazi ya kuipatia uhuru nchi hiyo. Bibi Titi anasema;

67) BITITITI: …*Yale makusudi ya Mola wangu*
*Kuniumba na kunileta duniani ili*
*Niupiganie uhuru wa Tanganyika*
*Ima faima lazima yatimie.* (Uk. 49)

Bibi Titi katika mazungumzo haya anawasilisha dhamira ya kutokukata tamaa katika maisha. Mhusika huyo anajipa moyo dhidi ya changamoto zinazomkabili katika harakati za kupigania uhuru wa Tanganyika. Bibi Titi anakubali kuwa kuna changamoto kali zinazowakabili katika kupigania uhuru wa nchi. Hata hivyo mhusika huyo anajipa moyo, anajitia tumaini kwamba hatarudi nyuma. Mhusika anaapa kuwa atapambana hadi nchi ya Tanganyika ipate uhuru inaoutafuta kutoka kwa Muingereza kitambo sasa.

Mtunzi teule, Emmanuel Mbogo amenukuu semi kutoka kwenye Biblia kuhusu lengo la Mwenyezi Mungu kumuumba mwanadamu. Biblia inaeleza kuwa kila mwanadamu aliyeko hapa duniani, Mwenyezi Mungu alimuumba kwa lengo mahsusi. Kwa kutambua hilo Bibi Titi naye anakiri kuumbwa na kuletwa Tanganyika kwa lengo mahsusi, kuipatia Tanganyika uhuru. Mhusika huyo anasema, *'Yale makusudi ya Mola wangu kuniumba na kunileta duniani ili niupiganie uhuru wa Tanganyika ima faima lazima yatimie".*

Dai analoeleza Bibi Titi kuhusu lengo la Mwenyezi Mungu kumuumba limeelezwa awali kwenye Biblia. Mfalme Suleimani, kiongozi wa Wayahudi hapo kale ndiye ametoa fundisho hilo kwa Wayahudi, wananchi anaotawala. Mfalme anawajulisha Wayahudi kuwa, kila mtu ulimwenguni ameumbwa kwa kusudi maalum hata watu wabaya waliumbwa kwa lengo la kutimiza ubaya siku ikifika. Hivyo anawaasa kuishi kwa kuchukuliana. Mfalme Suleiman anasema;

> "*Bwana amefanya kila mtu kwa kusudi lake; naam hata wabaya kwa siku ya ubaya"*
> (Mithali 16:4)

Wahakiki wa Nadharia ya Mwingilianomatini wanaeleza kuwa, matini za kisanaa uhusiana na kutegemeana kwa njia moja ama nyingine ili kuzalisha maana (Kristeva, 1986). Mhimili huu unaeleza kuwa, hadhira inaweza kung'amua maana ya matini iliyoko kiganjani kwa kuihusianisha matini hiyo na matini nyingine.

Dhamira ya kutokukata tamaa maishani imejadiliwa awali katika matini ya Biblia. Semi ya Biblia aliyoitumia mtunzi teule, kuhusu lengo la Mwenyezi Mungu kumuumba mwanadamu yeyote limeelezwa awali katika Biblia. Katika matini hiyo watu mbalimbali huko Uyahudi walikumbana na mateso katika maisha lakini hatimaye walifanikiwa. Mfano: Ibrahim, Yusuf Yakobo, Nabii Musa, Samson, Daniel, Shedrak, Meshaki, Abednego, Ayubu na wengineo. Wahusika hao wote walikabiliwa na masaibu mbalimbali lakini waliishia kwenye ushindi.

Emmanuel Mbogo katika tamthiliya hii, anafundisha hadhira kutokukata tamaa kwenye mateso mbalimbali wanayokabiliana nayo kila uchao. Hadhira ikihusisha semi ya Biblia iliyotumika katika tamthiliya hii na jinsi ilivyotumika katika Biblia inabaini dhamira ya kutokukata tamaa katika maisha. Mfalme Suleiman alikuwa akiwatia moyo Wayahudi kwamba waishi kwa matumaini, wasikate tamaa.

Mfalme Suleiman alishadidia kuwa lengo la Mwenyezi Mungu kumuumba mwanadamu yeyote ni jema pia lazima litimie tu. Hakuna jambo la kulibatilisha lengo hilo. Kiongozi huyo wa Wayahudi akawatia moyo wanaokutana na magumu katika maisha kutokata tamaa.

Kwa hivyo, katika mazungumzo ya Bibi Titi hadhira wanaelezwa kujithamini na kupigania ndoto zao hata wafanikiwe katika maisha. Changamoto zote

zinazowakabili katika maisha zisiwe ukuta wa kufikia malengo yao. Bali wapambane hadi mwisho. Waamini wa dini ya Kikristo katika kitabu cha Biblia, wanafundishwa vivyo pia, wasikate tamaa. Mambo magumu yakiwajia wanapaswa kusimama imara kumuomba Mola na kupambana katika magumu hayo hadi washinde. Tamthiliya hii, Malkia Bibi Titi Mohamed, mhusika mkuu ameapa kupambana hadi Tanganyika ipate uhuru. Ndoto hiyo ilitimia siku moja, Tanganyika ikapata huru 1961.

### 4. 3. 5 Nafasi ya Ubatizo kwa Waumini wa Kikristo

Dhamira nyingine tuliyobaini kupitia fani za Biblia zinazotumika katika tamthiliya teule ni nafasi ya ubatizo kwa waumini wa Kikristo. Ubatizo ni nini? Jibu la swali hili litakuwa nuru njema kumsaidia msomaji wa utafiti huu kubaini dhamira inayowasilishwa katika matini teule.

Jamieson (2018) anasema, "Ubatizo ni kitendo cha kanisa kuthibithisha na kuonyesha ushirika wa mkristo na Kristo kwa kumzamisha kwenye maji, na pia ni kitendo cha mkristo kudhihirisha hadharani kujitolea kwake kwa Kristo na watu wake, na kwa hivyo kuunganisha mkristo na kanisa na kumtofautisha na dunia." Mwanazuoni huyu anaendelea kueleza kuwa, Ubatizo ni kitendo kinachoratibiwa na kanisa. Ubatizo ni jambo ambalo mtu, kanisa humfanyia mtu mwingine.

Vilevile ubatizo ni ibada ya kuosha na maji kama ishara ya utakaso, kusafisha inayofanyika kwa namna mbalimbali na wafuasi wa dini ya Kikristo (Fairchild, 2023). Mwandishi huyu anaendelea kueleza kuwa, Ibada hii imefanyika tangu kale hadi sasa. Hivyo kwa namna moja imekuwa sehemu ya utamaduni kwa wafuasi wa dini ya Kikristo. Jambo lililopelekea wafuasi wa Kikristo kuamini hawajakamilika

kiimani wasipobatizwa katika madhehebu wanayoabudu. Maji ndiyo dawa kuu inayotumika kubatiza waumini wa dini ya Kikristo.

Kimsingi, Ubatizo si maji matupu au tendo la kuzamisha mtu kwenye maji pekee, bali ni maji yanayotumika kulingana na amri ya Mungu na kuchangamana na Neno la Mungu. Wakristo wanapofanya ibada hiyo katika imani yao huwa wanatimiza agizo lililotolewa na Mtume wao, Yesu Kristo. Kwamba, kila mfuasi wake atakayemuamini shurti abatizwe.

Matokeo ya utafiti yamebaini dhamira hii, nafasi ya ubatizo kwa waumini wa dini ya Kikristo katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya* (2016). Fani za Biblia zilizotumiwa na mtunzi zimedhihirisha dhamira hiyo. Mtunzi teule katika tamthiliya hii anafundisha Wakristo kwamba, ili imani yao ikamilike wanapaswa kuzingatia mhimili wa ubatizo. Hilo tendo la kubatizwa, Wakristo waliagizwa na mtume wao, Yesu Kristo. Kila mfuasi wake, abatizwe. Familia ya Ndiege katika tamthiliya ya Nyota ya Tom Mboya (2016) inajadili kumpeleka mtoto wao Kanisani ili akabatizwe, kutimiza mhimili na agizo la Kikristo. Ndiege anasema;

68) NGIEGE: *Tutakapompeleka Kanisani kule Romani Katoliki,*
*Mimi nitamwambia Padri ambatize, aitwe Thomas.*
(Uk. 8)

Familia ya Ndiege wamepata mtoto wa kiume katika mji wao. Zoezi la kumpa mtoto jina ndilo limewafanya kukumbuka habari za ubatizo. Waumini wa dini ya Kikristo wanapozaliwa wanapaswa kubatizwa. Wakristo wanapobatizwa hupewa jina jipya linaloendana na misingi ya imani yao. Ndiege amechagua mtoto wake akaitwa ‘Thomas’ ubatizo utakapofanyika.

Yesu Kristo, mtume wa dini ya Kikristo kupitia Biblia alitoa agizo la wafuasi wake kubatizwa. Hivyo basi, wafuasi wa dini ya Kikristo kila mmoja kwa namna yake hutimiza agizo hilo. Agizo la kubatizwa kwa Wakristo katika Biblia linasomeka namna hii;

> *Basi akawaambia, "Nendeni ulimwenguni kote mkahubiri. Habari Njema kwa kila mtu. Anayeamini na kubatizwa ataokolewa; asiyeamini atahukumiwa."*
> (Marko 16:15 – 16)

Yesu aliwatuma wanafunzi wake kwenda ulimwenguni wote kuhubiri habari zake. Pamoja na hayo aliwaasa kubatiza waumini wote wanaomwamini ili waokolewe. Mwinjili Marko Mtakatifu ameeleza agizo hilo kama tulivyonukuu.

Nadharia ya Mwingilianomatini inawahusu wahusika wakuu wote wa kazi za fasihi; watunzi na hadhira (Wafula, 2007). Mwanazuoni huyu anaweka bayana kuwa hadhira huitumia pia Nadharia ya Mwingilianomatini katika kusoma na kubaini maana zinazowasilishwa katika matini wanazochunguza.

Mhimili mojawapo wa Nadharia ya Mwingilianomatini unaeleza kwamba ishara, misamiati fulani inaweza kuleta maana katika kazi ya fasihi. Hadhira anaweza kuhusisha misamiati anayokutana nayo na jinsi zilivyoelezwa katika matini alizokutana nazo awali. Matumizi ya msamiati huu, 'Ubatizo' katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya* yanaashiria umuhimu wake katika dini ya Kikristo. Wakristo wanaaelekezwa kwamba ili mtu akamilike kiimani, awe mfuasi halisi wa Kikristo anapaswa kutimiza nguzo ya ubatizo. Mwamini wa Kikristo anapaswa kwenda Kanisani, kwenye nyumba za ibada kuomba kubatizwa na watumishi wa Mungu kama vile Mapadri (Romani Katoliki), Wachungaji (Lutherani, Pentekoste n.k.)

Kwa hivyo, hadhira inaposoma tamthiliya hii kupitia msamiati uliorejewa ‘ubatizo’, anabaini dhamira hii; nafasi ya ubatizo katika imani ya Kikristo. Dhana hii ilidhihirika awali katika Biblia, ikielezwa kama mhimili mkuu wa mfuasi wa Kristo kukamilika kiimani. Dhana ya ‘ubatizo’ kujitokeza sasa katika tamthiliya teule tuliyosoma inarejesha watu wa dini ya Kikristo kwenye mafundisho ya dini ya Kikristo. Mafundisho hayo yaliyotolewa kwao hapo kwanza kabla ya kukutana na matini hii. Kimsingi, matumizi ya misamiati ya Biblia; ubatizo, padri n.k. yameibua maana katika tamthiliya teule kama tulivyobainisha. Hivyo basi, fani hizo zimetumika kueleza dhamira ya nafasi ya ubatizo kwa waumini wa dini ya Kikristo.

**4. 3. 6 Waumini wa Kikristo kuwa Makini na Manabii wa Uongo**

Manabii wa uongo ni wafanyakazi wadanganyifu ambao hujifanya kuwa mitume wa Kristo (Paulo, 2 Korintho 11). Mwinjilisti huyo ameweka bayana kuwa, manabii wa uongo huigiza ili waonekane watu wema, watumishi wa haki wa Mwenyezi Mungu kumbe sivyo.

Yesu Kristo anafasili manabii wa uongo kama wakristo wa uongo ambao hufanya ishara na miujiza mikubwa, wakihusisha habari za Kristo ingawa si wafuasi halisi wa Kristo (Mathayo 24: 23 – 26). Ishara na miujiza hiyo inayofanyika kwenye makusanyiko ya manabii wa uongo huwavuta watu kutoka pande mbalimbali kushiriki ibada zinazoratibiwa na watu hao. Ishara na miujiza hiyo uhusishwa na miungu isiyomhusu Kristo.

Kimsingi, manabii wa uongo ni wakristo wa uongo wanaoigiza kuwa wafanyakazi wa Mungu huku dhahiri wakiwa wafuasi wa Shetani. Watu hao hujifanya kuwa

wafuasi wa Kristo lakini si kweli. Zama hizi wamekuwa wengi katika jamii na mahekalu yanafurika watu lukuki kutokana na ishara na miujiza inayoonekana katika makanisa yao (Katubayemo, 2022).

Matokeo ya utafiti huu yamebaini dhamira ya Wakristo kuwa makini na manabii wa uongo katika tamthiliya teule *Nyota ya Tom Mboya* (2016). Katika tamthiliya hiyo, waumini wa Kikristo wanafundishwa kuwa makini na watu wanajitokeza katika jamii na kujipachika utume wa Mwenyezi Mungu almaarufu kama manabii wa uongo. Jamii inaelezwa kuwa siyo kila aliyevaa joho la Uchungaji, Upadri ni mtumishi halisi wa Mwenyezi Mungu. Watu wengine ni waongo tena hutumia hata mashetani katika kufanya ishara na miujiza mbalimbali ili kuwapumbaza wafuasi wao.

Kupitia tamthiliya hii tumeona familia ya Wanjiru na Kanoga ikitembelewa na mtu mmoja katika nyumba yao anayejiita ‘Nabii Eglon’. Nabii huyu wa uongo akiwa nyumbani kwa Kanoga, inafanyika ibada isiyoruhusu mwanamke, mama mwenye nyumba kushiriki. Ndipo sasa mke wa Kanoga, Wanjiru anaambiwa aenda kukaa chumbani hata ibada ikamilike. Ibada hiyo ikiendelea, Wanjiru, mama mwenye nyumba anajongea ghafla na kutamka maneno *“BLOOD OF JESUS”*. Mzuka wa Abdulla aliokuja nao Nabii Eglon unaotaka kumuua Kanoga, unakimbia na Kanoga anapona. Mtunzi amewasilisha dhana hiyo namna hii;

69) WANJIRU: {Anaingia ghafla. Kavaa nightdress. Kwa sauti ya kukemea}:
*BLOOD OF JESUS!!*
(Kufumba na kufumbua: Mzuka wa Abdulla unakimbia; muziki wa Kihindi unanyamaza na wote watatu wanamtazama Wanjiru kwa mshangao... Lakini Kanoga anachezesha ulimi kama kiboko.

> Wanjiru anamkimbilia.
> Anamkumbatia}
> Ooh! Darling!
> (Uk. 59)

Kimsingi, dhamira ya kuwa makini na manabii wa uongo imeelezwa na Yesu Kristo katika matini ya Biblia. Mwalimu Yesu Kristo alifundisha wafuasi wake kwamba siku za mwisho watatokea manabii wengi wa uongo. Manabii wanaofanya ishara na miujiza kama inayofanyika katika nyumba za ibada. Waamini wa dini ya Kikristo walikumbushwa wasiwasadiki. Wabaki katika imani zao. Yesu Kristo katika Biblia anasema;

> *"Wakati huo mtu akiwaambia, 'Tazama! Kristo yuko hapa!' au 'Kristo yule pale!' msisadiki. Kwa maana watatokea makristo na manabii wa uongo na watafanya ishara za ajabu na miujiza mingi ili kuwadanganya, hata ikiwezekana, wateule wa Mungu. Angalieni, nawatahadharisha mapema." Yesu Kristo*
> (Marko 24: 23 – 25)

Dhana hizi; 'Makristo' na 'Manabii wa uongo' zimebeba ishara hasi kwa watu watakaokuja baadaye kudanganya watu katika dini ya Kikristo. 'Makristo' ina taswira ya majibu mabaya, majibu yasiyostahili. Waumini wa dini ya Kikristo wanapewa tahadhari, wawe macho na majitu hayo kwani yatawaharibu kiimani.

Kristeva (1986) anaeleza kuwa, kuwa matini za fasihi husemezana na wasomaji wake. Vilevile mwanazuoni huyo anaendelea kushadidia kuwa dhamira katika matini za fasihi haziwasilishwi kama bidhaa kamilifu, bali huwasilishwa kwa namna inayompa msomaji fursa ya kubaini maana kwa namna yake. Katika usomaji wa matini, hadhira ana fursa ya kuhusisha lolote linaloweza kumsaidia kubaini maana katika matini.

Matumizi ya sajili ya Biblia "BLOOD OF JESUS" katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya,* na mrejesho ulitokea baada ya kutamkwa sajili hiyo kumeeleza hadhira kwamba jamii ina watu wanaojiita mitume wa Mwenyezi Mungu, kumbe sivyo. Hadhira inaweza kupata fursa ya kutambua nguvu na uweza uliomo ndani ya hiyo silaha 'BLOOD OF JESUS' iliyohusishwa katika tamthiliya hii. Tukio la Nabii Eglon kuhangaika na mzuka wa Abdulla wakiwa kwa Kanoga, limedhihirisha kuwa nabii huyo si mkweli. Ni mtume muongo kwani kama angekuwa nabii halisi silaha iliyorejewa wakati wa ibada isingemdhuru yeye na wasaidizi wake.

Hali kadhalika, sajili ya Biblia 'BLOOD OF JESUS' imetumika kuwasilisha dhamira ya waamini wa Kikristo kuweka tumaini katika Yesu Kristo. Mbogo anawasilisha dhamira hii kwa waamini wa Kikristo. Waamini wa Kikristo wameelezwa kutokumpokea kila anayejitambulisha kama mtume wa Mwenyezi Mungu. Hadhira ya matini hiyo inaelekezwa kuwa ishara na maajabu yanayofanyika na wanaojiita manabii wa Mungu zisitumike kama kigezo cha kupima uaminifu kwa wanaojiita mitume wa Mwenyezi Mungu. Ishara na maajabu hayo zinaweza kufanywa pia na 'Makristo na  manabii wa uongo'.

**4. 3. 7 Nafasi ya Shukurani kwa Mwenyezi Mungu**

Shukurani ni neno linaloashiria kukubali hisani uliyofanyiwa; asante (Kamusi Kuu ya Kiswahili, 2016). Wanaisimu katika Kamusi Kuu ya Kiswahili wanaeleza kuwa neno shukrani hutolewa na mtu kwa mwingine kama ishara ya kukubali mema aliyotendewa na mtu huyo.

Hali kadhalika TUKI (2013), wanafasili shukurani kama neno linaloonyesha kuridhika kwa wema aliotendewa mtu. Taasisi hii ya Taaluma za Kiswahili inatanabaisha dhana ya shukurani na neno 'asante' ambalo mtu hulitoa kwa ukarimu aliotendewa na mwenzake.

Kimsingi, dhana ya shukurani inaweza kufasiliwa kama neno au ishara ya kurudisha fadhila kwa sababu ya kitu chema mtu alichotendewa. Katika jamii utamaduni huu umetawala na unanasibishwa na utu wema. Kwamba, watu wanaotamka neno 'shukurani' au kuonyesha ishara ya shukurani huonekana waadilifu, wenye tabia njema (Esili, 1999). Kinyume chake, watu wasiotoa shukurani baada ya kutendewa ukarimu huonekana wakaidi. Jambo hilo hufunga milango ya kutendewa wema wakati mwingine kwa ukaidi waliofanya.

Aidha muktadha wa dini unaeleza shukurani kama kitendo cha kumwambia Mungu asante kwa kila jambo hata kama hajafanya ulilomuomba (Gibe, 2020). Mwalimu huyu anaendelea kufundisha kuwa, mtu anapoamka asubuhi anatakiwa kumshukuru Mungu kwa mema yote aliyomtendea. Mathalani kumlinda usiku wote hata wakati huo. Mwalimu huyo anaeleza kuwa somo hili ni muhimu sana kwa waamini wa dini zote. Kila dini, inafundisha wafuasi wake kujenga tabia ya kumshukuru Mungu kila uchao kwa wema na fadhili anazowatendea.

Utafiti tuliofanya umebaini kwamba, dhana ya shukrani imetumika kama tendo la kurudisha shukurani kwa Mwenyezi Mungu kwa kudra na fadhili zake anazoachilia kwa wanadamu kila uchao katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora* (2016). Mtunzi teule anafundisha jamii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa mema mengi anayowatendea kila uchao. Waamini wa dini ya Kikristo wanafundishwa kuwa

mambo yote mema wanayotendewa, yanaratibiwa na Mungu Mwenyezi huko juu Mbinguni, hivyo ni neno jema kumshukuru kwa fadhili hizo.

Uzima na afya ni moja ya mibaraka kutoka kwa Mwenyezi Mungu, ndipo sasa ni jambo jema kumshukuru Mola (Mwakasege, 2017). Mhusika Mondlane katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora (2016)* ameonyesha moyo wa shukrani kwa Mwenyezi Mungu kwa kurejeshewa afya. Mondlane yupo kwenye kuuguza jeraha la kidonda cha risasi lakini ameanza kupona. Mondlane kwa maneno ya kinywa chake anakiri kuwa Mungu Mwenyezi ndiye aliyemsaidia hata akaendelea kupona kidonda cha mguu wake. Mondlane anasema;

70) MONDLANE: *Namshukuru Mungu kupata nafuu*
(Uk. 54)

Data Na. 71 inarejea mafundisho katika Biblia kuhusu kumshukuru Mungu Mwenyezi kwa wema wake kwa wanadamu, yamefundishwa na waandishi mbalimbali. Biblia inaeleza waumini wa dini ya Kikristo kumshukuru Mwenyezi Mungu hata kabla ya kupokea kile wanachomuomba. Wakristo wanakumbushwa kutengeneza tabia ya kumshukuru Mungu kila uchao kwa mema na mabaya yanayojili kwenye maisha kwani yote yanatotukia yanaegemezwa kwenye kuratibiwa na Mungu wanayemuamini. Biblia imeeleza hivi;

*"Furahini siku zote; Ombeni bila kukoma; Shukuruni kwa kila jambo; maana hayo ni mapenzi ya Mungu kwenu katika Kristo Yesu." (Mtume Paulo)*
(1 Wathesalonike 5: 16)

Mtume Paulo, mwandishi wa kitabu cha Wathesalonike ndani ya Biblia anawakumbusha watu wafuasi wa dini ya Kikristo kumshukuru Mungu kwa kila

jambo. Tungo hii *'Shukuruni kwa kila jambo; …'* imebeba dhamira hiyo. Hivyo ni jambo jema kwa waumini wa dini ya Kikristo kumshukuru Mola kwa yote anayowajaalia.

Clayton na Bothstein (1991) wanaeleza kwamba, kuielewa matini ya fasihi kunachagizwa na matini nyingine aliyowahi kukutana nayo msomaji awali. Washadidi hao wa Nadharia ya Mwingilianomatini wanadai, hilo linatokana na uhusiano wa matini tangulizi na matini fuatizi. Matini yoyote imefumwa kama mesto wa unukuzi kutoka matini nyingine.

Dai la wanazuoni hawa kuhusu hadhira kubaini maana katika matini kwa mujibu wa Nadharia ya Mwingilianomatini linafanya tubaini kuwa, kwa vile matini uhusiana na kuathiriana basi, utambuzi wa maana ya matini hutokana na matini nyingine aliyokutana nayo msomaji.

Mtume Paulo katika Biblia anafundisha kanisa la Thesalonike kumshukuru Mungu kwa mambo yote yanayojili katika maisha yao. Kwamba, mwanadamu akikutana na mambo mazuri au changamoto zozote katika maisha afahamu kuwa ni kudra za Mwenyezi Mungu. Hivyo amshukuru Mwenyezi Mungu wake kwani kudra zake kwa watu wake ni njema daima.

Fauka ya hayo, Emmanuel Mbogo katika tamthiliya hii tuliyosoma, *Mondlane na Samora* (2016) anawasilisha dhamira hiyo. Mhusika mkuu Mondlane anarudisha shukrani zake kwa Mungu Mwenyezi kwa kupata ahueni kutokana na majeraha anayopitia baada ya kujeruhiwa katika harakati za ukombozi wa nchi ya Msumbiji akisema, *'Namshukuru Mungu kupata nafuu'*.

Hivyo basi, wasomaji wa tamthiliya hii waliowahi kukutana na Biblia, wakirejea nukuu ya Biblia iliyotumika kuhusu shukrani katika tamthiliya teule, wanabaini dhamira inayowasilishwa. Kwamba wanadamu wanapaswa kumshukru Mwenyezi Mungu kwa mema yote anayowajaalia. Mbogo ametumia nukuu hiyo kuwasilisha dhamira ya shukrani kwa Mwenyezi Mungu. Nukuu aliyotumia ni ngazi murua ya kudhihirisha dhamira aliyokusudia kwa hadhira lengwa.

**4. 3. 8 Kuheshimu Wazazi na Walezi katika Jamii**

Vilevile mtafiti alibaini dhamira ya kuheshimu wazazi na walezi katika jamii ikijadiliwa katika matini teule. Watunzi wa bunilizi hizo kwa namna mbalimbali watumewasilisha dhamira hiyo kwa jamii ndani ya matini tulizotafiti. Pengine tufasili dhana ya kuheshimu wazazi na walezi kabla ya kuanza kuichambua katika matini teule.

Dhana ya kuheshimu inaelezwa kama tendo la kumfanyia adabu mtu, kama ishara ya kumthamini; ni kumuweka mtu katika hadhi ya juu katika jamii (TUKI, 2013). Wanazuoni wa taasisi ya taaluma za Kiswahili wanaeleza kuwa tendo la kuheshimu wazazi na walezi uhusishwa na mwenendo mwema katika jamii. Tamaduni nyingi ulimwenguni zimeweka tendo hili kama kipimo cha utu wema katika jamii.

Vilevile tamaduni za jamii zinaelekeza watoto kuheshimu wazazi na walezi wao (Hananja, 2011). Watoto wanaelekezwa kuwa na adabu machoni pa wazazi, walezi wao. Wakati mwingine mafanikio ya mtoto yameambatishwa na heshima anayoonyesha kwa wazazi, walezi wake. Hivyo hilo linaonekana kama nguzo msingi ya kumsaidia mtoto, kijana kufikia mafanikio katika maisha.

Matokeo ya utafiti huu yamebaini dhamira ya watoto kuheshimu wazazi, walezi katika jamii. Fani za Biblia zilizojitokeza katika tamthiliya hizo zinadhihirisha dhamira ya heshima kwa wazazi na walezi. Utafiti huu ulibaini dhamira hii ikielezwa katika tamthiliya moja pekee, miongoni mwa tamthiliya sita tulizotafiti. Tamthiliya hiyo ni *Tanzia ya Patrice Lumumba* (2015).

Tamaduni nyingi kwa mkabala wa dini, zinafundisha jamii zao kuishi vizuri na wazazi na walezi wao. Katika dini ya Kikristo kufanikiwa au kushindwa katika maisha, kumehusishwa na nidhamu nzuri kwa wazazi. Mtunzi wa tamthiliya hii amenukuu amri ya nne ya Mwenyezi Mungu kutoka kwenye Biblia inayoelekeza watoto kuheshimu wazazi wao; Baba na Mama. Amri hiyo ya nne inaeleza pia kuwa watoto wakifanya hivyo, watapata heri duniani, watafanikiwa katika maisha yao. Mtunzi teule amewasilisha dhamira hiyo namna hii;

71) MOBUTU: *Wacha niwaambie siri.*
*Lumumba maisha yake yatakuwa mafupi sana kwani leo Patrice kavunja amri ya nne isemayo,*
*Waheshimu baba na mama yako ili upate kuishi miaka mingi ...*
(Uk. 12)

Dhamira inayoelezwa na Mobutu, ya kuheshimu wazazi imenukuliwa kutoka Biblia, kitabu cha Kutoka, Agano la Kale. Agizo la kuheshimu wazazi lilitolewa na Mungu kwa Wayahudi wakati wakiwa safarini kutoka utumwani Misri, kurejea nchi yao ya ahadi Kanaani. Nabii Musa alitoa fundisho hilo kwa Wayahudi kama alivyoagizwa na Mwenyezi Mungu kupitia amri kuu kumi kwa watu wake. Amri hiyo ya kuheshimu wazazi ni ‘Amri ya Nne’. Katika Biblia inasomeka hivi;

> *“Waheshimu baba yako na mama yako; siku zako zipate kuwa nyingi katika nchi upewayo na Bwana Mungu wako.”*
> (Kutoka 20:12)

Katika Biblia Wayahudi walifundishwa kwamba, wakitaka kuishi maisha marefu, miaka mingi basi wawaheshimu wazazi wao huko Kanaani wanakokwenda. Amri hiyo ya nne ilitolewa kama ngazi ya kuleta mafanikio katika maisha yao.

Wahakiki wa mkondo wa mwingilianomatini wanasema kuwa, maana ya matini haipatikani katika matini yenyewe, bali inajengwa na msomaji katika matini husika na mseto wa matini nyingine zinazotajwa na kurejelewa katika usomaji huo (Wafula, 2007). Tamthiliya teule, *Tanzia ya Patrice Lumumba* ni zao la matini nyingi tangulizi, Biblia ikiwemo kama tulivyobaini kupitia nukuu ya 'Amri ya Nne ya Mungu' (Data Na. 72). Hivyo msomaji wa matini akihusisha matini lengwa na Biblia, anabaini maana inayowasilishwa.

Dhamira ya kuheshimu wazazi na walezi imedhirika katika tamthiliya teule kupitia nukuu iliyorejelewa. Msomaji wa matini teule; Biblia na tamthiliya ana fursa ya kubaini umuhimu wa kuheshimu wazazi na walezi katika jamii. Mtunzi amenukuu hiyo 'Amri ya Nne' ya Mwenyezi Mungu katika tamthiliya hii kuwakumbushwa jamii kutii na kuheshimu wazazi na walezi. Jamii inaelezwa kuwa wazazi na walezi wana mchango mkubwa sana katika maisha ya wanadamu katika ngazi mbalimbali.

Hadhira ikihusisha nukuzi ya amri ya nne ya Mungu kwa jamii ya Kiyahudi na jinsi ilivyotumika katika tamthiliya inang'amua ujumbe anaowasilisha mtunzi kwa hadhira yake; Afrika Mashariki na Kati sambamba na ulimwengu wote kwa jumla inakotumika fasihi ya Kiswahili. Nukuzi ya Biblia iliyotumika imebeba dhamira ya kuheshimu wazazi na walezi katika familia, jamii kwa jumla. Katika Biblia ilitumika kueleza jambo hilo pia. Hivyo kujitokeza kwa nukuu hii, kunadhihirisha dhamira ya kuheshimu wazazi kama tulivyobainisha.

### 4. 3. 9 Umuhimu wa Elimu katika Jamii

Zaidi ya hapo, utafiti ulibaini dhamira ya umuhimu wa elimu katika jamii ikiwasilishwa katika matini teule kupitia fani mbalimbali za Biblia zilizotumiwa na mtunzi, Emmanuel Mbogo. Elimu ni maarifa yanayotolewa kwa mfumo maalum wa kufundishia na kujifunzia (Longhorn, 2016). Wachapishaji hawa wanaendelea kueleza kuwa, maarifa yanayotolewa kwa jamii huongozwa kwa sera rasmi zinazoandaliwa na kuratibiwa na vyombo vya utawala katika jamii. Taasisi mbalimbali huanzishwa katika jamii ili kutoa maarifa hayo. Mathalani; Shule, Taasisi za Utafiti, Vyuo vya Kati, Vyuo Vikuu n.k kutegemea na malengo ya taifa.

Fauka ya hayo elimu inafasiliwa kama upitishaji wa maarifa kwa mtu, kwa lengo la kukuza uwezo wa kiakili, wa kuathiri na wa maadili sawa (Mlyauki, 2014). Mtafiti huyo anaendelea kueleza kuwa katika jamii elimu inachukuliwa kuwa jambo muhimu sana kwani hukuza stadi na maadili yanayofanya jamii kuishi vizuri. Elimu huwawezesha watu kufanikiwa katika maisha. Kupitia elimu watu hukabiliana na changamoto mbalimbali zinazoibuka kila uchao katika uso wa nchi.

Fasihi huelimisha jamii (Ponera, 2014). Mtafiti huyu anaeleza kuwa fasihi andishi ya Kiswahili kupitia kumbo zake; nathari na ushairi imeakisi dhamira hii. Watunzi wengi katika bunilizi zao wanatoa elimu za nyuga mbalimbali katika jamii kama vile: utawala bora, afya salama, utamaduni, uchumi endelevu, n.k. Dhamira hii inazingatiwa kwani inachukuliwa kama nguzo, ufungo wa maisha kuanzia ngazi ya mtu binafsi hadi taifa.

Matokeo ya utafiti yamebaini dhamira ya umuhimu wa elimu katika jamii katika tamthiliya ya *Mtumwa hadi Siti Binti Saad* (2018). Fani za Biblia zilizojitokeza zinadhihirisha dhamira hiyo. Mtunzi wa drama hii, Emmanuel Mbogo anafundisha jamii kuwa elimu ni nguzo ya maisha. Hivyo ni vema wanajamii kuizingatia na kila mmoja ahakikishe anaipata. Elimu haina mwisho hivyo isizingatiwe kwa watoto tu hata watu wazima wanaweza kuipata wakati wowote wakipata fursa.

Mhusika mkuu katika tamthiliya ya *Mtumwa hadi Siti Binti Saad*, Siti Binti Saad amechorwa kupata fursa ya kwenda nchini India kurekodi muziki wa taarab. Mfadhili wake amebaini kwamba mwanamuziki huyo hakufanikiwa kupata elimu awali. Hivyo mfadhili anatafuta Mwalimu wa kumfundisha kusoma na kuongea lugha ya Kiarabu vizuri. Elimu hiyo ilikuwa muhimu kwani ilimsaidia Siti kufikia mafanikio makubwa katika tasnia ya muziki ingawa aliitapa ukubwani. Habari hiyo ilionekana kushangaza wengi, inawezekanaje mtu mzima huyo aanze kusoma? Ni jambo lisilotarajiwa. Mbogo ameeleza jamii kuwa inawezekana watu wazima kupata elimu pia.Tazama mazungumzo haya;

72) NONGWA: *Mwalimu anamfundisha Mtumwa kuongea Kiarab,*
*Kusoma Kur'ani na kuimba taarab.*

73) BONGA: *Aaah! Inawezekana kweli?*
*Nakwambia Nongwa ukisikia maajabu ya nabii Musa ndiyo hayo.*
(Uk. 78)

Kimsingi nukuu hii 'Maajab ya Nabii Musa' (Data Na. 74) katika majibizano ya wahusika hao imetumiwa na mtunzi kueleza kuwa inawezekana pia watu wazima kujifunza, kupata elimu na wakanufaika nayo katika maisha kama ilivyotukia kwa Bibi Titi. Simulizi kuhusu maajabu ya Nabii Musa zinazoelezwa kwenye Biblia zinaeleza kufanyika kwa mambo magumu mno ambayo katika hali ya kawaida

yalionekana hayawezekani. Kwa mfano ajabu la fimbo kuinuliwa juu kisha ikagawanya Bahari ya Shamu pande mbili, Wayahudi wakapita nchi kavu (Kutoka 15: 19 – 27).

Barthes (2002) katika Nadharia ya Mwingilianomatini anaeleza kwamba, mawasiliano baina ya mtunzi wa kazi ya fasihi na msomaji huambatana na mwingiliano uliopo baina ya maneno na jinsi yalivyokuwa yakitumika katika matini tangulizi. Hivyo basi, msomaji wa matini anaweza kubaini dhamira katika matini anayosoma kwa kuihusisha na fani zilizotumika awali katika matini nyingine. Urejesho huo humuwezesha hadhira kubaini dhamira inayowasilishwa.

Fani hii ya Biblia 'Maajab ya Musa' imetumiwa na mtunzi kueleza kwamba, hata watu wazima kwenda shule kupata elimu inawezekana. Jambo hilo katika fikra za jamii ya Kiafrika lilionekana kuwa haliwezekani. Hadhira ikihusisha taswira ya 'Maajab ya Musa' kutoka kwenye Biblia na habari anazozungumza mtunzi ina nafasi ya kubaini dhamira hii. Kwamba watu wazima kupata elimu kama inavyokuwa kwa watoto wadogo, inawezekana.

Kwa hivyo, dhamira ya umuhimu wa elimu katika maisha imedhihirika kupitia fani ya Biblia iliyorejewa katika tamthiliya hii. Matokeo aliyoyapata Siti binti Saad baada ya kupata elimu yanathibitisha dai kwamba, elimu ni ufunguo wa maisha. Siti kujifunza lugha kumemsaidia kwenda nje ya nchi, India kurekodi nyimbo za muziki. Uwezo aliopata wa kujifunza lugha za kigeni, kama vile Kiarabu na Kiingereza umemsaidia kuongeza hadhira yake. Hivyo akapokewa na kukaribisha katika mataifa mbalimbali kutoa burudani ya muziki.

### 4. 3. 10 Mapenzi na Ndoa katika Jamii

Matokeo ya utafiti huu yamebaini kwamba katika tamthiliya teule mtunzi ameeleza dhamira ya mapenzi na ndoa katika jamii. Dhamira hiyo imeelezwa kwa kuhusisha fani mbalimbali kutoka kwenye vitabu vya Biblia. Pengine kabla ya kusonga mbele kueleza dhamira hii, tunaona vema kwanza tufafanue dhana hizi; mapenzi na ndoa.

Abdalla (2018) anafasili mapenzi kama hisia nzito za moyoni zinazomfanya mtu avutiwe, athamini na ajali mtu, kitu au jambo. Mwanazuoni huyu anaendelea kudadavua kuwa, mapenzi yanaweza kujengeka kupitia misingi ya uvumilivu, hekima, busara, uwazi, upendo na heshima. Wasanii katika tanzu mbalimbali za kisanaa huakisi dhamira ya mapenzi katika bunilizi zao.

Vilevile mapenzi yanaelezwa kama muktadha wa uhusiano kati ya mume na mke kwa watu waliooana au ambao wako kwenye mwelekeo huo (Mwananchi, 2018). Wanahabari hawa kwao dhana ya uhusiano wa mume na mke walioko kwenye ndoa au wanaotaraji kufunga ndoa ndiyo mapenzi. Kumbe mahusiano mengine yasiyo katika muktadha ya ndoa, si mapenzi.

Kimsingi, dhana ya mapenzi ni terezi. Inafasiliwa kwa namna mbalimbali na wanazuoni katika miktadha tofauti. Hoja ya msingi inayorejewa wakati dhana hii inapofasiliwa, ni uhusiano baina ya watu wawili. Uhusiano huo unaweza kuwa wa kingono (mume na mke) au usiyo wa kingono (baba na mwana, kaka na dada n.k).

Katika jamii mahusiano yana sura mbili; mahusiano ya kweli, dhati na mahusiano ya ulaghai (Abdalla, 2018). Mtafiti huyu anaendelea kueleza kuwa mahusiano ya dhati huonekana madhubuti, huwa imara pasina fitina yoyote. Mapenzi ya uongo hujawa na ulaghai ndani yake. Watu uhusiana tu kwa malengo mahsusi.

Katika utafiti tuliofanya dhana ya mapenzi ilichukuliwa kama mahusiano ya kingono baina ya mume na mke, walio kwenye ndoa. Hivyo popote iliporejelewa dhana hiyo katika utafiti huu, ieleweke kwa mtazamo huo. Vilevile ieleweke kwamba, mahusiano ya kimapenzi yanaweza kuwa ya dhati au kilaghai kama tulivyoeleza.

Ndoa ni muunganiko wa mwanamke na mwanamume wa kuishi pamoja kama mume na mke katika misingi ya uadilifu na sheria (Quran, 4:3). Kitabu hiki katika imani ya kiislamu kinafasili dhana ya ndoa kwa jinsi hiyo, mume na mke waungane na kuishi pamoja kwa kufuata maadili na sheria zilizowekwa kuhusu wanandoa.

Ndoa ni muunganiko wa pekee wa kudumu ambao mume na mke wanakuwa mwili mmoja (Hananja, 2017). Mtheolojia huyu anaendelea kueleza dhana ya ndoa kama tendo la kumkubali mtu (mume au mke) kuwa sehemu ya nafsi yako mwenyewe. Mke anakuwa sehemu ya mume wake na mume anakuwa sehemu ya mke wake, na hao wawili wanakuwa mwili mmoja hadi kifo kiwatenganishe. Mafundisho ya Hananja kuhusu ndoa yamenukuliwa kutoka kitabu cha Biblia kama hivi;

> *"BWANA Mungu akasema, Si vema huyo mtu awe peke yake, nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye."*
> (Mwanzo 2:18)
>
> *"Alichokiunganisha Mungu, mwanadamu asikitenganishe."*
> (Marko 10:9)

Hivyo, Biblia inafasili ndoa kama muunganiko wa watu wawili; mwanamke na mwanamume kuunganika kuwa mwili mmoja na kuishi pamoja hadi kifo kiwatenganishe. Kibiblia, watu wakishafunga ndoa hawaruhusiwi kutengana kwa lote liwalo hadi mauti. Mtu huwa huru kuoa au kuolewa na mtu mwingine baada ya kufiwa na mwenza wake. Waliyefunga naye ndoa hapo kwanza.

Sheria ya Ndoa Tanzania (1977) inafasili ndoa kama muunganiko wa hiari kati ya mwanamke na mwanamume, unaokusudiwa kudumu kwa maisha yao yote. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika sheria ya ndoa wamesaidia kuwa, dhana ya ndoa ihusishwe na muungano wa hiari baina na mwanamke na mwanamke wenye nia ya kudumu milele. Kuna ukakasi pahala katika fasili hii, Je, uhusiano wowote baina ya mwanamke na mwanamme ni ndoa?

Kimsingi, ndoa inafasiliwa kama muungano wa mwanamume na mwanamke, walioamua kwa ridhaa yao wenyewe kuishi kama mume na mke mpaka mwisho wa maisha yao. Sheria ya ndoa nchini Tanzania, inatambua ndoa za namna mbili pekee; ndoa ya mume mmoja na mke mmoja (Kikristo) na ndoa ya wake wengi; mume mmoja (Kiislam). Kimsingi, katika utafiti tuliofanya, mapenzi na ndoa yalijadiliwa kwa muktadha wa mahusiano ya kingono baina ya mume na mke.

Utafiti huu umebaini dhamira ya mapenzi na ndoa katika tamthiliya teule. Dhamira hii imejitokeza katika tamthiliya zote sita tulizotafiti. Fani za Biblia zilizojitokeza katika tamthiliya hizo zinadhihirisha dhamira ya mapenzi na ndoa barabara.

Katika kubaini maana ya matini, Nadharia ya Mwingilianomatini ina mhimili unaoelekeza jambo hilo. Mhimili huo unasomeka namna hii, ili hadhira ibaini maana ya kazi yoyote ya fasihi ni muhimu ihusishe kazi hiyo na vipengele vingine, nje ya matini inayosomwa au kusikilizwa (Wafula, 2007). Utafiti huu umebaini kuwa fani za Biblia zilizojitokeza katika matini teule, zilitumika awali kuwasilisha dhamira ya mapenzi na ndoa katika jamii. Tuhitimishe kuwa, hadhira ikihusisha fani hizo wakati wa kusoma tamthiliya teule inaweza kubaini dhamira inayowasilishwa na mtunzi wa kazi ya fasihi.

Katika sehemu inayofuata, mtafiti amejadili dhamira ya mapenzi na ndoa katika tamthiliya teule zote akihusisha fani za Biblia zilizorejewa katika matini teule. Nia kuu ilikuwa kutimiza lengo mahsusi la tatu katika utafiti huu, kubainisha dhamira zinazojitokeza kutokana na matumizi ya fani za Biblia katika matini teule.

Matokeo ya utafiti yamebaini dhamira ya mapenzi na ndoa katika tamthiliya ya *Wangari Maathai* (2015). Katika tamthiliya hiyo mtunzi anaelekeza wanandoa kuwa na kiasi katika shughuli za uzalishaji wanazofanya. Kiasi ni uwezo wa kujitawala, kudhibiti jambo lisipitilize mipaka yake (Chamba, 2014). Kupitia mwalimu huyu tunabaini kwamba, dhana 'kiasi' inarejea hali ya kutenda jambo kwa sehemu.

Mtunzi anawasilisha dhamira hii kupitia ndoa ya Bw. Mwangii na Bi. Wangari. Ndoa inaonekana iko kwenye mgogoro mkubwa kwa sababu ya mwanandoa mmoja, Bi. Wangari kufanya shughuli zake za uzalishaji kupitia kiasi. Hali iliyo inachangia mwanandoa huyo kushindwa kutekeleza wajibu wake kama mke, mama katika familia ya Bw. Mwangii. Hivyo jamii inaelezwa kuwa wanandoa wanatakiwa kufanya shughuli za uchumi, siasa, jamii kwa kiasi. Wakifanya hivyo wataweza kutekeleza wajibu mwingine katika ndoa, familia kwa jumla.

Mwangii, mume wa Wangari ameingia kwenye mgogoro na mke wake Wangari. Mke huyo amejikita zaidi kwenye harakati za kupigania mazingira na kutelekeza familia. Muda mwingi Wangari anautumia kwenye harakati za demokrasia na mazingira. Tamaduni zinaeleza kuwa mke mwema ni mtu anayejali familia yake; mume na watoto wake pamoja. Mwangii analalamika mbele ya mke wake alfajiri na mapema ndani ya nyumba yao. Mume huyo alipoamka alfajiri, anakuta mke wake amekaa mezani akiandika makala. Mtunzi amemchora Wangari, mama mwenye

nyumba kama mwanamke aliyejikita zaidi kwenye taaluma na kusahau kutimiza wajibu wake kama mke na mzazi katika familia kama hivi;

74) MWANGII: You see! Uprofesa wako ndio unaokupa kiburi.
Ama kweli hizi ni mbigi ndani huu ubongo wangu.
Hakika, hawa ni tandu lukuki ndani ya huu ubongo wangu.
*Mwanamume yeyote anahitaji neema ya Mungu ili kuyakumbatia mapenzi kama haya.*
[anabamiza mlango kwa nguvu, anatoka*]"*
(Uk. 7)

Fani ya Biblia iliyotumika katika mazungumzo ya mhusika huyu ni semi, '*neema ya Mungu'* (Data Na. 75). Neema ya Mungu katika Biblia inaelezwa kama zawadi ama upendeleo wa Mungu kwa wanadamu ambao hawakustahili (Matiku, 2016). Mwanazuoni huyu akirejea Biblia anaendelea kudadavua kwamba, upendeleo usio na sababu ndiyo neema. Wasomaji wa Biblia huamini kuwa, Mungu wanayemuamini huwatendea mema wema na wabaya, pasina ubaguzi wowote. Hivyo, hiyo huwa neema kwa wote.

Semi hii *'Mwanaume yeyote anahitaji Neema ya Mungu ili kuyakumbatia mapenzi kama haya …'* (Data Na. 75) kama inavyorejelewa na mhusika Mwangii, mume wa Wangari katika dua yake, inajenga taswira hasi kuhusu ndoa hiyo. Kwamba, Wangii, mume wa Wangari pekee hawezi kufanikiwa kuishi na mke wake. Dhana ya 'Neema ya Mungu' ilivyotumika katika Biblia, hurejea zawadi isiyo upendeleo, mtu alipata zawadi bila jitihada. Neema ya Mungu inaelezwa pia kama nguvu ya uwezesho ili kufanikiwa katika jambo fulani hata kama huna uwezo. Wangii anaomba asaidiwe ili aishi na mke wake. Mhusika huyo anaeleza kwamba peke yake hawezi.

Mume wa ndoa kuomba neema ya Mungu ili aweze kuishi na mke ni dua nzito. Kwamba, mwanamume mwenyewe kwa jitihada zake hawezi kufanya hivyo. Ila

akiwezeshwa na Mungu Mwenyezi, akipewa zawadi hiyo kutoka kwa Mungu atafanikiwa kuishi na huyo mke batili, asiye na kiasi. Tendo la mke kumtelekeza mume usiku na kumwacha pweke faragha kisha anakwenda mezani kufanya shughuli za kiofisi limehesabika kuwa si uungwana. Wangari amechorwa kama mke asiye na kiasi katika harakati zake za kupigania mazingira nchini Kenya.

Hivyo basi, mtunzi kupitia fani hiyo aliyotumia anawakumbusha wanandoa kufanya shughuli zao za uzalishaji kwa kiasi ili kutimiza wajibu wao katika ndoa na familia zao. Msomaji akihusisha 'Neema ya Mungu' katika na mafanikio ya ndoa ya Wangii na Wangari, kama Nadharia ya Mwingilianomatini inavyoeleza anabaini dhamira hii ya ndoa. Msomaji anaweza kupata maana kuwa jitihada za kibinadamu zimeshindwa kunusura ndoa hii. Msaada wa Mungu ndiyo suluhu ya kuponya ndoa hiyo. Si taswira njema kwa ndoa.

Kwa jumla, msanii teule katika tamthiliya hii ametumia dhana 'Neema ya Mungu' kuonyesha hali ngumu zinazopitia ndoa mbalimbali katika jamii. Wanandoa wanaelezwa kuwa na kiasi katika kazi za ofisi, uchumi na nyinginezo. Wanandoa wamekumbushwa kila shughuli wanazofanya zifanywe kwa kiasi. Kwa kufanya hivyo watapata fursa ya kuwajibika ipasavyo katika ndoa zao. Hivyo ndoa zao zitaimarika kila uchao na kuwa salama.

Hali kadhalika katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya* (2016), Emmanuel Mbogo amejadili dhamira ya mapenzi na ndoa. Fani za Biblia zilizojitokeza katika tamthiliya hii zinadhihirisha dhamira hiyo. Mtunzi teule anaendelea kueleza wanandoa kuwa na kiasi katika shughuli zao za kila uchao ili kustawisha ndoa zao. Katika tamthiliya hii ndoa ya Tom na Pamela ndiyo imekuwa ngazi ya kuwasilisha dhamira hii. Mhusika

mkuu wa tamthiliya hii Tom Mboya, mume wa Pamela amechorwa kuipunja ndoa yake kwa kufanya shughuli za siasa kupita kiasi.

Tom Mboya amechorwa kufanya shughuli za siasa zaidi na kutelekeza ndoa yake. Hali hiyo inaibua mgogoro baina yake na Pamela, mke wake. Pamela, mke wa Tom Mboya amefedheheshwa na hali ya kumkosa mume wake nyumbani hata anafikia pahala pa kutamani mume wake asijishughulishe tena na harakazi za kisiasa. Pamela anasema;

75) PAMELA: Unajua sisi wanawake tumeolewa
Lakini ninyi wanaume hufunga ndoa na kazi zenu.
Kwetu sisi wanawake, mahusiano kati ya binadamu ni muhimu zaidi kuliko kazi.
*Lakini mwanamume siku zote ana mitala, yaani mkewe na kazi yake pia.*
*Wakati mwingine anamuhusudu huyu wa pili; akamkumbatia kuliko mwenye Pete kidoleni.*
(Uk. 34)

76) PAMELA: *Nasema; Natamani ningekuwa na uwezo; ningekuwa na ujasiri wa kuamuamuru Tom ampe talaka huyu mwanamke anayeitwa siasa.*
*Aoe mrembo aitwae, kwa mfano: The Rusinga Fishing Company...*
*Lakini siasa! Kila kukicha, siasa.*
(Uk. 34)

Emmanul Mbogo ametumia fani za Biblia (Data Na. 76 & 77) kujadili dhamira ya ndoa katika jamii ndani ya tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya (2016)*. Fani za Biblia zilizojitokeza katika kujadili dhamira hii katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya* ni hizi zifuatazo; nukuu za Biblia kuhusu ndoa, misamiati ya Biblia kwa habari za ndoa mf: talaka, pete kidoleni na mitala. Fani hizo zilitumika awali kwenye Biblia kuzungumza habari za mahusiano ya mke na mume katika jamii kama tulivyobainisha.

Nadharia ya Mwingilianomatini inatueleza kuwa ngazi nzuri ya kumsaidia msomaji kubaini maana ya matini anayosoma ni kuhusisha misamiati ilivyokuwa ikitumika awali katika matini tangulizi na matini mpya aliyokutana nayo (Barthez, 2007). Msomaji akihusisha fani hizo ana nafasi kubwa ya kubaini dhamira inayowasilishwa. Mathalani msamiati ‘talaka’. Dhana hii ikihusishwa ilivyotumika katika matini tangulizi, inaibua dhamira hii barabara.

Talaka ni utaratibu wa kuvunja mkataba wa ndoa (Sanchez, 2021). Mtafiti huyu anaendelea kueleza kuwa, kwa maneno ya kisheria, talaka ni kufutwa kwa mkataba wa ndoa, kulingana na ambayo pande zote mbili zitalazimika kujadili majukumu yao ili kuendelea na maisha yao kwa uhuru.

Biblia inaeleza dhana ya talaka kama tendo la kuvunja ndoa baina ya mume na mke, kisha kila mmoja awe huru kuishi maisha yake (Kimaro, 2022). Hata hivyo kulingana na mpango wa Mungu juu ya ndoa, ndoa haikupaswa kuvunjika. Agizo lilikuwa kwamba, watu wakioana waishi daima hadi mauti iwatenganishe. Tatizo au kwazo lolote baina ya wanandoa halikuchuliwa kama uhalali wa kuwatenganisha wanandoa (Biblia).

Hivyo basi, mabadiliko ya tamaduni za Kiyahudi baadaye yalileta hatma kwamba, mke na mume waachane kwa kosa la uasherati (Mathayo 5:32 na 19:9). Uasherati ni tendo la mtu kufanya mapenzi na mtu mwingine, nje ya ndoa yake. Hilo pekee ndilo lilichukuliwa kama kigezo cha kuwatenganisha wanandoa, kuvunja ndoa.

Mhusika Pamela kutamani Tom Mboya, mume wake avunje mkataba na kazi yake ili arejee kwenye familia kunaakisi hali isiyostahili katika ndoa ya Pamela na Tom

Mboya. Msamiati 'Talaka' unaonyesha sikitiko kuu lililoujaza mtima wa Pamela kutokana na ndoa yake kutelekezwa. Hadhira waliosoma tamthiliya hii, wakihusisha msamiati 'Talaka' na jinsi ulivyotumika awali unajenga taswira mbaya inayopitia ndoa hiyo.

Fauka ya hayo, dhana ya talaka hutumika kufundisha watu kuheshimu na kuzipa nafasi ndoa zao ili wasiachane. Wanandoa wanaelekezwa wasitelekeze ndoa, familia na kujikita zaidi katika shughuli nyingine za maisha. Mtunzi katika tamthiliya hii teule tuliyotafiti amewagusa zaidi wanaume kama watu wanaoharibu ndoa zao. Mwanamke Pamela anajitetea kwamba, wanawake hufunga ndoa na familia. Wanaume hufunga ndoa na kazi zao. Hivyo basi, wanaume wanaaswa kuzingatia ndoa zao si kazi za mikono pekee zinazowaingizia kipato.

Pamoja na hayo, dhamira ya mapenzi na ndoa inajadiliwa katika tamthiliya ya *Malkia Bibi Titi Mohamed (2016).* Misamiati kuhusu ndoa kama vile uasherati, umalaya, talaka n.k. imetumika kuwasilisha dhamira hii. Misamiati hiyo ikihusishwa wakati wa usomaji wa tamthiliya hii ikihusishwa kama ilivyotumika katika Biblia inaakisi dhamira mapenzi na ndoa katika familia ya Tatu na mumewe. Ndoa imechorwa kuwa na taswira hasi kwani misamiati hiyo inarejea taswira hasi katika uga wa mapenzi na ndoa.

Mhusika, Tatu, mwanaharakati anayepigania uhuru nchini Tanganyika amekumbwa na mgogoro katika ndoa yake. Mume anapambana na Tatu kwa kuitelekeza familia pweke, kisha kujikita kwenye siasa zaidi. Kukosa kiasi kwenye shughuli za siasa kumemnyima Tatu fursa ya kuhudumu kama mke na mama katika familia. Dhamira hiyo imewasilishwa hivi;

77) TATU: *Leo asubuhi kaamka na kunipandishia jazba,*
*"We mwanmke! Nimechoka na umalaya wako!*
*Mnaenda huko na huko, mnajifanya kuuza kadi za TANU, kumbe mnafanya uasherati!*
*Siwezi kurudi nyumbani nakuta watoto peke yao, mwanamke kiguu na njia. Siwezi!*
(Uk. 16)

78) TATU: ...
*Akanitupia talaka si mke wangu:*
*"Kwenda mwana kwenda weeh!*
*Shetani...! Ibilisi mkubwa!"*
(Uk. 17)

Mtunzi wa tamthiliya hii, Emmanuel Mbogo anafundisha wanawake walioolewa kuheshimu ndoa zao. TATU, miongoni mwa wanaharakati wanaopigania uhuru nchini Tanganyika ameingia kwenye kadhia nzito kwenye ndoa yake hadi akaachwa na mume wake kwa kupewa talaka. Maneno yaliyotumika katika tamthiliya hii (Data Na. 78 & 79) ni makali kuashiria hali ngumu iliyowakumba wanandoa hawa. Mf. Shetani, Ibilisi, Kiguu na njia n.k. Misamiati inayorejewa katika mgogoro huo baina ya wanandoa inaonyesha ishara mbaya kuhusu hali ya ndoa ya Tatu na mume wake.

Dhana za Shetani, Ibilisi na watu viguu na njia (wazurulaji) hutumika kurejea watu waovu, maadui au watu wasiofaa katika jamii kwa mujibu wa vitabu vya kiimani (Chamba, 2014). Hivyo Tatu kuitwa majina hayo na mume wake kunajenga taswira hasi kama hadhira itayahusisha namna yanavyotumika katika Biblia. Majina hayo ni zao la Tatu kukosa kiasi kwenye shughuli zake za kisiasa. Mtunzi teule anaendelea kusisitiza wanandoa kufanya shughuli zao bila kupitiliza. Wanandoa wakizingatia maarifa wanayopewa kuhusu ndoa watahudumu vema katika ndoa, familia kwa jumla katika furaha na amani.

Vilevile matokeo ya utafiti yamebaini dhamira ya mapenzi na ndoa katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora* (2016), kupitia fani za Biblia zilizojitokeza. Dhamira hiyo imejadiliwa kwa kuegema kwenye ndoa baina ya Samora na Josina. Wahusika hao wakiwa Msituni, katika uwanja wa kupigania uhuru nchini Msumbiji, mioyo yao imependana. Pendo hilo linaamsha nia ya kufunga pingu za maisha, ndoa huko huko katika uwanja wa mapambano, Msituni. Tukio hili limewasilishwa namna hii;

79) MONDLANE: Hivyo tangazo langu kwenu ni kuwa: kama anga zitakuwa shwari; bila kuchafuliwa na makombora ya Salazar, *arusi ya kuwaunganisha hawa wawili*, *Samora na Josina*, itafanyika wiki ijayo hapa Msituni.
(Uk. 16)

80) JOSINA: Mimi nakuchagua wewe
Nakutaka wewe tu Samora
Tazama, ndevu zako nzuri.
Nyeusiiii!!!
*Nasubiria siku tutakayofunga ndoa*; ...
(Uk. 17)

81) JOSINA: Hata mimi nakupenda (kimya)
*Samora... nina hamu... natamani uipande hima mbegu ya penzi lako hapa.*
*Ukamuumbe kiumbe ndani ya tumbo hili la kike ili nikuzalie pacha! (Samora anacheka) Usicheke!*
*Nitakuzalia pacha mvulana na msichana.*
*Kisha tutawaondoa pacha wetu huku vitani*.
(Uk. 19)

Mazungumzo ya wahusika tajwa (Data Na. 80 – 82) yamewasilisha dhamira ya mapenzi na ndoa baina ya wapambanaji, Josina na Mondlane. Mtunzi teule ametumia fani za Biblia kujadili dhamira ya mapenzi na ndoa. Mosi, kuna nukuzi kuhusu dhana ya ndoa. Mtunzi teule anaijadili ndoa kama muunganiko wa watu wawili. Pili, lengo la ndoa limeambatishwa kama Biblia inavyoeleza. Kwamba, mke na mume wanaoana kwa lengo la kuzaa watoto ili kuendeleza kizazi.

Fani zilizotumika katika kuwasilisha dhamira ya mapenzi na ndoa ni mwangwi wa lengo la Mungu Mwenyezi kuanzisha taasisi ya ndoa. Agizo alilotoa Mwenyezi Mungu kwa wanandoa wote, kwamba wakishafunga ndoa wanapaswa kuzaa na kuujaza ulimwengu limesikika tamthiliya teule. Biblia inaeleza kwamba, Mola aliwaumba Adam na Hawa (Eva), akawafungisha ndoa kisha akawapa agizo kwenda kuzaa ili kuujaza ulimwengu. Biblia inaandika;

> ‘Mungu akawabarikia, Mungu akawaambia, Zaeni, mkaongezeke, mkaijaze nchi, na kuitiisha, mkatawale Samaki wa baharini, na ndege wa angani, na kila kiumbe kiendacho juu ya nchi.”
> (Mwanzo 1:28)

Kimsingi, fani za Biblia kuhusu dhana ya ndoa na madhumuni ya ndoa kutoka kwenye Biblia ni daraja zuri kwa hadhira kubaini dhamira hii. Katika fasihi ya Kiswahili kupitia tamthiliya teule, Emmanuel Mbogo anazungumza kuhusu mapenzi na ndoa. Humo ameeleza dhana ya ndoa na lengo au kusudi la ndoa. Ndoa imeelezwa kama muungano wa watu wawili; mke na mume.

Kusudi la ndoa katika tamthiliya hii limewekwa bayana kuwa ni kuendeleza kizazi cha wahusika. Vilevile kwa mujibu wa Biblia, kusudi kuu la wanandoa ni kuzaa na kuujaza ulimwengu. Ndiyo maana hata Josina anatoa miadi ya kuzaa mapacha punde anapoingia kwenye ndoa. Fani hizo zote ni ngazi kwa wasomaji kubaini dhamira hii, kama Nadharia ya Mwingilianomatini inavyoelekeza kwa msomaji kubaini maana katika matini. Hadhira ikihusisha fani hizo na jinsi zilivyotumika katika Biblia inabaini mengi kuhusu dhana ya ndoa; fasili na malengo ya ndoa ulimwenguni kama Mungu alivyoelekeza kupitia wanandoa wa kwanza, Adam na Eva/Hawa.

Pamoja na hayo matokeo ya utafiti yamebaini kwamba dhamira ya mapenzi na ndoa inadhihirka kupitia fani za Biblia katika tamthiliya ya *Mtumwa hadi Siti Binti Saad*

(2018). Wahusika wawili katika tamthiliya hii, wachumba wamekutana kusemezana kuhusu ndoa na hatma ya ndoa yao endapo watafanikiwa kufunga ndoa. Wahusika hao ni Siti na Khamis. Tamthiliya hii inaeleza;

82) KHAMIS: ...
*Tafadhali kimwana, likubali ombi la penzi langu.*
*Tuoane; tuwe mume na mke. Mola akitujaalia tuzae watoto na tuijaze dunia* (Uk. 7).

Mtunzi teule, Emmanuel Mbogo kupitia maongezi ya mhusika Khamis (Data Na. 83) anaendelea kufundisha jamii kuhusu dhamira, kusudi la ndoa katika jamii. Mbogo anatanabaisha kuwa, miongoni mwa lengo la watu kuoana ni kuzaa na kuujaza ulimwengu. Kusudi hili la ndoa limeelezwa kwenye Biblia. Mungu alipowaumba wanadamu, mke na mume aliwaagiza waoane kisha wazae na kuujaza ulimwengu.

Vilevile, Emmanuel Mbogo amejadili dhamira ya mapenzi na ndoa katika tamthiliya ya *Tanzia ya Patrice Lumumba* (2015). Tamthiliya imebeba dhamira ya mapenzi ya ulaghai. Mtunzi teule anawaasa wanandoa kuwa makini na mapenzi ya ulaghai. Kwamba, mapenzi ya ulaghai ni mwiba kwa wanandoa. Fani za Biblia zilizojitokeza katika tamthiliya hii zinaakisi mapenzi ya ulangai kwa wanandoa katika jamii. Tshombe anasema;

83) TSHOMBE: *Pauline, mimi siko tayari kufa kama Adam.*
*Adam alijua fika kuwa tunda lile lilikuwa sumu, lakini kwa ushawishi na ulaghai wa mwanamke,*
*Adam alichukua ufu, akautafuna, akaumeza, akafa*
(Uk. 54)

Mtunzi teule, katika kisa hiki ametumia simulizi kutoka katika Biblia, kitabu cha Mwanzo 2:17. Dhamira ya ulaghai kwa wanandoa imezungumzwa humo. Adam alidanganywa na mke wake, akavunja agizo alilopewa na Mwenyezi Mungu hatimaye akahukumiwa adhabu ya kifo. Hadithi hiyo inaeleza kuwa, Mwenyezi

Mungu aliwapa wanandoa hao; Adam na Eva kibali cha kula matunda yote katika bustani ya Edeni, isipokuwa matunda ya mti mmoja tu. Baadaye mke wa Adam, Bi. Eva alitembelewa na Shetani akadanganywa ale tunda lililokatazwa tena akachukua sehemu ya tunda akampa tunda mume wake naye ale. Mungu akawashukia na kuwahukumu kifo. Biblia imeeleza hivi;

> "*Adamu akasema, Huyo mwanamke uliyenipa awe pamoja nami ndiye aliyenipa matunda ya mti huo, nikala. BWANA Mungu akamwambia mwanamke, Nini hili ulilolifanya? Mwanamke akasema, Nyoka alinidanganya, nikala..."*
> (Mwanzo 3: 12 – 13, 16 – 19)

Kwa jumla, matokeo ya utafiti huu yamebaini kwamba mtunzi amerejea fani mbalimbali kutoka katika Biblia kuwasilisha dhamira ya mapenzi na ndoa. Nukuzi za Biblia; Maneno ya Biblia; Simulizi za Biblia; Misemo ya Biblia kuhusu ndoa imetumika katika tamthiliya teule zote sita kama tulivyobainisha. Dhamira hiyo ilijadiliwa awali katika Biblia. Fani mbalimbali alizohusisha mtunzi teule kueleza dhamira hii zinadhihirisha dhamira hiyo barabara. Emmanul Mbogo katika tamthiliya teule ameonyesha matokeo hasi kwa wanandoa kukosa kiasi katika shughuli zao. Hali hiyo imesababisha waume; Mwangii, Tom, Khamis na wake; Wangari, Tatu, Bibi Titi kushindwa kutimiza wajibu vema katika ndoa. Wanandoa wanakumbushwa wasitende shughuli za uzalishaji kupitiliza. Kazi zinazofanyika na wanandoa hazipaswi kuwa chachu ya kuharibu mapenzi na ndoa katika jamii.

Nadharia ya Mwingilianomatini inaeleza kuwa, katika kubaini maana ya matini ni muhimu kuhusisha vipengele vingine nje ya matini inayosomwa au kusikilizwa (Wafula, 2007). Katika kuwasilisha dhamira hii mtunzi ametumia fani za Biblia. Fani hizo zinazungumza kuhusu dhana ya ndoa, malengo ya ndoa na hali mbaya

zinazokabili ndoa katika jamii zama hizi. Vilevile mapenzi ya ulaghai kwa wanandoa yameelezwa. Matini ya Biblia, matini awali ilitumia fani hizo kuwasilisha dhamira hiyo pia kama tulivyobainisha. Hivyo basi, kuhusishwa kwake katika usomaji wa tamthiliya hii, ni ngazi nzuri kwa hadhira kubaini dhamira hii kama ilivyowasilishwa na mtunzi teule, Emmanuel Mbogo.

### 4. 3. 11 Ukombozi wa Kisiasa Afrika

Mbali na hiyo, matokeo ya utafiti huu yamebaini dhamira ya ukombozi wa kisiasa Afrika iliyowasilishwa kupitia fani mbalimbali za Biblia katika tamthiliya teule. Mtunzi teule, Emmanuel Mbogo ametumia fani za Biblia kuwasilisha dhamira hii. Sehemu inayofuata hapa chini, mtafiti amechambua dhamira hiyo barabara akihusisha fani za Biblia katika tamthiliya teule pamoja na Nadharia ya Mwingilianomatini.

Ukombozi ni kitendo cha kubadilika kutoka hali duni ya maisha na kuingia katika hali nzuri ya maisha katika nyanja za kiuchumi, utamaduni, siasa na kijamii (Abdallah, 2018). Mtafiti huyu akifasili dhana ya ukombozi anashadidia kwamba, mtu anayetoka daraja la chini katika nyuga mbalimbali za maisha kama vile siasa, uchumi na jamii kuingia daraja la juu ndiye mkombolewa.

Pia ukombozi wa kisiasa unaelezwa kama ukombozi unaohusu taifa kuwa huru na kufanya mambo yake yote ya kisiasa likiwa na mamlaka kamili (Mlaga, 2015). Maelezo yanayotolewa na mwanazuoni huyu yanashadidia kuwa, mamlaka ya taifa kufanya maamuzi na kutekeleza mambo bila masharti, chuki wala vitisho kutoka nchi nyingine ndiyo huitwa ukombozi wa kisiasa.

Basi, dhana ya ukombozi wa kisiasa Afrika katika utafiti huu imetumiwa kurejea hatua mbalimbali zilizochukuliwa na nchi za Afrika ili kujipatia uhuru wa kisiasa kutoka kwa Wakoloni. Yunus (2013) anaeleza kuwa kuanzia miaka ya 1900 nchi nyingi barani Afrika zilianza kupambana na Wakoloni kutoka Ulaya kufa na kupona ili zijitawale. Jamii nyingi za Afrika zilitaka kuondokana na ukoloni mkongwe uliowakalia kooni karne lukuki. Kwa mfano; Msumbiji ilitawaliwa na Ureno miaka mia nne na ushee.

Wakoloni walipata faida kubwa sana kwa kutawala Afrika hivyo hawakuwa tayari kuachia uhuru kwa nchi za Afrika kwa njia rahisi (Omary, 2011). Mtafiti huyo anaweka bayana kuwa Wakoloni walinufaika mno na rasilimali za Afrika kama vile madini, masoko ya bidhaa zao, ardhi, bidhaa za kilimo na rasilimali watu katika shughuli zao mbalimbali za kiuchumi. Nchi za Afrika kupata uhuru ilichagiza hofu kwenye mitima yao kupata hasara kubwa kama Afrika itakuwa huru. Hivyo, Wakoloni nao sehemu kubwa walipambana nan chi za Afrika kufa na kupona kutoachia uhuru kwa namna nyepesi. Baadhi ya nchi za Afrika zilipata uhuru kwa kumwaga damu. Mathalani; Afrika Kusini, Msumbiji, Demokrasia ya Kongo n.k.

Kwa jumla, fasihi ya andishi ya Kiswahili katika kumbo zake kuu; nathari na nudhumu imezungumza dhamira ya ukombozi wa kisiasa Afrika kwa namna mbalimbali (Mulokozi, 2017). Mwanazuoni huyu anaendelea kueleza kuwa watunzi wanaoeleza dhamira ya ukombozi wa kisiasa Afrika kwa kuhusisha harakati za ukombozi kabla ya uhuru. Dhamira hii inaweza kubainika kwenye riwaya, tamthiliya na diwani za watunzi wa Kiswahili kabla ya uhuru.

Pia dhamira hii inaelezwa kwa kuhusisha harakati zilizoendelea ndani ya nchi za Afrika baada ya uhuru (Mlaga, 2015). Harakati hizo za ukombozi zilikuwa zikipinga utawala wa kibeberu uliondelezwa na viongozi walioshika hatamu kutawala nchi za Afrika. Viongozi wengi wazawa waliendeleza sera za dhuluma, uonevu, ubaguzi, unyanyasaji na uporaji wa rasilimali za nchi kwa manufaa yao binafsi si taifa zima kama iliyopaswa. Hali hii iliibua wazawa mbalimbali kwenye nchi Afrika kupambana ili wajikomboe tena.

Kimsingi, dhana ya ukombozi wa kisiasa Afrika katika utafiti huu ilitumika kurejea harakati mbalimbali za ukombozi zilizokuwa zikifanyika barani Afrika kabla ya uhuru na baada ya uhuru. Ukombozi kabla ya uhuru ulipiganiwa kutoka kwa Wakoloni, jamii za Ulaya zaidi. Ukombozi baada ya uhuru ulipiganiwa kutoka kwa watawala wazawa, walioachiwa nchi na Wakoloni kisha wakatawala kwa ubadhirifu.

Matokeo ya utafiti huu yamebaini kwamba ukombozi wa kisiasa Afrika kutoka kwa Wakoloni wa Ulaya na viongozi wazawa Afrika ni miongoni mwa dhamira iliyomshughulisha zaidi mwandishi teule, Emmanuel Mbogo katika bunilizi teule. Fani za Biblia zilizojitokeza katika tamthiliya teule zilikuwa ngazi kuwasilisha dhamira ya ukombozi wa kisiasa Afrika kabla ya uhuru na baada ya uhuru.

Nchi za Afrika zilipambana kufa na kupona karne ya 19, kupata uhuru wao kutoka kwa wakoloni kutoka Ulaya na pande mbalimbali za ulimwengu. Afrika ilipopata uhuru, watawala wazawa wengine wakaendeleza kasumba za Kikoloni. Jamii zikainuka tena kukabiliana na viongozi hao dhalimu.

Mtafiti alipochunguza tamthiliya ya *Wangari Maathai* (2015) alibaini dhamira ya ukombozi wa kisiasa ndani yake. Mbogo katika drama hii ametumia fani mbalimbali za Biblia kueleza dhamira ya ukombozi nchini Kenya, baada ya taifa hilo kupata uhuru. Mhusika mkuu Wangari Maathai amechorwa akifanya harakati mbalimbali za amani, demokrasia, utawala bora na matumizi sahihi mazingira na rasilimali za nchi ya Kenya. Tamthiliya hii inadokeza migogoro ya kisiasa nchini Kenya kupitia maisha ya Wangari Maathai.

Dhamira ya ukombozi wa kisiasa katika tamthiliya hii kupitia imedhihirishwa kupitia fani za Biblia; nukuu za Biblia na sajili mbalimbali zenye taswira ya Biblia. Mtunzi teule anaeleza;

84) WANGARI: ...
Ndipo watakapotambua kuwa,
*Mungu wa Profesa Wangari Maathai*
*Halali wala hasinzii*!
(Uk. 53)

Emmanuel Mbogo kupitia mhusika Wangari katika tamthiliya hii anazungumza kuhusu harakati za ukombozi nchini Kenya (Data Na. 85). Viongozi dhalimu nchini humo baada ya Kenya kupata uhuru kutoka kwa Wakoloni waliwaonea Wakenya na kuwafanya watumwa. Ndipo sasa walipoibuka raia wanaharakati, Wangari na wenzake kupambania ukombozi wa kweli katika nchi yao.

Wangari amechorwa kupambana kufa na kupona kupigania amani, demokrasia na utawala bora taifa la Kenya. Maelezo ya Wangari yanamuonyesha Wangari akiwatia moyo raia wa Kenya kwamba, iko siku watakuwa huru kweli kweli (Data Na.85). Mwanaharakati huyo anatangaza mbele ya hadhara kuwa, ‘Mwenyezi Mungu’ anayemuamini atawasaidia wapate uhuru dhahiri waliougonja kitambo kirefu.

Emmanuel Mbogo amenukuu sajili kutoka katika Biblia inayoeleza habari za Mwenyezi Mungu akaiweka kinywani mwa Wangari. Biblia inaeleza habari za Mfalme Daudi, kiongozi wa taifa la Israel. Mfalme huyo aliwajulisha raia wake kuwa, Mungu wanayemuani ni Mungu anayekaa macho muda wote; mchana na usiku. Hivyo basi, hatawaacha wavamiwe na taifa lolote. Mfalme Daudi anasema;

> *"Naam, hatasinzia wala hatalala usingizi. Yeye aliye mlinzi wa Israel"*
> (Zaburi 121:4).

Mfalme Daudi, mwandishi wa kitabu cha Zaburi katika Biblia alinukuu maneno hayo kuwatia moyo raia wake wakati wa mapambano vitani. Mtawala huyo aliwaambia raia wasiogope wala kukata tamaa katika mapambano wanayoyaendea. Kwamba, taifa lao Israel litakuwa salama daima kwani Mungu wao yuko macho saa ishirini na nne akiwalinda. Mchana na usiku, jicho la Mwenyezi Mungu wao huwa macho kuwalinda watu wake, taifa la Israel.

Hivyo basi, nukuzi hiyo ya Biblia ikihusishwa wakati wa usomaji wa tamthiliya teule kama ilivyotumika awali, inadhihirisha dhamira ya ukombozi wa kisiasa. Wangari Maathai anapozungumza na Wakenya kuhusu ukombozi wao anawatia moyo, wasiogope. Punde ukombozi wa kweli utapatikana Kenya.

Wangari anamuasa kila raia ajitie nguvu hadi waupate ushindi maana Mungu anayemuamini yuko na Wakenya wanaoonewa. Mungu huyo anaelezwa kuwalinda wanyonge nchini Kenya saa ishirini na nne. Wakenya wengi walitamani kukombolewa kutoka kwenye ufisadi, ukabila na hali ngumu ya maisha kutoka kwa viongozi walioongoza taifa hilo baada ya uhuru mwaka 1964. Mathalani Mzee Jomo

Kenyatta (1964 – 1978), Mzee Daniel Arap Moi (1978 – 2002), Mwai Kibaki (2002 – 2013) na wengine waliofuata baada yao.

Hali kadhalika utafiti huu ulibaini pia dhamira ya ukombozi wa kisiasa katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya* (2016). Emmanuel Mbogo katika kazi hii anaendelea kueleza harakati mbalimbalii za kisiasa zilizofanywa na wanaharakati baada ya nchi ya Kenya kupata uhuru kutoka kwa Wakoloni, Waingereza.

Historia ya Afrika inaeleza kuwa viongozi wazawa nchini Kenya walioachiwa dhamana ya kuongoza nchi kutoka kwa Wakoloni, walifanya isivyo katika nafasi zao (Ngai, 2022). Pamoja na Kenya kupata uhuru, raia waliendelea kuteseka. Jambo hilo lilipelekea jitihada mpya kutoka kwa raia ili kuikomboa nchi yao dhidi ya uovu huo. Thomas Mboya alikuwa miongoni mwa wanaharakati mashuhuri waliobuka kupambana na kiza hicho kilichoibuka punde nchi hiyo ilipopata uhuru. Mwaka 1969 mwanaharakati huyo aliuawa, chini ya utawala wa Mzee Jomo Kenyatta.

Dhamira ya harakati za ukombozi wa kisiasa nchini Kenya kupitia fani za Biblia katika tamthiliya hii imedhihirika namna hii;

85) KANOGA: Inabidi tujipange kabla ya Mkutano na Rais
Watu walijitoa mhanga!
*Watu walitoa sadaka kwa uhai wa damu iliyomwagika*.
Walichinjwa kama Mbuzi
*Damu yao ikawa kafara kwa ajili ya nchi hii*.
*Na ardhi nayo ikaachama na kuinywa damu hiyo* kama lijabu ya madonda yaliyotokana na mtutu wa bunduki ya Mkoloni
(Uk. 14)

Mazungumzo ya Kanoga ndani yake mtunzi amerejea simulizi ya ukombozi wa kiimani wa mwanadamu katika Biblia (Data Na. 86). Biblia imeandika simulizi

inayoeleza kwamba, Mtume Yesu Kristo alitumwa na Mwenyezi Mungu kuja duniani ili kumkomboa mwanadamu. Basi, ili kufikia lengo hilo ilibidi mtume huyo atolewe kafara kwa ajili ya wengi. Yesu Kristo auawe kwa kumwaga damu yake ili wanadamu wote ulimwenguni wapate ukombozi. Dhana ya ukombozi katika simulizi hiyo inanasibisha ukombozi wa jamii na umwagaji wa damu. Biblia imeandika hivi;

> *"Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya mti, tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi, tuwe hai kwa mambo ya haki; na kwa kupigwa kwake mliponywa."*
> (1 Petro 2:24).

> *"Nanyi mfahamu kwamba mlikombolewa si kwa vitu viharibikavyo, kwa fedha au dhahabu; mpate kutoka katika mwenendo wenu usiofaa mlioupokea kwa baba zenu; bali kwa damu ya thamani, kama ya mwana-kondoo asiye na ila, asiye na waa, yaani, ya Kristo."*
> (1 Petro 1:18, 19"

Mtunzi teule amehusisha simulizi ya Biblia kuhusu ukombozi wa mwanadamu akiwasilisha dhamira ya ukombozi wa kisiasa nchini Kenya. Simulizi hiyo ilihusisha ukombozi wa mwanadamu na kutolewa kafara kwa mtu mmoja ili kuwasaidia watu wote. Yesu Kristo akafa, wanadamu wote wakakombolewa.

Dhamira hii katika tamthiliya teule, kupitia mhusika Kanoga imelezwa kama jambo gumu mno. Kwamba, ili taifa la Kenya lipate ukombozi murua wa kisiasa ilipasa watu wachache watoe sadaka ya damu yao, wakafa kwa mtutu wa Bunduki. Ndipo sasa uhuru ukapatikana. Hivyo Kanoga anashauri uhuru huo utunzwe na kuheshimiwa barabara kwani ulipatikana kwa gharama kubwa.

Hivyo basi, dhamira hii inahusiana baina ya vitabu teule. Fani ya Biblia iliyotumika ikihusishwa wakati wa usomaji na hadhira iliyowahi kukutana na Biblia awali ni daraja murua kwa hadhira kubaini dhamira inayoelezwa na mtunzi kwa jamii kuhusu ukombozi wa kisiasa Afrika kabla ya uhuru na baada ya uhuru.

Zaidi ya hapo, matokeo ya utafiti huu yamebaini dhamira ya ukombozi wa kisiasa nchini Tanganyika, kabla ya uhuru katika tamthiliya ya *Malkia Bibi Titi Mohamed* (2016). Emmanuel Mbogo amemchora mhusika mkuu, Bibi Titi kama mwanaharakati wa aliyepigania uhuru nchini Tanganyika na Afrika Mashariki miaka ya 1950 hadi 1960. Mhusika huyo kupitia kipawa chake cha kuimba taarab aliweza kuhamasisha Watanganyika kuinuka juu ili kupigania uhuru wa nchi yao.

Mtunzi teule ametumia fani za Biblia katika bunilizi hii katika kuwasilisha dhamira ya ukombozi wa kisiasa nchini Tanganyika miaka ya 1960. Fani hizo zikihusishwa wakati wa kuchunguza tamthiliya hii, kama mhimili wa Nadharia ya Mwingilianomatini unavyoelekeza dhamira hiyo inabainika dhahiri. Mbogo anawasilisha dhamira ya ukombozi akihusisha sajili za Biblia. Sajili hizo zinabainika namna hii;

86) BIBITITI: ...
*Mungu amepanda mbegu ndani mwetu*.
Na tazama mbegu imeota,
*Mungu ametupa uwezo huu*,
Bila ushirikiano wetu hatutapata uhuru...
(Uk. 31)

Malkia Bibi Titi katika maelezo yake anazungumza na wanawake wenzake kuhusu kupigania uhuru wa taifa la Tanganyika (Data Na. 87). Mpambanaji Bibi Titi anawaasa Watanganyika wanawake, washikamane kumng'oa mkoloni, Muingereza. Bibi Titi anakiri kwamba, ngazi ya kupata uhuru ni umoja na mshikamano baina yao ambao Mwenyezi Mungu amepanda ndani yao. Mtunzi teule, Emmanuel Mbogo kupitia bunilizi hii anafundisha jamii kwamba, wanawake nao wana nafasi katika kuleta ukombozi wa kisiasa katika mataifa yaliyomo; Afrika na ulimwengu wote kwa jumla.

Harakati za ukombozi wa Tanganyika kupitia Bibi Titi Mohamed zimehusishwa na mchango wa wanawake katika kuleta ukombozi Afrika. Biblia nayo imeeleza, nafasi ya wanawake katika kupigania uhuru, ukombozi wa kisiasa katika jamii zao. Kitabu hicho cha Biblia kinawatambulisha wanawake kama jeshi kubwa. Aidha, waandishi wa Biblia wanaandika kwamba, kama wanawake wakishikamana na kuwa pamoja, hakuna vita wanayoweza kushindwa (Zaburi 68:11).

Hali kadhalika Bibi Titi anawaasa Watanganyika kudai uhuru kwa njia ya amani si kumwaga damu tena kama walivyofanya viongozi tangulizi. Mtunzi teule katika kueleza hilo ametumia sajili za Biblia kama vile;

87) BIBITITI: *Tunadai uhuru wetu kwa njia ya amani,*
Hatutaki vita.
*Hatutaki umwagaji wa damu.*
Babu zetu mashujaa, akina Kinjeketile, walidai uhuru kwa vita vya Majimaji.
Babu zetu mashujaa, akina Mkwava, walidai uhuru
kwa njia ya vita.
*Nasi leo tunaitukuza na kuikumbuka damu yao iliyomwagika*
*ili Mwafrika awe huru...*
(Uk. 38)

Fani ya Biblia iliyotumika ni simulizi ya Biblia kuhusu dhamira ya ukombozi wa mwanadamu hapa ulimwenguni kupitia mateso na mauti yake Yesu Kristo (Data Na. 88). Biblia inaeleza kuwa ukombozi wa mwanadamu hapa ulimwenguni ulipatikana kwa mtu mmoja kufa kwa ajili ya wengi. Kafara ya mtu mmoja tu, ikawasaidia walimwengu wote (Mathayo 27: 1 - 42).

Mtunzi teule amerejea fani hiyo kueleza ukombozi wa kisiasa nchini Tanganyika tangu enzi za ukoloni (Data Na. 88). Ndipo sasa hadhira inabaini kwamba, jitihada za Tanganyika kupata uhuru zilianza tangu zamani kwa viongozi wazawa kujitoa

Kafara ili wakomboe taifa hilo. Mathalani Kinjeketile Ngwale kutoka huko Ngarambe, Tanganyika aliyepambana na wakoloni kutoka Ujerumani katika Vita ya Maji Maji (1905 – 1907).

Kimsingi, viongozi wengi Afrika katika harakati za ukombozi wa nchi zao kutoka kwa wakoloni kabla ya uhuru walitumia njia za mapigano. Baadhi ya wapambanaji wa mwanzo katika nchi ya Tanganyika walikuwa Chifu Kinjeketile Ngwale na Chifu Mkwawa wa Uhehe. Kinjeketile Ngwale alipambana na wakoloni wa Kijerumani katika vita ya Majimaji mwaka 1905 – 1907 (Jacob, S. 2018). Chifu mwingine aliyepambana na Wakoloni, Wajerumani miaka ya 1890 ni Chifu Mkwawa. Kiongozi huyo kutoka Iringa, jamii ya Wahehe alifanya vita katika sehemu mbalimbali akipambana na Wajerumani hata kiongozi mmoja wa kutoka Ujerumani, Emil Von Zelewsk akafariki Agosti 17, 1891.

Emmanuel Mbogo anaeleza kwamba, miaka ya 1960 ili kupata ukombozi wa kisiasa Watanganyika waliona watumie njia ya amani kupata uhuru wao. Wasitumie njia ya kumwaga damu tena kama ilivyokuwa awali. Bibi Titi katika tamthiliya hii anahamasisha jamii isimwage tena damu. Mwanaharakati huyu anawaasa Watanganyika wapate uhuru kwa njia ya amani.

Pamoja na hayo, matokeo ya utafiti yamebaini kuwa, dhamira ya ukombozi wa kisiasa barani Afrika kwa kutazama harakati mbalimbali za ukombozi katika bara la Afrika, ukirejea nchi ya Msumbiji. Katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora* (2016) mtunzi amejadili dhamira ya ukombozi wa kisiasa. Mondlane na Samora walikuwa viongozi wa mwanzo katika nchi ya Msumbiji. Viongozi hao waliongoza raia wa Msumbiji kupambana na Wareno ili kupata uhuru wao. Pamoja nao Mhe. Julius

Kambarage Nyerere kutoka Tanganyika (sasa Tanzania) alishikamana nao hata nchi yao ikakombolewa. Fani za Biblia zimetumika kudhihirisha dhamira hiyo.

Dhamira ya ukombozi wa kisiasa nchini Msumbiji inadhihirika namna hii katika bunilizi teule tuliyotafiti;

88) NYERERE: *Katika hadubini ya moyo wangu, ninaona hatua kwa hatua, udongo wa Kenya na Uganda; Udongo wa Rwanda na Burundi; Udongo wa Afrika Mashariki na Kaskazini; Udongo toka nchi zote za Afrika ukiungana ndani ya chungu cha Umoja wa Afrika*
[Kelele shangwe... Hashimu Mbita anampokea Kibuyu]
(Uk. 83)

Mtunzi teule amemchora mhusika Nyerere kama mwanaharakati wa mwanzo katika kupigania uhuru barani Afrika (Data Na. 89). Mwanaharakati huyu alishirikiana na wapambanaji wengine kutoka mataifa mbalimbali ili kuzipatia nchi zao uhuru. Kupitia maelezo ya Nyerere akiwa nchini Msumbiji, tunabaini kwamba kiongozi huyo alikuwa akihubiri ukombozi wa kisiasa nchini humo. Juu ya hilo alishauri mataifa yote za Afrika kuungana, yawe na Jumuiya ya Afrika ambayo ndiyo ingekuwa ukuta wa kuwalinda na kutetea mataifa ya Afrika dhidi ya maonevu mbalimbali kutoka jamii za Ulaya.

Kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika katika tamthiliya hii kumenasibishwa na simulizi ya uumbaji wa mwanadamu na viumbe mbalimbali katika Biblia. Kitabu cha Biblia kinaeleza kwamba, Mungu alipoumba vitu alichukua udongo akafanya aliyotaka. Mwanadamu ni miongoni mwa viumbe vilivyoumbwa kwa udongo. Hivyo, jumuiya ya Afrika ilipaswa kuumbwa kwa kuchanganya udongo kutoka mataifa yote wanachama (Data Na. 89). Juu ya uumbaji wa mwanadamu Biblia inaandika;

> *"Kwa jasho lako utajipatia chakula mpaka utakaporudi udongoni ulimotwaliwa; kwa maana wewe ni mavumbi, na mavumbini utarudi."*
> Mwanzo 3:19

Mtunzi teule ametumia simulizi hii katika Biblia kubainisha kwamba, ili mataifa ya Afrika yapate uhuru wa kweli yalipaswa kuchukua udongo katika nchi zao na kuuweka kwenye chungu kimoja, zikae kwa umoja na mshikamano. Nyerere ametaja mataifa yote za Afrika Mashariki mathalani Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Uganda na Tanganyika kuungana.

Simulizi kutoka kwenye Biblia kuhusu uumbaji wa mwanadamu, dunia na vyote vilivyomo ndani yake anayorejea Mbogo kupitia mhusika Nyerere inadhihirisha dhamira ya ukombozi wa kisiasa Afrika kabla ya uhuru. Tumeelezwa na waasisi wa Nadharia ya Mwingilianomatini kuwa, maana ya matini ya kazi ya fasihi inapatikana kwa hadhira kuhusisha vipengele vingine nje ya muktadha wa fani inayotendwa au inayowasilishwa wakati wa kutazama, kusikiliza ama kusoma kazi ya fasihi. Simulizi ya Biblia dhidi ya uumbaji inaeleza udongo kuchukuliwa kutoka pande mbalimbali, kufinyangwa kuwa kitu kimoja ndipo dunia ikapatikana. Mtunzi anaeleza Afrika huru, isiyotawaliwa na mkoloni inaweza kupatikana kwa udongo wa nchi zote za Afrika kuwekwa pamoja na kuwa mji mmoja. Afrika ikiwa moja itakuwa na nguvu kubwa za kupambana ukoloni mkongwe na ukoloni mamboleo barani Afrika.

Pamoja na hayo, utafiti ulibaini dhamira ya ukombozi wa kisiasa barani Afrika katika tamthiliya ya *Tanzia ya Patrice Lumumba* (2015). Mtunzi teule katika tamthiliya hii amezungumza kuhusu harakati za ukombozi wa kisiasa huko Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (JKK). Fani za Biblia zimetumika kuwasilisha dhamira hiyo. Hadhira wanaweza kuhusisha fani hizo na matini teule ili kung'amua dhamira

aliyowasilisha mtunzi teule. Dhamira hii inadhihirika namna hii katika tamthiliya teule;

89) MOBUTU: …*Imebidi mtu mmoja fedhuli afe kwa faida ya Wakongomani wote*...”
(Uk. 41)

90) PAULINE: [Kwa sauti kubwa! Hasira!]
*Tshombe! Shetani!!*
[Anatafakari, analia akimkumbatia Patrice]
Oooh! Patrice! *Kwa nini Mungu alikupangia kifo cha mateso na huzuni kiasi hichi*? [Analia]
*Namuomba Mola, damu yako hii Patrice iwe sadaka na baraka kwa Wakongomani* lakini iwe majuto na laana kwa maadui na wadhalimu wako.
(Uk. 54)

Kupitia mazungumzo ya wahusika hawa wawili; Mobutu na Pauline mtunzi amewasilisha dhamira ya ukombozi wa kisiasa nchini Kongo akiihusisha simulizi za ukombozi wa wanadamu katika Biblia (Data Na. 90 & 91). Itikadi za ukombozi katika vitabu hivi viwili; Biblia na *Tanzia ya Patrice Lumumba* zinafanana. Kwamba, ili jamii hizi mbili zikombolewe na kuwekwa huru ilibidi mtu mmoja atoe uhai wake kwa ajili ya watu wote ndani ya jamii. Ndipo sasa mkombozi wa Kongo, Mhe. Patrice Lumumba kifo chake kinahusishwa na ukombozi wa taifa lake. Hivyo basi, ilibidi afe yeye ili taifa lote la Kongo lipate uhuru wa kisiasa. Patrice alipambana kupigania uhuru wa Kongo na katika jitihada hizo akapoteza maisha yake kwa kuuawa na Wakoloni.

Basi, utafiti umebaini kwamba kisa cha ukombozi wa kisiasa nchini Kongo kinaendana na simulizi ya ukombozi wa taifa la Israel katika Biblia. Simulizi inaeleza kwamba, Wayahudi walikombolewa kwa kuuawa mtu mmoja, Yesu Kristo. Biblia kuhusu ukombozi wa taifa la Israel inaeleza kuwa, ili taifa hilo likombolewe

kutoka kwenye maasi waliyofanya mbele za Mwenyezi Mungu ilibidi mtu mmoja afe, amwage damu yake ndipo Wayahudi wakombolewe na kurejeshewa tena mahusiano na Mola wao kama ilivyokuwa awali kabla Adam na Eva/Hawa hawajatenda uasi katika Bustani ya Eden. Biblia inaandika;

> *"Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya mti, tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi, tuwe hai kwa mambo ya haki; na kwa kupigwa kwake mliponywa."*
> (1 Petro 2:24).

Kimsingi, hadhira ya *Tanzia ya Patrice Lumumba* aliyewahi kukutana na simulizi za ukombozi wa mwanadamu katika Biblia, akihusisha matini hizi anaweza kung'amua vema dhamira hii. Kwamba, zoezi la kuikomboa nchi si swala rahisi. Linahitaji wapambanaji waliojitoa muhanga ndipo wafanikiwe. Patrice na wanaharakati wenzake nchini Kongo walipambana kufa na kupona kuipatia Kongo uhuru. Pamoja na changamoto mbalimbali walizokumbana nazo, wengine wakapoteza maisha njiani lakini bado walishikamana hadi wakafanikiwa kuikomboa nchi ya Kongo kutoka Wakoloni wa Ulaya.

Kwa jumla, matokeo ya utafiti huu yamebaini kwamba, dhamira ya ukombozi wa kisiasa barani Afrika imedhihirika kwa namna mbalimbali katika tamthiliya teule. Dhamira hiyo imeelezwa katika tamthiliya teule sita zote tulizorejea katika utafiti tuliofanya. Mtunzi teule ametumia fani mbalimbali kutoka kwenye Biblia kudhihirisha dhamira hiyo.

Nadharia ya Mwingilianomatini inahusishwa na jumla ya maarifa na mbinu zinazoifanya matini kuwa na maana (Mningo, 2015). Kwa hivyo maana ya matini katika nadharia hii huangaliwa kama inayotegemea matini nyingine. Fani za Biblia

zilizojitokeza katika tamthiliya teule ni ngazi muafaka kwa wasomaji kubaini dhamira hii. Fani zinazoeleza dhamira ya ukombozi wa kisiasa Afrika kabla na baada ya uhuru, zimehusisha mbinu mbalimbali zilizotumika awali kwenye Biblia. Mathalani viongozi wa Kiafrika kubaini kwamba, ukombozi wa nchi mbalimbali ulihusishwa kwa watangulizi kujitoa mhanga, kujitoa kufara, kufa kwa ajili ya wengi. Kwa kufanya hivyo, nchi zilifanikiwa kupata ukombozi wa kisiasa. Itikadi hiyo imerithiwa kutoka kwenye kitabu cha Biblia kama tulivyobainisha.

Wasomaji wa tamthiliya teule wakiihusisha fani hizo na jinsi zilivyotumika katika

Biblia, wanaweza kung'amua vema analowasilisha mtunzi. Kwamba, ukombozi wa kisiasa si jambo rahisi bali unahitaji moyo wa dhati. Utafiti huu unaunga mkono dai la wahakiki wa mwingilianomatini kwamba, maana ya matini moja hutegemea matini nyingine iliyotangulia kabla yake. Fani za Biblia zote zilizorejewa zimedhihirisha dhamira hiyo, ukombozi wa kisiasa. Wasomaji wakizihusisha kutoka matini hiyo wanabaini dhamira iliyowasilishwa barabara.

### 4. 3. 12 Ukombozi wa Kifikra

Fikra ni mawazo au mafikirio ya mtu juu ya kitu fulani (Emmanuel, 2021). Mtaalam huyu anazidi kunyambua kwamba, mawazo hayo aliyonayo mtu juu ya kitu fulani ndiyo hutengeneza msimamo wa kiutendaji ndani yake. Hali kadhalika uwezo wa kufikiria hutofautiana kutoka kwa mtu mmoja, kwenda kwa mtu mwingine. Baadhi ya watu ulimwenguni wanasemwa kuwa na uwezo mkubwa wa kufikiri kuliko wengine. Watu wenye fikra pana, huwaza mambo makubwa na wenye fikra finyu, huwaza mambo madogo (Julius, 2018).

Aidha mwanazuoni Fungavyema (2020) anafasili dhana ya fikra kama mtazamo alionao mtu juu ya jambo fulani ndiyo maana utasikia mtu anasemwa ana fikra chanya au hasi kuhusu jambo fulani. Fauka ya hayo Fungavyema (Ktj) anaendelea kudadavua kuwa fikra hutengenezwa ndani ya ubongo au akili ya mtu katika hali isiyoonekana. Mtafiti kupitia mwanazuoni huyo amebaini kuwa, fikra ndani ya mtu hujengwa na vitu mbalimbali vinavyopatikana katika mazingira mahsusi mathalani utamaduni, utawala, mifumo ya elimu, mahusiano, malezi n.k.

Fauka ya hayo fikra inaweza kufasiliwa kama mipango au mawazo ya mtu kwenye kichwa chake kuhusu jambo fulani (BAKITA, 2022). Wanazuoni hawa wanaeleza kuwa fikra inaweza kuchukuliwa kama maoni au mtazamo wa mtu dhidi ya jambo fulani. Fikra zinahusianishwa na mtazamo wa mtu binafsi zaidi dhidi ya uga fulani mahsusi.

Hivyo, tunapowasoma wanazuoni wote hawa kuhusu dhana ya fikra tunaweza kufasili fikra kama mawazo, mtazamo au maoni aliyonayo mtu ndani yake dhidi ya jambo fulani. Mawazo aliyonayo mtu dhidi ya jambo fulani ndiyo huwa ngazi kwa mtu kuratibu maisha katika nyanja mbalimbali za maisha.

Jamii nyingi katika karne tuliyomo inanasibisha dhana ya maendeleo kama chipukizi la fikra chanya (Butiku, 2023). Andiko la Butiku (Ktj) linaeleza kuwa watu wanaoshindwa katika hali mbalimbali katika maisha wamewekwa katika kundi la watu wenye fikra duni. Wahenga uswahilini katika idili za maisha wametuachia semi hii, ‘Kimjazacho mtu, ndicho kimtokacho’. Vile mtu anavyowaza ndivyo hutenda. Mambo yote yanayojiri katika maisha ya mwanadamu ni zao la fikra ndani yake.

Barani Afrika, makazi ya mtu mweusi kuna dai kuwa hali ngumu ya maisha iliyotawala barani humu ni tokeo la fikra duni zilizojengwa ndani ya watu wake (Adolf, 2021). Wakazi wengi katika bara hili wanajiona kuwa watu walioshindwa maisha. Fikra hizo hasi ni tokeo la ukoloni na mfumo wa matabaka katika jamii. Jamii za Kiafrika zinajengwa katika matabaka makubwa mawili. Mosi, matabaka yenye neema zaidi au maisha bora. Pili, matabaka yenye laana zaidi au maisha duni. Waafrika wanaoishi katika tabaka hili la pili wamekata tamaa ya maisha.

Kazi za fasihi huwasilisha fikra mbalimbali za watunzi wa kazi hizo. Dhamira ya ukombozi wa kifikra hujadiliwa kwenye kazi za sanaa. Wasanii wa kazi za fasihi ya Kiswahili nao wamejadili dhamira hii. Hali ya kukata tamaa iliyowakumba wakazi wengi wa bara ya Afrika imewashughulisha waandishi katika bunilizi za fasihi (Faustine, 2020). Watunzi hupanda fikra chanya ndani ya hadhira zao ili jamii zikombolewe kifikra. Ndipo sasa zisonge mbele katika maisha bora.

Emmanuel Mbogo, mtunzi teule katika utafiti huu ni miongoni mwa watunzi katika fasihi ya Kiswahili aliyeshughulika mno na dhamira ya ukombozi wa kifikra katika jamii. Bunilizi zake nyingi katika fasihi ya Kiswahili zinabeba dhamira hii. Mtunzi huyo anapanda fikra chanya kwa hadhira yake dhidi ya mambo wanayofikiri kwamba hayawezekani. Mbogo anapanda mafundisho kwamba, maisha bora yenye neema yanaweza kutokea kwa mtu awaye yote ndani ya jamii. Nguzo msingi katika kufikia hiyo neema ni kuongeza juhudi katika kufanya kazi mbalimbali za mikono yetu. Kwa hivyo tutafanikiwa.

Kwa jumla matokeo ya utafiti tuliofanya yamebaini kwamba, Emmanuel Mbogo katika tamthiliya teule amejadili dhamira ya ukombozi wa kifikra. Mtunzi huyu teule katika kujadili dhamira hii amehusisha fani za Biblia. Fani hizo zina mwangwi wa dhamira ya ukombozi wa fikra ndani yake. Katika sehemu inayofuata hapa chini, tumejadili dhamira ya ukombozi wa kifikra katika kazi teule tukihusisha fani za Biblia zilizojitokeza katika tamthiliya teule moja baada ya nyingine.

Dhamira ya ukombozi wa kifikra imewasilishwa katika tamthiliya ya *Mtumwa hadi Siti Binti Saad* (2016). Dhamira hiyo imewasilishwa ikihusisha fani za Biblia. Mbogo anafundisha jamii mchango wa maono katika kufikia mafanikio. Jamii inaelekezwa kuamini na kufanyia kazi ndoto zao, maono yao kwani iko siku maono hutimia juhudi kubwa ikifanywa na mhusika. Mtunzi huyu anapanda fikra za ushindi kwa hadhira. Jamii katika tamthiliya hii inaelezwa kuwa, ushindi katika maisha ni jambo linalowezekana kwa mtu yeyote. Jambo hilo halizingatii muktadha au tabaka anaotoka mhusika. Kwa hivyo, mwanajamii anayetoka familia duni, ya watu maskini anaelezwa kama mtu anayeweza kufanikiwa kiuchumi, kupata maendeleo katika maisha.

Dhamira ya ukombozi wa fikra katika tamthiliya imeelezwa zaidi kupitia mhusika mkuu, Siti Binti Saad. Mhusika huyo amechorwa kutoka familia duni, utumwani huko Zanzibar. Hata hivyo kutokana na maono aliyokuwa nayo katika tasnia ya muziki na jitihada alizofanya kutimiza maono yake muhusika huyo alifanikiwa mno.

Matokeo ya utafiti yamebaini kwamba dhamira hii inadhihirika kupitia simulizi za Biblia, nukuu za Biblia na sajili za Biblia. Fani hizo zinadhirisha fikra chanya anazopanda mtunzi kwa hadhira kuhusu mafanikio katika maisha. Mhusika Siti ana

maono ya kufanikiwa siku moja maishani ingawa amekumbana na kuta nyingi zinazomzuia kusonga mbele katika maisha. Hata hivyo anaapa kupambana kufa na kupona hadi ndoto zake zitimie. Siti anasema;

91) SITI: *[Machozi yanamtoka]*
*Aah! Ni kama njozi ya jinamizi.*
*Hii ni tanzia ... kila nikigeuka na kutazama nyuma, naona giza, naona wingu la nuksani imeyazinga na kuyazingira maisha yangu.*
*Labda ni jini la kukataliwa!*
(Uk. 60)

92) SITI: *Kwanza jina – Mtumwa laendelea kunikataa.*
Kisha ndoa na Rashidi- Rashidi alinikataa.
Hata udongo wa ufinyazi ulinikataa.
Na sasa hivi vidonda na talaka ya Khamisi.
Ama kweli ndoa ndoano …
*Basi, naiambia nafsi yangu: wacha kulia.*
*Tulia. Anza maisha mapya.*
*Ndiyo. Si rahisi lakini majira na wakati vitanipa shufaa hatua kwa hatua …*
(Uk. 61)

Mazungumzo ya mhusika Siti yamebeba sajili za Biblia zinazodhihirisha nafasi ya maono katika kufikia mafanikio kwenye maisha kama tulivyobainisha (Data Na. 92 & 93). Mtunzi anaeleza kuwa mateso ni sehemu ya maisha hivyo hayapaswi kuwa ukuta wa kutimiza maono yetu katika maisha. Bibi Titi amekutana na changamoto nyingi, sawa lakini anaahidi kupambana vyovyote iwavyo hadi maono yake yatimie.

Mtunzi teule ametumia simulizi kutoka kwenye Biblia kuwasilisha dhamira hii. Simulizi hiyo inahusu habari za Mtume Yesu kukataliwa huko kwao Uyahudi. Pia amenukuu sehemu wa mstari wa Biblia. Simulizi za Biblia zinaeleza kuwa Mtume Yesu Kristo alikuja ulimwenguni kwa nia njema, akafanya mengi mazuri lakini bado jamii ya Wayahudi haikumpokea. Biblia inaeleza haya kuhusu mhusika Yesu Kristo;

> *"Alidharauliwa na kukataliwa na watu. Akawa mtu wa huzuni nyingi Ajue masikitiko na kama mtu ambaye watu humficha nyuso zao alidharauliwa wala hatukuhesabu kuwa kitu ..."*
> (Isaya 53:3)

Simulizi za Biblia hapo juu zinaeleza kuwa pamoja na Mtume Yesu kukabiliana na changamoto ya kukataliwa katika jamii ya Wayahudi, alipambana hadi ndoto zake zikafanikiwa. Fikra zake zilitimia kwa kupigwa, kusulubiwa na kuuawa ili amkomboe mwanadamu. Kupitia simulizi hizo walimwengu wakafundishwa kuwa mateso si kuta za kufikia malengo au maono aliyojiwekea katika maisha. Jamii inaelekezwa kupambana katika maisha hadi kutimiza ndoto lengwa.

Vilevile dhamira ya ukombozi wa kifikra inaelezwa kupitia mazungumzo baina ya Siti na Banji, Mfanyabiashara wa Kihindi. Mgeni huyo amehusisha sajili ya Biblia, 'Miujiza ya Mungu' na kiwango alichokiona kwa muimbaji Siti. Banji anasema;

93) BANJI: Mtumwa Binti Saad. Mimi iko kuja Unguja.
Mimi iko tafuta klabu nzuri ya taarab.
Taka peleka klabu kwetu, Bombay, India.
Kisha mimi nafanya recording.
Jana mimi pata fursa, meona shoo yenu.
Mimi jana sikiliza veve.
Haa haaa! Mimi nazunguka Nguja ote, lakini taarab ote mbaya.
Haiko na kwalite.
*Lakini jana mimi naona muujiza ya Mungu.*
*Haa! Haa! Veve Mtumwa iko talenti.*
*Veve iko imba, majuri sana ...*
(Uk. 72)

Sajili ya 'Miujiza ya Mungu' iliyohusishwa na Banji (Data Na. 94) inaelezwa kama matendo makubwa yasiyotarajiwa kirahisi anayofanya Mwenyezi Mungu ulimwenguni (Mastai, 2018). Dhana hiyo katika tamthiliya hii inaashiria kwamba, watu hawakutaraji mtu kama Siti, binti wa kitumwa kuimba vizuri nyimbo za taarabu. Siti aliimba hadi nyoyo za watu kwenye kusanyiko zikafurahi. Ndipo sasa mwanamuziki Siti akafanikiwa maishani.

Hali kadhalika mtunzi wa tamthiliya hii, Emmanuel Mbogo ametumia nukuu ya Biblia kuwasilisha dhamira ya ukombozi wa kifikra. Hadhira lengwa imeelezwa nafasi ya maono katika kufanikiwa kwenye maisha. Mtunzi anafundisha jamii kuwa, maono ndiyo ngazi ya kupanda juu kuyafikia mafanikio yoyote. Wanadamu wanapaswa kuongozwa na maono waliyonayo wanapoishi ulimwenguni (Butiku, 2023). Bonga anasema;

94) BONGA: *Ama kweli Mungu anaweza kumtoa mtu kwenye matope na kumwinua juu katika utukufu na enzi.*
(Uk. 79)

Mtunzi teule kupitia mhusika Bonga katika tamthiliya teule amenukuu semi ya Biblia kueleza jinsi maono yanavyoweza kutimia kwa mtu yeyote katika jamii (Data Na. 95). Jambo hilo linachagizwa kwa nukuu kwamba, Mola anaweza kumtoa mtu kwenye matope hadi kwenye daraja la juu akaketi na wakuu. Mtumwa Siti ameinuliwa kutoka kwenye matope, kupitia muziki akapanda hadi kuketi meza moja na watawala, sambamba wafanyabiashara wakubwa kama Banji (Data Na. 95).

Pamoja na hayo waandishi wa Biblia wamewasilisha dhamira kuhusu nafasi ya maono katika mafanikio ya mtu kwenye maisha. Dhamira hii imejadiliwa pahala pengi na mitume mbalimbali. Nabii Samweli ni miongoni mwa manabii walioeleza nafasi ya maono katika kufanikiwa kwenye maisha. Mwandishi huyo ametumia kisa cha mwanamke mmoja aliyeitwa Hana kuwasilisha dhamira hiyo. Huyo mama aliolewa na mtu mmoja anayeitwa Elikana. Wanandoa hao walikuwa na maono ya kupata watoto lakini walikaa kitambo pasina mtoto. Mama mwenye nyumba, Hana alihuzunika sana kwa jambo hilo. Siku zikapita, Mwenyezi Mungu akasikia sala na

dua zao, Hana akapata mtoto. Ilikuwa shangwe kubwa kwa familia, na mama aliyeteseka na utasa. Shangwe iliujaza moyo wa Hana, kwa kupata mtoto.

Nukuu ya Biblia inayoeleza nafasi ya maono katika kufanikiwa aliyotumia mtunzi teule inasomeka namna hii;

95) *"*BWANA hufukarisha mtu, naye hutajirisha;
Hushusha chini, tena huinua juu.
*Humwinua mnyonge kutoka mavumbini,*
*Humpandisha mhitaji kutoka jaani,*
*Ili awaketishe pamoja na wakuu,*
Wakakirishi kiti cha enzi cha utukufu;
Kwa maana nguzo za dunia zina BWANA,
Naye ameuweka ulimwengu juu yake*."*
(1Samweli 2: 7 – 8)

Kwa jumla, hadhira lengwa ya tamthiliya hii ikihusisha mazungumzo ya wahusika; Bonga na Nabii Samwel katika vitabu teule, dhamira ya ukombozi wa kifikra kwa jamii kuhusu maisha inabainika. Jamii inaelezwa kuwa ndoto za watu hutimia bila kujali kitambo kirefu inachokaa. Hana mke wa Elikana alikaa kitambo bila kupata mtoto (Data Na. 96). Hata hivyo siku ilifika ndoto yake ikatimia. Familia ikapata kicheko maishani kwa mama kufunguliwa tumbo na kumzaa mtoto aliyeitwa Samweli. Mtoto huyo alikuja kuwa nabii mkubwa sana katika taifa la Israel, huko Uyahudi.

Basi, mtunzi teule kupitia mhusika Bonga mkazi wa Unguja kwa niaba ya wenzake, amethibitisha kwamba kweli maono katika maisha yanaweza kutimia kwa mtu yeyote. Mbogo anaeleza kuwa hata watu wa tabaka la chini wanaweza kuinuliwa na kufika tabaka la neema, maisha bora. Mtumwa mmoja viunga vya Unguja amepandishwa juu hadi akabadilishiwa anuani, akaitwa Siti Binti Saad badala ya jina la Mtumwa Siti Binti Saad alilokuwa akiitwa awali. Mtumwa huyo alianza muziki

katika daraja la chini, siku moja akafika daraja la juu hata kurekodi muziki wake nchi za nje, mathalani India kama tulivyoonyeshwa.

Pamoja na hayo dhamira ya nafasi ya maono katika mafanikio maishani imeelezwa pia katika Biblia. Kitabu cha Biblia kimewasilisha dhamira hiyo kupitia simulizi ya kijana mmoja aliyeitwa Yusufu Yakobo Isaka Ibarahim. Kijana huyu alikuwa na uwezo mkubwa wa kuota ndoto. Kupitia ndoto hizo alieleza wenzake jinsi atakavyokuwa maishani mwake siku za usoni. Ndoto hizo zilikuwa chukizo kwa ndugu zake hadi wakaishia kumuuza utumwani Misri.

Watheolojia[1] wanashadidia kwamba, Biblia ilimtumia Yusufu kueleza nafasi ya maono katika mafanikio. Ndoto huanza kwanza ndani ya moyo wa mtu kisha baadaye inadhihirika waziwazi. Uwezo wa maono aliyokuwa nayo Yusufu umenasibishwa na maono yaliyoujaza mtima wa Siti. Yusufu alipelekwa utumwani, akapelekwa gerezani lakini siku moja ndoto za kutawala wenzake zikatimia. Yusufu akawa kiongozi mkuu wa pili ugenini katika taifa la Misri, baada ya Mfalme Faraoh (Mwanzo 37 – 43).

Basi, Emmanuel Mbogo katika tamthiliya teule tuliyotafiti amewasilisha dhamira ya ukombozi wa kifikra. Mhusika mkuu Siti Binti Saad katika tamthiliya hii amechorwa kama mtu aliyekataliwa na jamii yote, wakiwemo waume zake. Shughuli yoyote aliyofanya ili kumuongezea kipato haikufanikiwa. Pamoja na hayo mhusika huyo alijipa moyo na kuamua kuendelea na mapambano hata akafanikiwa kutimiza maono

[1] Watheolojia; ni watu mwenye ujuzi wa Biblia, wanaokiri au kutenda yale yanayohusiana na Mungu Mwenyezi.

yake. Uamuzi wa kuacha kulia na kuinuka tena ili kuendelea na mapambano ya maisha ulimsaidia. Siku moja maono yaliyokuwa ndani ya mwanamuziki huyo kutoka utumwani na kufanikiwa katika muziki zikatimia.

Pamoja na hayo, utafiti huu ulibaini pia dhamira ya ukombozi wa kififikra katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora* (2016). Katika tamthiliya hii, Mhusika Nyerere akiwa nchini Msumbiji alihubiri elimu mpya, ili taifa hilo likombolewe kwenye fikra zao. Nyerere anaeleza kwamba nchi za Afrika, Msumbiji ikiwa miongoni zilipandikizwa fikra duni na Wakoloni. Fikra hizo zilieleza kwamba, Afrika haiwezi jambo bila kutegemezwa na Wakoloni kutoka Ulaya.

Mtunzi teule katika tamthiliya hii anabainisha kuwa wageni kutoka Ulaya katika mimbari mbalimbali walihubiri kuwa, Afrika ni duni. Habari hizi zilififisha fikra za wakazi wengi wa Afrika. Ndipo sasa baada ya nchi za Afrika kupata uhuru, zikapata changamoto ya kujitawala kwani bado wengi waliona hawawezi wenyewe bila msaada wa wageni. Jambo hilo liliinua ari kwa wanaharakati wa ukombozi Afrika kabla ya uhuru, mathalani Nyerere kuanza kuhubiri elimu mpya, kupanda fikra mpya katika mbongo za watu weusi. Nyerere alihubiri kwamba, watu wa bara la Afrika nao wanaweza kujitawala na kufanya mambo yote ambayo watu weupe wanayafanya pasina usaidizi. Fikra hizo zimewasilishwa hivi katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora*;

96) *NYERERE:* Mkoloni bila kukoma
Usiku hata mchana
Aliendelea, masikioni sumu
Kututapikia: Wewe ni bwege!
Wewe!
Si mtu!
Ni kijitu!

Ni kima!
Ni panzi!
Mnyoo!
Jongoo!
Inasemwa: *Imani huja kwa kusikia.*
*Na kusikia, na kusikia ...*
(Uk. 61)

Mhusika Nyerere anabatilisha fikra mbalimbali potofu walizopanda Wakoloni katika mbogo za raia wa mataifa ya Afrika (Data Na. 97). Hadhira inaelezwa kwamba, nao ni watu kama walivyo watu wa kigeni. Maono duni yaliyopandwa dhidi yao yalitumiwa kufifisha jitihada mbalimbali za kukabiliana na maisha hata wafanikiwe.

Mhusika Nyerere katika tamthiliya teule anawafundisha Wanamsumbiji kwamba, uhuru wanaopigania ni kwa watu wote. Si uhuru wa tabaka mahsusi pekee. Mawazo ya Wakoloni yaliyopandwa ndani ya fahamu za watu weusi kwamba, watu weusi ni watumwa na watawaliwa, anayapinga.

Emmanuel Mbogo amemkaririsha mhusika Nyerere mstari kutoka katika Biblia unaoeleza kuhusu nafasi ya fikra kwa mtu. Mstari huo unaeleza hivi;

> *"Basi, imani chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Kristo"*
>
> *Warumi 10:17.*

Mtume Paulo mwandishi wa kitabu Warumi katika Biblia alikuwa akifundisha kanisa huko Roma, Italia (Mastai, 2018). Mtume huyo aliwafundisha watu kwamba, ili waimarike kiimani basi wasichoke kufundishana habari za Mwenyezi Mungu kila uchao. Basi, mitume wakifanya waumini watawasikia na kuimarika zaidi katika dini ya Waroma. Paulo anakiri kuwa, watu ambao watakuwa wazito kuwafuata, wakisikia habari za imani mara nyingi, watageuka na kuwa wafuasi wao.

Hivyo basi, Emmanuel Mbogo anaiasa jamii yote kuendelea kupanda fikra mpya ndani ya mbongo za watu. Mbogo anaeleza kwamba Afrika nao ni watu tena wana haki ya kujitawala. Mtunzi huyu ana maono haya, Afrika wanastahiki zote alizonazo mtu mweupe, Mzungu. Jamii inajulishwa kwamba njia nzuri ya kupanda fikra chanya ndani ya mbongo za Waafrika ni kuzidisha juhudi kuhubiri jukwaani tena na tena kwamba Afrika inaweza hadi bara zima likombolewe. Hivyo basi katika tamthiliya hii mtunzi amejadili dhamira ya ukombozi wa kifikira akihusisha nukuzi, sajili na simulizi za Biblia kama tulivyobainisha.

Hali kadhalika utafiti huu umebaini dhamira ya ukombozi wa kifikra katika tamthiliya ya *Wangari Maathai* (2015). Katika tamthiliya hii mtunzi anamtumia mhusika mkuu Wangari Maathai, mwanaharakati katika jiji la Nairobi, nchini Kenya kujadili dhamira hiyo. Wangari amechorwa kama mwanaharakati wa mazingira, mtetezi wa wanyonge na mpigania demokrasia ya kweli nchini Kenya. Katika kufikia malengo yake, Wangari aliingia na kutoka nchi mbalimbali ndani na nje ya Afrika. Ndipo sasa siku moja akafanikiwa kupewa tuzo ya kimataifa ya amani 'Noble Peace Prize' mwaka 2004 (wikiwand, 2023). Kuhusu mapambano dhidi ya kulinda tabia ya nchi, mazingira, mtunzi amemsawiri namna hii;

97) WANGARI: *Dunia yote lazima ijue kuwa Kenya hatutaiharibu*
*Ardhi kamwe.*
*Ni wajibu wangu mimi na wewe,*
*Tuitunze misitu, miti tusiing'oweng'owe,*
*Mazingira tuyabembeleze.*
(Uk. 26)

Mtunzi teule katika tamthiliya hii anapanda fikra ndani ya hadhira kuhusu umuhimu wa kutunza mazingira (Data Na. 98). Jamii inaelezwa kuwa raia ndiyo wenye dhamana ya kutunza mazingira katika maeneo wanayoishi. Mhusika Wangari

anafundisha akina mama nchini Kenya kuhusu hilo. Wanawake wanampokea na kumuelewa hata wanaamua kushikamana naye kutunza mazingira. Wanawake wengi walimpokea Wangari kwa fikra alizokuwa akipanda ndani yao kuhusu mazingira. Dhamira hii imewasilishwa hivi;

98) STEFANO: *Yaah! Na yule kiongozi wao Sister wa Roman Katoliki?*
KACHERO: *Naye yupo, kajaa tele.*
*Sister Wangari Maathai anawafundisha wanawake*
*'A Gikuyu Traditional Stripease'*
ANGEL: *That is stupid joke.*
*Are you nuts? [kimya]*
*Bosi wakati wa usiku utaona maelfu ya mishumaa*
*ya nuru ya matumaini imewashwa.*
*Akina mama wanakesha wakiimba*
*Wakiomba na kumtukuza Mwenyezi Mungu*
(Uk. 40)

Emmanuel Mbogo amemchora Wangari kama mwanamke aliyefanikiwa kuamsha fikra chanya kwa wanawake wenzake (Data Na. 99). Wanawake wa Kenya wameelimishwa kuhusu utunzaji wa mazingira na mambo ya utawala bora. Ingawa Wangari amesumbuliwa sana na vyombo vya dola katika harakati hizo, hakukata tamaa hadi akafanikisha azma yake. Kwa hivyo siku ikafika Kenya ikakombolewa na mwanaharakati huyo akatangazwa mshindi duniani kwa utetezi wa mazingira. Serikali pamoja na vyombo vya dola navyo vinajitokeza kukiri ushindi kupitia elimu aliyoitoa Wangari kwa Kenya na ulimwengu kwa ujumla.

Fikra chanya za kutunza vema tabia ya nchi zinanasibishwa na simulizi moja katika Biblia. Biblia katika kitabu cha Mwanzo, imemweleza Adam kama mwanadamu wa kwanza kuumbwa ulimwenguni. Simulizi za Biblia zinaeleza kuwa mwanadamu huyo alipoumbwa na Mungu alipewa makazi bustani ya Edeni. Ndipo sasa akapewa wajibu wa kutunza makazi, bustani hiyo (Mwanzo 2: 26 – 3:24).

Kimsingi, Emmanuel Mbogo anapanda fikra chanya kwa jamii kwamba mwanamke ni chombo imara katika kuyafikia maendeleo. Fikra hasi zilizopandwa katika fahamu za watu weusi kwamba, mwanamke hawezi ni chombo duni zimebatilishwa na mtunzi huyu. Wangari amelitendea makubwa taifa la Kenya hadi likatambuliwa na kupewa tuzo za kimataifa. Mbogo amethibitisha kwamba, wanawake wanaweza wakipewa fursa sawa na wanaume katika jamii. Katika kueleza dhamira hii mtunzi ametumia sajili za Biblia 'Wanawake kukesha wakiimba na kumtukuza Mungu' na simulizi za Biblia kuhusu 'Bustani ya Edeni' na wajibu aliopewa Adam kuitunza.

Fauka ya hayo utafiti umebaini kuwa tamthiliya ya *Malkia Bibi Titi Mohamed* (2016) imebeba dhamira ya ukombozi wa kifikra. Emmanuel Mbogo katika tamthiliya hii anaifundisha jamii kwamba, mwanamke ni chombo imara na anaweza kufanya mambo makubwa hata katika ukombozi wa kisiasa katika mataifa mbalimbali. Barani Afrika hata sasa sehemu pana katika fikra za watu, fikra hasi dhidi ya mwanamke zimetamakani. Bara hili la watu weusi linamchora mwanamke kama kiumbe duni, asiyeweza kuleta jambo zuri katika jamii (Gichamba, 2005).

Mbogo anapanda fikra mpya katika jamii, kwamba wanawake wanaweza. Tena ni nyenzo imara ambayo ikipewa fursa sawa kama wanaume wanavyopewa basi inaweza kutenda mambo makubwa. Katika kuwasilisha dhamira hii, Mbogo anasema;

99) BIBITITI: ...
*Mungu ametupa wanawake mamlaka!*
*Mungu ametupa matumbo ya kutunza uhai, vifua vya kuwanyonyesha,*
*Na migongo ya kuwabeba wana . . .*
(Uk. 31)

Maelezo ya mtunzi teule kupitia Bibi Titi anafundisha jamii jinsi wanawake walivyokuwa wa thamani (Data Na. 100). Mbogo anashadidia kuwa wanawake hawapaswi kuchukuliwa kama vyombo duni kwani Mwenyezi Mungu amewakirimia talanta kubwa ya kuzaa, kulisha na kubeba watoto. Basi, nafasi waliyopewa wanawake na Mola, ni vema wakaheshimiwa na kutambulika katika nafasi mbalimbali za maendeleo ya jamii. Bibi Titi anawaalika wanawake kwa umoja na mshikamano wao, wainuke kupambania ukombozi wa taifa la Tanganyika na Afrika kwa jumla.

Fauka ya hayo dhamira ya ukombozi wa fikra dhidi ya mwanamke imejadiliwa katika Biblia. Waandishi wa kitabu hicho wanaiasa dunia kumthamini na kumheshimu mwanamke kwa nafasi yake katika jamii. Wanawake katika Biblia wameelezwa kama jeshi kubwa, ambalo likishikamana linaweza kutenda mambo makubwa katika jamii (Zaburi 68:11).

Kimsingi utafiti umebaini dhamira ya ukombozi wa kifikra kwa jamii katika tamthiliya hii. Mtunzi anapanda fikra chanya kuhusu mwanamke, kumkomboa mwanamke kutokana na mateso anayopata katika jamii dhidi ya fikra hasi zilizopandwa juu yake. Dhamira hiyo imejitokeza katika vitabu teule; *Biblia* na tamthiliya ya *Malkia Bibi Titi Mohamed*. Dhamira inayowasilishwa na Mbogo kwa jamii, fikra chanya kuhusu mwanamke vilevile imeelezwa kwenye Biblia. Mfalme Daudi katika kitabu cha Zaburi katika Biblia amekiri mwanamke ni jeshi kubwa. Jeshi hilo likitaka kufanya lolote linaweza. Fani za Biblia zilizotumiwa na mtunzi katika tamthiliya hii zimekuwa daraja zuri la kuwasilisha dhamira hii.

Hali kadhalika Emmanuel Mbogo katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya* (2016) amewasilisha dhamira ya ukombozi wa fikra akihusisha fani za Biblia. Mbogo anafundisha jamii kwamba, maono, fikra zina nafasi kubwa katika mafanikio ya mwanadamu na taifa kwa jumla.

Fauka ya hayo mtunzi huyo anahubiri kwamba, jinsi mtu alivyo sasa ni tokeo la fikra alizokuwa nazo awali. Mhusika Tom katika tamthiliya hii anakiri kuwa, ndani yake ana maono ya kuikomboa nchi yake. Jitihada zote anazofanya ili kuikomboa nchi ya Kenya ni zao la maono yaliyoujaza mtima wake. Mbogo anafundisha jamii kuwa na fikra tunduizi kama alizokuwa nazo Tom Mboya nchini Kenya. Katika tamthiliya hii kuhusu fikra na maono mtunzi ameandika hivi;

100) WAIRIMU: *Tom, I admire your guts.*
*We ni muota ndoto kama Yusufu mwana wa Yakobo***.**
MBOYA: Hiyo ni ndoto yangu. Ni mimba iliyo ndani ya Ubongo wangu...
(Uk. 49)

Tom Mboya anakiri mbele ya Wairimu kuwa mapambano anayofanya kufa na kupona kuipigania nchi ya Kenya ni ndoto ya maisha yake tangu kale (Data Na. 101). Mhusika huyo aliazimia kuipambania Kenya kutoka kwa viongozi wazawa, akina Jomo Kenyatta waliokuwa wanaongoza nchi vibaya. Hali hiyo ilipelekea vita baina yake na tabaka tawala. Mboya akiendelea na mapambano, ndipo sasa siku moja akiwa njiani kutoka duka la dawa wakati wa jioni akapigwa risasi na watu wasiojulikana akafariki. Nyota yake ikazimika na Kenya kubaki gizani hata sasa.

Dhamira kuhusu ukombozi wa fikra, ama nafasi ya fikra, maono katika kufikia malengo maishani imesemwa pia katika kitabu cha Biblia. Kijana mmoja kutoka

familia ya Mzee Yakobo ainayeitwa Yusufu alipitia changamoto nyingi katika maisha hapo kwanza kabla ya kufanikiwa. Pamoja na hayo kutokana na maono, ndoto alizokuwa nazo siku moja akafanikiwa na kuwa mtu mkuu katika taifa la Israel. Simulizi za kijana huyo, Yusufu zinapatikana katika kitabu cha Mwanzo (37 – 50).

Kwa hivyo dhamira ya ukombozi wa fikra katika kazi teule; *Nyota ya Tom Mboya* imewasilishwa kwa kupitia simulizi za *Biblia* (Simulizi za muota ndoto Yusuf Yakobo). Fani iliyotumika kuwasilisha dhamira hii ni daraja imara la kuwasaidia hadhira kupokea dhamira inayowasilishwa. Waandishi teule wa *Biblia* na tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya* wameshikana mkono kuhubiri nafasi ya maono, ndoto katika mtu, taifa kufikia mafanikio katika yote wanayonia. Mtu akiwaza vema, taifa likiwaza vema litatimiza mipango yake.

Hali kadhalika dhamira ya ukombozi wa kifikra imejadiliwa na mtunzi wetu teule, Emmanuel Mbogo katika tamthiliya ya *Tanzia ya Patrice Lumumba* (2015). Fani mbalimbali za Biblia zimetumika katika tamthiliya teule kuwasilisha dhamira hii. Fani hizo zikihusishwa na yanayoelezwa katika kazi teule, hadhira inaweza kuwa katika nafasi bora zaidi ya kuelewa maana ya matini kutokana na dira ya usomaji kwa miwani ya mwingilianomatini.

Mtunzi teule katika bunilizi hii anapingana na fikra hasi kuhusu mwanamke katika jamii. Mbogo anapanda fikra chanya katika jamii kwamba, mwanamke ni chombo imara. Vilevile mwanamke anaweza kuifungua jamii dhidi ya pingu zote zilizoifunga. Mhusika Pauline ndiye aliyetumiwa na Emmanuel Mbogo kueleza

dhamira hiyo katika drama teule. Mbogo anafundisha kuwa, fikra duni zilizotapakaa katika jamii kuwa wanawake hawawezi zipingwe vikali katika zama tulizomo. Jamii inaelezwa kuwa kushindwa kwa mwanamke mmoja (kama yupo) katika jamii hakupaswi kutumika kama dira ya kuwahukumu wanawake wote katika jamii tulizomo. Dhamira hiyo imewasilishwa hivi;

101) PAULINE: *[Anaongea na Sanamu la Bikira Maria] ...*
*Ninaomba roho saba za ujasiri wa Simba wa Yuda...*
*Ninaomba roho saba za ujasiri wa Malkia Esther ziingie ndani ya maji haya ya baraka!*
*Naomba roho saba za mabinti wa Zelophehad...*
*Naomba roho saba za mamlaka ya Debora...*
*Ushujaa na werevu wa Yokebedi na Miriam*
(Uk. 43)

Mhusika Pauline katika mazungumzo ameinuka kujipa moyo mkuu ili kuanza mapambano ya kufa na kupona hadi amuokoe mume wake, Patrice na taifa lote la Kongo. Wahusika wote anaorejea mtunzi teule ni wanawake walioandikwa kwenye Biblia (Data Na. 102). Wanawake hao walitumika kufanya mambo makubwa kuhusu ukombozi wa jamii zao katika vitabu mbalimbali ndani ya Biblia. Mambo hayo walifanya wahusika waliorejewa kutoka kwenye Biblia yamebainishwa ndani ya utafiti huu (Jedwali Na. 4. 4).

Kimsingi, Emmanuel Mbogo katika tamthiliya hii anaeleza kuwa wanawake wanaweza kufanya mambo makubwa katika jamii. Hivyo waaminiwe na kupewa fursa ya kushiriki shughuli mbalimbali za maendeleo. Fikra za kuwadunisha wanawake zisipewe nafasi sasa katika mimbari mbalimbali ndani ya jamii. Afrika ili ikombolewe inapaswa kuhusisha wanawake katika jitihada mbalimbali kama Kongo walivyofanya kumtumia Pauline, mke wa Patrice Lumumba. Nchini Tanzania miaka ya karibuni 2020, wamefanikiwa kuwa dira nzuri katika kumuamini mwanamke na

kumuachia kiti cha uongozi mkuu wa nchi. Sasa nchi hii inatawaliwa na mwanamke, Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mhimili wa Nadharia ya Mwingilianomatini katika kubaini maana ya matini unaeleza hivi, ili hadhira ielewe dhamira zilizokusudiwa katika matini lengwa, uhusisha vipengele vingine kutoka nje ya kazi za fasihi (Kristeva, 1969). Msomaji wakati akiisoma matini, uhusisha vipengele vingine kutoka nje ya matini. Mchakato huo humsaidia hadhira kubaini maana iliyokusudiwa katika matini lengwa.

Fani mbalimbali za Biblia zilizotumika katika bunilizi teule alizoandika Emmanuel Mbogo zimetumika kuwasilisha dhamira ya ukombozi wa fikra katika nyanya mbalimbali. Fani hizo zikihusishwa wakati wa usomaji wa tamthiliya teule zinadhihirisha dhamira hii. Fani zilizotumika kuwasilisha dhamira hii ni nukuzi za Biblia, wahusika wa Biblia, simulizi za Biblia na sajili za Biblia. Fani hizo zilitumika kuwasilisha dhamira ya ukombozi wa kifikra katika Biblia hapo kwanza.

Pamoja na hayo Nadharia ya Mwingilianomatini inaendelea kutanabaisha kuwa, matini yoyote huchagizwa na matini nyingine tangulizi. Wakati wa usomaji hadhira uhusisha matini iliyo mbele yao na matini nyingine zilizopita ndipo ing’amue anachosema mtunzi. Jinsi Mbogo anavyowasilisha dhamira hii ya ukombozi wa fikra ananasibiana na dhamira hiyo ilivyowasilishwa katika Biblia. Washadidi wa Nadharia ya Mwingilianomatini wanaeleza kuwa, kazi za fasihi huathiriana kifani na kimaudhui. Biblia katika dhamira hii ya ukombozi wa fikra anayozungumza Emmanuel Mbogo imemwathiri mtunzi kama tulivyobainisha.

Emmanuel Mbogo anapendekeza mbinu ya kupanda fikra mpya na chanya katika mbogo za watu weusi, Afrika. Kwamba, wanaharakati wafundishe tena na tena kwenye majukwaa kwamba, Afrika nao wanaweza kujitawala na kujiletea maendeleo wenyewe. Wakirudia kufundisha hivyo kila uchao, iko siku jamii itawapokea na kuwaelewa.

Mbinu anayotumia Mbogo katika kufundisha fikra mpya na chanya kwa kurudia kila uchao kuwaeleza hadhira jambo moja kila siku ilishatumiwa na mtume Paulo katika Biblia akiliongoza kanisa la Roma. Mtume huyo alitaka watu wafundishane kwa bidii mambo ya imani. Akishadidia kuwa mtu akisikia jambo mara dufu, huishia kuamini.

Kazi teule; tamthiliya na Biblia kuhusu dhamira ya ukombozi wa fikra zimeathiriana kifani. Wasomaji wakihusisha matini hizi kama tunavyoelezwa na Nadharia ya Mwingilianomatini, wanang'amua njia zinazofaa katika kupanda fikra mpya na umuhimu wake katika kufanikisha maono ya mtu katika maisha.

Kwa jumla utafiti huu umebaini dhamira hii ya ukombozi wa kifikra katika tamthiliya teule zote sita kama tulivyobainisha. Ukombozi huo umezungumza kuhusu nafasi ya maono katika kufanikiwa kwenye maisha, nafasi ya mwanamke katika jamii zama hizi tulizomo, njia nzuri za kupanda fikra mpya chanya katika jamii n.k. Emmanuel Mbogo ametumia fani mbalimbali za Biblia katika kujadili dhamira hii. Fani hizo ni ngazi nzuri kwa hadhira kung'amua dhamira inayowasilishwa endapo zitahusishwa wakati wa usomaji kama mhimili wa Nadharia ya Mwingilianomatini unavyoeleza. Fani za Biblia zilizojitokeza zinadhihirisha dhamira hii kama tulivyowasilisha.

### 4. 3. 13 Kutunza Historia ya Jamii

Mlaga (2015) anaeleza kwamba historia na fasihi zina uhusiano. Andiko la mwanazuoni linashikilia kuwa fasihi kupitia tanzu zake, huakisi matukio mbalimbali yaliyowahi kujitokeza katika jamii. Kwa hivyo kumbo kuu za fasihi; fasihi simulizi na fasihi andishi husawiri matukio yanayojili katika jamii. Tamthiliya ya Kiswahili ni miongoni mwa tanzu za fasihi andishi inayotumika kuwasilisha matukio ya kihistoria katika jamii ya Waswahili. Ndipo sasa watu wakizisoma tamthiliya hizo wanaweza kubaini historia za jamii mahsusi zinazorejewa na wabunifu ndani yake.

Kimsingi, Mlaga (Ktj) ametuwezesha kung'amua kwamba historia za jamii hudhihirika katika kazi za fasihi ya Kiswahili. Utanzu wa tamthiliya unaelezwa kama moja ya tanzu mashuhuri ya fasihi andishi ya Kiswahili inayotumika kuwasilisha dhamira hii zaidi. Kazi teule katika utafiti huu zilitoka kwenye utanzu wa tamthiliya ya Kiswahili. Hivyo basi tulikuwa sehemu sawia katika kuchunguza dhamira hii inavyojitokeza katika tamthiliya hizo teule.

Kutunza historia ya jamii ni dhamira iliyojitokeza katika tamthiliya ya Kiswahili (Mlelwa, 2021). Dhamira hii huonekana vema namna inavyojitokeza wasomaji wakitumia nadharia ya uhalisia na nadharia ya falsafa ya historia (Mlaga, 2015). Wanazuoni hawa wanaeleza kuwa pamoja na kwamba fasihi ni tawi la sanaa lakini huakisi hali mbalimbali zinazojitokeza katika jamii katika nyanja zote za maisha; uchumi, siasa, utamaduni n.k.

Matokeo ya utafiti huu yamebaini kuwa, katika bunilizi teule tulizotafiti mtunzi ametumia fani za Biblia kuwasilisha dhamira ya kihistoria. Historia iliyochorwa

katika tamthiliya teule imejumuisha historia ya nchi ya Tanzania, nchi za Afrika Mashariki na Afrika kwa jumla katika jitihada za ukombozi wa mataifa yao. Lengo mahsusi la tatu katika utafiti huu lililenga kubainisha dhamira zinazodhihirika katika fani za Biblia zilizojitokeza ndani ya tamthiliya teule. Ndipo sasa tukachunguza dhamira ya kihistoria tukihusisha fani za Biblia zilizotumiwa kuiwasilisha.

Sehemu inayofuata hapa chini mtafiti amechambua dhamira ya kihistoria katika matini teule. Matokeo ya utafiti yamebaini kuwa dhamira hii imedhihirika katika tamthiliya teule zote katika utafiti huu. Fani za Biblia kutoka matini teule zimetumika kuwasilisha dhamira hiyo. Historia za nchi hizi; Tanganyika, Zanzibar, Kenya, Msumbiji, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Afrika Kusini imeelezwa kwa mitindo mbalimbali. Hadhira lengwa wakikutana na fani za Biblia zilizojitokeza katika tamthiliya teule, wanabaini dhahiri shayiri pasina kiza chochote historia za ukombozi wa nchi mbalimbali zilizojumuishwa kwenye bunilizi teule.

Emmanuel Mbogo ameandika historia ya nwanaharakati mmoja nchini Kenya baada ya uhuru, Profesa Wangari Maathai katika tamthiliya ya *Wangari Maathai* (2015). Tamthiliya hii inawajulisha wasomaji mchango mkubwa alioutoa mwanaharakati huyo katika kupigania mazingira, amani, demokrasia na utawala bora nchini Kenya. Kadhia mbalimbali alizopitia mwanaharakati huyo katika shughuli zake zimebainishwa katika tamthiliya hii.

Kwa jumla harakati za mwanamama huyo zilisikika sehemu kubwa ya ulimwengu hadi akafanikiwa kutunukiwa tuzo ya amani ya kimataifa ‘Noble Peace Award 2004’. Tukio hilo liliipa heshima kubwa nchi ya Kenya hata ikafanya sherehe ya

kitaifa kumpongeza Wangari kwa mchango wake mkubwa alioufanya kuitangaza kwa wema nchi nzuri ya Kenya. Mtunzi teule anaandika hivi;

102) RAILA: *[anasimama] Wananchi, Profesa Wangari Muita Maathai ametuvika Joho la Utukufu sisi Wakenya wote. Profesa ametuvua taji ya miiba; ...*
(Uk. 50)

Maneno ya Raila, Rais wa nchi ya Kenya akihutubia wananchi siku ya pongezi kwa Wangari Maathai yanadhihirisha wema aliotenda mpambanaji Wangari (Data Na. 103). Mtawala wa taifa hilo anaweka bayana kwamba tuzo aliyopewa mwanaharakati Wangari imeipa heshima kubwa taifa la Kenya. Tamthiliya hii imejulisha watu tukio lililotokea huko nyuma katika taifa la Kenya.

Pamoja na hayo mazungumzo ya Rais wa Kenya, Raila katika tamthiliya hii yamebeba sajili za Biblia ndani yake. Sitiari alizotumia kiongozi huyo ni taifa la Kenya 'kuvikwa Joho la utukufu' na 'kuvua taji ya miiba' (Data Na. 103). Biblia imetumia sitiari hizo inapozungumza harakati za ukombozi wa taifa la Israel zilizokuwa zikifanywa na Mtume wa Wayahudi, Yesu Kristo. Mwanaharakati huyo aliteswa kwa 'kupigiliwa misumari' na 'kuvikwa taji ya miiba kichwani' (Yohana 19:2, 5; Marko 15:17 na Mathayo 27:29).

Watheolojia wanaeleza 'Taji ya Miiba' na 'Joho la Utukufu' kama dhana zenye taswira mahsusi. Taji ya miiba katika theolojia huelezwa kama taswira ya uduni, mateso, dhiki alizopitia Yesu Kristo akiwa kwenye mateso (Hananja, 2007). Ndipo sasa kutokana na taswira hiyo, tunang'amua kuwa, nchi ya Kenya ilikuwa katika hali duni kabla Wangari hajatunukiwa tuzo hiyo. Raia wa Kenya, Wangari kupewa tuzo

hiyo kuliifutilia mbali taswira ya uduni, uovyo wa utawala wa kidemokrasia iliyokuwa imetamakani katika fikra za Walimwengu dhidi ya taifa la Kenya.

Kimsingi, tamthiliya ya *Wangari Maathari* inaeleza historia halisi ya taifa la Kenya na matukio yaliyomsibu Wangari Maathai katika jitihadi zake za kupigania tabia ya nchi, demokrasia na maadili kwa viongozi katika taifa la Kenya. Sajili za Biblia na simulizi za Biblia zilizohusishwa katika ujenzi wa tamthiliya hii zimewasilisha vema dhamira hii. Mbogo amefanikiwa kutunza historia ya Kenya na mwanaharakati Wangari Maathai kwa yote yaliyomsibu zama za uhai wake alipokuwa akipambana dhidi ya mazingira, amani, demokrasia na maadili mema ya viongozi wa umma kwa jumla.

Hali kadhalika mtafiti amebaini dhamira ya utunzaji wa historia katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya* (2016). Kazi hii teule ni drama ya kihistoria. Emmanuel Mbogo ameandika kuhusu maisha ya Bw. Tom Mboya, mwanaharakati mahiri aliyelenga kuleta maendeleo dhahiri katika taifa la Kenya miaka ya 1960. Mwanaharakati Mboya alipokuwa katika jitihada hizo, alikumbana na mikinzano mbalimbali kutoka serikali ya Kikoloni, chini ya Waingereza.

Mtunzi wa drama hii, Mbogo (2016) katika sehemu ya utangulizi anaeleza kwamba aliandika tamthiliya hiyo ili kutunza historia ya huyu ndugu mahiri katika historia ya ukombozi wa Afrika. Tom Mboya alitaka kuisadia nchi ya Kenya na Afrika yote kupata ukombozi dhahiri wa kisiasa. Pamoja na hayo Mboya alitoweka ghafla kabla ya ndoto yake kutimia. Kupitia tamthiliya hii hadhira wanaweza kubaini yaliyomsibu Tom Mboya na harakati alizofanya enzi za uhai wake huko nchini Kenya, kabla ya Kenya kupata uhuru 1963 na miaka sita mbele akauawa, 1969.

Vilevile mhusika mkuu katika tamthiliya hii tuliyochunguza ni halisi. Tom Mboya alikuwa akiishi nchini Kenya, kabla ya kuuawa ghafla tarehe 5 Julai 1969. Tom Mboya aliuawa kwa kupigwa risasi na mshukiwa mmoja anayejulikana kama Nahashon Njoroge (Ojiambo, 2019). Matokeo ya utafiti huu yamebaini kwamba, Emmanuel Mbogo ameandika tamthiliya hii kutunza historia ya mwanaharakati huyo mashuhuri katika uga wa siasa kutoka nchini Kenya.

Aidha fani ya Biblia iliyotumika kuwasilisha dhamira hii ya kihistoria katika tamthiliya teule ni 'simulizi ya Biblia' kuhusu mtume Yesu Kristo tangia kuzaliwa hadi mauti yake na kusudi la kuzaliwa kwake. Vilevile mtunzi teule ameeleza historia ya Tom Mboya tangu kuzaliwa hadi kifo chake. Tom Mboya anapozaliwa, mtunzi ameweka angani nyota yenye mng'aro mkali kama ishara ya kuzaliwa kwake. Nyota hiyo inawashtua hata wazazi wake wakiwa kwenye mazungumzo. Kuzaliwa kwa Mboya kumeelezwa hivi;

103) NDIEGE: *[Anakunywa ... kilio cha utungu ndani ...]*
*(Ghafla kunasikika radi; wote wawili wanashtuka; na papo kwa papo, wakiwa wanaangalia angani inatokea Nyota yenye mng'aro wa ajabu.)*
(Uk. 7)

*'Nyota yenye mng'aro wa ajabu'* imeonekana angani anapozaliwa Tom Mboya (Data Na. 104). Hali kadhalika anapozaliwa Mtume Yesu Kristo katika jamii ya Wayahudi wananajulishwa na wataalam wa anga, Mama Jusi kwamba '*Nyota yenye mng'aro mkali'* imetokea angani. Simulizi hizi zinashabihiana. Hivyo zinaweza kukamilishana kimaana kama Nadharia ya Mwingilianomatini inavyoelekeza.

Vilevile historia kuhusu mauti ya Tom Mboya imebainishwa katika tamthiliya hiyo teule. Mwanaharakati Tom Mboya alikutana na kifo akiwa katika jitihada za ukombozi wa kisiasa wa taifa la Kenya. Mtunzi teule ameeleza hivi;

104) PAMELA: *We Suzi! {anaharakisha kumfuata Suzi}*
*Suzi!*
*(Wakati huo huo Pamela anapishana na Chatu. Kisha Chatu anapishana na Mboya. Hatua mbili au tatu, kwa kasi, Chatu anageuka. Anaita, "Tom!" Mboya anageuka. Chatu anampiga Mboya risasi mbili ... Anatoweka ...*
(Uk. 30)

Tom Mboya ameuawa kwa kupiga risasi na Chatu (Data Na. 105). Mauti hii imemkuta mhusika huyo akiwa katika harakati za ukombozi wa taifa la Kenya. Pamoja na hayo mauti ilimkuta Yesu kwa Wayahudi akipambana kuleta ukombozi, nyota yake ikazimika ghafla (Marko 15:33 – 47).

Kimsingi, matokeo ya utafiti huu yamebaini kwamba simulizi ya Yesu Kristo imetumika kama ngazi njema ya kubuni tamthiliya hii ya kihistoria. Simulizi ya mhusika huyo kutoka kwenye Biblia imeelezwa tangu kuzaliwa kwake hadi kifo chake. Mtunzi ametumia simulizi hiyo kuhifadhi historia ya Tom Mboya huko Kenya. Simulizi baina ya wahusika hawa; Yesu Kristo na Tom Mboya zinahusiana. Hadhira ikihusisha simulizi ya maisha ya Yesu Kristo na tamthiliya ya *Tom Mboya*, anaitambua historia msingi ya mwanasiasa huyo maarufu aliyepata kutokea nchini Kenya.

Hadhira mahsusi ya tamthiliya hii teule inaelezwa kwamba, Tom Mboya alijitoa kupigania nchi yake, lakini akaishia mauti. Nyota yake iliyochanua ghafla alipozaliwa, ilizimika bila kutarajia baada ya kuuawa na watu punde alipotoka duka la dawa kupata mahitaji kama tulivyobainisha katika wasifu wake.

Kupigwa risasi kwa mwanasiasa huyo, mkombozi wa nchi ya Kenya kunanasibishwa na kuuawa kwa Yesu Kristo, anayeelezwa kama mkombozi wa wanadamu huko Uyahudi katika Biblia. Mboya alikuja kwa ajili ya kuwakomboa Wakenya, lakini wakaishia kumuua. Yesu Kristo anaelezwa kuwajia wanadamu huko Uyahudi lakini watu aliowajia wakamuua.

Basi, 'Chatu' anayemuua Tom Mboya ananasibishwa na mhusika Nyoka (Data Na. 105). Biblia inamnasibisha mnyama Nyoka na Ibilisi Shetani (Mwanzo 3:1). Watheolojia wanaamini kuwa Nyoka huyo ndiye aliyeratibu mateso ya Yesu hadi kifo huko Uyahudi, kisha akatoweka alipokamilisha kazi yake.

Vilevile mtafiti alibaini dhamira ya kihistoria katika tamthiliya nyingine teule, tamthiliya ya *Malkia Bibi Titi Mohamed* (2016). Matokeo ya utafiti yalibaini kuwa tamthiliya hiyo iko katika mkondo wa kihistoria. Mtunzi teule katika kazi hii ameeleza maisha ya Bibi Titi Mohamed, aliyekuwa mwanaharakati katika kupigania uhuru wa Tanganyika na Afrika Mashariki miaka ya 1960. Bibi Titi, mhusika mkuu katika tamthiliya hii alikirimiwa kipaji cha uimbaji na Mwenyezi Mungu. Kupitia uimbaji aliweza kuwashawishi wanawake wengi Afrika kuinuka ili kupigania uhuru wa nchi zao, Tanganyika ikiwemo.

Kimsingi, mtu akiisoma tamthiliya hii anabaini historia ya Tanganyika katika harakati zake za kupigania uhuru kutoka kwa Wakoloni wa Kiingereza. Pamoja na hayo mtunzi amerejea harakati mbalimbali za ukombozi Afrika miaka ya 1960 katika mataifa mbalimbali ya Afrika.

Matokeo ya utafiti huu yamebaini kuwa dhamira ya kihistoria inadhihirika katika fani za Biblia alizotumia mtunzi katika tamthiliya ya *Malkia Bibi Titi Mohamed* (2016). Fani hizo zimekuwa na mchango kwa hadhira kuing'amua dhamira hii barabara kama Nadharia ya Mwingilianomatini inavyoelekeza.

Mhimili mojawapo wa Nadharia ya Mwingilianomatini unaelekeza kuwa, ili hadhira ibaini maana ya matini inapaswa kuhusisha vipengele vingine nje ya matini inayosomwa kiganjani (Kristeva, 1980). Ndipo sasa hadhira akiisoma tamthiliya hii huku akihusisha fani za Biblia zinazorejewa humu anaweza kubaini dhamira hii ya kihistoria barabara.

Mtunzi teule akitumia fani za Biblia amewasilisha dhamira ya kihistoria kwa namna mbalimbali. Dhamira hii imewasilishwa namna hii;

105) BIBITITI: Tunadai uhuru wetu kwa njia ya amani …
Babu zetu mashujaa, akina Kinjeketile, walidai uhuru kwa vita vya Majimaji.
Babu zetu mashujaa, akina Mkwava, walidai uhuru kwa njia ya vita.
*Nasi leo tunaitukuza na kuikumbuka damu yao iliyomwagika ili Mwafrika awe huru...*
(Uk. 38)

Maelezo ya mhusika Bibi Titi yanawasilisha dhamira ya historia ya Tanganyika katika harakati za ukombozi dhidi ya ukoloni (Data Na. 106). Historia inayoelezwa hapo ni halisi. Machifu wa mwanzo nchini Tanganyika waliorejewa waliojitoa kupambana na Wakoloni kwa njia ya vita; Kinjeketile na Mkwava ni dhahiri katika taifa hilo. Machifu hao waliwahi kuishi nchini Tanganyika (Sasa Tanzania) kabla Tanzania haijapata uhuru.

Pamoja na hayo tamthiliya hii imeeleza mchango wa wanawake katika kupigania uhuru wa nchi. Kwamba, zoezi la kupigania uhuru wa nchi ya Tanganyika lilijumuisha watu wa jinsi zote katika jamii. Hakuna kundi lililobaki nyuma. Bibi Titi aliwakilisha wanawake hao.

Vilevile mhusika mkuu, Malkia Bibi Titi amenasibishwa na mhusika mmoja kutoka kwenye Biblia; Malkia Esta (Esta 1 – 7). Mhusika Esta amechorwa kama mwanamke aliyesimama kidete kupigania uhuru wa taifa la Israel, Wayahudi hata wakaokolewa na adhabu ya kifo. Biblia inaeleza kuwa utumwani, ikatolewa amri wote wauawe lakini mke wa Mfalme, Malkia Esta myahudi mwenzao akawapigania hata amri ya Wahayudi wote kuuawa ikabatilishwa.

Kwa jumla Wahenga wa Kiswahili wanaeleza kwamba, ‘Umoja ni nguvu, Utengano ni udhaifu’. Tamthiliya hii inamchora Bibi Titi akishikamana na wanawake wenzake, wameungana pamoja na wanaume akina Mwalimu Nyerere kupigania uhuru wa nchi. Simulizi ya Malkia Bibi Titi (katika tamthiliya teule) na Malkia Esta (kutoka kwenye Biblia) zinashabihiana. Watunzi wanaeleza jinsi wanawake katika jamii hizi zote walivyoshikamana kukomboa jamii zao. Bibi Titi ameshiriki kukomboa nchi yake ya Tanganyika. Esta ameshiriki kukomboa nchi yake ya Israel. Kazi hizi za fasihi zimefanikiwa kueleza nafasi ya mwanamke katika ukombozi wa mataifa. Hadhira inajifunza historia ya harakati wa ukombozi wa Tanganyika (Tanzania) zilivyoenda hata siku moja 9 Disemba 1961, Tanzania ikapata uhuru.

Hali kadhalika katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora* (2016), dhamira ya utunzaji wa historia kupitia sajili za Biblia imeelezwa. Kupitia uga wa mwingilianomatini utafiti umebaini kuwa tamthiliya hii ni zao halisi la historia ya

Msumbiji. Mosi, ilianza historia ya Msumbiji katika harakati zake za ukombozi kutoka kwa Wakoloni. Pili, ikaandikwa tamthiliya ya *Mondlane na Samora* (2016). Ndipo sasa tunaeleza kwamba, Historia ya Msumbiji ndiyo malighafi ya kuumba tamthiliya teule tuliyotafiti.

Tamthiliya hii inahusu historia ya ukombozi wa nchi ya Msumbiji, uliopatikana kwa mtutu wa bunduki mwaka 1975. Viongozi wa mwanzo wa taifa hilo, Edwardo Mondlane na Samora Machel walipambana hadi nchi yao ikakombolewa. Hata hivyo maisha ya wanaharakati hawa yalipotea kwa vifo vya ajabu. Mwaka 1968 Mondlane alilipuliwa kwa Bomu Dar es Salaam, nchini Tanzania. Samora Machel akafa kwa ajali ya ndege mwaka 1986 (Mbogo, 2016).

Mtunzi wa tamthiliya hii ameonyesha jitihada mbalimbali walizozifanya viongozi wa mwanzo nchini Msumbiji ili kulikomboa taifa hilo kutoka ukoloni wa Kireno uliodumu nchini humo zaidi ya miaka mia nne. Pamoja nao mtunzi amehusisha viongozi wengine wa Afrika katika ukombozi wa taifa hilo. Miongoni mwa viongozi wa Afrika wanaotajwa kushiriki katika ukombozi wa taifa la Msumbiji ni Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kutoka nchini Tanzania. Basi tamthiliya hii imesheheni historia ya ukombozi wa Msumbiji. Hadhira wakiisoma watabaini mengi kuhusu ukombozi wa nchi hiyo.

Mtunzi teule anapoeleza dhamira ya historia ya ukombozi wa Msumbiji amehusisha fani ya Biblia. Fani ya Biblia inayodhihirisha dhamira hii ni simulizi ya Biblia kuhusu taifa la Israel kukaa utumwani, Misri kwa miaka 430 kabla ya kupata uhuru kurejea kwao Kanaani (Sasa Israel). Taifa la Israel lilikaa Misri kama watumwa, likatawaliwa katika nyanja zote za maisha (Kutoka 12:40).

Kwa jumla, historia za ukombozi wa mataifa mawili; Israel na Msumbiji kutoka kwenye Biblia na tamthiliya teule mtawalia, zinahusiana. Hadhira iliyowahi kukutana na simulizi kuhusu taifa la Israel kukaa utumwani zaidi ya miaka 400 huko Misri, inaweza kuelewa dhahiri historia ya taifa la Msumbiji kutawaliwa miaka 430 na Wareno. Simulizi hiyo ikuhusishwa inadhihirisha dhamira ya historia ya ukombozi wa Msumbiji kwa namna rahisi kwenye Medula Oblangata za wasomaji waliowahi kukutana na simulizi ya Israel kutawaliwa miaka 400 huko Misri.

Harakati za ukombozi wa taifa la Israel kutoka utumwani Misri kurejea nchini kwao Israel, ilihusisha ushirika wa viongozi wawili mashuhuri; Nabii Musa na Haruni. Manabii hao ndiyo walioanzisha harakati za ukombozi wa Israel Misri, kwa muongozo wa Mwenyezi Mungu. Changamoto mbalimbali ziliwakabili wakiwa katika safari ya kurejea kwao Israel. Simulizi zinaandika walifia njiani. Ndipo sasa Nabii Yoshua akainuliwa ili kuikamilisha safari ya ukombozi wa taifa la Israel baada ya watangulizi wake kutoweka.

Vilevile safari ya ukombozi wa taifa la Msumbiji iliongozwa na wanaharakati wawili; Mondlane na Samora. Mondlane alianzisha safari ya ukombozi wa taifa hilo, kisha Samora akampokea na kuliongoza taifa kwa muda wa miaka 11 kabla ya kulipuliwa kwa ndege, akafa.

Simulizi ya Biblia na mtindo wa ukombozi unaotumika katika hizi matini teule; *Biblia* na tamthiliya ya *Mondlane na Samora* zinahusiana. Hadhira wanaelezwa kuwa safari ya ukombozi wa taifa la Msumbiji haukuwa jambo jepesi. Hilo lilichagizwa na taifa la Ureno kutawala nchi hiyo zaidi ya karne nne. Hivyo Wareno

walikuwa na mizizi mirefu nchini humo. Ndipo sasa wanaharakati wa kuikomboa Msumbiji wakakabiliwa na ukuta mkubwa hata Msumbiji ilipopata uhuru mwaka 1975. Muhula wa Ureno kutawala Msumbiji kitambo umewasilishwa hivi;

106) BBC 2: *Usisahau BBC 1 kwamba:*
*Wareno wameitawala Msumbiji kwa takribani*
*miaka 400...*
(Uk. 95)

Wareno kutawala Msumbiji miaka mianne ni historia dhahiri ingawa imeelezwa katika kazi hii ya fasihi ya Kiswahili (Data Na. 107). Simulizi hiyo inaendana na taifa la Misri kutawala Israel miaka mia nne kabla ya kujikomboa. Hivyo basi katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora* mtunzi ametumia simulizi ya ukombozi wa Israel kutoka utumwani Misri kueleza ya historia wa taifa la Msumbiji. Fani hiyo imetumiwa kudhihirisha harakati zote zilizotukia nchi ya Msumbiji hata taifa hilo likapata uhuru. Ukombozi wa taifa hilo ulitokana na jitihada za viongozi wa awali wawili; Mondlane na Samora. Ndipo sasa tunaweza kuhitimisha kwamba, Mondlane na Samora walikuwa Musa na Yoshua wa taifa la Israel katika nchi ya Msumbiji.

Pamoja na hayo Emmanuel Mbogo anaendelea kuwasilisha dhamira ya historia katika drama ya *Mtumwa hadi Siti Binti Saad* (2016). Utafiti huu umebaini kuwa tamthiliya hii ni kazi ya kihistoria kwani inasawiri maisha ya Siti Binti Saad. Mwanamama huyo alikuwa mwimbaji mashuhuri wa taarab kutoka Visiwani Zanzibar. Mhusika Siti amechorwa kutoka katika familia duni, utumwani.

Historia inaeleza kuwa Siti Binti Saad alifanikiwa kimaisha kupitia muziki hadi kufika daraja la juu hata akapata fursa ya kuketi na wakuu wa nchi. Jamii ya Wazanzibar hawakutaraji kumuona Siti katika daraja hilo. Kupitia mwimbaji huyo

jamii ilibaini kwamba, katika maisha mtu yeyote anaweza kufanikiwa katika maisha hata kama ametoka familia duni. Tamthiliya inadhihirisha hilo kama hivi;

107) BONGA: *Ama kweli, Mwenyezi Mungu anaweza kumtoa mtu kwenye matope na kumwinua juu katika utukufu na enzi.* (Uk. 79)

Nukuu iliyorejewa na mtunzi kupitia mhusika Bonga ni zao la Biblia (Data Na. 108). Nukuu hiyo hutumika kueleza jamii kwamba, mafanikio yanaweza kumpata mtu kutoka tabaka lolote. Vilevile Emmanuel Mbogo ametumia simulizi ya kijana mmoja kutoka kwenye Biblia, Yusufu bin Yakobo kuumba mhusika Siti Binti Saad.

Biblia inamweleza kijana huyo kama mtoto wa mwisho katika familia ya Mzee Yakobo Isaka huko Uyahudi. Simulizi za Kiyahudi kutoka katika Biblia zinaeleza kuwa, Yusufu alipendwa mno na Baba yake kuliko kaka zake. Kijana huyo anaelezwa kuwa na maono pamoja na nidhamu binafsi, ndiyo maana Baba akampenda kuliko watoto wake wengine. Hali hiyo ilipelekea ndugu zake kumwonea wivu, wakamchukia mno. Walilenga mabaya mengi dhidi yake. Siku moja wakamuuza ndugu yao kama mtumwa kwa wafanyabiashara wa Midiani. Wafanyabishara hao walimchukua hata nchi ya Misri, wakamuuza huko.

Aidha Bw. Yusuf akiwa utumwani Misri masaibu mbalimbali yalimsibu, akaishia kufungwa gerezani. Mfalme wa Misri alipoota ndoto moja, akatafuta wafumbuzi wote nchini mwake wakakosekana. Ndipo sasa mfungwa wa Kiyahudi kutoka gerezani, Yusuf mwana wa Yakobo akaitwa na kutafsiri ndoto ya Farao. Jambo hilo lilikuwa ngazi ya Yusuf kupandishwa daraja la maisha. Kijana huyo alitoka gerezani kama mfungwa akaishia kupangiwa jukumu la Uwaziri mkuu katika nchi ya Ugeni, Misri (Mwanzo 30:22 – 50:26).

Historia ya Yusufu imetumiwa na mtunzi teule kutunza historia ya Siti binti Saad. Mhusika huyo amechorwa kutoka utumwani hadi kuwa Malkia wa Taarabu, Upwa wa Afrika Mashariki. Maisha ya mhusika huyu yananasibiana na Yusufu ambaye naye alitoka utumwani akaishia kwenye kiti cha utukufu, Uwaziri mkuu.

Hadhira inaelewa vema historia ya mwanamama Siti binti Saad na mchango wake katika ukombozi huko Visiwani Zanzibar. Kupitia historia ya mwanamama Siti Binti Saad, hadhira inajifunza nafasi ya maono katika maisha. Kwamba, maono ndiyo daraja kuu la mafanikio ya mipango mengi katika uso wa dunia. Mhusika akiwa na maono anaweza kupambana hadi ndoto zake zikatimia. Mtunzi teule anafundisha kuwa maono hayapaswi kuzuiwa na ukuta wowote. Changamoto katika kufikia maono zinapaswa kuchukuliwa kama ngazi ya kupata ushindi si kurudi nyuma. Siti alikutana na makwazo mengi katika maisha lakini alipambana kufa na kupona hadi ndoto zake katika uga wa muziki na ukombozi wa Zanzibar zikatimia.

Hali kadhalika mtafiti amebaini dhamira ya kihistoria katika tamthiliya ya *Tanzia ya Patrice Lumumba* (2015) iliwasilishwa kupitia fani za Biblia. Mtunzi teule ametumia fani za Biblia katika drama hiyo kueleza historia ya Patrice Lumumba. Mhusika huyo, Patrice alikuwa mwanaharakati wa kisiasa nchini Kongo kuipatia Kongo uhuru. Patrice ndiye alipigania ukombozi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo miaka ya 1950 hadi 1960. Ndipo sasa akafanikiwa kuwa waziri wa kwanza wa Kongo, mwaka 1960 (Habari za UN, 2016).

Kupitia kazi hii, hadhira inaweza kutambua vema mengi yaliyojiri zama za ukombozi wa taifa la Kongo, chini ya uongozi wa Patrice Lumumba. Patrice

Lumumba alikuwa waziri mkuu wa kwanza katika nchi ya Kongo. Historia inaeleza kuwa aliitawala nchi ya Kongo kwa muda wa miezi sita tu, tangu nchi hiyo ipate uhuru 30/6/1960 (Mbogo, 2019). Tarehe 17/1/1961, kiongozi huyo akauawa kikatili. Hivyo nchi ya Kongo ikakumbwa na tanzia nzito sana. Tamthiliya hii imeeleza mambo mbalimbali yaliyomsibu Lumumba dhidi ya Wabelgiji na washirika wao kutoka Marekani, Ufarasa na Uingereza.

Matokeo ya utafiti huu yamebaini kwamba, historia ya Patrice Lumumba katika tamthiliya hii inanasibishwa na simulizi za Yesu Kristo kutoka kwenye Biblia. Patrice Lumumba amechorwa kama mkombozi wa Wakongo. Yesu Kristo amechorwa kama mkombozi wa Walimwengu. Katika harakari za ukombozi wa taifa la Kongo, Patrice Lumumba ameteswa hadi mauti. Hali kadhalika, Yesu Kristo katika harakati za ukombozi wa Walimwengu, ameteswa hadi mauti. Wahusika wote wawili wameishia kufa wakati wakipambania ukombozi wa jamii zao. Mbogo anahusisha kisa cha mateso ya Yesu Kristo na Patrice Lumumba namna hii:

108) MOBUTU: *Lumumba! Nimekuja kukuona kwa mara ya mwisho... Imebidi mtu mmoja fedhuli afe kwa faida ya Wakongomani wote..."*
(Uk. 41)

Historia ya Yesu Kristo katika Biblia (1Petro 2:24, Isaya 53:5 – 6, Luka 23: 44 – 49) inanasibiana na habari za Patrice Lumumba, mkombozi wa Kongo (Data Na. 109). Msomaji aliyewahi kuisoma historia ya Ukombozi wa Wayahudi, kupitia Yesu Kristo katika Biblia akihusisha vipengele hivyo kama miwani kuisoma tamthiliya teule, *Tanzia ya Patrice Lumumba* anaweza kubaini vema historia ya ukombozi nchini Kongo. Patrice Lumumba alijitoa mhanga, kufa na kupona katika kupigania ukombozi wa nchi yake. Jambo hilo halikuwa jepesi kwani alikuwa akishindana na

mataifa yenye nguvu, Ulaya na Marekani. Damu ya Patrice Lumumba ilikuwa kafara ya mtu mmoja kuwakomboa Wakongo.

Kwa jumla, matokeo ya utafiti huu yamebaini dhamira ya historia za watu na mataifa mbalimbali katika tamthiliya teule tulizotafiti. Dhamira hiyo imebainika kupitia fani za Biblia zilizotumiwa na mtunzi teule. Kwa hivyo hadhira inanufaika pakubwa kubaini historia za mataifa yaliyohusishwa katika harakati mbalimbali za ukombozi barani Afrika kutoka kwa viongozi wazawa wakaidi na wakoloni kutoka barani Ulaya.

Dhamira ya kihistoria za ukombozi wa mataifa katika tamthiliya teule imedhihirika kupitia fani za Biblia zilizotumiwa na mtunzi teule. Fani hizo ni kama vile sajili za Biblia, wahusika wa Biblia na simulizi za Biblia. Mhimili wa Nadharia ya Mwingilianomatini unaeleza kuwa usukaji wa maana ya matini hutokana na matini nyingine. Washadidi wa Nadharia ya Mwingilianomatini wanaeleza kwamba, kazi ya fasihi ni tokeo la kazi nyingine tangulizi (Kristeva, 1980). Mhimili huu unaeleza kuwa watunzi hutumia vipengele mbalimbali kutoka kazi nyingine zilizotangulia na kuvijumuisha katika kazi zao. Ndipo sasa tunasema, mtunzi teule ametumia vipengele kutoka kwenye Biblia kuumba kazi zake.

Aidha wanamwingilianomatini wanafafanua kuwa kutokana na mtagusano baina ya matini za fasihi, ngazi nzuri ya kumsaidia hadhira kubaini dhamira zinazowasilishwa katika kazi ya fasihi ni kuhusisha vipengele vya kifani vingine mbali ya matini iliyo mbele ya macho yake. Kutokana na mawazo ya wanamwingilianomatini, hadhira ikihusisha fani hizo kutoka kwenye Biblia itapambanua vema dhamira hii ya historia

katika nchi hizi; Tanganyika, Unguja, Kenya, Msumbiji, Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo na Afrika yote kwa jumla.

Mbogo, mtunzi wa tamthiliya teule katika mihtasari ya bunilizi hizo ameandika kwamba, historia ndiyo ilitangulia ndipo akabuni kazi zake. Aidha mtunzi huyu anaeleza Mungu wa sanaa ‘Muse’ alipomshukia alitamani sana kutunza historia ya wanaharakati mbalimbali wa ukombozi barani Afrika ambao wamezikwa katika kaburi la sahau. Ndipo sasa Mbogo akaandika tamthiliya teule kusawiri habari za Mondlane na Samora, Thomas Mboya, Bibi Titi Mohamed, Siti Binti Saad, Patrice Lumumba na Wangari Maathai.

Mwandishi teule anaendelea kueleza kuwa, ni vizuri wanaharakati waliopigania ukombozi wa nchi za Afrika wakakumbukwa na kuenziwa katika nchi zao na bara zima la Afrika. Mchango waliotoa kukomboa nchi ni mkubwa. Fasihi ya Kiswahili, kama chombo cha kutunza historia imetumiwa na mtunzi teule kupitia kutunza historia za mataifa mbalimbali kama tulivyobainisha. Fani za Biblia zimetumiwa ipasavyo kudhihirisha dhamira hiyo, kila zinapohusishwa na wasomaji waliokutana na matini tangulizi, Biblia iliyoandikwa kabla ya tamthiliya tulizotafiti.

### 4. 3. 14 Burudani kwa Jamii

Fasihi ni sanaa inayojishughulisha na masuala yanayomhusu binadamu na matatizo yake, ndoto zake, matumaini yake, migogoro yake na mazingira yake (Wamitila, 2004). Mwanazuoni huyu akizungumza kuhusu dhima za fasihi katika jamii anaeleza kwamba, dhima mojawapo ya fasihi ni kuburudisha jamii kupitia tanzu na vipera vyake vyote. Mwandishi au fanani yeyote anapowasilisha kazi ya fasihi hulenga

kufurahisha, kutumbuiza na kusisimua hadhira. Mtunzi wa kazi za fasihi anaweza kutumia nyimbo, semi, hadithi, ngoma, drama pamoja na vipera mbalimbali vya fasihi kuburudisha jamii.

Maeda (2021) anasema, "Fasihi huweza kutumiwa kama burudani kwenye mikusanyiko ya watu." Mtafiti huyu anakiri kwamba dhima mojawapo wa fasihi ni kuburudisha watu kwenye mikusanyiko. Ili kufanikisha dhamira hiyo, watunzi hutumia tanzu kama hadithi, ushairi, semi na sanaa za maonyesho ili kuburudisha hadhira.

Kimsingi, burudani kwa jamii ni moja ya dhamira inayojitokeza katika kazi za fasihi; fasihi simulizi na fasihi andishi mtawalia. Fanani, watunzi wa kazi za fasihi pamoja na dhamira mbalimbali wanazolenga kuwasilisha kwa jamii, pia hulenga kufurahisha hadhira lengwa. Fasihi ya Kiswahili imewasilisha dhamira hii pia kupitia fani mbalimbali ndani yake.

Matokeo ya huu utafiti tuliofanya yamebaini kwamba, Emmanuel Mbogo alilenga kuburudisha hadhira kupitia fani za Biblia alizotumia katika tamthiliya teule. Nadharia ya Mwingilianomatini inaeleza kuwa, mawasiliano baina ya mtunzi na msomaji huambatana na mwingiliano uliopo baina ya maneno na namna yalivyokuwa yakitumika awali (Wafula, 2007). Hivyo hadhira wakihusisha hizo fani za Biblia na jinsi zilivyotumika katika matini teule, wanabaini dhamira hii na shangwe zinajaa mtimani mwao.

Sehemu inayofuata hapa chini tumejadili dhamira ya burudani ilivyoelezwa katika kazi teule kwa kutumia fani za Biblia. Tumejadili dhamira hii katika tamthiliya zote teule zilizotumika katika utafiti tulioufanya.

Mtunzi teule katika tamthiliya ya *Wangari Maathai* (2015), amelenga kufurahisha hadhira lengwa. Dhamira hii imewasilishwa kwa kutumia fani za Biblia, mathalani semi za Biblia. Ndani ya tamthiliya hii, kuna pahala raia wa Kenya wamekusanyika kwenye hafla ya kitaifa kumpongeza Wangari Maathai. Siku ya pongezi uhusisha shangwe, furaha, mashangilio kwa hadhira. Sajili ya Biblia inayotumika kuburudisha na kujaza tumaini katika mitima ya hadhira lengwa imewasilishwa hivi;

109) ORENGO: *Wananchi na wazalendo wa nchi yetu tukufu ya Kenya, nitegeeni masikio mawili.*
*Leo ni siku iliyotukuka; siku inayomshawishi kila mzalendo kuishangilia kwa sababu ya matendo makuu aliyotutendea Mwenyezi Mungu sisi Wakenya wa makundi ya tabaka zote.*
(Uk. 48)

Sajili za Biblia; *nchi tukufu, siku iliyotukuka na matendo makuu aliyotutendea Mwenyezi Mungu* zinaashiria mashangilio kwa raia wa Kenya (Data Na. 110). Emmanuel Mbogo katika sajili hizi anafundisha hadhira kwamba, jamii inapopata ushindi katika maisha ni vema kufanya mashangilio kwa ushindi huo. Watu wanapaswa kufanya matukio ya shangwe kwa ushindi wanaopata kama nchi ya Kenya inavyofanya kwa ushindi aliopata raia wake Wangari Maathai (2004).

Dhamira hii imejadiliwa awali na waandishi wa vitabu mbalimbali katika Biblia. Kupitia kitabu hicho tunabaini kuwa mara nyingi Wayahudi, walipopata ushindi katika vita na adui zao walikusanyika pamoja kumshangilia Mungu wa Baba yao Ibrahim, wakiamini ndiye aliyewawezesha kupata ushindi husika. Mathalani,

Wayahudi walipovuka Bahari ya Shamu kwa miguu wakitoka Misri walishangilia mno (Kutoka 15: 1 – 27). Biblia imeeleza;

> "*Ndipo Musa na wana wa Israeli wakamwimbia Bwana wimbo huu wakanena, na kusema, Nitamwimbia Bwana, kwa maana ametukuka sana; Farasi na mpanda farasi amewatupa baharini.*
> *Bwana ni nguvu zangu, na wimbo wangu; Naye amekuwa wokovu wangu. Yeye ni Mungu wangu, nami nitamsifu; Ni Mungu wa baba yangu, nami nitamtukuza. Bwana ni mtu wa vita, Bwana ndilo jina lake. Magari ya Farao na jeshi lake amewatupa baharini, Maakida yake wateule wamezama katika bahari ya Shamu. Vilindi vimewafunikiza, Walizama vilindini kama jiwe"*
> (Kutoka 15: 1- 5).

Kimsingi, Wahusika wote katika matini teule; tamthiliya na Biblia wanamshangilia Mwenyezi Mungu kwa kuwapatia ushindi kwenye maisha. Sajili za Biblia zinazotumiwa zinarejesha heshima na tukuzo kwa Mwenyezi Mungu. Mtunzi teule ametumia sajili za Biblia kuburudisha hadhira kama tulivyobainisha.

Vilevile, dhamira ya burudani imeelezwa na mtunzi teule katika tamthiliya ya *Malkia Bibi Titi Mohamed* (2016). Sajili za Biblia zimetumika kuwasilisha dhamira hii katika utani unaofanyika baina ya wahusika. Utani ni hali ya uchekeshaji ambao ndani yake kuna ujumbe maalum uliokusudiwa mtu kuupata. Hata hivyo, tunaweza kueleza kuwa utani ni hali ya kufanyiana mzaha, dhihaka masihara na kutaniana. Kwa kawaida utani hufanywa na watu wenye uhusiano maalumu unaoruhusu watu kutaniana (Othman, 2015). Wahusika wa utani hulenga kufurahishana.

Mtunzi wa tamthiliya ya *Malkia Bibi Titi Mohamaed* ametumia mtindo wa utani, kejeli baina ya wahusika wawili; Christina na Bibi Titi. Kupitia majibizano ya wahusika hao, yenye lengo la kufurahishana mtunzi teule amehusisha fani za Biblia kama hivi;

110) CHRISTINA: *Mtakuwa mmeitoa wapi? Mliiumba? Bibi Titi acha kujifanya Mungu.*
BIBITITI*:* *Mungu apitishie mbali ...*
(Uk. 2)

Christina anatumia kejeli, dhihaka wakati akizungumza na Bibi Titi (Data Na. 111). Mhusika huyo anamkumbusha mwenzake Bibi Titi asijitape kuitoa nchi ya Tanganyika mbali. Christina anaona ni kichekesho kudai hivyo. Tanganyika inaamini kuwa ailiyeisadia nchi yao ikafika mahala ilipo ni Mwenyezi Mungu pekee. Hivyo asijitokeze mwanadamu kujitapa kwamba yeye ndiye aliyefanya juhudi kufa na kupona hadi Tanganyika ikapata uhuru.

Dhana ya uumbaji katika Biblia imehusishwa na Mwenyezi Mungu. Kwamba, mwenye uwezo wa kuumba vitu vyote vilivyoko katika dunia, ni Mungu Mwenyezi. Hivyo mwanadamu kujitapa kwamba ameumba nchi, ikafika ilipo kimekuwa kichekesho kwa jamii. Msomaji wa tamthiliya akisoma mazungumzo baina ya wahusika hawa, anaburudika kwani ndani yake kuna dhima ya kuchekesha. Utani baina ya wahusika katika tamthiliya hii ni burudani kwa wasomaji wa tamthiliya teule.

Pamoja na hayo matokeo ya utafiti huu yamebaini matumizi ya fani za Biblia katika kuwasilisha dhamira ya burudani kwa hadhira mahsusi katika tamthiliya ya *Mondlane na Samora* (2016). Mtunzi teule ametumia simulizi za Biblia kufanikisha hilo. Mathalani simulizi za Nabii Musa na mizungu mbalimbali iliyofanyika chini ya mkono wake akiliongoza taifa la Israel kutoka utumwani Misri na kurejea kwao Israel. Mbogo ameandika hivi;

111) JANET: *Sijui. Ila Samora alininong'oneza kuwa; baada ya mashambulizi yale ghafla,*

*Nyerere alimshika Samito, akainua kafimbo kake juu na mara wakayeyuka.*
(Uk. 86)

112) NESI: *Aaah! Ajabu ya Mungu hii!*
*Nasikia ile fimbo alipewa na mamaake.*
*Ni fimbo iliyojaa ishara na miujiza*.

JANET: *Kabisa! Nasikia ni kama ile fimbo ya Nabii Musa iliyogawa bahari ya shamu*

NESI: *[akicheka] Unajua hata hapa Dar watu wamembatiza; wanamwita Nyerere, Nabii Musa. Anatupeleka Kanaani, nchi ya Asali na Maziwa.*
(Uk. 88)

Simulizi kuhusu Nabii Musa na mizungu mbalimbali katika Biblia zinazorejewa katika tamthiliya hii (Data Na. 112 – 113) zimeelezwa kitabu cha Kutoka 12 – 15. Emmanuel Mbogo katika tamthiliya hii ametumia fani hiyo kuburudisha jamii. Dhamira hiyo imehusishwa na miujiza mbalimbali inayotendwa na Mwalimu Nyerere katika tamthiliya hii teule.

Uwezo uliomo katika fimbo ya Mwalimu Nyerere kufanya mizungu mbalimbali katika jamii, una dhima ya kufurahisha hadhira. Kwa mfano, fimbo kuwa na uwezo wa kuyeyusha watu (wakapotea ghafla), watu wasionekane na adui zao kwenye uwanja wa vita n.k. Maajabu hayo yamewafurahisha hata wahusika wanaosemezana kuhusu yanayojiri katika jamii kwa fimbo ya Mwalimu Nyerere. Matokeo ya utafiti yamebaini kwamba, Mbogo ametumia simulizi za Biblia kuburudisha jamii lengwa.

Hali kadhalika dhamira ya burudani kwa hadhira kwa kutumia fani za Biblia imesawiriwa katika tamthiliya ya *Mtumwa hadi Siti Binti Saad* (2016). Fani ya Biblia inayotumika kuwasilisha dhamira hii ni ushairi, kipera cha nyimbo. Uga wa fasihi unaeleza dhima mojawapo ya kazi za fasihi ni kuburudisha jamii (Mulokozi, 2017).

Ndipo sasa tunatambua kwamba, nyimbo zinazoimbwa katika tamthiliya hii teule zina dhima ya kufurahisha na kuchangamsha hadhira. Dhamira hii imewasilishwa hivi;

113) SITI: [anaingia na kuanza kuimba. Katulia, anajiamini ... *sauti kama Malaika ... ukumbi wote kimya]*
Cha alifuleila.
Nyumba ya udongo
Ghorofa ya mama
Uliponitaka
Nilikaa nawe
Sasa sikutaki
Sina haja nawe
(Uk. 68 & 69)

Mtunzi ametumia utanzu wa nyimbo kuburudisha hadhira yake (Data Na. 114). Mhusikia Siti anaimba wimbo wa shangwe mbele za umati unaoinuka kumshangilia. Katika wimbo huo tashbiha yenye mwangwi wa Biblia imetumika. Sauti ya Bibi Titi imelinganishwa na sauti ya Malaika kwa jinsi ilivyo nzuri.

Biblia inawaeleza Malaika kama viumbe wa Mwenyezi Mungu wanaomuimbia nyimbo sifa na tukuzo mchana na usiku kila uchao. Viumbe hao wanatajwa kuwa na sauti nzuri zinazovutia na kuchangamsha viumbe wa Mwenyezi Mungu huko juu Mbinguni. Dhima ya Malaika mbele za Mungu imeelezwa hivi;

> "*Hata alipokitwaa kile kitabu, hao wenye uhai wanne na wale wazee ishirini na wanne wakaanguka mbele za Mwana-Kondoo, kila mmoja wao ana kinubi, na vitasa vya dhahabu vilivyojaa manukato, ambayo ni maombi ya watakatifu. Nao waimba wimbo mpya wakisema wastahili wewe …*
>
> *Nikaona nikasikia sauti ya malaika wengi pande zote za kile kiti cha enzi, na za wale wenye uhai, na za wale wazee, na hesabu yao ilikuwa elfu kumi mara elfu kumi na elfu mara elfu, wakisema kwa sauti kuu, Astahili Mwana-Kondoo* aliyechinjwa, kuupokea uweza na utajiri na hekima na nguvu na heshima na utukufu na baraka.
> (Ufunuo 5: 8 – 12)

Dhamira ya Malaika katika Biblia imehusishwa na kuimba nyimbo mbele za Mungu kwa kutumia vinanda, vinubi, tarumbeta n.k. Dhamira ya nyimbo hizo imelenga kumsifu na kumshangilia Mwenyezi Mungu. Ndipo sasa tunasema nyimbo zililenga kuburudisha hadhira, Mwenyezi Mungu na viumbe wake.

Kimsingi, ushairi ni sanaa maarufu inayotumiwa na mwanadamu kujiburudisha (Sengo, 2009). Fani hii hutumika zaidi nyakati za jioni, baada ya kumaliza shughuli za kutwa (Angushi, 2019). Mtunzi teule katika tamthiliya tuliyosoma ametumia nyimbo anazoimba Siti katika tamasha aliloalikwa, kuburudisha hadhira. Emmanuel Mbogo kulinganisha sauti ya Siti na sauti ya Malaika ni ngazi njema kueleza namna sauti ya mhusika huyo ilivyo nzuri kupita kifani. Hadhira akiyasoma mashairi anayotoa Siti, mwenye sauti nzuri kama Malaika anaburudika ndani yake.

Hali kadhalika mtafiti amebaini dhamira ya burudani kwa hadhira kupitia matumizi ya fani za Biblia katika tamthiliya ya *Tanzia ya Patrice Lumumba* (2015) amewasilisha dhamira ya burudani kwa hadhira lengwa. Dhamira hiyo imewasilishwa kwa kuhusisha simulizi za Biblia sambamba na lugha ya kejeli, kinaya kwa lengo la kuchekesha hadhira. Dhamira hiyo imewasilishwa hivi;

114) TSHOMBE: Pauline mimi siko tayari kufa kama Adam.
Adam alijua fika kuwa tunda lile lilikuwa sumu,
Lakini kwa ushawishi na ulaghai wa mwanamke,
*Adam alichukua ufu, akautafuna, akaumeza,*
*akafa!...*(Uk. 54)

Simulizi inayorejewa hapa inahusu uasi wa mwanadamu wa kwanza, Adam aliyeumbwa na Mungu katika Biblia (Data Na. 115). Hadithi hiyo inaeleza kuwa, alivunja agizo alilopewa na Mola kwa kula matunda aliyokuwa amekatazwa kula

katika bustani ya Edeni. Adam alivunja agizo hilo kupitia mke wake, Eva. Uasi huo ulipelekea hukumu ya kifo kwa Adam na Eva.

Kwa jumla mtunzi wa tamthiliya hii ametumia kinaya, kejeli kumdhihaki Adam kwa maamuzi aliyofanya. Mbogo anaeleza kwamba, Adam alijua kabisa tunda alilokatazwa kula ni sumu lakini akashikilia msimamo wake akala. Hadhira inaburudika kupitia maamuzi hayo yasiyo na tija, kama simulizi inavyoeleza. Kejeli inasomeka namna hii, 'Adam aliuchukua ufu, akautafuna, akaumeza, akafa…' Fani hii ina dhima ya kuburudisha jamii. Mwanadamu kuchukua kifo na kukimeza ni kichekesho.

Mbali na hayo dhamira ya burudani imejadiliwa katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya* (2016). Mtunzi katika tamthiliya hii ametumia mtindo wa kishairi kutoka kwenye Biblia kuwasilisha dhamira hiyo. Mtindo huo umewasilishwa kupitia mhusika Pamela (Mke wa Tom Mboya). Mwanamama huyu anaimba wimbo wa shangwe kuonyesha tumaini lake kwa Mwenyezi Mungu. Dhamira inawasilishwa namna hii;

115) PAMELA: {anasema taratibu} ya pili ni uhai wake.
{kimya} uhai na usalama wa Tom.
Wakati mwingine nahofia maisha yake ...
*Wimbo wetu wa Taifa unasisitiza suala la kumtegemea Mungu*
*{akiimba pamoja na watu waliomzunguka}*
*Ee, Mungu nguvu yetu*
*Ilete baraka kwetu*
*Haki iwe ngao na mlinzi*
*Na tukae na undugu, amani na uhuru.*
*Raha tupate na ustawi.*
{Watu wanashangilia ...Mboya na familia yote inatoka}
(Uk. 66 & 67)

Mtindo wa kishairi uliotumika katika tamthiliya hii una dhima ya kuburudisha hadhira (Data Na. 116). Sajili za Biblia alizohusisha katika wimbo huo zimechangamsha mioyo ya watu. Ndipo sasa wakashangilia kwa mashairi yake. Mbogo anaeleza, *"Watu wanashangilia ...Mboya na familia yote inatoka."* Hivyo fani ya ushairi, iliyohusisha sajili za Biblia imedhihirisha dhamira ya burudani kwa hadhira.

Kitabu cha Biblia kimetumia mtindo wa kishairi kuandika kitabu chote cha Zaburi. Mwandishi wa kitabu hicho anajulikana kama Mfalme Daudi. Biblia inamweleza Mfalme huyo kama mmoja wa viongozi wa Wayahudi aliyependelea mno sanaa ya uimbaji. Daudi alitumia nyimbo kufanya mashangilio mbalimbali mbele za Mwenyezi Mungu mara nyingi alipotoka vitani na ushindi. Daudi anasema;

116) *"Haleluya. Ee nafsi yangu, umsifu Bwana.*
*Nitamsifu Bwana muda ninaoishi,*
*Nitamwimbia Mungu wangu ningali ni hai ..."*
(Zaburi 146: 1 -2)

Kwa jumla, maana ya matini haipatikani katika matini yenyewe, bali inajengwa na msomaji katika matini husika na mseto wa matini nyingine zinazotajwa na kurejelewa katika usomaji huo (Koyle, 1990). Dai la mtafiti huyo linatambuliwa kama mhimili wa Nadharia ya Mwingilianomatini, unaotumiwa na hadhira katika kubaini dhamira katika matini wanazosoma. Mhimili huo metusaidia kueleza namna fani za Biblia zilivyotumiwa kuwasilisha dhamira katika matini teule. Hadhira watabaini maana katika matini teule za Emmanuel Mbogo tulizotafiti wakihusisha na Biblia, matini tangulizi.

Zaidi ya hayo utafiti tuliofanya umebaini kwamba, tamthiliya teule tulizotafiti ni zao la matini nyingine, Biblia. Fani za Biblia alizotumia mtunzi teule, Emmanuel Mbogo kwa lengo la kuburudisha hadhira lengwa zimechotwa kutoka matini ya Biblia. Kwa mfano, Kejeli iliyotumika kuhusu *'Adam kula tunda la ufu'* ni chipukizi la Biblia. Hadhira iliyowahi kukutana na simulizi katika Biblia inaweza kufurahi kutokana na jinsi mtunzi alivyoliwasilisha jambo hilo. Sauti ya Siti kunasibishwa na sauti ya *Malaika*, inatoa taswira chanya kwa hadhira ambayo inaibua hisia za shangwe ndani mtima wa msomaji.

Hivyo basi, mtafiti anaeleza kuwa Emmanuel Mbogo alilenga kuburudisha jamii kupitia fani za Biblia katika tamthiliya teule tulizotafiti. Mtunzi huyu amehusisha fani mbalimbali kutoka matini ya Biblia ili kuwasilisha dhamira hiyo. Fani za Biblia zilizojitokeza ni simulizi za Biblia, sajili za Biblia, wahusika wa Biblia na mitindo ya Biblia kama vile ushairi. Hadhira ikihusisha fani hizo na jinsi zilivyojitokeza awali kama nadharia inavyoelekeza ili ibaini maana katika matini ya fasihi, inabaini dhamira ya burudani kwa wasomaji, jamii lengwa. Fani za Biblia zikihusishwa jinsi zilivyotumika awali na wakati huu katika matini teule, zinadhihirisha lengo la mtunzi teule, kuburudisha jamii. Fani hizo zimeibua hisia za shangwe, mashangilio, furaha kwa jinsi zilivyotumiwa na mtunzi teule, Bw. Emmanuel Mbogo.

## 4. 5 Muhtasari

Katika sura hii tumechambua na kuwasilisha data za utafiti huu. Uchambuzi huo ulijikita katika malengo mahsusi matatu ya utafiti huu. Mosi, tumebainisha fani za Biblia katika tamthiliya teule. Pili, tukaeleza sababu za kujitokeza kwa fani za Biblia

katika tamthiliya teule. Tatu, tumebainisha dhamira zinazojidhihirisha kutokana na matumizi ya fani za Biblia katika tamthiliya teule.

Matokeo ya utafiti huu yamedhihirisha kuwa, katika tamthiliya teule tulizotafiti kuna matumizi ya fani za Biblia. Fani za Biblia zilizojitokeza ni hizi zifuatazo; nukuu za Biblia, simulizi za Biblia, sajili ya Biblia, wahusika wa Biblia, mandhari ya Biblia na mitindo ya Biblia. Pamoja nazo mtafiti ameeleza sababu za kujitokeza kwa fani hizo katika tamthiliya teule, zaidi akiegema katika mihimili ya Nadharia ya Mwingilianomatini.

Vilevile katika sura hii tumebainisha dhamira mbalimbali zilizojidhihirisha kwenye tamthiliya teule kutokana na matumizi ya fani za Biblia ndani yake. Matokeo ya utafiti yamebaini dhamira zifuatazo: nafasi ya dini katika jamii; nafasi ya viongozi wa dini katika jamii; uadilifu na unyenyekevu katika jamii; kutokukata tamaa katika maisha; nafasi ya ubatizo kwa waumini wa dini ya Kikristo na waumini kujihadhari na mitume wa uongo.

Fauka ya hayo dhamira kama wajibu wa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa waumini wa dini ya Kikristo; kuheshimu wazazi na walezi; nafasi ya elimu katika maendeleo ya jamii; mapenzi na ndoa; ukombozi wa kisiasa Afrika; ukombozi wa kifikra; historia ya mataifa ya Afrika na kuburudisha jamii.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5. 1 Utangulizi

Sura hii inahitimisha andiko la tasnifu yetu. Sura imejegwa katika sehemu kuu tatu. Mosi, muhtasari wa matokeo ya utafiti. Pili mtafiti ameeleza hitimisho la utafiti huu. Hatimaya sehemu ya tatu mtafiti anawasilisha mapendekezo kutokana na utafiti uliofanyika.

## 5. 2 Muhtasari

Utafiti tuliofanya ulilenga kuchunguza fani za Biblia katika fasihi ya Kiswahili: mifano katika tamthiliya teule za Emmanuel Mbogo. Ili kufikia lengo hilo kuu, tulikuwa na malengo mahsusi matatu. Mosi, kubainisha fani za Biblia zilizojitokeza katika tamthiliya teule. Pili, kueleza sababu za matumizi ya fani za Biblia katika tamthiliya teule. Tatu, kubainisha dhamira zinazojidhihirisha kutokana na fani za Biblia zilizojitokeza katika tamthiliya teule. Malengo haya mahsusi yalijibiwa na maswali matatu ya utafiti huu. Tamthiliya teule tulizotafiti zilikuwa; Tanzia ya Patrice Lumumba (2015), Wangari Maathai (2015), Mtumwa hadi Siti Binti Saad (2016), Nyota ya Tom Mboya (2016), Malkia Bibi Titi Mohamed (2016) na Mondlane na Samora (2016).

Aidha kuhusu tatizo la utafiti huu, mtafiti alipata sababu ya kufanya utafiti huu baada ya kuona kwamba lengo kuu sambamba na malengo mahsusi yalikuwa hayajatafitiwa katika tafiti tangulizi. Tafiti kuhusu fani za Biblia katika fasihi ya

Kiswahili kwa kuegema katika Nadharia ya Mwingilianomatini na matini teule alizoandika Emmanuel Mbogo ilikuwa bado haijachunguzwa kabla yetu.

Hali kadhalika, kubainisha fani za Biblia, kueleza sababu za matumizi ya fani hizo katika fasihi ya Kiswahili na nafasi ya fani hizo katika kudhihirisha dhamira katika tamthiliya teule, hakukuwa kumechunguzwa kabla. Hivyo tatizo la utafiti huu lilikuwa kuchunguza fani ya Biblia katika fasihi ya Kiswahili: Mifano kutoka katika tamthiliya za Emmanuel Mbogo. Mtafiti katika uchunguzi huu alitumia Nadharia ya Mwingilianomatini au usemezano kama inavyotambulika katika vyanzo mbalimbali vya maarifa.

Vilevile mbinu za utafiti katika utafiti tuliofanya zimejadiliwa zaidi katika sura ya tatu. Katika sura hiyo, mtafiti ameweka bayana kuwa eneo lake la utafiti huu lilikuwa Dar es Salaam, Dodoma na Zanzibar. Mtafiti alipita maktaba mbalimbali katika ndaki za elimu ya juu kukusanya data kwa mbinu ya usomaji matini kama alivyonia.

Fauka ya hayo utafiti huu ulihusisha sampuli moja; sampuli lengwa. Sampuli lengwa katika utafiti huu ilirejea Biblia na maandiko teule ya Emmanuel Mbogo. Data yoyote ya fani ya Biblia iliyorejewa katika tamthiliya teule ilitumika katika kuwasilisha na kuchambua data za matokeo ya utafiti huu.

Pamoja na hayo utafiti huu ulihusisha data za msingi pekee. Data hizo zilikusanywa katika tamthiliya teule na Biblia. Data hizo zilikusanywa katika maktaba na makavazi za Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili – Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Dodoma na Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere.

Hali kadhalika mtafiti alitumia mbinu ya usomaji matini kukusanya data za utafiti. Mbinu hii ilimuwezesha kubaini fani za Biblia katika tamthiliya teule zote. Hali kadhalika kusoma machapisho mbalimbali yaliyotuwezesha kupata data katika matini tangulizi kwa ajili ya kurutubisha utafiti huu. Data za utafiti huu zimechambuliwa kwa kutumia mkabala wa maelezo ama ufafanuzi. Kwa sehemu kubwa maelezo ndiyo yametumika kuwasilisha data za utafiti huu. Hadi kufika mwisho wa utafiti, mtafiti amehusisha data za maktaba katika kupata matokeo bora ya utafiti huu.

Kimsingi, matokeo ya utafiti tuliofanya yametokana na maswali matatu mahsusi ya utafiti huu. Maswali hayo yalikuwa chipukizi la malengo mahsusi ya utafiti. Matokeo ya utafiti huu ni haya; Emmanuel Mbogo ametumia fani za Biblia katika tamthiliya zote sita tulizotafiti. Fani hizo ni Sajili ya Biblia, Wahusika wa Biblia, Simulizi za Biblia, Mandhari ya Biblia na Mitindo ya Biblia. Swali la kwanza la utafiti ndilo lilitufikisha hapa, kwamba ni fani zipi za Biblia zilizotumika katika tamthiliya teule za Emmanuel Mbogo?

Fauka ya hayo, kupitia matokeo ya utafiti tuliofanya tumebaini kuwa tamthiliya teule zote sita tulizotafiti ni zao la athari ya imani ya Kikristo inayotumia kitabu cha Biblia katika mafundisho yake. Utafiti umebaini kuwa Mtunzi teule ni mfuasi wa imani hii tangu kuzaliwa. Fani hizo za Biblia zilizotumika katika tamthiliya teule zimetumika kama mbolea ya kustawisha talanta ya uandishi iliyomo katika mtima wa mtunzi teule.

Msingi mkuu wa Nadharia ya Mwingilianomatini unaodai kwamba, kazi yoyote ya fasihi ni chipukizi lingine la matini tangulizi ulitusaidia kueleza sababu za kujitokeza kwa fani za Biblia katika tamthiliya teule. Nukuu za Biblia alizotumia Emmanuel Mbogo na fani nyinginezo zimetokana na mtunzi, Emmanuel Mbogo kuathiriwa na kitabu cha Biblia. Hivyo basi, tamthiliya zote sita teule tulizotafiti zimechagizwa na kitabu cha Biblia, kilichokuwapo miaka mingi kabla ya tamthiliya teule sita kuundwa miaka ya 2010. Emmanuel Mbogo anafumbata fani za Biblia ndani ya maandiko yake (Ngai, 2022).

Swali la tatu la utafiti huu lilitaka mtafiti aeleze nafasi ya fani za Biblia katika kudhihirisha dhamira katika tamthiliya teule. Matokeo ya utafiti huu yamebaini kwamba fani za Biblia zote zilizotumiwa na mtunzi katika tamthiliya teule hazikujitokeza kinasibu. Mtunzi alinuia kuwasilisha dhamira mbalimbali kupitia fani hizo. Miongoni mwa dhamira alizowasilisha Emmanuel Mbogo kupitia fani za Biblia katika tamthiliya teule ni hizi zifuatazo; Ukombozi (Kisiasa & Kifikra), Historia, Mapenzi na Ndoa, Nafasi ya Mwanamke katika Jamii, Nafasi ya Viongozi wa Dini katika Jamii, Maadili na Unyenyekevu kwa Viongozi, Kuishi kwa Matumaini, Nafasi ya Dini katika Jamii n.k.

Kimsingi dhamira ya ukombozi ndiyo dhamira kuu katika tamthiliya zote sita teule alizoandika Emmanuel Mbogo. Mtunzi teule ameegema katika dhamira ya kihistoria. Fauka ya hayo mtunzi teule katika dhamira hiyo amebainisha harakati mbalimbali za ukombozi zilizokuwa zikitamakani wakati nchi za Afrika zikipigania uhuru kutoka kwa Wakoloni miaka ya 1950 hadi 1970. Pamoja na hayo, mtunzi ameeleza harakati mbalimbali za utawala bora na demokrasia mara baada ya nchi za Afrika kupata

uhuru kutoka nchi za Ulaya. Utafiti umebaini kwamba, Emmanuel Mbogo amekusudia kutunza historia ya Afrika kupitia fasihi ya Kiswahili. Wahusika wakuu waliotumiwa katika tamthiliya teule, wote ni wanaharakati wa ukombozi katika nchi zao.

Nadharia ya Mwingilianomatini imewezesha tubaini kwamba, Emmanuel Mbogo ameathiriwa na Biblia kifani na kimaudhui. Fani na dhamira anazojadili zilishawasilishwa awali katika kitabu cha Biblia kuhusu jamii ya Israel. Hata hivyo mtunzi huyu anahusisha upya fani na dhamira hizo akihusisha jamii za Afrika, zaidi katika harakati za ukombozi wa kisiasa kutoka kwa Wakoloni - Ulaya. Dhamira ya ukombozi iliyojengwa kupitia fani za Biblia ina mwangwi wa dhamira ya ukombozi iliyoelezwa katika kitabu cha Biblia.

Lengo mahsusi la pili katika utafiti huu lilitaka tueleze sababu za kujitokeza kwa fani za Biblia katika tamthiliya teule za Emmanuel Mbogo. Kupitia Nadharia ya Mwingilianomatini iliyoongoza utafiti huu, tulibaini kwamba sababu inayochagiza fani za Biblia kujitokeza katika bunilizi zake teule ni athari za kitabu cha Biblia alichokisoma mwandishi hapo kwanza kabla ya kuandika tamthiliya teule zote. Mhimili wa mwingilianomatini unaeleza kwamba, kila matini ya fasihi ni zao la kazi nyingine iliyotangulia awali. Hivyo basi fani na maudhui anayohusisha kutoka kitabu Biblia katika tamthiliya zake ni ithibati kwamba chipukizi lake kuu ni Biblia. Mathalani kuonyesha kwamba suluhu ya tatizo la majini ndani ya mtu ni maombi na maombezi ni kuongeza sauti yanayoelezwa katika kitabu cha Biblia yafike mbali zaidi. Dhamira ya ukombozi wa jamii kisiasa katika tamthiliya zake kuhusishwa na

umwagaji damu kwa baadhi za wanaharakati inashadidia alilofanya Yesu Kristo kwenye Biblia. Kwamba alibidi yeye afe ili dunia yote ipone.

**5. 3 Hitimisho**

Kimsingi, utafiti umebaini kuwa, fani za Biblia zimejitokeza katika utunzi wa tamthiliya teule zote sita zilizoandikwa na Emmanuel Mbogo. Katika tamthiliya hizo Mbogo amehusisha fani za Biblia, ambazo ni chipukizi la kitabu cha Biblia kilichokuwapo mapema kabla ya kazi hizo. Tamthiliya hizo teule ziliandikwa zote ndani ya muongo mmoja (2010 – 2020). Hivyo fani zake zinahusiana. Fauka ya hayo upande wa maudhui mtunzi anaeleza hadhira siri za ushindi katika kadhia mbalimbali maishani. Pia wasomaji wamejuzwa kuhusu hukumu ya mwisho na adhabu itakayotolewa kwa waasi huko Jehanamu. Hali kadhalika mwelekeo chanya alionao mtunzi kuhusu Biblia umechagizwa na malezi ya Kikristo aliyokulia enzi na enzi. Tamthiliya ya Nyota ya Tom Mboya imetokana na simulizi za Yesu Kristo tangu kuzaliwa na harakati zake katika ukombozi wa mwanadamu kutoka katika Biblia. Tamthiliya ya Mtumwa hadi Siti Binti Saad imetiwa mbolea na simulizi za mtumwa mmoja katika Biblia, aitwaye Yusufu Yakobo huko Misri. Mbogo ameifundisha jamii kutokata tamaa kwamba, hata mtu masikini, aliyekata tamaa anaweza kuinuliwa katika maisha hata kuketishwa na wakuu kama ilivyokuwa kwa Siti binti Saad. Kwamba alianza katika utumwa lakini baadaye akainuliwa hadi kuwa Malkia wa Taarab, Upwa wa Afrika Mashariki.

5. 4 Mapendekezo

Utafiti tuliofanya ulihusisha tamthiliya sita teule alizoandika Emmanuel Mbogo katika fasihi ya Kiswahili. Tamthiliya hizo ni Nyota ya Tom Mboya, Wangari

Maathai, Tanzia ya Patrice Lumumba, Mondlane na Samora, Mtumwa hadi Siti Binti Saad na Malkia Bibi Titi Mohamed. Hata sasa mtunzi huyu ameandika tamthiliya mbalimbali katika fasihi ya Kiswahili. Mtafiti anapendekeza kwamba, tafiti katika maandiko mengine ya Emmanuel Mbogo zifanyike. Tafiti hizo zichunguze kama Mbogo ametumia fani za Biblia au fani nyingine katika bunilizi zake zote kwa mkabala wa mwingilianomatini.

Miaka ya 2020 Emmanuel Mbogo ameandika tamthiliya nyingine mathalani tamthiliya ya Julius Nyerere Kizimbani (2022) na Mwinyi na Manyani ya Adili (2022). Pamoja na hayo ameandika riwaya na hadithi fupi mbalimbali. Hivyo ni vyema watafiti wapitishe jicho kwenye kazi hizo ili kubaini mitindo mbalimbali aliyotumia mtunzi huyu katika fasihi ya Kiswahili. Wanahistoria katika bara la Afrika na ulimwenguni kwa ujumla pia wamepata hazina nzuri inayotunza historia ya Afrika. Wafanye tafiti tena na tena kubaini historia anazowasilisha mtunzi teule kupitia bunilizi zake.

Kimsingi, katika utafiti huu tumebaini kwamba vitabu vya kiimani huathiri watunzi katika kubuni kazi zao. Emmanuel Mbogo na Euphrase Kezilahabi wamewekwa bayana kama watunzi walioathiriwa na Biblia katika fasihi andishi ya Kiswahili. Pamoja nao, fasihi andishi ya Kiswahili inajumuisha watunzi kutoka imani ya Kiislam wanaotumia kitabu cha Kurani katika imani yao. Je, fani za Kurani zinatumika katika fasihi ya Kiswahili? Fani hizo zinapotumika zimelengwa kuwasilisha dhamira yoyote kwa hadhira ima watunzi huzitumia kibubusa? Watafiti wajikite katika eneo hili ili fasihi ya Kiswahili ipanue maarifa kuhusu fasihi ya Kiswahili na mwingiliano wa matini za kiimani. Waswahili kutoka ndaki mbalimbali za elimu hapa ulimwenguni wanufaike tena na tena.

## MAREJELEO

Adolph, E. M. (2021). Ukombozi wa kifikra miongoni mwa watanzania kwa maendeleo ya taifa. *Jamii Forums*. https://www.jamiiforums.com/threads/ukombozi-wa-kifikra-miongoni-mwa-watanzania-kwa-maendeleo-ya-taifa.1907561/

Alter, R. B. (1981). *The arts of biblical narrative*. Basic Books.

Amando, A. E. (2022). *Changamoto katika tafsiri za biblia ya kiswahili* (Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino). Makavazi ya Chuo.

Ambrose, K. N. (2014). *Mwingilianomatini katika tamthiliya za Kiswahili: Mashetani na kijiba cha moyo* (Haijachapishwa). (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania). Makavazi ya Chuo.

Angushi, M. E. (2019). *Mchango wa tamasha za muziki katika ufundishaji wa uanishaji wa nyimbo katika shule za upili nchini Kenya* (Haijachapishwa). (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kibabii Kenya). Makavazi ya Chuo.

Ayiera, E.; Ontieri, J. O.; Ayodi, N. (2017). Mchango wa mazingira ya mwandishi katika matumizi ya mafumbo. *International Journal of Arts and Education* (1): 1 – 17. http://hdl.handle.net/123456789/7168

Bakhtin, M. (1981). *The dialogic imagination: Four essays*. Ed. Michael Holquist. Trans. University of Texas Press.

BAKITA (2022). *Kamusi Kuu ya Kiswahili.* Ilisomwa Mei 22, 2023. Katika https://play.google.com/store/apps/details?id=com.mds.apps.kamusi&hl=en_US&pli=1

Barry, A. L. (2017). ‘Ubatizo mtakatifu’. Ilisomwa Mei 23, 2023. Katika https://media.lhfmissions.org/file/lhf-missions/pdfs/Swahili-Kuhusu-Jambo-Gani-Ubatizo-Mtakatifu-Holy-Baptism.pdf

Barthes, R. (2002). *Oeuvres complètes II (1962-1967) (2)*. Ilisomwa Mei 4, 2023. Katika https://www.amazon.com/Books-Roland

Bosire, T. B. (2016). *‘Mwingilianomatini katika mkaguzi kuu wa serikali na mstahiki meya’* (Haijachapishwa). (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi). Makavazi ya Chuo.

Butiku, J. W. (2023). Barua ya wazi kwenda kwa mheshimiwa rais samia suluhu hassan. Dar es Salaam. Gazeti la Nipashe Juz. 8.

Bwelele, E. (2016). *Mtindo katika tamthiliya za sadaka ya john okello na nyerere na safari ya kanaani* (Haijachapishwa). (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania). Makavazi ya Chuo.

Chamba, J. E. (2014). *Misingi inayodumisha ndoa*. Morogoro. Kanisa la Kiadventisti Tanzania.

Clayton, J. & Eric R. (1991). Figures in the Corpus: Theories of Influence and Intertextuality. Influence and Intertextuality in Literary History, ed. (pp. 3-36.) by Jay Clayton & Eric Rothstein. Madison & Wisconsin: The University of Wisconsin Press.

Clemence, S. M. (2015). *Kuchunguza Mbinu za Kiaristotle katika Tamthiliya za Fumo Liyongo na Sundiata* (Haijachapishwa). (Tasnifu ya Uzamili). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Esili, A. M. (1999). *Adili za Wafipa na Ukristo.* Parokia ya Nkundi.

Fadhili, E. F. (2014). *Kuchunguza Dhima ya Mtindo katika Tamthiliya za Kihistoria:*

*Utafiti Linganishi wa Tamthiliya za Morani na Kinjekitile* (Haijachapishwa). (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania). Makavazi ya Chuo.

Fairchild, M. (2023). Ubatizo ni nini? Ilisomwa Mei 25, 2023. Katika https://sw.eferrit.com/ubatizo-ni-nini/

Faustine, S. (2020). Uafrikanishaji katika Riwaya ya Kiswahili. *Mulika* – Toleo Na. 38. (Uk. 55 – 73). Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Forster, E. M. (1927). *Aspects of the Novel*. Penguin Books.

Forster, E. M. (1949). *Aspects of the Novel (2nd Ed.).* Penguin Books.

Fungavyema, L. (2020). Fanya Hivi Ili Kumjengea Mtoto Uwezo wa Kufikiri. Ilisomwa tarehe 18 Novemba 2022. Katika https://mbunifu.home.blog/2020/11/22/fanya-hivi-ili-kumjengea-mtoto-uwezo-wa-kufikiri-2/

Fungavyema, L. (2020). Jinsi ya Kupambana na Pepo la Kukata Tamaa. Ilisomwa Mei 24, 2023. Katika https://mbunifu.home.blog/tag/nini-maana-ya-kukata-tamaa/

Gibe, 2. (2020). *Shukrani Mbele za Mwenyezi Mungu*. Shiloh United Wordwide Ministries.

Gichamba, J. M. (2005). *Sifa za Shujaa na Umuhimu wao kwa Jamii Zao: Ulinganishi wa Fumo Liyongo na Shaka Zulu*. Ilisomwa tarehe 21/11/2022. Katika http://erepository.uonbi.ac.ke/bitstream/handle/11295/18381/JULIUS_MUNGAI_GICHAMBA_M.A_2005.pdf;sequence=3.

Habari za UN (2016). Mfahamu Patrice Lumumba Kupitia Simulizi za Brian Urquhart wa UM. *Makala za Umoja wa Mataifa*. Ilisomwa Mei 18, 2023. Katika https://news.un.org/sw/story/2016/08/461742

Habari za UN (2022). Viongozi wa Serikali na Dini Lindeni Waathirika wa Ukatili. Guterres. Ilisomwa Mei 25, 2023. Katika https://news.un.org/sw/story/2022/08/1151122

Hananja, R. (2007). Pendo la Mungu Halipimiki. *Upendo Media*. Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania.

Hananja, R. (2009). Inuka Ufanye Kazi ya Bwana. *Harambee ya Ujenzi wa Kanisa*. Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania.

Hananja, R. (2011). Twenzetu kwa Yesu. *Tamasha la Vijana*. Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania.

Hananja, R. (2017). *Misingi ya Inayodumisha Ndoa*. Soma Biblia Tanzania.

Herman, L. B. (2011). Mwingilianomatini kwenye Hadithi za Watoto katika Kiswahili. *Kioo cha Lugha* (Juz. 79). Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Hichens, A. (1972). *The End of Inequality? International Socialism* (1st Series). Ilisomwa Mei 6, 2023. Katika https://www.marxists.org/history/etol/newspape/isj/1972/no050/hitchens.htm

Hoppenau, A. na Hahn, J. (2009). *Mwongozo wa Utamaduni: Kubadilishana Tamaduni za Kijerumani na za Kitanzania – Toleo 1*. Ulisomwa Mei 06, 2023. Katika

https://dtpev.de/storage/app/uploads/intranet/public/5bb/46b/e04/5bb46be04d9f4895644632.pdf

Isaac, S. & Michael, W. B. (1978). *Handbook of Research Revolution: A Collection of Principles, Methods and Strategies useful in the Planning, Design and Behavioral Science*.San Diego. Edips.

Ismail, F. H. (2019). *Kuchunguza Mtindo wa Dhamira katika Tamthiliya ya Mondlane na Samora* (Haijachapishwa). (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania). Makavazi ya Chuo.

Jacob, S. (2018). *Mjue Kinjeketile*. Ilisomwa Januari 19, 2023 katika https://www.dw.com/sw/mjue-kinjekitile-ngwale/av-42308520.

Jamieson, B. (2018). 'Mafundisho ya Biblia kuhusu Ubatizo'. Ilisomwa Mei 23, 2023. Katika https://zaidikumhusuyesu.files.wordpress.com/2020/01/mafundishoya-biblia-kuhusu-ubatizo.pdf

Japheth, K. (2017). 'Kuwatii na Kuwanyenyekea Viongozi wa Dini ni Agizo la Mungu'. Ilisomwa Mei 23, 2023. Katika https://www.facebook.com/1314965715288718/posts/kuwatii-na-kuwanyenyekea-viongozi-wa-dini-ni-agizo-la-munguwatiini-wenye-kuwaong/1487825764669378/

Jilala, H. (2015). *Misingi ya Fasihi Linganishi: Nadharia, Mbinu na Matumizi*. Daudi Publishing House.

Johnson, J. (1986). *The Epic of Son-Jara*. Bloomington: Indiana University Press.

Julius, M. (2018). Nafasi ya Maono katika Maisha. Katika *Semina ya Vijana – Tabata Segerea*. Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania.

Kapuya, J. (1997). *Sera ya Taifa ya Utamaduni*. Ilisomwa Mei 05, 2023. Katika http://www.tzonline.org/pdf/serayautamaduni.pdf

Karisa, B. & Mwinyifaki, A. (2013). Iktibasi katika Tenzi za Mwanakupona na Al-Inkishafi. *Kioo cha Luga* (11), 30 – 45. Makavazi ya Chuo.

Katubayemo, E. (2022). Maombi ya Kufunga na Kuomba (Mahubiri). Usharika wa Kijitonyama, Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania.

Kaufuman, P. (1976). *Existentialism, Religion and Death*. Meridia.

Keys, A. (1980). *Seven Countries: A Multivanate Analysis of Death and Coronary, Health Desease.* Havard University Press.

Kezilahabi, E. (1976). *Shaaban Robert: Mwandishi wa Riwaya* (Haijachapishwa). (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam). Makavazi ya Chuo.

Khamis, S. A. (2017*). Matumizi ya Lugha na Dhamira katika Tamthiliya Teule za Emmanuel Mbogo* (Haijachapishwa). (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania). Makavazi ya Chuo.

Khatibu, M. (2011). *Chanzo cha Matakwa ya Mwanamume katika mwili wa Mwanamke Ulinganisho wa Ushairi wa Muyaka bin Haji na Shaaban Robert.* (Haijachapishwa). (Tasnifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Dodoma). Makavazi ya Chuo.

Kimambo, S. J. (2015). Kuchunguza Matumizi ya Lugha katika Riwaya za Kiswahili: Uchunguzi Kifani wa Riwaya za Vipuli vya Figona Siri za Maisha (Haijachapishwa). (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania). Makavazi ya Chuo.

Kimaro, E. (2015). Mipango ya Mungu Haizuiliwi. Semina ya Vijana. Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania.

Kimaro, E. (2022). Ndoa ni Mpango wa Mungu. Semina ya Wanandoa. Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania.

Kiprotich, P. J. (2013). *Mchango wa Mbazi za Biblia katika Ukuzaji wa Fasihi Andishi ya Kiswahili.* (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Kenyatta). Katika https://ir-library.ku.ac.ke/handle/123456789/14026

Kohm III, J. (2016). *25 Examples of the Bible's Influence of Literature*. Regent University.

Kothari, R. C. (1992). *Research Methodology: Methods and Techniques (3rd Ed.).* Vishwa Parashan.

Kristeva, J. (1969). *Desire in Language: A Semiotic Approach to Literature and Art.* Columbia University Press.

Kristeva, J. (1980). *Desire in Language: A Semiotic Approach to Literature and Art.* Columbia University Press.

Kyovi, P. K. (2015). *Mwingilianomatini katika Utenzi wa Mwanakupona na Nyimbo za Harusi za Kisasa* (Haijachapishwa). (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi). Makavazi ya Chuo.

Lemaster, T. (2012). What is "Intertextuality"? United States: University of Wisconsin-Madison. Ilisomwa Mei 6, 2023 katika View of Mwingilianomatini katika Tamthilia ya Utangamano Wetu Ushindi Wetu (2017) ya Anitha E. Mgimba (eanso.org)

Lyimo, E. (2018). Nduni za Fasihi ya Watoto: Mifano kutoka katika Vitabu vya Kiswahili vya Fasihi ya Watoto nchini Tanzania. *Mulika* Tol. 33 (1), 33 - 45. Ilisomwa Mei 01, 2023. Katika https://journals.udsm.ac.tz/index.php/mj/article/view/1534/1431.

Macha, N. (2013). Matumizi ya Mwingilianomatini kwenye Tendi. Ilisomwa Mei 03, 2023. Katika http://chomboz.blogspot.com/2013/05/800x600-normal-0-21-false-false-false_23.html#

Madumulla, J. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi.* Mture Education Publishers.

Maguo, O. & Rashid, A. (2020). Kuchunguza Mtindo katika Riwaya za Euphrase Kezilahabi na Mohamed Suleiman. *RUJASS Tol. 6*. Chuo Kikuu Katoliki Ruaha. Ilisomwa Mei 08, 2022. Katika https://rucu.ac.tz/assets/doc/RUJASS%20VOLUME%206,%201%20-%202020.pdf

Maguo, O. (2011). *Siasa katika Ushairi wa Kezilahabi: Uchunguzi wa Karibu Ndani (1988) na Dhifa (2008)* (Haijachapishwa). (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam). Makavazi ya Chuo.

Majeche, S. K. (2017). *Nafasi ya Ufeministi katika Jamii zetu Kabla ya Kristo mpaka Leo* (Haijachapishwa). (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Mt. Agustino). Makavazi ya Chuo.

Malugu, A. (2015). ‘Nafasi ya Fasihi katika Kusawiri suala la Dini’. Ilisomwa Mei 20, 2023. Katika https://journals.udsm.ac.tz/index.php/kiswahili/article/view/743

Marisya, P. (2017). *Mchango wa Sajili za Dini katika Kufanikisha Riwaya Mbili: Kidagaa Kimemuozea na Ndoto ya Almasi za Ken Walibora. (Haijachapishwa). (*Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Nairobi). Ilisomwa April 20, 2023. Katika http://erepository.uonbi.ac.ke/bitstream/handle/11295/101893/Marisya_Mchango%20Wa%20Sajili%20Ya%20Kidini%20Katika%20Kufanikisha%20Riwaya%20Mbili%20Za%20Ken%20Walibora%20%28Kidagaa%20Kimemwozea%20Na%20Ndoto%20Ya%20Almasi%29.pdf?sequence=1&isAllowed=y

Martin, I. (2021). Nafasi ya Fani katika Kufanikisha Maudhui katika Fasihi ya Watoto (Haijachapishwa). (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Rongo). Ilisomwa Oktoba 17, 2023. Saa 5:40 Asubuhi katika http://repository.rongovarsity.ac.ke/bitstream/handle/123456789/2375/Nafasi%20ya%20fani%20katika%20kufanikisha%20maudhui%20katika%20fasihi%20ya%20watoto.pdf?sequence=1&isAllowed=y

Masatu, J. F. na wenzake (2020). Mafunzo Yanayotawala Ushairi Andishi wa Kiswahili wa Kipindi cha Utandawazi: Mifano Kutoka Diwani ya Kimya! (2020) ya Rehema N. Mbwambo. Iliyosomwa Juni 20, 2023. Saa 11: 15 Jioni). Katika https://journals.eanso.org/index.php/eajss/article/view/199

Masatu, J. F na wenzake (2020). 'Mwingilianomatini katika Tamthiliya ya Utangamano Wetu Ushindi Wetu (2017) ya Anitha Mgimba.' Chuo Kikuu Katoliki Mwenge. Moshi-Kilimanjaro. Ilisomwa 2 Mei 2023, Saa 5:30 Asubuhi. Katika View of Mwingilianomatini katika Tamthilia

ya Utangamano Wetu Ushindi Wetu (2017) ya Anitha E. Mgimba (eanso.org)

Masoud, S. (2018). Kutathmini Matumizi ya Mitindo na Dhamira katika Tamthiliya za Mashetani na Mashetani Wamerudi: Utafiti Linganishi (Haijachapishwa). (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania). Makavazi ya Chuo.

Mastai, W. (2018). Ukuu na Uweza wa Mungu Hauelezeki (Mafundisho ya Neno la Mungu). Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania.

Mastai, W. (2023). Mungu Humtumia Yeyote Kufanya Kazi yake (Mafundisho ya Neno la Mungu). Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania.

Materu, M. & Mhando, P. (1976). 'Fani ya Hadithi na Riwaya.'*Kioo cha Lugha* (1). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mayo, F. F. (2020*). Matumizi ya Maneno ya Biblia katika Riwaya ya Rosa Mistika na Gamba la Nyoka za Euphrase Kezilahabi* (Haijachapishwa). (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania). Makavazi ya Chuo.

Mbatia, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Text Books Graphics and Publishers.

Mbogo, E. (2016). *Nyotaya Tom Mboya*. Vision Strategic Impact.

_______ (2016). *Mtumwa hadi Siti Binti Saad*. Print Plus.

_______ (2016). *Malkia Bibi Titi Mohamed.* Afro Plus Industries.

_______ (2016). *Mondlane na Samora*. Vision Strategic Impact Ltd.

_______ (2015). *Wangari Maathai*. Print Plus.

_______ (2015). *Tanzia ya Patrice Lumumba*. Africa Proper Educational Network.

Mboka, A. M. (2018). *Uhakiki wa Fasihi ya Kiswahili: Shule za Sekondari*. Bubujiko la Maarifa. Ilisomwa tarehe 28 Desemba 2022. Katika http://chomboz.blogspot.com/2018/12/tasnifu.html#.

Mhariri Mkuu Wikiwand (2022). 'Ureno Nchini Msumbiji'. Ilisomwa Septemba 8, 2022. Katika https://www.wikiwand.com/sw/Msumbiji

Mhariri Mkuu Wikiwand (2023). 'Tuzo ya Amani ya Noble'. Ilisomwa Mei 8, 2023. Katika https://www.wikiwand.com/sw/Tuzo_ya_Nobel_ya_Amani

Milton, J. (1667). *Paradise Lost.* England. Samuel Simmons.

Mkufya, E. (2005). 'Mazungumzo na Lutz Diegner juu ya Riwaya yake Ziraili na Zirani'. *Swahili Forum* (12), 37 – 62.

Mlacha, S. A. K. & Madumulla, J. S. (1993). *Riwaya ya Kiswahili.* Dar es Salaam University Press.

Mlacha, S. A. K. (1991). *A Linguistic Study of the Novel.*Berlin. Schreiber.

Mlaga, K.W. (2015). Uhistoria katika Riwaya ya Kiswahili: Mifano katika Riwaya ya Ndoto ya Ndaria, Gamba la Nyoka na Miradi Bubu ya Wazalendo. Katika *Jarida la Kiswahili*. Juz. 78 Na. 1. Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mlaga, K.W. (2017). *Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Fasihi*. Taasisi ya Elimu Rwanda.

Mlaga, W. K. (2012). *Fasihi ya Kiswahili na Propaganda*. Dodoma. Chuo Kikuu cha Dodoma.

Mlaga, W. K. (2015). Kuchunguza Dhamira ya Ukombozi wa Kisiasa Afrika katika

Fasihi ya Kiswahili: Mifano kutoka Waandishi wa Tanzania. *Nuru ya Kiswahili*. Chuo Kikuu cha Dodoma.

Mlama, P. (1983). *Tanzania Traditional Theater as a Pedagogical Institution* (Not published). (PhD Thesis, University of Dar es Salaam). University Repository.

Mlelwa, A. A. (2017). *Falsafa ya Kiafrika katika Vitabu Teule vya Fasihi: Dunia Uwanja wa Fujo na Ngoma ya Ng'wanamalundi* (Haijachapishwa). (Tazimili, Chuo Kikuu cha Dodoma). Makavazi ya Chuo.

Mlelwa, E. (2021). *Nafasi ya Fasihi katika Kutunza Historia* (Haijachapishwa). (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dodoma). Makavazi ya Chuo.

Mlyauki, G. (2014). Elimu ni Hazina (Mhadhara Darasani). Kitivo cha Elimu - Chuo Kikuu cha Dodoma.

Mningo, R. A. (2015). *Tathimini ya Mwingilianomatini katika Utunzi wa Emmanuel Mbogo: Utafiti Linganishi wa Ngoma ya Ng'wangamalundi na Fumo Liyongo* (Haijachapishwa). (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania). Makavazi ya Chuo.

Mollel, R. (2006). *Ufafanuzi kuhusu Maadili ya Utumishi wa Umma*. Ofisi ya Rais. Dar es Salaam. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Msacky, E. Y. (2015). *Kuchunguza Dhamira za Kijamii na Kisiasa katika Riwaya ya Siri za Maisha* (Tasnifu ya Uzamili, Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Dar es Salaam.

Msami, J. (2019). *Tathimini ya Mfumo wa Kitaasisi wa Maboresho ya Utumishi wa Umma*. REPOA.

Msangi, E. O. (2018). *Kuchunguza Ubiblia katika Tamthiliya za Emmanuel Mbogo* (Haijachapishwa). (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania). Makavazi ya Chuo.

Mulokozi, M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili*. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mulokozi, M. (1999). Nafasi ya Mwanamke katika Fasihi ya Kiswahili: Mifano kupitia Semi za Kiswahili. *Kiswahili*. Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

Mulokozi, M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili: Kozi za Fasihi Vyuoni na Vyuo Vikuu.* Dar es Salaam. KAUTTU Publishers.

Mwakasege, C. (2017). Mshukuru Mungu kwa Kila Jambo (Semina). Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania.

Mwamakula, E. B. (2022). 'Tanzania Inahitaji Diplomasia Komavu Kuhusu Vita Dhidi ya Urusi na Ukraine'. Ilisomwa Mei 23, 2023. Katika https://www.facebook.com/photo/?fbid=3190641114542143&set=gm.651072646170434&idorvanity=576225880321778&__cft__[0]=AZUR5pCuzylVl3YBI4s0IRezvS_Cmlax5vYDoGVLf8Jz5FSl6iMEmepa3IzthHElwBpRF9Xp9HwTqhems0oCe4aVrElJUWqDHJ0Ad4ZoN8u3XBBgGplU6rZcj9Rlk8QPBxHsxxJdrXyxLDCsOtrgz0fd&__tn__=EH-R

Mwananchi (2021). 'Mbalamwezi ya Kiswahili: Fasihi ni Mwarobaini wa Matatizo ya Kiafya.' Ilisomwa Mei 23, 2023. Katika https://www.mwananchi.co.tz/mw/habari/makala/maarifa/mbalamwezi-ya-kiswahili-fasihi-ni-mwarobaini-wa-matatizo-ya-kiafya-2858074

Myinga, G. (2019). 'Unyenyekevu wa Moyo'. Ilisomwa Mei 24, 2023. Katika

https://www.scribd.com/document/416325415/UNYENYEKEVU-WA-MOYO

Ng'etich, K. D. (2011). 'Dini kama Chombo cha Kuwadhulumu Waumini:Mifano kutoka Fasihi ya Kiswahili' (Haijachapishwa). (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Kenyata). Makavazi ya Chuo.

Ngai, E. (2022). *Fasihi na Historia* (Haijachapishwa). (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania). Makavazi ya Chuo.

Ngugi, W. (2004). *Mchango wa Biblia katika Fasihi*. Kongamano la 57- Baraza la Kitaifa la Makanisa Nchini Kenya.

Njogu, K. & Chimerah, R. (2011). *Ufundishaji wa Fasihi:Nadharia na Mbinu*. Jomo Kenyatta Foundation.

Njogu, K. & Wafula, R. M. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Jomo Kenyata Foundation.

Nyabunga, V. A. (2005). Uhakiki wa Binadamu (2002) na Musaleo (2004) (Haijachapishwa). (Tasnifu ya Uzamili katika Kiswahili, Chuo Kikuu Nairobi). Makavazi ya Chuo.

Ojiambo, D. (2019). Miaka 50 Tangu Kifo cha Tom Mboya, Je, Kwa nini aliuawa? ). Ilisomwa Mei 24, 2023. Katika https://radiojambo.co.ke/habari/2019-07-05-miaka-50-tangu-kifo-cha-tom-mboya-je-kwanini-aliuawa/.

Oiko, F. G. (2017). Uhakiki wa Mtindo katika Tamthilia za Arege (Haijachapishwa). (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Maasai). Makavazi ya Chuo.

Okemwa, M. (2017). Mchango wa Fasihi Simulizi katika Fasihi Andishi: Mfano wa Visasili katika *Mafuta* na *Walenisi* (Haijachapishwa). (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Kenyata).

Omukabe, O. (2020). Eleza kati ya Fasihi Simulizi na Utamaduni wa Jamii (Matini Huria). Ilisomwa Mei 06, 2023. Katika https://www.academia.edu/34828872/ELEZA_UHUSIANO_KATI_YA_FASIHI_SIMULIZI_NA_UTAMADUNI_WA_JAMII

Osore, M. (2015). *'Fasihi Andishi ya Kiswahili na Dini:Mifano ya Riwaya za Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi.'* CHAKAMA.

Ponera, A. (2014). *Utangulizi wa Nadharia ya Fasihi Linganishi*. Karljamer Print Technology.

Ponera, A. (2019). *Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasnifu*. Central Tanganyika Press.

Poveteva, E.V. (2012). Intertextuality in European Literature Expresses Through Precednt Situation and Characters. European Journal of History.

Ren, X. (2015). *The Literary Interpretation of the Influence of Bible*. Studies in Language and Literature. UCT.

Ryken, L. (2014). *A Complete Handbook of Literary Forms in the Bible*. Heko Publishers Limited.

Sanchez, M. (2021). 'Maana ya Dini'. Ilisomwa Mei 5, 2023. Katika https://sw.warbletoncouncil.org/religion-3171

Sanchez, M. (2021). 'Maana ya Talaka'. Ilisomwa Februari 3, 2023. Katika https://sw.warbletoncouncil.org/divorcio-3276

Sengo, T. (1993). *'Misingi ya Uhakiki katika Fasihi ya Kiswahili'*. *Jarida la Kiswahili*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Sengo, T. S. Y. (2009). *Tungizi za Mnyagatwa*. Al-Amin Education and Research Academy.

Senkoro, F. E. M. K. (2011). *Fasihi: Mfululizo wa Lugha na Fasihi*. KAUTTU.

Shemweta, G. (2015). *Itikadi katika Tamthiliya za Emmanuel Mbogo: Utafiti Linganishi wa Ngoma ya Ng'wanamalundi na Fumo Liyongo*. (Haijachapishwa). (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania). Makavazi ya Chuo.

Swahili Union Version (1997). *Biblia ya Kiswahili.* Tanzania. Bible Society of Tanzania.

Syambo, B. & Mazrui, A. (1992). *Uchambuzi wa Fasihi.* East African Educational Publishers.

Wafula, R. (2015). Mwingilianomatini katika Cheche za Moto na Kidagaa Kimemuozea (Haijachapishwa). (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Kenyatta).

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele vyake.* Phoenix Publishers Ltd.

Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*. Focus Publications.

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi za Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Vide Muwa Publishers Ltd

Wamitila, K.W. (2010). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi.* Vide Muwa Publishers Ltd.

Wanjiru, N. S. (2022). *Mwingilianomatini katika Tamthiliya za Kinjeketile na Majira ya Utasa* (Haijachapishwa). (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Maasai). Makavazi ya Chuo.

Watchtower, B. T. P. (2017). *Biblia Takatifu – Tafsiri ya Ulimwengu Mpya*. New York. Watchtower Bible and Tract Society of New York, Inc.

Yin, R. K. (1994). *Case Study Research: Design and Methods* (2nd ed., 1st ed., 1984; rev. ed., 1989). Thousand Oaks, CA: Sage Publications.

Yunus, M. K. (2013). *Masuala ya Kisiasa katika Ushairi wa Kandoro: Mifano Kutoka Katika Mashairi Yake* (Haijachapishwa). (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania). Makavazi ya Chuo.

Zelda, E. (2018). 'Mbinu za Utafiti – OSW 616'. (Semina, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania). Mfumo wa Masomo ya Masafa 2018 – 2019.